# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 21 Mei, 2019

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe.Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu!

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU MIFUGO NA UVUVI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu tunaendelea.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Semguruka Mbunge wa Viti Maalum alize swali lake.

Na. 262

**Kuonge Shule za Kidato cha Tano na Sita – Karagwe**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza:-

Wilaya ya Karagwe ina Sekondari moja tu ya kidato cha Tano na Sita ambayo ni Bugene Sekondari.

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Sekondari za Nyabionza na Kituntu ili ziwe shule za kidato cha Tano na Sita?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepeleka kiasi cha shilingi milioni 190 katika shule Nyabionza kwa ajili ya ujenzi

wa madarasa mawili na mabweni mawili. Aidha, ujenzi na ukarabati wa maabara tatu, bweni moja la wasichana, maktaba, bwalo na jiko unaendelea kwa kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe. Vilevile Shule ya Sekondari Kituntu, imepokea jumla ya shilingi milioni 52.5 ambazo zinatumika kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili na bweni moja ambalo liko katika hatua ya umaliziaji. Kadhalika, halmashauri inaendelea na ujenzi wa maktaba moja, bweni moja la wavulana, madarasa mawili, bwalo la chakula na jiko kwa kutumia mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli hizi za ujenzi wa miundombinu ni maandalizi ya kuzipandisha hadhi shule hizo mara tu zitakapokamilika ambapo zitasajiliwa na kupangiwa wanafunzi wa kidato cha tano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oliver swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(i) Je, Serikali itapeleka lini fedha ilizoahidi kwa ajili ya kujenga mabweni na maktaba pale Bugene Sekondari ambao ni *A-level* peke yake ya Serikali kwenye wilaya ya watu laki tatu na tisini?

(ii) Je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kuambatana na mimi pamoja na Mbunge wa Jimbo Mheshimiwa Bashungwa ili ukajionee mlundikano wa wanafunzi Bugene Sekondari kwa sababu ya upungufu wa mabweni?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Oliver kwa maswali mafupi ya nyongeza ya kibunge kabisa Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza naomba nianze kujibu swali la pili kwa kwanza nipo

tayari tutaambatana pamoja hakika tutaenda kufanya kazi nzuri tu kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifupi niseme nimpongeze sana Mheshimiwa Oliver, kwa sababu yeye na Mbunge Mheshimiwa Innocent wamekuwa wakipambana sana kuhakikisha Halmashauri ya Karagwe inafanya vizuri. Eneo hili ndio maana hata ile shule ya kwanza tuliyoipatia shilingi 190 ni kwa ajili ya maombi yao waliyoyaleta ofisi kuhakikisha tunasaidia wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na upande wa Bugene sekondari tunajua ni wazi kweli idadi ya wanafunzi ni wengi, naomba nikuhakikishie Serikali itafanya kila liwezekanalo kuhakikisha tunaongeza fedha pale kwa ajili miundombinu ile iweze kuimarika vizuri tuweze kupokea watoto ambao tunatarajia si muda mrefu tutawatangaza. Kwa hiyo, hii ni *commitment* ya Serikali tutafanya kila liwezekanalo tutaongeza fedha kuimarisha miundombinu ya pale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali, katika jimbo langu la Bunda kuna maboma ya maabara na hasa katika Shule ya Sekondari Salama. Mheshimiwa Waziri hatudhuliani ni ndugu yangu, katika ile shule kumekuwepo na maboma mawili ambayo kuna mabati na mbao zinaenda kuonza ni muda mrefu, wananchi hali yao ni mbaya wamekuwa na michango mingi kwenye maeneo mbalimbali. Nakuomba Waziri hili ni ombi rasmi nakuomba Waziri unisaidie kunipelekea milioni 30 tu kwenye shule ya sekondari salama ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue ombi la Mbunge Boniphace kwa sababu nikifahamu eneo lake lile kwa kweli kuna changamoto nyingi mbalimbali na nikiri wazi kwamba eneo hilo lazima tulipe

kipaumbele kwa sababu kuna fedha tu kidogo zinahitajika tutaangalia mfuko ukoje halafu tutashirikiana mimi na wewe kuangalia jinsi gani tutafanya kuhakikisha hiyo miundombinu ambayo wananchi wamejitolea isiweze kuharibika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leah Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru shule ya wasichana Nyalanja yenye kidato cha tano na sita ina mchepuo mmoja tu lakini inayo madarasa sita zaidi ya miaka mitano hayatumiki.

Je, Serikali haioni haja ya kutupatia bweni kwa ajili ya kuongeza mchepuo mwingine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi kwa swali hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna miundo mbinu kama hiyo, naomba nilichukue jambo hilo kwa sababu hivi sasa ukingalia tuna vijana wengi sana ambao kwa kweli ufaulu umeongezeka. Kwa mfano mwaka huu tuna vijana zaidi laki moja *plus* ambao wote wanatakiwa wape nafasi kwa ajili ya kidato cha tano na kuendelea. Kwa hiyo, kama kuna fursa kama hiyo ya madarasa yapo tutaangalia nini tufanye ikiwezekana tukatafute fedha kwa haraka tuongeze pale bweni kwa ajili kuhakikisha kwamba tunaongeza mchepuo mwingine vijana wengi wa kitanzania waweze kupata nafasi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo wanafunzi wengi wa kike wamekuwa wakipata mimba katika mazingira magumu.

Je, Serikali ina mikakati gani kujenga *hostel* za watoto wa kike ili wapate kujistiri waondokane na vishawishi vya barabarani?

**MWENYEKITI:** Haya ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo kwa kifupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ndio maana azma ya Serikali juzi juzi mwezi wa tatu Serikali imetoa takribani shilingi bilioni 54.6 ambayo katika hili lengo lake ni kujenga madarasa takribani 988 lakini mabweni mapya 210 kwa hiyo ni *commitment* ya Serikali kuhakikisha jinsi gani mabweni haya yanjengwa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa dada yangu naomba nikuhakikishie kwamba tutafanya kila liwezekano tutaangalia nini tufanye licha tunaanza kujenga mabweni 210 katika maeneo mbalimbali lakini juhudi ya Serikali itaendelea kuhakikisha vijana hawa wa kike tunawaondoa katika hali hatalishi zaidi hasa kwa watu ambao wana nia mbaya kuhakikisha wanaharibu *future* ya watoto wa kike. Kwa hiyo, tunaendelea kulichukua kwa ajili ya Serikali kulifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi Mbunge wa Mpanda Mjini sasa aulize swali.

Na. 263

**Bajeti ya TARURA Mkoa wa Katavi**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Katika Bajeti ya mwaka 2018/2019 Mkoa wa Katavi ulitengewa kiasi kidogo cha fedha kuliko mikoa yote.

Je, Serikali iko tayari kuongeza mgao wa fedha kwa Mkoa wa Katavi kwa kuzingatia jiografia na kilomita za mtandao wa barabara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi Mbunge wa jimbo la Mpanda Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kupanga bajeti kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara kwenye Mamlaka za Serikai za Mitaa. Serikali inazingatia vigezo mbalimbali ikiwemo kigezo cha mtandao wa barabara ullisajiliwa. Mkoa wa katavi katika mwaka wa fedha 2018/2019, uliidhinishiwa shilingi 3.62 kwa kuzingatia matandao wa barabara uliopo ambao ni kilomita 1,441.3. Vigezo vingine vinavyozingatiwa na pamoja na tabaka la barabara hali ya mtandao wa barabara, idadi ya magari yanayotumia barabara na idadi ya watu wanaohudumiwa na barabara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia bodi ya mfuko wa barabara inaendelea na zoezi la uhakiki wa mtandao wa barabara zinazosimamiwa na TARURA ili kuishauri Serikali kufanya mapitio ya mgawo wa fedha za mfuko wa barabara na kuhakikisha barabara zinazohudumiwa na TARURA zinatengewa bajeti ya kutosha kwa ajili ya matengenezo hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapufi.

**MHE. SEBASTIANA S. KAFUPI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru pamoja na majibu mazuri ya Serikali Mkoa wa Katavi ni kati ya mkoa ambayo haijafunguka kwa maana ya kuunganishwa na mikoa mingine. Kitendo cha kupewa kilomita hizo chache kinafanya mkoa huu uendelee kujifunga. Serikali inasema nini katika hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo kama haitoshi kigezo cha idadi ya magari yanayopita katika barabara ni tunda la uzuri wa barabara. Serikali inasema nini kwenda kuboresha barabara ili baadaye idadi ya magari iongezeke?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa maswali hayo ya nyongeza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nami ni shahidi kwa sababu nimefika Mkoa wa Katavi mara kadha na Mheshimiwa Kapufi anafahamu, na ndio maana Serikali hata katika Manispaa yake pale tunawekeza fedha nyingi sana kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu wa barabara za lami. Lakini hata hivyo ni kweli vigezo hivi vimewekwa kwa mujibu wa utaratibu kama pale itakapobidi tutaangalia nini kifanyike kuhakikisha kwamba Mkoa wa Katavi unapatiwa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo naomba nikuhakikishie kwamba jukumu la wizara yetu yale maeneo yenye changamoto kubwa tutahakikisha kwamba kama maoni yako ulivyotoa hayo tutahakikisha jinsi gani tunaipa nguvu. Na ndio maana hata katika *addition finance* ya sasa hivi ambayo bado hatua *disclose* tumeweka kipaumbe kwa ajili ya kuongeza katavi kupata fedha nyingi za ziada nini kifanyike katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hivyo katika suala nzima la *traffic* ya magari kama ulivyosema ni jukumu la Serikali sisi tunahakikisha kwamba tunaimarisha miundombinu ya barabara hizo lengo kubwa ni kwamba barabara zikifunguka magari mengi yatapita. Kwa hiyo, ni jukumu la Serikali kwa hiyo Mheshimiwa Kapufi usihofu Serikali ipo kwa ajili yakuwahudumia wananchi.

**MWEYEKITI:** Mheshimiwa Hasna Mwilima.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Halmashuri ya Uvinza ni halmashauri ambyao kijiografia na kimuundo imekaa katika mazingira magumu sana. Lakini kwenye mgao wa bajeti Halmashauri ya Uvinza imekuwa ikipata pesa dogo, na huku inashindwa kutekeleza miradi ya kimaendeleo katika halmashauri yake. Mheshimiwa Waziri ni shahidi aliona ukubwa wa jimbo na mazingira jinsi yalivyo na alituahidi kutuongezea fedha katika mgao wa bajeti.

Je, Mheshimiwa Waziri katika bajeti ya 2019/2020 umezingatia kuongeza pesa za maendeleo katika Halmashauri ya Uvinza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nami nilikuwepo Uvinza mara kadhaa na juzi juzi nilikuwanae Mheshimiwa Mbunge. Na ni kweli ukitoka makao Makuu ya uvinza mpaka unafika kule kalya karibu kilomita 300 na jimbo kweli ni kubwa, kwa hiyo, jukumu la Serikali tutafanya kila liwezekanalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana katika bajeti ya mwaka huu kuna fedha kidogo tumeiongeza Mheshimiwa Mbunge na hata katika kipaumbele tukaona hata pale mjini kidogo japo angalau tuongeze na tabaka la lami.

Kwa hiyo, kuna bajeti ya kuweka tabaka lami pale mjini lakini hata hivyo tunajua kwamba changamoto kubwa ipo katika Uvinza kwa siku za usoni tutaendelea kwa kuifanyia kazi eneo hili kwa sababu kasungura kenyewe kadogo tutajitahidi kufanya kila liwezekano lengo kubwa ni kuimarisha Uvinza iende vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maftaha Nachuma.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri pale Mtwara Mjini Manispaa ya Mtwara mjini nimekuwa naulizia barabara kwa muda mrefu barabara ya kutoka Mikindani, Lwelu mpaka Dimbuzi lakini barabara ya kutoka kata ya ufukoni, Mbaye mpaka Mbawala chini. Lakini barabara ya kutoka Mtawanya mpaka Namayanga. Barabara hizi nimekuwa nikizungumza ndani ya Mbunge hapa kwa muda mrefu na hivi sasa TARURA imekuwa inasuasua kuzitengeneza barabara hizi ambazo ni muhimu kwa wananchi wa Manispaa ya Mtwara Mikindani.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzitengeneza barabara hizi kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi ya swali hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuchukue jambo hili kama ulivyosema Mheshimiwa Mbunge. Lakini naomba kuweka takwimu sawa kwamba katika maeneo ambayo tumeyapa kipaumbele sana ni Mtwara Mikindani. Katika mpango wetu wa miji mikakati, miji ile ambayo nane ambayo inahusisha Tanga, Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Ujiji lakini vilevile Mikindani ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndio maana leo ukiangalia ya miaka mitano iliyopita na Mtwara ya leo ni vitu tofauti. Lakini huwezi ukafanya mambo yote kwa siku moja, imani yangu Serikali tutaendelea kupambana lengo kubwa ni kuwahudumiwa wananchi hasa wa Mtwara mikindani na maeneo mengine waweze kuhakikisha barabara zao zinapitika kwa wakati wote.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Jafo tunaendelea na Waziri Wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Maulid Said Mtulia Mbunge wa Kinondoni sasa aliuze swali lake.

Na. 264

**Hitaji la CT- SCAN na MRI Mashine Hospitali ya Rufaa Mwananyama**

**MHE. MAULID S. MTULIA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itanunua *CT-SCAN Mashine* na MRI mashine kwa ajili ya Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala ili kupunguza msongamono katika Hospatali ya Muhimbili na kuongeza ufanisi katika hospitali hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maulid Said Mtulia Mbunge wa Kinondoni kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mwongozo ulikuwepo huduma za *CT- Scan* na *MRI* hazikuwepo kwenye hospitali za Rufaa za Mikoa. Hata hivyo, kufuatia mabadiliko ya kiuchumi na uhitaji wa huduma hizi kwa wananchi wizara yangu ilifanya mabadiliko ya mwongozo kwa kutengeneza mwongozo wa vifaa vya Radiolojia nchini wa mwaka 2018 *standard Medical Radiology and imaging Equipment Guidelines – SMRIEG* ambapo pamoja na mangineyo huduma za *CT-SCAN* sasa zinapatikana katika ngazi ya hospitali za rufaa za mikoa na huduma za *MRI* zitapatikana katika ngazi ya hospitali za rufaa za kanda na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokana na mabadiliko hayo Serikali inakusudia kufunga *CT-SCAN* katika Hospitali ya rufaa ya mikoa ya Mwananyamala ambapo utelekezaji wake umeshaanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtulia swali la nyongeza.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Hospitali yetu ya rufaa ya Mwananyamala ni miongoni mwa hospitali inayotoa huduma kwa wagonjwa wengi sana. Kiasi kwamba kwa siku moja inahudumiwa wangonjwa takribani 2000. Na idadi ya madaktari wetu si zaidi ya madaktari ambao wanajigawa katika *shift* tatu. Je, Serikali ina mpango gani kuongeza Watumishi Manesi,

Wakunga na madaktari ili hospitali yetu iweze kutoa huduma bora zaidi?

(ii) Kwa kuwa hospitali yetu ya Mwananyamala imezungungwa na baadhi ya kata ambazo hazina hata zahanati, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni ametoa pesa zaidi ya milioni 90 ili kujenga zahanati katika Kata ya Makumbusho. Je, Serikali ina waahidi nini wananchi wa Kata ya Makumbusho kuongeza ili ile zahanati ile iweze kukamika kwa haraka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nimpongeze sana Mheshimiwa Maulid Mtulia, kwa jinsi anavyofuatilia upatikanaji wa huduma za Afya kwa wananchi wa Kinondoni, hakika Kinondoni imepata Mbunge wa Chama cha Mapinduzi ambaye anajua kufuatilia changamoto zinazowakumba wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ni lini tutaongeza watumishi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwananyamala nakubaliana na Mbunge hata ukiangalia tu takwimu za wagonjwa ambao wanahudumiwa katika Hospitali zetu za Rufaa za Mikoa ishirini na nane, Mwananyamala inaona wagonjwa kwa mwaka takribani laki tatu. Ukilinganisha na Mount Meru inaona wagonjwa elfu ishirini na nne kwa mwaka, Manyara wagonjwa elfu ishirini na saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge haja ya kuongeza madaktari wauguzi na wataalamu wengine wa Afya katika Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala. Nikuahidi tu Mheshimiwa Mbunge tunafanya mchanganuo wa hali halisi ya watumishi wa Afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Wilaya, Zahanati na Vituo vya Afya ili kabla ya kupata nyongeza ya watumishi tuweze kuwagawanya upya. Kwa sababu

unaweza ukakuta kuna Mkoa wagonjwa wanaona ni wachache lakini wana watumishi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hilo tayari tumelibainisha katika ngazi ya Wizara, lakini swali lake la pili kwamba kuna kata hazina Zahanati ikiwemo Kata ya Makumbusho, Mheshimiwa Mbunge tumeongea suala hili, na Ndugu yangu Mheshimiwa Jafo ambaye ni kaka yangu, ni pacha wangu katika utoaji wa huduma za Afya ngazi ya msingi yuko hapa, kwa hiyo tutalishughulikia, na tutahakikisha katika fedha ambazo tunazipata kwa ajili ya utoaji uboreshaji wa miundombinu ya huduma za afya za msingi basi tunakuletea Makumbusho ili kukuunga mkono kuweza kumaliza Zahanati ya Makumbusho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza; pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kwamba sasa Serikali iko tayari kutuletea mashine za *CT-SCAN* na *MRI* katika Hospitali za Mikoa, ikiwemo Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado tuna changamoto kubwa, katika Hospitali zetu za Mkoa wa Dar es Salaam hatuna mashine za kufulia nguo, hali ambayo inasababisha tuishiwe mashuka mara kwa mara, kwa sababu mashuka yanafuliwa katika Hospitali ya Muhimbili ndiyo yaletwe Temeke, Je, Serikali ina Mpango gani sasa wa kutuletea mashine za kufulia nguo katika Hospitali zetu za Temeke, Mwananyamala na Amana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mariam Kisangi hasa kwa jinsi anavyofuatilia

huduma za afya hasa, afya ya mama ya mtoto kwa Wanawake wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mashine za kufua nguo kama nilivyoeleza wakati tunawasilisha Bajeti yetu, tumezipokea Hospitali za Rufaa za Mikoa kuanzia tarehe 1 Julai, 2018 na tumejipanga kama Wizara kuhakikisha tunaboresha huduma zote ikiwemo miundombinu pamoja na kufunga na kununua mashine za kufulia katika Hospitali zetu zote za Rufaa za Mikoa sambasamba na kuweka Madaktari bingwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lini, naomba nilichukue halafu tutatoa majibu ndani ya Bunge hili, lini tutaanza kuweka vifaa hivyo lakini kama nilivyoeleza tumeshaanza kuondoa vifaa vya kuweka kwa ajili ya Hospitali zetu za Rufaa za Mikoa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay. Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Hospitali ya Mji wa Mbulu ni Hospitali iliyokuwa inahudumia Wilaya ya Babati, Karatu na Mbulu. Hospitali hiyo iliyojengwa toka enzi za koloni imekabiliwa na changamoto lukuki, moja ya changamoto iliyoko ni uchakavu wa gari la *ambulance*, na kwa kuwa Hospitali hiyo iko mpakani mwa Jimbo la Mbulu Vijijini, Jimbo la Karatu na Jimbo la Babati na Hospitali za Rufaa ni *Haydom* na *KCMC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mbulu inashindwa kusafirisha wagonjwa wake, kutokana na upungufu wa wataalamu na vifaa chakavu.

Je, ni lini Mheshimiwa Waziri ataisaidia Hospitali ya Mji wa Mbulu kuipatia gari la *ambulance*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Issaay kwa swali lake zuri, kuhusu hali ya Hospitali ya mji wa Mbulu hasa upatikanaji wa gari la wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeagiza na yanakaribia kuingia nchini magari ya wagonjwa hamsini kwa hiyo naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha gari moja linaenda Mbulu na kwa Waheshimiwa Wabunge ambao labda mnataka pia kuomba *Ambulance*, tumeagiza tena *ambulance* hamsini, kwa hiyo tunatarajia kuwa na magari ya wagonjwa mia moja, tutayagawa katika maeneo ya vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo nitaomba tu wenye maswali kidogo watuvumilie tutakapoleta orodha ya mgao wa *Ambulance* basi tutaweza kuongeza zaidi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza suala linalohusiana na Hospitali ya Mwananyamala juu ya *CT*–SCAN inafanana kabisa na suala ambalo liko Mkoa wa Mtwara hasa Hospitali ya Ndanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba Serikali ilifanya Hospitali ya Ndanda kuwa Hospitali ya Rufaa ya Kanda, na Wamisionari wale wamejitahidi sasa hivi wanatoa huduma ya dialysis na huduma nyingi tu na ndiyo sehemu kubwa hasa inayotumika kama Hospitali ya Wilaya kwa sababu Hospitali ya Mkomaindo haina *facilities* nyingi, sasa swali langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wanafanya kazi hii na Ubia wa Serikali, Je, Serikali haioni haja ili kupunguza msongamano wa watu kupelekwa Muhimbili na Rufaa hizo kuwapelekea Hospitali ya Ndanda *CT-SCAN* pamoja na *MRI* machine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Cecil Mwambe Mbunge wa Ndanda kwa swali lake zuri, kwanza nataka kutambua umuhimu au kazi nzuri inayofanywa na Mashirika ya Dini katika kutoa huduma za Afya na sisi Sera yetu ya Afya ya mwaka 2007 inatambua na kuthamini mchango wa Mashirika ya Dini katika utoaji wa huduma za Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa, je tutapeleka *CT-SCAN* na *MRI* katika Hospitali ya Rufaa ya Ndanda ni kweli Hospitali hizi tumezipandisha hadhi mwaka 2010 kuwa Hospitali za Rufaa za Mikoa. Lakini Mheshimiwa Mwambe utakubaliana na mimi, tunayo Hospitali pia ya Serikali ya Rufaa ya Mkoa Ligula.

Kwa hiyo, sasa mtuambie wana Kusini, wananchi wa Mtwara kwamba tupeleke Ligula, au tupeleke Ndanda? Lakini ambaye nasimamia moja kwa moja, Hospitali zangu za Serikali kipaumbele unajenga kwako kabla hujajenga kwako kabla hujajenga kwa mwingine. Tutaendelea kuthamini na kuheshimu mchango wa Mashirika ya Dini na ndiyo maana zaidi ya asilimia 70 ya watumishi waliokuwepo katika Hospitali hizi za Mashirika ya Dini wanalipwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, zikiwepo nyingi tutapeleka Ndanda na Ligula, lakini ukiniambia nichague, nitaanza na Ligula kwa sababu ndiko pia wananchi wengi wanaenda kupata huduma za Afya katika ngazi ya Mkoa wa Mtwara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto swali fupi la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali kwa kazi nzuri ambayo anafanya kusambaza baadhi ya mashine kwenye Hospitali mbalimbali za Rufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuwa wagonjwa wa ugonjwa wa Kisukari umeongezeka kwa kasi na kwa kuwa mashine za kusafirishia figo ziko sehemu chache ikiwepo Dar es Salaam, *KCMC* na Dodoma na wagonjwa wanapata shida sana kwenda kusubiria kusafisha figo, je Serikali sasa haioni imefikia wakati muafaka wa kuhakikisha kila Hospitali ya Rufaa kunakuwa na mashine hizo za kusafishia figo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Kaka yangu Venance Mwamoto kwa swali zuri, Mbunge wa Kilolo, ni kweli kuna ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza hasa wagonjwa wa Kisukari, wagonjwa wa Moyo, Saratani na kuhusu sasa tuweke huduma za *dialysis* za kusafisha damu katika Hospitali za Rufaa za Mkoa nakubaliana naye na habari njema tunategemea kupata mashine zaidi ya sitini kutoka Saudi Arabia, ambazo tutaziweka katika baadhi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo nakabaliana nayo sasa kama Waziri ni upatikanaji wa wataalamu ambao wanatakiwa kutoa huduma hiyo, lakini tunaongea na Serikali ya Saudi Arabia ikiwezekana tuwe na mpango wa haraka wa kupeleka wataalamu katika Hospitali zao na Hospitali nyingine kwa mfano KCMC, Muhimbili, *JKCI* na Bugando ili tuweze kuongeza ujuzi. Mashine tutaweka, naomba niseme siyo kuanza na Hospitali zote, tutaangalia kwa mfano Katavi, hatutegemei mtu atoke Katavi mpaka Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaangalia maeneo ambayo hayafikiki Katavi, Ruvuma, Rukwa, Lindi kwa hiyo, tumebainisha kama Hospitali tano za kuanza nazo. Labda nitoe angalizo tusisubiri mpaka muda wa kwenda kupata huduma za *dialysis*, yapo mambo ambayo tunaweza kufanya kama wananchi kama Watanzania, ili kuepukana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza ikiwemo kufanya mazoezi mara kwa mara kuangalia ulaji wa vyakula vyetu,

lakini pia kupunguza matumizi ya tumbaku na sigara itatuepusha na magonjwa yasiyo ya kuambukiza, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu, maswali ya Afya ni mengi na kwa leo yanatosha tuendelee na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali la Mheshimiwa Machano Othman Said. Mheshimiwa Machano.

Na. 265

**Upungufu wa Wafanyakazi katika Idara ya Uhamiaji Zanzibar**

**MHE. MACHANO OTHMAN SAID** aliuliza:-

Kwa muda mrefu kumekuwa na upungufu mkubwa wa Wafanyakazi wa Idara ya Uhamiaji Zanzibar hali inayopunguza ufanisi wa kazi katika Idara hiyo?

(a) Je, ni lini Serikali itaajiri Wafanyakazi wa kutosha katika Idara hiyo?

(b) Je, ni lini Serikali itaimarisha Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Mjini Magharibi ili kupunguza msongamano katika Ofisi kuu ya Uhamiaji Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Alhaj Masauni.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Machano Othman Said Mbunge wa Baraza la Wawakilishi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Uhamiaji imetengewa Bajeti ya kuajiri Watumishi 505 katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika mwaka wa fedha 2017/2018 Idara ya Uhamiaji limefanya upanuzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kuongeza vyumba vitatu kwa ajili ya kuimarisha huduma za Kiuhamiaji ikiwemo huduma ya pasipoti mtandao, pia katika Bajeti ya mwaka huo Idara ya Uhamiaji imetenga fedha kwa ajili ya upanuzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua hiyo Idara itakuwa imeongeza wafanyakazi, pia Ofisi ya Uhamiaji Mjini Magharibi itaimarika ili kupunguza msongamano uliopo katika Ofisi kuu ya Uhamiaji Zanzibar.

**MWENYEKITI:** Mheshiwa Othman Machano. *(Makofi)*

**MHE. MACHANO OTHMAN SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu lake lakini pamoja na majibu hayo nataka kumuuliza swali lifuatalo, kwa kuwa mwaka wa fedha 2018/2019 umebakisha kama mwezi mmoja kumalizika, na kwa kuwa ajira hizi bado hazijafanyika, na kwa kuwa upungufu huu wa wafanyakazi unasababisha wafanyakazi zaidi ya wale wa malindo kuingia kazini usiku na asubuhi kurejea tena kazini, Je, Mheshimiwa Waziri anatuhakikishia vipi kwamba ajira hizi 505 zitafanyika kwa wakati.

(b) lakini, Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mjini Magharibi inafanya shughuli zake, wananchi wengi wa Zanzibar badala ya kwenda kwenye Mkoa wanakwenda Makao Makuu, Ofisi Kuu kwa sababu kule Mkoa hakuna nyenzo za kufanyia shughuli zao hasa *passport*. Ni hatua gani Serikali itachukua ili kupunguza mzigo Ofisi Kuu na wananchi kwenda katika Mkoa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ajira, kama ambavyo nimezungumza kwamba tunatarajia kuajiri na hivyo, basi pale

ambapo kibali kitakuwa kimepatikana kutoka Utumishi vijana hao wataajiriwa, lakini swali lake la pili kuhusiana na kuboresha mazingira ya Ofisi ya Mjini Magharibi, ili kupunguza msongamano Makao Makuu nataka nimuhakikishie kwamba katika mwaka wa fedha tumetenga takribani shilingi milioni mia tatu kwa ajili ya kukamilisha matengenezo ili tuweze sasa kutumia vizuri zaidi, mara kazi hizo zitakapokamilika kwa mwaka huu, basi ni dhahiri kwamba sasa mazingira ya kazi katika Ofisi ya Mjini Magharibi yataboreka na msongamano utapungua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya juhudi kadhaa ambazo zimefanywa lakini bado unyanyasaji wa watu Maafisa Uhamiaji kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma, na hasa Manispaa ya Kigoma Ujiji kwenye masuala ya Uraia bado ni mkubwa, sasa Serikali haioni kwamba inge-*priortise* watu kupewa vitambulisho vya Uraia kwa haraka, ili kuweza kuhakikisha kwamba tunaondoa hili tatizo la watu kila wakati kukisiwa kwamba sio raia.? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimuhakikishie Mheshimiwa Zitto, kwamba, malalamiko ambayo yeye pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma ambayo walikuwa wanayatoa kipindi cha nyuma kuhusiana na unyanyasaji wa wananchi tuliyafanyia kazi na kipindi ambacho tulikwenda kwenye ziara nikiwa nimeambatana na Mheshimiwa Waziri Mkuu na yeye alikuwepo nadhani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulilithibisha hilo kwamba sasa hali siyo kama ilivyokuwa, hata hivyo nimpongeze kwa rai yake na nimuhakikishie kwamba rai ambayo amezungumza ndio rai ya Serikali na ndiyo maana katika Bajeti yetu iliyopita tulieleza kwa mapana kuhusu malengo ya Serikali ya kuhakikisha kwamba tunafikia yale malengo tuliyoyapanga ili wananchi waweze kupata Vitambulisho hivi

na hatimaye iweze kurahisisha mambo mbalimbali ikiwemo hayo ambayo yamezungumzwa, lakini na mambo mengine mengi ambayo yanatokana na faida za kuwa na kitambulisho hiki cha uraia.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 266

**Huduma za Chakula Mgerezani**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO** aliuliza:-

Je, nini Mkakati wa Serikali kuhakikisha Magereza zetu zinajitegemea kwa chakula?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha Jeshi la Magereza linajitosheleza kwa chakula cha wafungwa na mahabusu, Serikali imeendelea kulipatia Jeshi zana na pembejeo mbalimbali za Kilimo kupitia fedha za matumizi ya kawaida na za miradi ya maendeleo. Kwenye Bajeti ya mwaka 2018/2019 Serikali imetenga fedha kwa miradi ya maendeleo ya jumla ya shilingi Bilioni tatu kwa ajili ya ununuzi wa zana mbalimbali za Kilimo na kukamilisha miundombinu ya umwagiliaji Gereza Idete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza linaendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa miaka mitano wa mwaka 2018/2019 mpaka 2022/2023 kwa kutumia raslimali zilizopo ambapo katika msimu wa mwaka 2018/2019 Jeshi

limelima jumla ya ekari 5,110 za mazao ya chakula kwa mchanganuo ufuatao; mahindi ekari 3,505, mpunga ekari 1,050 na maharage ekari 555 kwa matarajio ya kuvuna jumla ya tani 9,509.25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika Awamu ya II ya utekelezaji wa Mkakati huu, Jeshi linaendelea kukamilisha andiko la Mapinduzi ya Kilimo kwa mwaka 2019/2020 na mwaka 2023/2024 likiwa na lengo la kuondokana na utegemezi wa chakula kwa wafungwa na mahabusu kutoka Serikalini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nashukuru kwa majibu japo hayajajitosheleza Kilimo cha Umwagiliaji ndiyo njia pekee ya kuhakikisha kwamba tunapata chakula cha uhakika, au mavuno kwa uhakika, lakini ukiangalia katika Magereza yote tuliyonayo nasema kwamba ni Gereza la Idete pekee ndiyo wenye Kilimo hicho cha Umwagiliaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata Bajeti ya mwaka huu, ya maendeleo bado Wizara hii imeendelea kutenga shilingi Bilioni tatu kwa ajili ya Kilimo, jambo ambalo bado litaendelea na utegemezi. Je, Wizara haioni sasa kuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba wanaendeleza Kilimo cha Umwagiliaji ili Magereza wetu na Mahabusu waweze kupata chakula? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa takwimu zinaonyesha kwamba mahabusu ni wengi kuliko wafungwa na kwa maana hiyo ndiyo sababu chakula hakitoshi, Je, Serikali haioni sasa kuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba mahabusu hasa wale wenye kesi za madai, kwa mfano kesi ya kuiba kuku nakadhalika nakadhalika, hawakai ndani ya Magereza kwa muda mrefu na kupewa shughuli nyingine ili wale wafungwa ambao ndiyo wanapaswa kufanya kazi, kwa sababu tunajua kwamba mahabusu hawaruhusiwi kufanya kazi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali isihakikishe kwamba wale mahabusu ambao ndiyo wengi kuliko wafungwa wanaondoka kwenye Magereza na kupata kazi nyingine za nje, ili sasa Magereza wetu au wafungwa waweze kufanya kazi na waweze kujitosheleza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimuhakikishie kwamba mawazo yake aliyoyatoa ni mawazo ya Serikali, na ndiyo maana katika Bajeti yetu ya mwaka huu tumeongeza kwa kutenga fedha hizo kwa ajili ya *specifically* kwenye eneo la Umwagiliaji, kwa Magereza kwa Kitengule na Isopilo, kwa hiyo siyo Idete peke yake, kuna Magereza mengine. Hata juzi juzi tu nilikwenda kwenye Gereza la Songwe na niliwasisitiza juu ya umuhimu wa kufikia malengo na tukakubaliana malengo hayo yatafikiwa kwa kuhakikisha kwamba wanatumia utaratibu wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hii hoja ya Umwagiliaji ni hoja ambayo ni ya msingi kama ulivyozungumza na sisi kama Serikali kupitia Jeshi la Magereza tumeiona na tunaifanyia kazi. Kuhusu suala la pili, kuhusu mahabusu ni kweli hatufurahishwi na msongamano wa mahabusu katika magereza yetu. Kama ambavyo nimejibu kwa kina wakati nikichangia bajeti hapa kwamba Serikali inafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha kwamba tunapunguza idadi ya mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini moja katika jambo ambalo ni la msingi ambalo nadhani hili wananchi watusaidie pamoja na wewe Mheshimiwa Mbunge ni kuhakikisha kwamba tunajitahidi kadri inavyowezekana kupunguza kufanya makosa. Tutakapopunguza kufanya makosa basi nadhani hata idadi ya mahabusu na wafungwa itapungua wakati ambapo Serikali inaendelea na jitihada nyingine mbalimbali ikiwemo kuharakisha ksi hizi ziweze kusikilizwa haraka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia, Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa muda mrefu baadhi ya vituo vya mahabusu, mahabusu wamekuwa wakitumia ndoo kama sehemu ya kujihifadhia wanavyokuwa mle ndani kwenye hivyo vituo. Je, kutumia hivyo vindoo ni sehemu ya adhabu? Kwa sababu imekuwa si tu inadhalilisha watu bali ni kukiuka haki za binadamu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba kwa kiwango kikubwa matumizi ya ndoo yanapungua na nina takwimu baadaYe nimpatie zinazoonesha kwmaba tumefanya jitihada za kutosha kupunguza matumizi ya ndoo kwa maana ya kuongeza ujenzi vya vyombo katika magereza yetu na kwa hakika kwa kasi hii ambayo tunaenda nayo basi miaka si mingi sana tutaondokana kabisa na tatizo hili la matumizi ya ndoo katika magereza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nsanzugwanko, Maria Chatanda.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza. Jeshi la Magereza ni kati ya taasisi ambazo zilipewa kazi maalum ya kuzalisha mbegu na hasa mbegu za nafaka. Ni kwanini hadi sasa Jeshi la Magereza pamoja na JKT hawafanyi kazi hiyo na tatizo la mbegu ni kubwa na Wizara ya Kilimo wamekiri kwamba jambo hili limekuwa ni zito sana kwao. Ni kwanini Jeshi la Magereza halifanyi kazi hiyo kikamilifu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango mkakati wetu wa

kujitosheleza na kilimo ambao nimezungumza kwamba tumeuandaa na tunauboresha kwa mwaka huu umegusia maeneo mengi. Nimesema kwamba katika mkakati huo kuna malengo ya kuhakikisha kwamba tuna magereza 10 ya kimkakati ya kilimo ambayo yatakuwa yanazalisha chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika kutimiza azma hiyo tunabidi tuliwezeshe Jeshi letu la Magereza kifedha ili liweze kutimiza malengo haya na ndiyo maana tunavyozungumza tayari tuna mazungumzo na Benki ya *TIB,* na *TID* kwa ajili ya kuweza kupata fedha kwa ajili ya shughuli hizo. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba katika mkakati huo, umeangalia maeneo mengi sio tu katika maeneo ya uzalishaji lakini unapozungumzia uzalishaji pamoja na zana za vitendea kazi, upatikanaji wa matrekta na ongezeko la idadi ya wafungwa katika magereza hayo ya kimkakati lakini pia na maeneo maalum ya kuweza kuhakikisha kwamba tunazalisha mbegu kwa ajili ya uzalishaji. Na hilo tutalianza katika gereza Kitwanga kule Kigoma kwenye Mkoa ambao Mheshimiwa Nsanzugwanko anatoka ili kuweza kwenda sambamba na ile dhana ya Serikali ya kuhakikisha kwamba zao la mchikichi linachukua nafasi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wazo lake ni zuri lakini ni sehemu ya mipango ambayo tunayo na mipango hii ambayo tunadhani kwamba ni muhimu sana na imetiliwa mkazo sana na Serikali hii kwa pamoja tukishirikiana tutafanikiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Chatanda, swali fupi la nyongeza.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Gereza la Kwa Mngumi lililopo Korogwe linafanya shughuli za kilimo pamoja na mabwawa ya samaki na kwa bahati nzuri Naibu Waziri umeshafika pale tukushukuru kwa kuwasaidia mashine zile za kufyatulia tofali. Je, sasa mtakuwa na mpango wa kuweza kuwasaidia kuwawezesha ili waweze kupanua yale

mabwawa pamoja na kilimo kama ambavyo mnaelekeza kwamba magerea waweze kujitegemea katika uzalishaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwenye gereza Kwamgumi lazima nikiri na naomba Mheshimiwa Mbunge hili alifikishe kama kuna uongozi ambao binafsi ulinivutia ni uongozi wa gereza la Kwamgumi wamefanya kazi kubwa sana. Ni gereza ambalo wenyewe kwa bidii zao wameweza kukamilisha miradi ya ujenzi wa nyumba nyingi kwa muda mfupi na kukamilisha zote, sio tu kufikia kile kiwango cha *lenter* lakini kukamilisha nyumba zote. Ndiyo maana ahadi ambayo tulitoa ya kuwapatia zile mashine za matofali tulitimiza kwa haraka na pia tukawaahidi kwamba tutawapatia mashine hizi *powertiller* kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, nina uhakika kwamba najua jitihada zako za kufuatilia, uendelee kunisumbuasumbua, ahadi yetu iko pale pale na nadhani tutakapoweza kufanikisha kupata *powertiller* tutazipeleka kwa sababu tunaamini uongozi wa gereza hili unaweza na hii iwe mfano wa magereza mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika ule mradi wa samaki, nimeshazungumza na kumuelekeza *CDP* kuhakikisha kwamba anapeleka fedha haraka ili mradi ule wa samaki wa ufugaji uweze kuendelea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nakubaliana na wewe kuhusiana na gereza hili, kazi nzuri ambayo inafanya na nikupongeze na wewe kwa kufuatilia na kuwa karibu na Jeshi letu la Magereza kufanikisha malengo hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 267

**Ujenzi wa Bandari Wete**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Katika jitihada za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki za kuboresha uchumi, viongozi wa Jumuiya hiyo walipitisha utengenezaji wa Bandari ya Wete – Pemba;

Je, mpango huo umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Bandari ya Wete ni mojawapo ya miradi 17 ya mfano *(flagship projects)* inayosimamiwa na wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyopitiswa katika mkutano wao wa kazi *(retreat)* uliofanyika mwezi Februari, 2018 Jijini Kampala, Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi inayotekelezwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki ni ile yenye sura ya kikanda (Mradi uweze kunufaisha nchi zaidi ya moja) ambapo nchi wanachama wamekubaliana kuitekeleza kupitia utaratibu wa kutafutiwa fedha kutoka kwa wabia wa maendeleo na kuitangaza kwa wawekezaji kikanda. Miradi hiyo hutekelezwa kwa kuzingatia mikataba inayoingiwa na nchi wanachama inayowezesha kukopeshwa fedha za utekelezaji.

Aidha, ulipaji na gharama za utekelezaji wa miradi hiyo hufanywa na nchi mwanachama inayonufaika moja kwa moja kutokana na mradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kuendeleza mradi wa Bandari ya Wete upo palepale Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendelea kuifanyia matengenezo bandari hiii ili iendelee kutoa huduma nzuri kwa wananchi. Matengenezo ambayo yamekwishafanyika ni pamoja na kutengeneza upana wa gati kufikia mita tisa na urefu wa mita tatu kuelekea baharini, na kulikarabati gati yote yenye urefu wa mita 54. Matengenezo hayo yaligharimu kiasi cha shilingi 473.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar imeshafanya mazungumzo na mwekezaji mzawa katika kuendeleza Bandari ya Wete. Tayari makubaliano ya mwanzo baina ya Wizara husika kupitia Shirika la Bandari Zanzibar na mwekezaji yameshafanyika na hivi sasa mwekezaji kwa kushirikiana na wataalam wa shirika la bandari wamo katika maandalizi ya kufanya upimaji *(surveying)* ya eneo lililopendekezwa kuwepo bandari ili kutayarisha michoro (usanifu) inayohitajika kuwezesha hatua nyingine za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki itaendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuhakikisha miradi ya kipaumbele iliyopitishwa na wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yenye maslahi mapana kwa Taifa letu inatekelezwa ikiwa ni pamoja na kufuatilia upatikanaji wa rasilimali fedha.

**MWENYEKIT:** Mheshimiwa Mgeni.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu hayo, si ya kuridhisha kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri Bunge

lililopita Abdallah Mabodi alishasema kuwa pesa zimeshatengwa kwa bandari hiyo lakini mpaka sasa hivi bado yaliyofanywa ni madogo tu. Je, ni lini itajengwa bandari hiyo kwa sababu ina umuhimu sana Bandari ya Wete?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Bandari iliyoko Zanzibar ni bandari kuu, ambayo huwa wafanyabiashara wote wanaitegema bandari hiyo na bandari hiyo ni ndogo inabeba meli moja tu kuteremsha mizigo na meli hiyo inapoteremsha mizigo inachukua kati ya wiki tatu mpaka nne na kusababisha meli kuondoka na kuteremsha mizigo Bandari ya Mombasa, nchi jirani na kuikosesha mapato Serikali ya Tanzania. Je, ni lini utafanyika upanuzi wa bandari hiyo ili tuondokane na matatizo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba Serikali ilitazama mahitaji kwa maana yale mahitaji ambayo nimejibu katika jibu la msingi yamefanyika, huu upanuzi ambao nimeutaja hapa lengo ni kuhakikisha kwamba wakati hizi juhudi kubwa zinafanyika za kufanya maboresho makubwa, zile huduma muhimu zinaendelea kufanyika katika bandari hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimtoe hofu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba nilikuwa najaribu kufanya rejea kwenye *commitment* nzima ya upanuzi wa bandari upande wa Zanzibar. Kiasi ambacho kilipitishwa na wakuu wa nchi kama level funding kwa ajili ya bandari za Zanzibar peke yake ni dola milioni 2.131. hii ni kuonesha kuwa wakuu wako *committed* kuonesha kwamba tunafanya maboresho makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati huo sasa utaratibu ule wa kutafuta fedha unaendelea kufanya upanuzi

mkubwa ndiyo maana unaona juhudi zimefanyika na juhudi zinaendelea ili kuhakikisha tunafanya maboresho makubwa. Kwa hiyo, nikutoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba upanuzi utafanyika, hii ni *commitment* ya hali ya juu ambayo inasimamiwa na wakuu wa nchi, tutakwenda kufanya upanuzi wa bandari hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mattar, Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MATTAR ALI SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Bandari ya Zanzibar kiukweli kwa sasa imekuwa ndogo sana na haiwezi kufanya kazi lakini Serikali zetu zimefanya mazungumzo na Benki ya Exim ya China, mpaka leo ni kimya hakuna kinachoendelea mpaka sasa. Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha hii bandari ya Mpigaduri inajenga. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mattar kwa sababu mara nyingi nimemsikia akizungumzia sana juu ya Bandari ya Mpigaduri. Mheshimiwa Matar nikuhakikishie kwamba kweli Serikali imefanya kazi kubwa, kumekuwa na hatua mbalimbali, jitihada nyingi zimefanyika kupanua bandari na wewe unafahamu kwamba juhudi za kupanua bandari zimeanza muda mrefu tangu mwaka 2011 lakini hatua ambayo imefikia sasa hivi baada ya hiyo Benki ya Exim kuchukua hatua za kufanya *funding* kwa ajili ya upanuzi wa bandari hii sasa hivi *draft financial agreement* ilishasainiwa kwa hiyo wanafanya mapitio ya mwisho ili sasa kwenda kwenye hatua ya kwenda kwenye *financing* na kuanza kufanya maboresho Bandari hii ya Mpigaduri au Maruhubi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud swali fupi la nyongeza.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri ni mara kadhaa Serikali imekuwa ikichukua ahadi ikisema kwamba itaweza kujenga Bandari ya Wete, hayo ni masuala ya mdomoni lakini ukija kwenye vitabu halisi, kwenye Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Kimataifa kwenye *Vote* 34 fedha hizo haziko, mmekuwa mkidanganya mara nyingi watu wa Pemba. Mmekuwa mkisema uongo mchana kweupe bila giza. Kwenye *Vote 34* ndiyo Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, fedha hizo huwa haziko, hamtengi lakini mmekuwa mkisema mdomoni tu. Mtuambie hasa mna mkakati gani wa ziada muone kama fedha hizi mara hii mtazipeleka na bandari hii ya Wete mtaenda kujenga. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimualike tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tuonane uone ile *document* ya *retreat* nzima. Ninapozungumza juu ya miradi 17 ambayo kwa Afrika Mashariki ambayo inasimamiwa na wakuu wa nchi, kuna *commitment* ya jumla ya dola 61,000,212, ni fedha nyingi sana na ukiangalia kwa undani utaona miradi ilivyochambuliwa na hatua zinazokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukiiangalia hii *document* na hii *commitment* ambazo tunzisema hapa ni *commitment* ambazo zinachukua muda mrefu na kuna *action plan.* Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, nikuombe tu tuonane ili kwa pamoja tuzungumze ili upate picha, na uweze pia kuisema kazi nzuri Serikali inayofanya kuhusu maendelezo ya bandari hii muhimu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 268

**Kuanzisha Wilaya ya *TANESCO* – Mji wa Mafinga**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha Wilaya ya *TANESCO* katika halmashauri ya Mji wa Mafinga ili kukabiliana na kasi ya ukuaji (kiviwanda na kimakazi) wa Mji wa Mafinga?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mufindi ina halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na Halmashauri ya Mji wa Mafinga. Katika halmashauri ya Mji wa Mafinga tayari ipo ofisi ya wilaya ya *TANESCO* inayotoa huduma kwa wananchi wa Mji wa Mafinga pamoja na wananchi wa Wilaya ya Mufindi. Kwa sasa, Ofisi ya *TANESCO* iliyopo Mafinga inakidhi mahitaji ya kutoa huduma kwa wananchi wote wa Mji wa Mafinga. Hata hivyo, Serikali kupitia *TANESCO* itaendelea kuboresha huduma za ofisi hiyo ili kukidhi ukuaji wa shughuli za biashara za wananchi wa Halmashauri ya Mafinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kusogeza huduma zaidi kwa wananchi, *TANESCO* ilifungua ofisi ndogo *(sub office)* katika maeneo ya Igowole, Kibao na Mgololo. Ofisi hizi ni kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha huduma zinatolewa kwa urahisi kwa wananchi wa maeneo husika. Katika hatua za muda mfupi za kukabiliana na kasi ya ukuaji wa viwanda na makazi katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga, Serikali kupitia *TANESCO* imeongeza njia ya pili ya umeme *(Ifunda Feeder)* ya msongo wa kilovoti 33 kutoka kituo cha kupooza umeme cha Tagamenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine, *TANESCO* ina mpango wa kujenga kituo kikubwa cha kupooza umeme *(Grid substation)* katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga na Kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika mwezi Januari, 2019 na ujenzi wa kituo unatarajiwa kukamilika Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato Chumi maswali ya nyongeza kama unayo.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alipopita pale Mafinga tuli-*raise* hii *concern* ya suala la umeme na Mheshimiwa Waziri akaahidi kutupatia transfoma tano ambazozitakwenda kwenye vijiji vya Itimbo, Isalavanu, Matanana na Ndolezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa vijiji hivyo wanasubiri hizo transfoma kwa hamu sana nimeambiwa wanashughulikia. Sasa maswali yangu mawili ya nyongeza kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi Mji wa Mafinga unakua kwa kasi kiviwanda na kimakazi kiasi kwamba uhitaji wa umeme ni mkubwa na hata *TANESCO* hivi sasa inakusanya mapato makubwa kushinda hata baadhi ya mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ninalouliza, je, Serikali iko tayari kujenga kituo cha kupoozea umeme ili wananchi hawa wa Mafinga ambao wanapoteza asilimia 30 ya muda wao wa kuzalisha mali, wapate umeme wa uhakika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ninaomba kuthubutu kusema kwamba, mtu aliyepewa kazi ya ku-*survey* maeneo ya kupeleka umeme *REA* Awamu ya III, hakufanya kazi yake kwa weledi na kwa ufanisi. Kwa sababu *scope coverage* ya maeneo mengi ya vijiji iko chini ya nusu, kiasi kwamba maeneo kama Zanzibar, Bandabichi, Dubai, Ndolezi, Rumwago, Ihongele na Matanana, ambako *surveyor*

alisema kuna kaya 33, lakini kuna kaya 700, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba ile *scope coverage* katika maeneo yale *REA* Awamu ya III inatekelezwa, inakwenda kuongezeka? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo kwa ufupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ni kwamba, Mkoa wa Iringa kwa kubahatika kupitiwa na huu msongo mkuu, yaani *backbone* ya umeme ya umeme wa *KV* 400, tunatarajia kuimarisha sana ili uweze kutoa *support* katika maeneo mengine, hasa inapotokea kuna changamoto ya umeme. Kwa hiyo, tunategemea kwanza kuboresha kwa kuongeza hiki kituo cha umeme ambacho kitakuwa cha msongo wa 220 mpaka 33 kwa kuweka *transformer* mbili zenye ukubwa wa 60 *MVA*, kwa hiyo, mara mbili ni 120 pale Mafinga, ili uweze pia kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika katika eneo la Kisada, tunategemea pale kwa ajili ya kupitiwa na hii *backbone* tuweke pia vituo, kituo ambacho kitakuwa ni cha msongo wa 400 *KV* kitakachokuwa mpaka 220 na mpaka 33 *KV* na kitakuwa na *transformer* mbili zenye saizi ya *MVA* 200 kila moja. Kwa misingi hiyo tunategemea kwamba eneo hilo litakuwa ni kitovu cha uimarishaji wa umeme katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa upande wa kusambaza umeme, ni kweli katika baadhi ya maeneo ambayo yanazunguka miji, siyo tu kwa Mkoa wa Iringa, yaani Mafinga, lakini pia hata maeneo mengine katika nchi. Tunao mradi wa kuendeleza, kusambaza umeme katika maeneo ya pembezoni mwa miji ambao unafadhiliwa na Benki yetu ya Afrika. Kwa hiyo, tunategemea kwamba kwa Mkoa wetu wa Iringa na maagizo haya ambayo alikuwa ameyatoa Mheshimiwa Rais utafanyiwa kazi na utakuwa mnufaika moja wapo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mendrad Kigola!

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Jimbo la Mufindi Kusini tuka kata 16, tuna vijiji 80, tuna vitongoji 365, lakini hatuna Ofisi Za *TANESCO*, na bahati nzuri tumeanza kujenga Hospitali kubwa sana pale Igohole na Halamshauri ya Mufindi itajengwa pale, Makao Mkuu. Je, Serikali ina mkakati gani sasa kujenga ofisi ya *TANESCO* kubwa kwa ajili ya kuhudumia vijiji nilivyotaja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Umeme *TANESCO* limekuwa likiweka ofisi kulingana na mahitaji na uhalisia wa upatikanaji wa fedha. Kwa sasa taratibu zinazotumika ni kwamba, sehemu ambayo ina wateja zaidi ya 10,000 na laini ya umeme kutoka inapochukuliwa mpaka kufikia huko, umbali wa kilomita 500, mara nyingi imekuwa ikiwekwa ofisi. Lakini vilevile tumekuwa tukiangalia mazingira halisi ya umbali kutoka katika makao makuu ya Serikali kwa maana ya mkoa au wilaya na vilevile pale ambapo inaonekana kwamba mazingira yake ni magumu kiasi kwamba upatikanaji wa huduma ni mgumu zaidi, tumekuwa tukiweka ofisi za *TANESCO* na kwa kuanzia tunaweka hata zile ofisi ndogo za kuhudumia wananchi.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba, eneo hilo litapewa umuhimu baada ya kutathmini hayo ambayo nimeyazungumza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje, swali fupi la nyongeza!

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika Jimbo la Mpwapwa, ni vijiji nane tu ambavyo havijapatiwa huduma ya umeme, na Vijiji hivyo

ni Kiyegea, Kazania, Tumaligo, Mkanana, Ngaramiro, Nana, Mafuto, Kiboriani, Majani na Namba 30.

Je, Mheshimiwa Waziri ni lini vijiji hivi vitapatiwa huduma ya umeme.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi katika mzunguko wa tatu, katika *REA phase III,* mzunguko wa kwanza, ni kwamba tunatarajia kufikia mwezi wa sita, vijiji vilivyokuwa katika mzunguko huo viwe vimekamilika kupewa umeme na vijiji vingine vyote vinavyofuata tunatarajia kwamba vitaingia katika mzunguko wa pili ambao unategemewa kukamilika ndani ya miaka hii kufikia mwaka 2021. Kwa hiyo, vijiji hivyo kama havikuwemo katika mzunguko huo wa kwanza, basi naamini kwamba vitaingia katika huu mzunguko wa pili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea na Wizara ya Madini, Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela Mbunge wa Viti Maalumu, sasa aulize swali lake.

Na. 269

**Kero za Wachimbaji Wadogo wa Madini Nchini**

**MHE. RHODA E. KUNCHELA** aliuliza:-

Sekta ya Madini inaongeza pato kubwa katika uchumi wa nchi.

Je, Serikali iko tayari kutatua kero kwa wachimbaji wadogo na vibarua ambao wananyanyasika katika migodi mbalimbali hapa nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Wizara kupitia Tume ya Madini imeendelea kuweka mikakati ya kuwatambua wachimbaji wadogo kwa kuwapatia leseni za uchimbaji. Aidha, Wizara ya Madini imeendelea kuhamasisha watanzania kote nchini kujiunga latika vikundi kwa mujibu wa sheria ya vyama vya ushirika, ili waweze kupatiwa elimu kiurahisi kuhusu uchimbaji salama, utunzaji wa kumbukumbu na uzalishaji na namna ya kupata mikopo kwa riba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara imedhamilia kuondoa kero za wachimbaji wadogo hasa za maeneo ya kuchimba ili kuwawezesha kujiajiri katika sekta ya madini. Aidha, nimeagiza Tume ya Madini kuhakikisha wamiliki wote wa leseni za utafiti ambazo hazifanyiwi kazi zifutwe ili maeneo hayo yamilikishwe wachimbaji wadogo wenye lengo la kuviendeleza ili kuongeza mchango kwa sekta ya madini katika pato la Taifa na kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migodi yote hapa nchini, inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na marekebisho yake ya Mwaka 2017 na kuzingatia kanuni za uchimbaji salama, mazingira na afya kwa wafanyakazi. Suala la unyanyasaji wa aina yoyote halikubaliki na mmiliki anayefanya hivyo atakuwa anavunja Sheria ya Madini na Sheria za Kazi Mahali pa Kazi. Aidha, natoa wito, kwa yeyote mwenye malalamiko ya msingi kutoa taarifa kupita ofisi za madini zilizoko mikoani mwao ili yaweze kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rhoda Kunchela!

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza, wachimbaji wadogo wadogo katika taifa hili wamekuwa ndiyo wagunduzi wa kwanza wa maeneo ya machimbo, hususan katika mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kutokana na ukiritimba unaoendelea kwa baadhi ya matajiri, *especially* katika Mkoa wa Katavi, wamekuwa wanapora maeneo ya wananchi baada ya kugundua kwamba kuna madini, wanawapora lakini wanakwenda kufanya mazingira ya rushwa kwenye ofisi za madini wanahakikisha wanapata leseni za uchimbaji na huku wakiwaacha wachimbaji hawa wakiendelea kutapatapa na kukosa maeneo ya kuweza kuchimba.

Nini sasa Serikali ifanye ili kuhakikisha inatatua janga hili ambalo linaleta umaskini mkubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mkononi hapa nina malalamiko ya wachimbaji wadogowadogo ambao wameajiriwa sasa kwenye haya machimbo, wamekuwa wanasainishwa mikataba ambayo ni feki, wananyanyaswa na wanapokuwa wanadai mafao yao au wanadai mishahara yao wamekuwa wakifukuzwa na kupigwa, wengine na kufunguliwa mashitaka. Migodi hiyo iko katika Kata za Idindi, Isulamilomo, Magula, Kasakalawe pamoja na *Society* ambako ni katika Kata ya Magama.

Niambie Mheshimiwa Waziri ni lini utakuja sasa kuwasikiliza wachimbaji hao wadogo na kero na unyanyasaji ambao wanafanyiwa katika migodi hii ambayo nimeitaja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo yanyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimhakikishie, katika swali la pili kwamba niko tayari kuja Katavi, kuja kutembelea na kusikiliza kero za wachimbaji wadogo na tumekuwa tukifanya hivyo na nilikwenda Katavi, lakini vilevile niko tayari kwenda tena kama kweli kuna *specific issue* ambayo ninaweza kwenda kusikiliza na kuweza kuitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile, labda nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba kama kuna

matatizo ya waajiriwa, kwa sababu kwenye wachimbaji wadogo kuna waliojiajiri na walioajiriwa, kama kuna matatizo ya walioajiriwa na migodi, tunaomba hizo taarifa mtuletee. Yetote aliyeajiri na ananyanyasa wafanyakazi, sisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inashughulika na masuala ya ajira ambao wanashikilia Sheria ya Kazi, tuko nao kushirikiana nao kuhakikisha kwamba tunatatua kero za wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika swali lake la msingi Mheshimiwa Mbunge ameuliza katika masuala ya ushirika, ni kweli. Kuna vikundi vya ushirika, acha ushirika wa mazao, ushirika wa madini, tumewapa watu leseni mbalimbali kuchimba kwa ushirika, lakini unakuta wale wafanyakazi wanaochimba au wanachama wa vikundi vile, wananyanyaswa na viongozi wa vikundi hivyo. Tunaomba kutoa wito na tunatoa onyo, kwa wale ambao ni viongozi wa vikundi, wanawanyanyasa wenzao, waache mtindo huo mara moja kwa sabahu sasa hivi tunawashughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hatusiti kuwanyang'anya leseni vikundi ambavyo havifanyo mikutano ya mwaka, havitoi taarifa ya mapato na matumizi, tuko tayari kuvifuta na kuwapa watu wengine kuchimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, vilevile, katika alipozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba, wachimbaji wadogo ndiyo wagunduzi wakubwa wa machimbo. Nikubaliane na yeye, kuna baadhi ya maeneo wachimbaji wadogo kweli unakuta ndiyo wamevumbua wachimbaji na wamekuwa wakinyanyasika, sasa hivi mtindo huu tumeukomesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kuna maeneo mengine watafiti wanakuwa wanagundua, wanapofanya kazi zao wa utafiti, wachimbaji wadogo wanavamia maeneo yale, kwa sababu wanaona kwamba kuna hali na dalili ya uchimbaji. Kwa hiyo, kunakuwa ni maeneo ambayo unaweza kukuta wachimbaj wadogo wametangulia au watafiti wametangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Tume ya Madini, tunayaangalia hayo na tunatatua kero mbalimbali zinazotokana na migogoro hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein, Mheshimiwa Esther, Mheshimiwa Silinde.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kwenye migodi yetu kuna watu ambao wamejiajiri kwa ajili ya kugonga kokoto zile zinazodhaniwa zina dhahabu, vibarua hawa wamekuwa wakilazimishwa kununua vitambulisho vya ujasiriamali na jana kumetokea sintofahamu, kuhusu hao vibarua na Mtendaji wa Kata ya Nyugwa na kusababisha wale vibarua kuondoka kwenye maeneo yao ya kazi kwa kulazimishwa kununua vile vitambulisho.

Je, Waziri, uko tayari kumwambia Mtendaji huyo aahirishe hilo zoezi? Kwa sababu hawa wanajiajiri wao kwa kugongagonga kokoto kwa mchanga mchana kutwa shilingi 2000, leo unakwenda kumlazimisha mgongaji kokoto huyu kitambulisho cha elfu 20. Je, Waziri uko tayari kusitisha hilo zoezi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna mgogoro mkubwa ambao pengine ni kutokutambua au kutokuelewa. Tunasema wajasiriamali, tamko la Mheshimiwa Rais amesema, wajasiriamali wote walipe elfu 20, ambao hawazidi shilingi milioni nne kwa mwaka, yaani mapato yao, hilo ni tamko na tayari kutekelezaji umeanza. Sasa katika masuala ya uchimbaji wa madini, kuna kodi za upande wa uchimbaji wa madini, ambazo kweli tunazitoza, mtu anapopata dhahabu kwa mfano, analipa asilimia sita mrabaha analipa asilimia moja kwa ajili ya *clearance*, hizo kodi zinaeleweka, lakini hao ni wachimbaji ambao tunawatambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wachimbaji wadogo, maeneo mengi, ma-*DC* wamekuwa wakienda kule na kuhakikisha kwamba, wale kwa sababu wanatambulika na wenyewe kama wajasiriamali, waliojiajiri. Nimshauri tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba, ukichukua elfu 20, ukaigawanya kwa siku 365 ni shilingi 54 tu kwa siku, haiwezekani mtu anafanya biashara, asilipe chochote kabisa. Kwa sababu ile ile biashara ya mawe inaishia huko tu, tunayem-*charge* kodi kwenye upande wa migodi ni yule ambaye anapata dhahabu, hao wengine tunawapata vipi. Kwa hiyo, wapewe vile vitambulisho, kwanza tuwafahamu, lakini cha pili na wao wachangie kidogo pato la Taifa kwa kulipa shilingi 54 kwa siku, ambayo ni sawasawa na shilingi 20 kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther, Mheshimiwa Shilinde halafu Mheshimiwa Kiruswa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Mji wa Tarime tuna Migodi midogo ya Buguti na Kibaga, tumekuwa tukishuhudia migogoro kwa wachimbaji wadogo kwenye mgodi wa Kibaga na Mgodi ule wa Kibaga leseni yake iko na Barrick kwa muda mrefu na nimeshawahi kuuliza hapa, Serikali ikasema kwamba ina-*revoke* leseni ya Barrick. Na kwa sababu leo Naibu Waziri imekiri kwamba zile leseni zote ambazo hazifanyiwi kazi mtaenda kuzifuta na kuwapa wachimbaji wadogo. Ningetaka kujua *specifically*, kwa wachimbaji wadogowadogo wale wa Kibaga, ni lini sasa ile leseni itaondolewa kwa Barrick ili waweze kupewa wachimbaji wadogowadogo wa Kibaga waweze kufanya kazi zao kwa ufasaha zaidi na bila kubughudhiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tumekwishakutoa tamko, kwa leseni zote

ambazo hazifanyiwi kazi, na hasa ambazo ziko kwenye utafiti na hazifanyiwi kazi, zirejeshwe, zirudishwe na sisi tuweze kutafuta namna ya kuwagawia wachimbaji wadogo na tunawagawia katika vikundi. Mheshimiwa Mbunge ameniuliza swali hilo lakini hakunipa *specific* namba ipi, naomba tu nilichukue suala hili, tuone ni leseni ipi, aidha ni ya uchimbaji, au ni leseni ya utafiti. Kama leseni ni ya utafiti na haifanyiwi kazi, sisi tutazirudisha, lakini nimhakikishie tu kwamba kuna leseni nne ambazo zilisharudishwa na watu wa Barrick maeneo hayo na wameshaturudishia sisi na walishaandika barua, tutaangalia namna ya kuangalia kuwagawia wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde swali fupi la nyongeza baadaye Mheshimiwa Kiruswa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, moja ya kero kubwa ya wachimbaji wadogo ilikuwa ni ile sheria ambayo tulipitisha hapa Bungeni, ya kodi ya zuio ya asilimia tano kwa bei ya kuuzia madini kwa wachimbaji wadogo, lakini Bunge lako tukufu mwaka huu mwezi wa pili tulibadilisha hiyo sheria na kuondoa hilo zuio.

Sasa nataka kujua utekelezaji baada ya kuondoa hiyo sheria umefikia wapi kwa sababu ile sheria ilikuwa inapelekea madini mengi kutoroshwa nje ya nchi?Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dotto Biteko, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Silinde la nyongeza. Ni kweli kama alivyosema tumekuwa tukipata malalamiko ya baadhi ya watu, hasa maeneo ya Arusha na mikoa mingine kwamba, pamoja na kwamba *withholding tax* na *VAT* zimefutwa kwa mujibu wa sheria, wako watu wanaendelea kuzitoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomab kutoa wito na kutoa maelekezo rasmi kwa watu wote wanaohusika kwenye utozaji wa kodi na tozo mbalimbali kwenye sekta ya madini. Kodi ambazo zimefutwa na Bunge hili hakuna mtu mwingine yeyote wa aina yoyote anaruhusiwa kutoza hizo kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninasema hili na iwe marufuku kwa mtu yeyote na tutakapopata taarifa tena, kwa mtu ambaye anaendelea kutoza hizo kodi, hatua kali zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri tunamalizia swali hilo na Mheshimiwa Kiluswa.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona, ili niulize swali la nyongeza kuhusu madini. Sisi katika Wilaya ya Longido tuna madini ya aina ya Ruby, na kuna mgodi wa miaka mingi, unaoitwa *Mundarara Ruby Mine* na sasa hivi wachimbaji wadogowadogo wameibuka wametokeza baada ya kujua madini haya yana thamani na ninaamini Serikali itakuja kuwajengea uwezo.

Lakini swali langu ni kwamba, huu mgodi ambao ulianzishwa tangu kabla ya uhuru, ni wa nani, na kama ni wa Serikali, Serikali inafaidikaje na huu mgodi na ni asilimia ngapi kama kuna *ownership* ya *joint venture* na mwekezaji?

**MBUNGE FULANI:** Agashanza, gashanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, pale Mundarara, kuna mgodi ambao ni mgodi wa uchimbaji wa Ruby. Mgodi ule kabla, miaka ya 60, ni kwamba mgodi ule ulikuwa ni mali ya Serikali, na sisi tumeweza kufuatilia na tuliunda Tume ili kuona ni namna gani mgodi ule uliweza kuporwa. Nipende tu kusema kwamba tumelifuatilia na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mgodi ule unamilikiwa sehemu na Serikali na kuna kampuni nyingine ambayo ilikuwa inamiliki, lakini mgodi ule mpaka

sasa hivi, asilimia 50 tunaumiliki sisi yaani Wizara ya Madini kupitia Shirika la Madini yaani la *STAMICO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, mgodi huu ulikuwa na mikiki mingi, ambako Tume tumeituma, tumetuma Tume ya watu maalumu, wafuatilie, watushauri tuone namna gani ya mgodi ule kuurudisha Serikalini au kutafuta namna ya kuweza kuungana na mchimbaji mwingine au mwekezaji mwingine na Serikali iweze kupata mapato yake kupitia shirika la madini la *STAMICO*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Madini tunamalizia Wizara ya mwisho, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi Mbunge wa Ukerewe aulize swali lake.

Na.270

**Kuifanya Ukerewe Kuwa Eneo la Utalii**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Visiwa vya Ukerewe bado havitumiki ipasavyo kama eneo mahsusi kiutalii ingawa vimo vivutio vingi vya utalii ikiwemo jiwe linalocheza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kushirikiana na vikundi kama vile vya mila na desturi Ukerewe *(KUMIDEU)* katika kukitangaza Kisiwa cha Ukerewe kama eneo la utalii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi Mbunge wa Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatambua kuwa Ukerewe ni miongoni mwa Visiwa vichache nchini vyenye rasilimali mbalimbali ikiwemo fukwe nzuri, utalii wa utamaduni pamoja na jiwe linalocheza. Vivutio hivi kwa miaka ya hivi karibuni vimekuwa vikivutia wageni wengi kutembelea maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wizara inaendelea na zoezi la kuainisha vivutio vya utalii kwa dhumuni la kuviendeleza pamoja na kuvitangaza. Katika mwaka wa Fedha wa 2019/2020 tunatarajia kutekeleza zoezi hilo hilo katika Mikoa mbalimbali ikiwemo Mwanza. Kazi hiyo hutekelezwa kwa kushirikiana na Uongozi wa Mkoa, Wilaya, Vijiji na wadau wa Sekta ya Utalii katika maeneo hayo, hivyo nimjulishe Mheshimiwa Mbunge, zoezi hilo litakapoanza kutekelezwa katika Mkoa wa Mwanza, Wataalam wangu watapita katika Kisiwa cha Ukerewe ikiwa ni pamoja na kufanya kazi hiyo kwa kushirikiana na kikundi cha Mila na Desturi cha Ukerewe cha (KUMIDEU)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hilo ni juhudi za makusudi za Wizara yangu za kupanua wigo wa mazao ya utalii kwa kubainisha vivutio vya utalii wa asili sehemu mbalimbali nchini. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa kusimamia na kuendeleza Sekta ya Utalii Kanda ya Ziwa, Wizara ilifungua Ofisi ya Kanda iliyohusisha Idara ya Utalii na Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB)* katika Jiji la Mwanza. Lengo likiwa ni kusogeza kwa karibu huduma kwa wadau wa Sekta ya Utalii walio katika Kanda ya Ziwa na maeneo jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada zake za kuhakikisha Sekta ya Utalii inazidi kuendelea na kukua hususani katika Kisiwa cha Ukerewe na Mkoa wa Mwanza kwa ujumla. Ifahamike kwamba Sekta ya Utalii ni Mtambuka na hivyo kazi ya uendelezaji sekta hii inahitaji juhudi za pamoja za wadau wa Sekta hii, Umma na Binasfsi. Hivyo, Wizara yangu itaendelea kushirikiana kwa karibu na wadau wa Sekta ya Utalii kuendeleza utalii nchini ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkundi swali la nyongeza, Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya kuuliza maswali ya nyoneza. Kwanza nipongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nitakuwa na maswali mawili, la kwanza kwa mujibu wa maelezo ya waziri, Wizara inafungua Ofisi za Kanda Mwanza pale zikijumuisha Idara ya Utalii pamoja na kodi ya utalii, lakini kuna taarifa kwamba *TANAPA* imegawa shughuli zake Kikanda, na moja ya Kanda hizo ni Kanda ya Kaskazini Magharibi na kwa mujibu wa taarifa tulizonazo ni kwamba uongozi wa bodi umeelekeza Ofisi za Kanda ziwe Bunda eneo ambalo ni jarani sana na Serengeti. Lakini ili kusaidia ukuzaji wa utalii kwenye maeneo ya Ukerewe, Saanane, Lubondo nakadhalika. Ni kwa nini Ofisi za *TANAPA* za Kanda hizi, Kanda ya Kaskazini Magharibi isiwe Mwanza ziliko Ofisi za Utalii pamoja na Bodi ya Utalii badala yake zipelekwe Bunda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kama Mheshimiwa Waziri alivyosema Wizara tayari imetambua uwepo wa vivutio vya utalii na sasa inahitaji kuviendeleza na kuvitangaza. Sasa ili kufanikisha hili ni kwa nini wizara sasa isiwekeze pesa pale Ukerewe kwa ajili ya maandalizi ya miundombinu lakini pamoja na ku-*train* wadau mbalimbali wakiwemo hizi *local groups* ambazo zimekuwa zikibainisha vivutio hivi ili kama maandalizi sasa ya kukuza na kutangaza utalii ulioko kwenye Visiwa vya Ukerewe? Nashukuru sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu halafu Mheshimiwa Mbatia ataulizia.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru kwa pongezi zake, kwa wizara ambazo amezitoa na kulidhika na majibu yake ya maswali ya msingi. Lakini Mheshimiwa Mkundi ameomba kufahamu kwamba *TANAPA* katika juhudi za kuboresha shughuli za kukuza na kusimamia uhifadhi na utalii

wamefungua Ofisi Kaskazini Magharibi, lakini Ofisi hiyo wameipeleka Bunda badala ya Mwanza na ameshauri kwa nini Ofisi hiyo isikae Mwanza ambapo kuna Ofisi za *TTB* na Ofisi za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge nitawasiliana na *TANAPA* na kuona sababu za msingi zilizowapeleka Bunda, lakini ninaamini kwamba ushauri wake ni wa msingi kwa sababu Mwanza bado ni kitovu cha Kanda ya Ziwa ambapo ingelikuwa rahisi zaidi kuwahudumia wateja kuliko Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wake wa pili swali langu la msingi limejibu kwamba baada ya kuziimarisha vituo hivi vyote vya mali kale tunajielekeza sasa kwenye kushirikiana na taasisi zetu mbalimbali ambazo tutazikabidhi kwenye maeneo mengi ili ziweze kuviambatanisha vituo hivi pamoja vivutio mbalimbali vya utalii kama nilivyosema Saanane na Lubondo. Kwa hiyo, nimuhakikkishie Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya vituo ambavyo tutahakikisha kwamba vinapata pesa kwa ajili ya uendelezaji na kwa ajili ya kuviimarisha itakuwa ni Ukerewe ili kuhakikisha kwamba Kisiwa cha Kirewe kinatumika kama Kisiwa cha utalii katika Ziwa Victoria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, mwaka 2014 Tanzania ilikuwa inashika nafasi ya pili kwa vivutio vya utalii kati ya nchi 133 vyenye kushindana kwenye ubora wa vivutio vya utalii duniani ambapo *GDP* yetu wakati huo ilikuwa ni asilimia 17 na miundombinu ya utalii ya vivutio ya kutoa ubora wa utalii ilikuwa tunashika nafasi ya 110 kati ya nchi 133.

Je, kwa mwaka huu Tanzania inashika nafasi ya ngapi kwenye ubora vivutio vya utalii duniani na tunashika nafasi ya ngapi kwenye miundombinu bora ya kuchochea vivutio bora vya utalii duniani? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASII NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba miaka hiyo 1984 anayosema Tanzania ilikuwa ni nchi ya pili kwa vivutio na bado ni nchi inayoongoza kwa vivutio vya utalii duniani na hivi karibuni nafikiri uliona mchakato wa kuingiza moja ya vivutio muhimu kabisa ambavyo vilikuwa vinatangazwa kwenye vivutio vya dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake kimsingi ili niweze kulijibu vizuri na kufahamu takwimu zote ambazo amezisema ni kwamba lilipaswa kuwa swali la msingi lakini nimuhakikishie Tanzania bado ni nchi yenye vivutio bora na ni nchi ambayo katika Afrika ni nchi ambayo ina vivutio bora zaidi na katika dunia ni nchi ambayo ni huwa nadhani ni nchi ya pili baada ya Brazil.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri Maliasili anataka kuongezea.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, utafiti uliofanyika kati ya mwaka 2012 mpaka 2014 ulitoa taarifa kwamba Tanzania inashika nafasi ya pili kwa vivutio vya *nature* duniani. Kutokea kipindi hicho mpaka sasa haujafanyika utafiti mwingine wa kuweza kutupa *position* yoyote ile tofauti na ile ya awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini matokeo ya katikati ya utafiti huu ambao unafanyika kila baada ya miaka mitano yalitoka Tanzania ilionekana imeshuka kutoka nafasi ya pili mpaka nafasi ya nane kwa vivutio vya *nature* duniani. Na sababu kubwa iliyosababisha Tanzania kushuka ilikuwa ni uharibifu wa mazingira pia ikiwemo uvamizi wa mifugo na makazi katika maeneo ya vivutio vya utalii vya *nature.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kazi kubwa imefanyika katika Awamu ya Tano ya kuwaondoa wananchi

ambao wamevamia maeneo hayo, pia kupandisha hadhi baadhi ya maeneo, ninauhakika watakapofikia *conclusion* ya utafiti huo baada ya miaka mitano ambao ni mwaka huu pengine matokeo ya nafasi ambayo Tanzania inashika katika vivutio vya *nature* inaweza ikawa imeongezeka zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi wa ziada, Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umepita na sasa ni wakati wa matangazo, tutaanza na matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Tutaanza na wegeni waliopo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, wageni wa Mheshimiwa Spika ni Maaskofu na Wachungaji kutoka nchi mbalimbali ambao ni Askofu Oscar Ongere kiongozi wa ugeni anatoka Mkoa wa Mbeya karibu sana, Askofu Rey John kutoka Canada, karibu sana, Askofu John Omondi kutoka Kenya karibu sana Askofu John Omondi, Askofu Patrick Mtware kutoka Rwanda karibu sana Askofu Patrick, Askofu Christopher Mwamulima kutoka Malawi karibu sana Askofu Mwamulima, ndugu Vincent Brown kutoka Mbeya karibu sana ndugu yetu, ndugu John Mkumbo kutoka Dodoma karibu sana ndugu John na Mchungaji Elikana Gonda kutoka Dodoma karibu sana Mchungaji.*(Makofi)*

Kuna wageni wengine 82 wa Mheshimiwa Luhaga Mpina Mbunge ambaye ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambao ni Profesa Elisante Ole Gabriel Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo, karibu sana Katibu Mkuu wetu, Dkt. Rashidi Tamatamah Katibu Mkuu Uvuvi karibu sana Katibu Mkuu wetu wa Wizara ya Uvuvi, Dkt. Charles Nyamrunda Katibu Mkuu Mstaafu Mifugo na Uvuvi karibu sana Katibu Mkuu Mstaafu, Dkt. Yohana Budeba Katibu Mkuu Mstaafu Uvuvi pia karibuni sana wastaafu wetu, Dkt. Mery Mashingo Katibu Mkuu Mstaafu Mifugo karibu sana Katibu wetu Mkuu Mstaafu, ndugu Paul Kimiti Mwenyekiti Bodi ya *NARCO* karibuni sana, ndugu Lucas Malunde Mwenyekiti wa Bodi ya Maziwa karibu sana Mwenyekiti wetu wa Bodi ya Maziwa, Profesa Sebastian Chenyambuga, Mwenyekiti wa Bodi ya wa TALIRI karibu sana, Profesa Ludovick Kazwala Mwenyekiti wa Baraza la Veterinary Tanzania karibu sana katika Bunge letu, Dkt. Bedan Masuruli

Msajili Baraza la Veterinary, Profesa Peter Msoffe Mwenyekiti wa Bodi ya *TVLA* karibu sana Mwenyekiti wetu wa Bodi ya *TVLA*, ngugu Fred Kafeero Mwakilishi wa *FAO* Tanzania. Pia hawa wameambatana na Wakurugenzi Wakuu wa Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo na wadau wa Sekta ya Uvuvi. *(Makofi)*

Wapo wazazi wa Mheshimiwa Mpina ambao ni ndugu Gabis Luchemba Mpina baba mzazi karibu sana baba yetu mzazi, pia ndugu Kabula Masaga mama mzazi karibuni sana baba na mama mzazi wa Mheshimiwa wetu Mpina. *(Makofi)*

Pia kuna wageni wengine 55 wa Mheshimiwa Mpina ambao ni viongozi wa CCM Wilaya ya Meatu ambao wameongozwa na ndugu Charles Mazuri Karibu wa CCM Wilaya ya Meatu karibuni sana wageni wetu 55 wa Mheshimiwa Waziri Mpina. Pia kuna Waheshimiwa Madiwani na wapiga kura wake kutoka Jimbo la Kisesa Wilaya ya Meatu nao pia wamo Mkoani Simiyu, lakini wakiongozwa na Mwenyekiti wa halmashauri ya Wilaya hiyo Mheshimiwa Juma Isack Mpina karibuni sana wageni wa Mheshimiwa wetu Waziri.*(Makofi)*

Wageni wengine ni Waheshimiwa Wabunge kuna wageni wanane wa Mheshimiwa Januari Makamba Mbunge, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ambao ni wanafunzi watano na Walimu watatu kutoka shule ya msingi *Baybridge* ya Jijini Dar es Salama wakiongozwa na ndugu Jigna Chandarana, karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo Mbunge Naibu Waziri wa Madini ambaye ni Katibu Mwenezi wa *CCM* Mkoa wa Shinyanga anatokea Maswa ndugu Daniel Bubinza karibu sana ndugu yetu Bubinza kutoka Mkoa wa Shinyanga Wilaya ya Maswa. Mgeni wa Mheshimiwa Victor Mwambalaswa Mbunge ambaye ni mtoto wake kutoka Jiji la Dar es Salam ndugu Isabella Mwambalaswa karibu sana mtoto wetu; wageni sita wa Mheshimiwa Hussein Amar Mbunge ambao ni viongozi wa *CCM* kutoka Mkoa wa Geita

wakiongozwa na Katibu wa *CCM* wa Mkoa ndugu Clemence Mkondya karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Hasna Mwilima Mbunge ambao ni viongozi wa *CCM* kutoka Jimboni kwake Uvinza Mkoa wa Kigoma karibuni sana wageni wetu kutoka Uvinza Mkoa wa Kigoma, wageni 60 wa Mheshimiwa Agnes Marwa Mbunge ambao ni Wenyeviti na Makatibu ya *UWT* kutoka Wilaya ya Tarime Mkoa Mara karibuni sana viongozi wetu wa *UWT* Wenyeviti na Makatibu wote kutoka Wilaya ya Tarime Mkoani Mara karibuni sana sana katika Bunge letu, wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda Mbunge ambao ni wafugaji kutoka Malinyi Mkoa wa Morogoro karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, Mgeni wa Mheshimiwa Venance Mwamoto Mbunge ambaye ni Mwalimu wa lugha ya Kichina kutoka Sengelema Mkoani Mwanza ndugu Irene Mushi karibu sana mwalimu wetu wa lugha ya Kichina kutoka huko. *(Makofi)*

Wageni wengine 63 wa Mheshimiwa Anna Lupembe Mbunge ambao ni Watumishi wa Mungu na timu ya wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, naona hawajaingia hao, wageni 17 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni kwaya ya *AIC* ya Kanisa la Ebenezer kutoka Ndachi Jijini Dodoma karibuni sana wanakwaya wetu wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, mgeni wa Mheshimiwa Julius Kalanga Mbunge ambaye ni Katibu wa *CCM* Wilaya ya Monduli ndugu Langolel Akyoo karibu sana Mheshimiwa, wageni 43 wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni wageni Wanakwaya ya Uvuke Kanisa la Anglikana kutoka Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wao ndugu Nicholaus Ndaru karibuni. *(Makofi)*

Wageni wengine waliokuja Bungeni kwa ajili ya wafunzo ni wanafunzi 111 na Walimu watatu kutoka shule ya sekondari ya John Merlini ya Jijini Dodoma, naona hawajaingia hao.

Baada ya matangazo hayo ya wageni kuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge ambaye ameomba

niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Kampuni ya Maziwa ya *ASASI* ya Mjini Iringa imetengeneza maziwa *a long life milk* na imeleta hapa Bungeni kwa ajili ya kuwagaiya Wabunge ili muweze kutambua bidhaa hiyo mpya. Waheshimiwa Wabunge wote leo saa saba mchana mtapatiwa chupa moja ya *milk shake* na *box* la *long life milk*, Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kuchukua maziwa hayo sehemu ya maonyesho nyuma ya Ukumbi wa Msekwa, Waheshimiwa maziwa hayo ni kwa ajili ya futali hata wale waliokuwa hawajafunga. *(Makofi)*

Kuna tangazo jingine, Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuna ratiba ya mashindano ya michezo kama ifuatavyo tarehe 01 Juni, 2019 Jumamosi Bunge *Sport Club verses* JKT Makutupora michezo itakayochezwa ni soka, pete na *volleyball* wanaume na wanawake, na kuvuta kamba wanaume na wanawake, tarehe 09 Juni Jumapili mechi ya Wabunge wapenzi na wanachama wa Simba dhidi ya wale wa Yanga michezo itakayochezwa ni soka na pete, tarehe 10 Juni Jumatatu hiyo Bunge *sport club verses* Mwanza Veterani michezo itakayochezwa ni soka na pete, tarehe 15 Juni, 2019 Jumamosi Bunge *sport club verses CRDB combine* michezo itakayochezwa ni soka, pete, *volleyball* wanaume na wanawake, kuvuta kamba wanaume na wanawake. *(Makofi)*

Tarehe 22 Juni 2019 Jumamosi Bunge *sport club verses NMB combine* michezo itakayochezwa ni soka, pete, *volleyball* wanaume na wanawake na kuvuta kamba wanaume na wanawake, asubuhi ya tarehe hii kutakuwa na mbio za taratibu *jogging* kwa wanamichezo wote zitakazoanzia Bunge mpaka uwanja wa Jamhuri. Michezo yote itafanyika uwanja wa Jamhuri Dodoma na udhamini wa mechi hizi uko wazi hivyo tunakaribisha udhamini kutoka kwa makampuni mbalimbali na watu binafsi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tusikilizane kwanza kuna jambo la Mheshimiwa Zitto Kabwe naomba nimkaribishe ili aweze kuwasilisha dakika tano.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa ruhusa kwa mujibu wa kanuni ya 47(1) kueleza jambo ambalo nitaomba maelezo ya Serikali au kauli ya Serikali kuweza kuona ni namna gani ambavyo tunalitatua na tunalikomesha. Katika Jimbo langu la uchaguzi Jimbo la Kigoma Mjini kumezuka kwa takribani miaka mitatu sasa tabia ya vijana kujipaka *oil* chafu na kuvamia wanawake hasa wajane na wanawake ambao hawana wenza wao wanaoishi nao na kuwabaka na wakati mwingine hata kuwaumiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usiku wa kuamkia jana mwana mama mmoja ambaye kwa stara siwezi kumtaja jina lake na yuko hospitalini sasa hivi amejeruhiwa kwa kupigwa nondo ya kichwa na mmoja wa hao vijana na mwingine amepigwa kisu na wapo hospitalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Shirika lisilo la Kiserikali la TAMASHA limefanya kazi ya kufanya *documentation* ya haya matukio toka mwaka 2016 na wame-*document* matukio 43 na waliniandikia barua kama Mbunge wa Jimbo, walimwandikia barua Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na taasisi mbalimbali zisizo za Kiserikali wakiwemo TWAWEZA, *Legal and Human center*, *Human Right Defenders* wameomba vikao na Wizara ya Mambo ya Ndani kwa ajili ya namna gani ya kushughulika na hili jambo lakini mpaka sasa hatujaona *seriousness* yoyote ya Serikali katika kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimelileta hapa Bungeni kwa sababu hiki ndio chombo cha wananchi na tukio kama hili ni tukio la aibu kwa kweli na kama Mbunge wa Kigoma Mjini inanisononesha, inanisikitisha na naona aibu sana kwamba tunaweza tukashindwa kulinda wakina mama zetu, dada zetu, shangazi zetu, watoto wetu kuweza

kufanyiwa vitendo vya kinyama ambavyo wanafanyiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Kiti nisingependa niombe mjadala kwa sababu ni jambo ambalo ndio kwanza nimelileta na watu hawatakuwa na *details* za kuweza kujadili. Lakini naomba kiti kielekeze Serikali ilete ndani ya Bunge taarifa ni hatua gani ambazo wamezichukua mpaka sasa za kukabiliana na hali hii, kukomesha vitendo hivi, na kuchukua hatua kali za kisheria kwa watu wote ambao wanadhalilisha, kuumiza na kunyanyasa wanawake hasa Kata ya Mwanga Kusini na Kata ya Katubuka katika Manispaa ya Kigoma Ujii, naomba maelekezo yako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge sina haja ya kurejea maelezo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Zitto naamini wote mmeyaelewa na Serikali wamesikia kwa upeo unaostahiki. Sasa nitoe agizo tu kwa vile Serikali tayari wanaambiwa walishapelekewa hiyo taarifa lakini kwa hilo la jana ambalo limetokea inawezekana siwezi jua kama wamelipokea ama hawakupokea. Lakini ninaomba niwaelekeze sasa Serikali kama wataweza kutoa tamko sasa hivi ama kama wataweza kuleta baadaye majibu hiyo ni juu yao siwezi kuwalazimisha kwa sababu hili jambo limetokea jana usiku. Kwa hiyo, naomba nimsikilize Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani azungumzie kuhusu suala hilo.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kusema maneno yafuatayo, kwamba ubakaji ni kosa la jinai na ni kosa ambalo linaadhibiwa kisheria kwa mujibu wa sheria ya kanuni ya adhabu, na kwamba vitendo hivi vya makosa ya aina hii vimekuwa vikitokea katika nchi yetu na si Kigoma tu katika maeneo mbalimbali ambapo makosa haya huwa yanadhibitiwa na Jeshi la Polisi na watuhumiwa wanapo unapopatikana ushashidi wanafikishwa mahakamani na kuadhibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nipende pia kusema bayana kwamba kwa Mkoa wa Kigoma matukio ambayo

Mheshimiwa Zitto Kabwe Mbunge wa Kigoma Mjini ameyazungumzia ni matukio ambayo ni kweli yanadhalilisha wakina mama, ni vitendo ambavyo sisi kama Serikali hatuwezi kuvipa nafasi na kuvivumilia na niseme bayana kwamba ailianzia mwaka 2014 ambapo wakinamama wa Kigoma ambao ni wajane au ambao hawana wanaume au waume zao wamesafiri walikuwa wanajikuta mtu ambaye haonekani kwa macho na mwanamama anajikuta sehemu zake za siri zimelowa halafu anaponyanyuka anaona kama mtu anapotaka kumshika yule mtu anateleza, kwa hiyo ndipo dhana ya udhalilishaji kwa mtindo wa teleza ulipoanzia. Na ikaonekana walikuwa wanaingilia kwenye pembe ya nyumba au kwenye kona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vitendo hivi vimeendelea kudhibitiwa na nilipopata barua hii na kushirikiana na Mheshimiwa Zitto Kabwe pamoja na Mkurugenzi wa Taasisi inayoitwa TWAWEZA Ndugu Aidan Eyakuze niliweza kutoa maelekezo kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kigoma. Lakini jambo hili si la ukubwa huo kama inavyoelezwa na hizi taasisis hizi zisizo za Kiserikali ambazo zinafanya huu utafiti ambao Mheshimiwa Zitto Kabwe anazisema na tukiangalia sisi kwenye kumbukumbu zetu za taarifa ya matukio kwenye vitabu vya Polisi pale Mkoani Kigoma mpaka jana katika mwaka huu hakuna taarifa yoyote ambayo inahusisha tukio la ubakaji kwa wamanamke yoyote isipokuwa matukio ambayo yamepungua…

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa, naomba ukae Mheshimiwa Kange Lugola.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto naomba usubiri amalize.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *No!* taarifa.

**MWENYEKITI:** Nitakupa ruhusu naomba amalize halafu nitakupa ruhusa. Haya Mheshimiwa Lugola naomba umalizie.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi sina sababu ya kutosema ukweli Mheshimiwa Zitto Kabwe awe na subira. Niseme tena kwamba mpaka kufikia leo hii katika kipindi cha mwaka mmoja ambacho huwa sisi Jeshi la Polisi tunatoa taarifa za uhalifu hakuna tukio lolote narudia kwenye vitabu vyetu vya Polisi pale Kigoma.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa naomba uniruhusu nitoe taarifa.

**MWENYEKITI:** Naomba amalizie nitakupa muda utazungumza hilo unalotaka kusema naomba Mheshimiwa Lugola malizia.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye vitabu vya Polisi ambalo linahusisha mwanamke kubakwa isipokuwa matukio ambayo yameripotiwa kwenye kituo cha Polisi yako matukio matatu ambayo yamehusisha wakinamama kujeruhiwa kwenye nyumba zao. Kwa hiyo, *report* zilizopo ni za kina mama wapatao watatu ambao wamejeruhiwa sasa inawezekana katika kujeruhiwa hawa ambao wanatuhumiwa hawakufika kwenye kiwango cha kutenda kosa la ubakaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tamko kama Serikali kwenye maeneo mbalimbali katika nchi yetu kuna baadhi ya taasisi au mtu mmoja mmoja wanapenda kukuza mambo na wanapoyakuza mambo haya yanajenga hofu miongoni mwa wananchi na kuonekana matukio haya yana kiwango kikubwa sana na hivyo kuzua taharuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme bayana taasisi ambazo zinakwenda kufanya utafiti mahala wanakuza mambo haya, taasisi hizo tumaanza kuziorodhesha na hivi punde tutachukua hatua na kama Mheshimiwa Zitto Kabwe ana taarifa za mwanamke yeyote ambaye ametoa taarifa kwenye kituo cha Polisi kesi yake ya ubakaji ikaorodheshwa Mheshimiwa Zitto Kabwe niko tayari sasa hivi kuondoka hapa kwenda Mkoa wa Kigoma, nakwenda kuchukua kesi zote

ambazo zimeorodheshwa kwamba wakinamama wamebakwa ili tuweze kuchukua hatua na hiki ninachokisema, huo ndio ukweli. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kidogo Mheshimiwa Selasini, *it very unfortunate* Waziri mwenye dhamana ya Usalama wa wananchi wetu wakiwemo wanawake kuzungumza kwa namna ambavyo amezungumza sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni mwaka 2016 kina mama hawa wali-*report* Polisi na tulikuwa na Mkuu wa Polisi anaitwa Mtui aliweza kudhibiti RPC wa pale Kigoma baadaye akahamishwa maa-*RPC* walifuata kina mama wakienda kuripoti polisi, polisi wanadhihaki wanawaita hawa ni wanawake wa teleza ni mwanamke gani anayejiheshimu ataenda kituo cha Polisi kutoa taarifa na kukejeliwa halafu arudi tena na hili jambo naomba nimalize tafadhali sana naomba unipe dakika mbnili nimalize. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Malizia basi haraka.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hoja gani tena hii maana yake ni...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri naomba uvumilie kidogo nitatoa...

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mbunge wa Jimbo hili, kama Mbunge wa Jimbo la Kigoma Mjini, ninawaomba wanawake ndani ya Bunge hili wafumbe macho wa-*imagine* kuingiliwa kwa namna ambavyo wanawake wa Kata ya Mwanga Kaskazini na Kata ya Katubuka wanaingiliwa na wanawake ambao wanatoa taarifa mfano mwanamke ambaye amepigwa yupo Mawenzi Hospitali leo...

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa niko tayari kwenda Kigoma hata leo sasa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto naomba ukae umeeleweka na Mheshimiwa Waziri naomba ukae wote wawili naomba mkae. Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Waziri kwa upande wake amejibu alivyoelewa yeye, Mheshimiwa Zitto kwa uzito wake ameeleza anachokielewa yeye.

Waheshimiwa Wabunge, ninachosema kama kiti, Mheshimiwa Waziri kama taarifa hizo huna hili jambo hata likiwadogo lapata hivi litaleta athari kubwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Subirini, suala la ubakaji awe mwanamke awe mtoto sio la kuvumiliwa tulieni kabisa sina eehee! Subirini. Mheshimiwa Kange uko sawa kama huelewi nakuomba nakuagiza uende Kigoma ukashughulikie ukubwa wa suala hilo. Mheshimiwa Zitto ukiwa kama Mwakilishi wa huo Mji unaotaja wenye mambo hayo kama wanawake hao wanaona haya chukua wewe orodha peleka. *(Makofi)*

Baada ya hayo naomba tuendelee Katibu.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Muda wetu umekwisha kwa kweli. Mheshimiwa *Chief Whip* naomba wewe peke yako nipokee muongozo wako. Waheshimiwa muda umeenda nampa ruhusu *Chief Whip* tu atoe mwongozo.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na kwa kweli usingenipa nafasi hii naona moyo ungepasuka. Kabla sijatoa mwongozo wangu nikushukuru sana kwa mwongozo uliotoa hili ambalo lilikuwa

linazungumza hapa. Mtanzania mmoja akipata tatizo lazima lishughulikiwe kama lingekuwa la Watanzania 1,000. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip* nimekupa ruhusa uombe mwongozo wako.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, jana Waziri wa Mambo ya Ndani alitoa mwongozo hapa Bungeni kwa swali ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Rehema Migilla kuhusu vijana wetu wa bodaboda wanavyokamatwa na kunyanyasika sehemu mbalimbali za nchi yetu na ilipofika saa tisa mchana jana katika Jimbo langu la Rombo eneo la Mashati kijana mmoja alipigwa sana, akaumizwa sana, akanyang'anywa fedha zake na imekuwa ni destruri katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu na ya Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuomba kwa sababu Serikali inafanya kazi zake kwa kuandika utoe mwongozo kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ili yale mambo mazuri aliyoyasema jana ayatoe kwa maandishi kwa ajili ya utekelezaji nchi nzima, vijana wetu waachwe kupigwa *na Mheshimiwa Ester Mmasi ambaye anawakilisha vijana hapa awe na adabu. (Makofi)***[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip* Mheshimiwa Selasini hilo jambo alishalitolea mwongozo Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani jana, kwa hiyo hata kama linaendelea kutokea kauli ya Serikali tayari ilishatolewa na ndio kauli ya mwisho inayotakiwa itekelezwe.

Kwa hiyo naamini na hilo litaendelea kutekelezwa kwa mujibu wa kauli ambayo ameitoa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani jana. Tuendelee Katibu.

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu Utaratibu, Mwenyekiti unakimbia eeh!

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza na hoja za Serikali namkaribisha Mheshimiwa Waziri aweze kuja kuwasilisha hoja yake katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa matumizi ya Wizara hiyo mwaka 2019/2020, karibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliombe Bunge lako lifuatilie kwa karibu hotuba hii ili waweze kuona mageuzi makubwa ya Mifguo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kuanza, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo, Maji ilichambua bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Fungu la 99 Mifugo na Fungu la 64 Uvuvi, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, niliombe pia Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi wa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo ili kuwasilisha hotuba yangu. Aidha, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa namshukuru sana Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kushika wadhifa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuiongoza nchi yetu kwa uhodari na umahili mkubwa katika kipindi hiki tangu tuingie madarakani ambapo ni miaka minne tu. Lakini tumeshuhudia mageuzi

makubwa ya uchumi na maendeleo na amekuwa Kiongozi wa mfano wa kuigwa Afrika na dunia. Utendaji wake umewaridhisha wananchi, Viongozi na hata taasisi kubwa zinazoaminika Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji wake umewaridhisha wananchi viongozi na hata taasisi kubwa zinazoaminika kimataifa. Mheshimiwa Rais pamoja na kuwepo kwakauli za kukatishwa tamaa zinazotolewa na baadhi ya watu, endeleza mapambano ya kusaka maendeleo ya Watanzania na sisi wasaidizi wako tupo imara na tutaendelea kufanya kazi usiku na mchana ili matarajio ya Watanzania katika Serikali ya Awamu ya Tano yatimie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongoza vyema nchi yetu na kwa hekima na busara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb) Waziri wa Fedha na mipango kwa hotuba zao ambazo zimefafanua vizuri sana mpango mkakati wa Serikali katika mwaka wa fedha 2019/2020 yenye lengo la kuimarisha na kuboresha huduma na uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza wewe binafsi; nampongeza sana Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge ukiwemo wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, mnavyoliongoza vizuri sana Bunge letu hili Tukufu. Ni imani yangu kuwa mtaendelea kuliongoza Bunge hili kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu na miongozo stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishukuru kamati ya kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti Mahmoud Hassan Mgimwa, (Mb), na Makamu wake Mwenyekiti Christine Gabriel Ishengoma (Mb), kwa ushirikiano na maelekezo yao kwa Kamati yao nzuri hiyo na ushauri mkubwa ambao wamekuwa wakiuleta kwa Kamati. Maelekezo yao hayo mazuri wanayoyatoa katika kipindi chote, hasa katika utekelezaji wa mpango wa bajeti wa Wizara wa mwaka 2019/2019 na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya mwaka 2019/2020,

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Khamis Ulega, Mbunge wa Mkuranga pamona na Makatibu Wakuu, Profesa Elisante Ole-Gabriel – Mifugo na Dokta Rashid Adam Tamatama – Uvuvi, kwa ushirikiano wao mkubwa katika kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa mara nyingine tena niwapongeze na kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Kisesa kwa kunichagua na kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili Tukufu. Bahati nzuri wako pale na leo imekuwa ya aina yake, msafara huu umeongozwa na Mzee Mpina mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo. Katika Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 idadi ya mifugo inakadiriwa kuongezeka ikilinganishwa na mwaka 2017/2018, ambapo idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka milioni 30.5 hadi milioni 32.2, mbuzi milioni 18.8 hadi milioni 20, kondoo kutoka milioni 5.5 hadi milioni 5.5.

Aidha kuku wameongezeka kutoka milioni 74.8 hadi milioni 79.1 ambapo kuku wa asili wameongezeka kutoka milioni 34.2 hadi milioni 38.5, kuku wa kisasa wameongezeka kutoka milioni 36.6 hadi milioni 40.6, nguruwe kutoka milioni 1.9 hadi milioni 2 na punda kutoka 595,000,160 hadi 636,000,997. Pia sekta ya mifugo katika mwaka wa fedha wa 2018 ilikua kwa asilimia 4.9 na ikichangia asilimia 7.6 katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2018/2019 biashara ya mifugo imeendelea kuimarika ambapo jumla ya shilingi trilioni 1.4 zimepatikana kutokana na mauzo ya ng'ombe 2,253,1000 na mbuzi 2,003,200 na kondoo 385,500 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.1 zilizopatikana katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 kutoka katika mauzo ya ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Bajeti. Mapitio ya mapato na matumizi ya fedha ya sekta ya mifugo katika kipindi cha mwaka 2018/2019, katika hotuba imeainishwa katika *para* ya 22 mpaka *para* ya 27 wanaofuatilia kitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makusanyo ya Maduhuli. Katika mwaka wa 2018/2019 Wizara ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi 18,467,945,100. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 kiasi cha shilingi 33,853,050,913 kimekusanywa kutoka katika sekta ya mifugo pekee, sawa na asilimia 183.31 ya lengo la makusanyo. Ongezeko hili linatokana na Wizara kuendelea kuimarisha udhibiti wa upotevu wa mapato pamoja na marekebosho katika ada na tozo mbalimbali zilizokuwa zinatozwa katika sekta ya mifugo. Mchoro pale unaonesha. Ukiangalia kwenye kitabu cha hotuba inaonesha kila chanzo cha mapato kimechangia kiasi gani katika ukusanyaji wa mapato hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imepitia orodha ya tozo na ada zinazotozwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, taasisi zake na Wizara nyingine chini ya sheria mbalimbali za mifugo na kubaini baadhi ya tozo na ada hizo kuwa ni kero kwa wafugaji na maendeleo ya sekta ya mifugo kwa ujumla. Katika mwaka 2019/2020 Wizara imetoa mapendekezo ya kuziboresha na kuomba kuziondoa, ili kuondoa usumbufu kwa wafugaji na hivyo kuongeza mapato katika sekta ya mifugo na kutoa huduma ya mifugo kwa wafugaji ambapo jumla ya tozo 10 zinapendekezwa kufutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeandaa kanuni chini ya Sheria ya Magonjwa ya Wanyama, Namba 17 ya Mwaka 2003 na Sheria ya Ustawi wa Wanyama Namba 19 ya Mwaka 2008. Kanuni zilizoandaliwa ni pamoja na Kanuni

ya Uogeshaji wa Mifugo. Wizara inatunga kanuni hii, ili kukabiliana na kuenea kwa magonjwa yaenezwayo na kupe na wadudu wengine. Kukabiliana na tatizo la uogeshaji wa mifugo usioratibiwa, yani holela, gharama kubwa ya uogeshaji, kutokuwepo kwa takwimu na taarifa ya matumizi ya dawa za kuogesha mifugo, kutokufanyika kwa upimaji wa nguvu ya dawa ya kuogesha mifugo na maji ya josho, kutokuwepo kwa usajili na ukaguzi wa majosho, kutokuwepo kwa mgawanyo wa dawa na maeneo yenye usugu, umiliki usioeleweka wa majosho na hatari ya kuchukuliwa ardhi iliyotengwa kwa ajili ya majosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, kanuni inayoandaliwa na Wizara yangu ni kanuni ya uzalishaji, uingizaji, usambazaji na uchanjaji wa mifugo. Wizara inatunga kanuni hii ili kuondoa changamoto za uzalishaji, uingizaji, usambazaji na utoaji wa chanjo nchini. Kasoro hizi ni kama gharama kubwa ya utoaji chanjo, muingiliano katika usimamizi, utunzaji hafifu wa taarifa na takwimu, kiwango kidogo cha uchanjaji na usiofikia maeneo yote ya magonjwa ya kipaumbele, kutokuwepo kwa udhibiti wa uchanjaji wa mifugo nchini na utunzaji wa chanjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni nyingine inayoandaliwa ni Kanuni ya Uhimilishaji, Uhawilishaji Kiinitete na Matumizi ya Madume Bora. Wizara inatunga kanuni hii ili kutatua changamoto zilizopo katika uzalishaji wa mifugo. Mfano, gharama kubwa ya uhimilishaji, uhawilishaji, matumizi holela ya madume ya mbegu, mapungufu katika utunzaji wa kumbukumbu, mapungufu katika mipango ya utambuzi na uhifadhi wa vinasaba vya mifugo bora na kutokuwa na vyanzo vya uhakika vya utunzaji wa vinasaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni nyingine ni Kanuni ya Ukamataji wa Mifugo. Wizara inafanya mapitio ya Kanuni ya Ukamataji wa Mifugo, ili kuzuia ukamatajni holela wa mifugo. Imejitokeza tabia ya baadhi ya wananchi na watendaji wa Serikali kukamata mifugo bila kuzingatia haki za mifugo ambazo zimeainishwa katika Sheria ya Ustawi wa Wanyama, Namba 19 ya Mwaka 2008 na Sheria ya Magonjwa ya

Wanyama, Namba 17 ya Mwaka 2003 pamoja na Kanuni zake. Ukiukwaji huu wa sheria umeleta mateso makubwa kwa wanyama kwa kukosa huduma muhimu kama malisho, dawa, chanjo na maji, Hali hii imesababisha mifugo mingi kufa huku ikiwa imeshikiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2019/2020 Wizara itaendelea kukamilisha sheria na kanuni zote za mifugo ili kuboresha huduma ya mifugo na mazao yake. Lengo kubwa ni kuhakikisha kuwa chanjo za mifugo zinapatikana kwa bei nzuri kwa ajili ya wafugaji. kuondoa matumizi ya dawa zilizoisha muda wa matumizi na kuendelea kutumika na kuzuia ukamataji hovyo na holela wa mifugo, maana imefikia mahali kila mtu anafikiri kwamba, anaweza akakamata tu mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uzalishaji na Usindikaji wa Zao la Maziwa. Uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita bilioni 2.4 mwaka 2017/2018 na kufikia biloni 2.7 hadi kufikia Aprili mwaka 2018/2019; kiambatisho hicho kimeonesha; ikiwa ni ongezeko la asilimia 12.5. Kati ya lita hizo bilioni 1.5 zinatokana na ng'ombe wa asili na lita milioni 900 ni ng'ombe wa kisasa. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa idadi ya ng'ombe wa maziwa kutoka milioni 1,100,000 hadi milioni 1,294,882; matumizi ya uhimilishaji, hali nzuri ya upatikanaji wa malisho na maji na kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji, kuongezeka kwa kiwango cha tozo kutoka shilingi 150 hadi shilingi 2,000 kwa lita ya maziwa inayoingia kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya mitamba ya ng'ombe ya maziwa 15,097 ilizalishwa na kusambazwa. Mitamba 637 ilizalishwa katika mashamba ya Serikali na 14,460 kutoka katika mashamba binafsi, ikilinganishwa na mitamba 13,735 iliyozalishwa katika mwaka uliotangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea na mkakati wa miaka mitatu wa mwaka 2018/2019 hadi mwaka 2020/2021 unaolenga kuzalisha mitamba 1,000,000 kwa mwaka kutokana na uhimilishaji wa ng'ombe wa asili milioni

3 ili kuongeza uzalishaji wa maziwa. Mkakati huu ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati Kabambe wa Mifugo wa Tanzania *(TLMP)* ambao umeainisha kuwa ifikapo mwaka 2021/2022 idadi ya ng'ombe wa maziwa inatarajiwa kuongezeka mara 3.8 kutoka 789,000 hadi 2,985,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza mkakati huo, Wizara imeendelea kuimarisha Kituo cha Uhimilishaji cha Taifa – *NAIC* kupitia Mradi wa Ushirikano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa ufadhili wa *Bill & Melinda Gates Foundation*. Katika mwaka 2018/2019, kituo kimeimarishwa kwa kupatiwa kichambuzi cha mbegu *(semen analyzer)* na madume bora matatu aina ya boran. Aidha, mradi wa *EU-IBAR* umefadhili madume matatu aina ya *sahiwal* na hivyo kufikia madume 31 ambao tunatoa mbegu pale *NAIC*. Pia, katika kutekeleza mkakati huu mradi umenunua mitungi 71 ya kuhifadhi kimiminika cha naitrojeni chenye uwezo wa kubeba lita 35, pikipiki 46 na vifaa vingine vya uhimilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020 Wizara itaendelea kuimarisha Kituo cha *NAIC* na kukipatia vitendea kazi ikiwa ni pamoja na kukarabati mabanda ya madume, mtambo wa kuzalisha kimiminika cha naitrojeni, kutoa mafunzo ya wahimilishaji 600. Wizara kupitia Bodi ya Maziwa itaendelea kuratibu na kusimamia usindikaji na biashara ya maziwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, Bodi ya Maziwa imetoa vibali 692 vya kuingiza maziwa, sawa na lita 18,617,659.07 zenye thamani ya shilingi bilioni 26.22 ikilinganishwa na maziwa lita milioni 20.9 zenye thamani ya shilingi bilioni 30.29 zilizoingizwa katika kipindi kama hiki mwaka uliopita wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usindikaji wa Zao la Nyama na Mayai. Uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kutoka tani 690,629 mwaka 2018/2019 ikilinganishwa na tani 679,992 mwaka 2017/2018, ambapo kiambatisho cha kwanza kimeoneshwa; hili ni sawasawa na ongezeko la 1.6. Aidha, jumla ya tani 516.63 za nyama zenye thamani ya Dola za

Marekani 2.16 ziliingizwa nchini mwaka 2018/2019 ikilinganishwa na tani 1,401.96 zenye thamani ya shilingi 4.36 zilizoingizwa nchini mwaka wa 2017/2018, sawa na upungufu wa asilimia 63.8. Upungufu huu umechangiwa na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji, kuongezeka kwa uzalishaji na udhibiti wa uingizaji holela wa nyama kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2019 jumla ya tani 1,759.12 za nyama zenye thamani ya bilioni 9.4 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na kiasi cha tani 2.6 zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 5.6 ziliuzwa nje ya nchi mwaka 2017/2018, hii ni pungufu kwa asilimia 48.3. Katika mwaka huu wa 2019, Wizara itaendelea kuhamasisha wadau wa tasnia ya nyama kupitia mashamba darasa ya unenepeshaji ili uwekezaji kwenye ufugaji wa kisasa ikiwemo wa ranchi na unenepeshaji wa mifugo kufikia ng'ombe 550,000 kwa mwaka. Pia, uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka bilioni 3.2 mwaka 2017/2018 hadi bilioni 3.6 mwaka 2018/2019, kiambatisho namba moja kinaelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara imejenga mnada wa mpakani wa Kirumi na kuuzindua. Ujenzi wa mnada wa mpakani Longido upo katika hatua za mwisho. Vilevile, ujenzi wa kituo cha Polisi cha ujio katika mnada wa mpakani wa Buhigwe, uzio katika mnada ya Kisesya na Nyamatala unaendelea kukamilika mwezi wa Mei, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Operesheni Nzagamba. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Mambo ya Ndani, Viwanda na Biashara, Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ofisi ya Rais TAMISEMI imeendelea na doria maalum ya Operesheni Nzagamba Awamu ya II ikiwa na malengo yafuatayo; Kudhibiti ukwepaji wa ulipaji wa maduhuli ya Serikali kwenye biashara ya mifugo na mazao yake unaofanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu, lakini pili Kulinda viwanda vya ndani na kudhibiti uingizaji holela wa bidhaa mbalimbali zinazoingizwa nchini kinyume cha sheria, kanuni na taratibu na tatu Kuwalinda wananchi

kwa kudhibiti uuzwaji wa bidhaa zisizokidhi viwango vilivyowekwa na *TBS* na *TFDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika awamu hii zoezi lililenga maeneo ya viwandani, minadani, mipakani, *supermarkets,* maeneo ya kupumzishia mifugo na maeneo mengine ya ukaguzi na ya kimkakati. Matokeo ya operesheni hii ni kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Jumla ya ngómbe 207,906, mbuzi na kondoo 266,048, nguruwe 1,356, ngamia 10, farasi tisa, punda 193 na sungura 102; ngozi vipande 162 na mbwa watano walikaguliwa na wamiliki walibainika kuwa na makosa mbalimbali. Jumla ya ngómbe 46,944, mbuzi 165,115 walikamatwa wakiwa wanatoroshwa kwenda nje ya nchi bila kulipiwa na bila vibali na bila kulipiwa ushuru stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni tani 26.3 za nyama na maziwa zilikamatwa zikiwa zinaingizwa nchini bila vibali, zilizokwisha muda wa matumizi na kuwa na ubora hafifu ambazo zote ziliteketezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Vifaranga 26,600 na mayai 21,500 viliingizwa nchini bila vibali navyo vilikamatwa na kuharibiwa kwa mujibu wa Sheria. Tani 25,427 za vyakula vya mifugo zilikamatwa na zikisafirishwa kwenda nje ya nchi bila vibali. Pia, jumla ya katoni 118 za dawa za mifugo zilikamatwa zikiuzwa katika maeneo yaliyosajiliwa bila kuzingatia utaalam; ni katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Arusha ambako ndiko zilikokuwa zimeingizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika operesheni hii wastani wa makusanyo ya mwezi kabla ya operesheni, wastani wa makusanyo ya mwezi yalikuwa shilingi bilioni 1.147 ya sekta ya mifugo, lakini operesheni tu ilipoanza makusanyo yalifikia shilingi bilioni 3.1 kwa mwezi. Hii ina maana kuwa bila udhibiti huu, Serikali inapoteza wastani wa shilingi bilioni mbili kwa mwezi kwa sekta ya mifugo peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika operesheni hii, wastani wa makusanyo ya mwezi, kabla ya operesheni, wastani wa makusanyo ya mwezi yalikuwa shilingi bilioni 1.47 ya Sekta ya Mifugo, lakini opaaresheni tu ilipoanza, makusanyo yalifikia shilingi bilioni 3.1 kwa mwezi. Hii ina maana kuwa bila udhibiti huu, Serikali inapoteza wastani wa shilingi bilioni mbili kwa mwezi kwa Sekta ya Mifugo peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la ngozi; jumla ya tani 16,012 za ngozi za ngozi za ng'ombe, mbuzi na kondoo zenye thamani ya bilioni 22.8 zimezalishwa hadi mwezi Aprili, 2018/2019 ikilinganishwa na tani 15,389,000 zenye thamani ya shilingi bilioni 22 zilizozalishwa katika mwaka wa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya kilo 5,384,735.79 za ngozi zilisindikwa kufikia hatua ya *wet blue* na bidhaa za ngozi zenye thamani ya shilingi bilioni 8.8 zimesafirishwa kwenda Ethiopia, China, Pakistan, Kenya na India. Kati ya hizo kilo 935,286.5 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.8 ni za ng'ombe na 387,135 zenye thamani ya shilingi milioni 778.96 ni za mbuzi na kondoo. Pia kilo 16,594 ni za ngozi zilizochakatwa zenye thamani ya shilingi 40,185,479 na kilo 26,985.54 ni bidhaa za ngozi zenye thamani ya shilingi 146,177,818 zilisafirishwa kwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya rasilimali ya ardhi, maji na malisho. Katika mwaka wa 2018/2019, Wizara inaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji, kukamilisha mabwawa ya Mbagala – Songwe, lambo katika Kijiji cha Chamwakweza – Bagamoyo, visima virefu katika Kijiji cha Mpapa – Manyoni, Solanga, Isimani – Iringa, ukarabati wa Bwawa la Nyakanga - Butiama umekamilika na ukarabati wa lambo katika Kijiji cha Wami Dakawa - Mvomero ambao unaendelea hivi sasa na hivyo kufanya idadi ya mabwawa na malambo kufikia 1,384 na visima virefu kufikia 103.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuimarisha upatikanaji wa maji kwa mifugo, kwa kufanya ukarabati wa malambo na mabwawa

katika Mikoa ya Manyara, Pwani, Simiyu, Arusha, Geita, Tabora na kuchimba visima virefu 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Katika kutatua migogoro ya ardhi, Wizara imechukua hatua mbalimbali; hadi Oktoba 2017, ilikuwa na migogoro 428 katika mikoa mbalimbali nchini. Hatua zilizochukuliwa ni kama ifuatavyo:-

Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa migogoro; na Kuunda timu ya wataalam kutoka Ofisi ya TAMISEMI, Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Chama cha Wafugaji Tanzania kwa lengo la kutatua migogoro katika mikoa mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu ilifanya kazi katika Wilaya za Uvinza, Kasulu, Kibondo, Kigoma, Tanganyika Mlele (Katavi), Kalambo na Nkasi (Sumbawanga), Rukwa, Chunya na Mbarali, Mbeya, Mkuranga, Kibiti, Rufiji, Kisarawe, Pwani ambapo migogoro 27 kati ya 43 sawa na asilimia 59.26 ilitatuliwa katika mikoa hiyo. Kazi hii inaendelea katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha kwamba migogoro yote na kama mnavyoona kwenye picha, Mawaziri wapo kazini kutatua migogoro mbalimbali ya wafugaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutafuta na kuanisha maeneo ya malisho ambapo Wizara imetenga jumla ya hekta 373,076.05 katika kiambatisho cha 12 kutoka katika maeneo yake na vituo vya kupumzishia mifugo, Ranchi za Taifa, mashamba ya *TALIRI*, mashamba ya *LMUs* ili yatumike kwa ufugaji kwa utaratibu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mashamba haya yametolewa ili kuweza kuwasaidia wafugaji katika maeneo mbalimbali, lakini Halmashauri za Tunduru, Mpanda, Biaharamulo, Muleba na Kyerwa zimetenga jumla ya hekta 199,827.3 kwa ajili ya malisho ya mifugo na pia kupunguza kero za wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kuzingatia hili la migogoro ya mifugo, imeanzisha Kurugenzi kwa lengo la kuendeleza na kusimamia maeneo ya malisho, vyanzo vya maji kwa mifugo na rasilimali za vyakula vya mifugo na hivyo kusaidia katika utatuzi wa migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatoa shukrani za dhati sana kwa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa agizo lake alilolitoa la tarehe 15 mwaka 2019 kwa Mawaziri nane. Agizo hili lilihusisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI; Ofisi ya Makamu wa Rais; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Kilimo; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Maji; na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kushirikiana kwa pamoja kutatua migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na kuitafutia ufumbuzi wa kudumu ambapo Mawaziri hao walitembea nchi nzima kuhakikisha kwamba migogoro hiyo inapata majawabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa magonjwa ya mifugo; katika mwaka 2018, Wizara iliandaa na kutekeleza mkakati wa kudhibiti magonjwa ya mifugo, matumizi ya dawa, chanjo na viuatilifu vya mifugo nchini ili kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe nchini. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutoa elimu na hamasa. Aidha, hadi mwezi wa Aprili, 2019, jumla ya michovyo 40,352,258 imefanyika, kati ya michovyo hiyo ng'ombe ni milioni 22.4; mbuzi ni milioni 12.83; na kondoo ni milioni 5.5. Ili kuchochea zoezi la uogeshaji wa mifugo, Wizara yangu ilitoa lita 8,823.3 aina ya *paranex* yenye thamani ya 300,000,000 na kuzigawa kwa majosho 1,486 yanayofanya kazi katika mikoa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ili kudhibiti ubora wa dawa za kuogesha nchini, Wizara kupitia *TVRA* imenunua kifaa cha kupima ubora wa dawa za kuogesha mifugo *(HPLC)* kwa shilingi milioni 120. Katika mwaka wa 2019/2020, Wizara itaendelea kuhamasisha uogeshaji na kutoa dawa za

kuogesha mifugo kwa majosho yote yatakayokuwa yanafanya kazi na tutafanya hivyo kila baada ya miezi sita tutaendelea kutoa dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, 2019, majosho yaliyopo nchini ni 2,533, yanayofanya kazi ni 1,486 tu, mabovu ni 1,047. Mahitaji ya awali ya majosho nchini ni 3,788 na hivyo kufanya upungufu wa majosho 1,255. Wizara itaendelea kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya majosho nchini na kuendelea kushirikiana na Halmashauri katika kujenga majosho mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara inakarabati majosho 161 kwa gharama ya shilingi 235.11 katika mikoa 20, ukiangalia Kiambatisho Na.15 utaona maeneo hayo ambayo tunaenda kukarabati majosho na hili ni zoezi la sasa kuishia Juni, majosho hayo 161 yawe yamekwishakarabatiwa. Halmashauri nazo zimekwishakarabati mpaka sasa hivi majosho 151 na tunazipongeza. Wizara inazitaka Halmashauri zote nchini kutekeleza Agizo la Chato la kukarabati majosho yote nchini ifikapo mwezi Juni, 2019. Halmashauri zote nchini ambazo hazitatekeleza agizo hili zitanyang'anywa mamlaka ya kukusanya mapato yatokanayo na mifugo na mazao yake. Vilevile, jumla ya Kamati 847 za kusimamia majosho zimeundwa ambazo pia zimefungua akaunti kwa ajili ya kusimamia majosho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 jumla ya lita 518,406 za dawa vimiminika za kuogesha mifugo zenye thamani ya shilingi 15.9 ziliingizwa nchini na nyingine kuzalishwa hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa kutokomeza magonjwa 11 yenye athari kijamii na kiuchumi. Jumla ya chanjo dozi milioni 301 ziliingia sokoni kwa ajili ya kukabiliana na magonjwa hayo. Kati ya dozi hizo, zimetajwa kwenye mgawanyiko mnaweza kufuatailia kwenye hotuba yangu ambavyo imeandikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020, Wakala wa Maabara ya *Veterinary Tanzania (TVLA)* imepanga kuzalisha dozi milioni 111 za chanjo za mifugo ikiwa ni pamoja na dozi 100,000,000 za chanjo ya Mdondo ya *TEMEVAC* I2; lakini vilevile chanjo ya *CBPP* 5,000,000; chanjo ya Kimeta 3,000,000; na chanjo ya Chambavu 3,000,000 . Aidha, Wakala inapanga kuanza majaribio ya kuzalisha chanjo dhidi ya ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo *(CCPP),* chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa na chanjo ya mapele ngozi. Hizi zote zitaanza kuzalishwa na taasisi yetu na kwa sasa tulikuwa tunaagiza kutoka nje, lakini kufikia muda nilioutaja, hizi zote zitazalishwa na taasisi yetu ya *TVI* hapa hapa nchini na hivyo tutaokoa fedha za kigeni ambazo zilikuwa zinatumika kuagiza chanjo hizi nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania *(TALIRI)* imefanya tafiti nane vituoni na kwa wafugaji kwa lengo la kuboresha mbari za ng'ombe wa maziwa na nyama, kuku, mbuzi na kondoo, uzalishaji wa punda, malisho bora na vyakula vya mifugo. Aidha, utaratibu wa kununua vifaa vya maabara ya viinitete iliyopo *TALIRI* Mpwapwa vyenye thamani ya shilingi milioni 189 kupitia Mradi wa Uhawilishaji wa Viinitete (*Multiple Ovulation and Embryo Transfer, (MOET*)) unaofadhiliwa na Serikali ya Tanzania kupitia C*OSTECH* unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manufaa yatakayopatikana kwa hapa ni kuwezesha ng'ombe jike kuzalisha viinitete nane mpaka 450; Kuzalisha, kuhifadhi na kufungasha viinitete kwa ajili ya uhimilishaji na uhawilishaji; na Kuongeza kasi ya uzalishaji wa mifugo nchini hasa mitamba na madume kwa ajili ya maziwa na nyama (ndama 50 kwa mwaka kwa ng'ombe mmoja).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *MOET* unatarajiwa kuanza kufanya kazi Julai, 2019 hapa Mpwapwa na ni mradi wa kipekee ambao unaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza kuwa na mradi huo katika Nchi za Afrika Mashariki na Kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika Sekta ya Mifugo; katika mwaka 2018/2019, Serikali kupitia Wizara imeweka mazingira wezeshi katika ujenzi wa viwanda vya utengenezaji wa chanjo na uchakataji wa mifugo na mazao yake. Uwekezaji huo umefanywa katika miradi ifuatayo:-

Moja, ujenzi wa jengo la kuzalishia chanjo za aina ya bakteria katika Kiwanda cha Serikali cha Kibaha *(TVI).* Gharama ya jengo hilo ni shilingi milioni 667. Jengo hilo linatarajia kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; ujenzi wa Kiwanda kikubwa cha Kuzalisha Chanjo za Mifugo cha *Hester Biosciences Africa Limited* cha Kibaha. Kiwanda hiki kinatarajiwa kuzalisha chanjo 27 zinazoagizwa kutoka nje kwa sasa. Gharama za uwekezaji wa kiwanda hicho ni Dola za Marekani milioni 18, sawa na shilingi bilioni 41 na kinatarajiwa kuanza uzalishaji wa chanjo Februari, 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; Kiwanda cha *TAN-CHOICE* (Kibaha), kiwanda hiki kinachojengwa ambacho kinaonekana pale, kina uwezo wa kuchakata ng'ombe 1,000 na mbuzi 4,500 kwa siku na uwekezaji wake ni Dola za Marekani milioni 5.5 sawa na shilingi bilioni 12.5 na kinatarajiwa kuanza kazi Septemba, 2019 pia kitaweza kutoa ajira 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha tano ni Kiwanda cha *Elia Food and Overseas Limited* kinachojengwa Longido sasa hivi, chenye uwezo wa kuchakata ng'ombe 500 na mbuzi 2,000 kwa siku. Ujenzi wake utagharimu Dola za Marekani milioni tano sawa na shilingi bilioni 11.3. Kiwanda hiki kitaanza kufanya kazi Septemba, 2019 na kinategemea kutoa ajira kwa zaidi ya watu 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha sita ni cha *Galaxy Food and Beverage Limited* cha Arusha kitakachokuwa na uwezo wa kusindika maziwa lita 75,000 tena katika kiwango cha *UHT* kwa siku na kitaajiri wafanyakazi zaidi ya 30. Gharama za uwekezaji wa kiwanda hicho ni Dola za Marekani milioni 2.5, sawa na shilingi bilioni 5.7. Kiwanda

hiki tayari kimeshaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, unaweza kuona viwanda vikubwa kama hivyo vinavyojengwa kwa muda mfupi huu wa Serikali ya Awamu ya Tano na huyo ndiye Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Mifugo ya Tanzania kwa mara kwanza kwa miaka mingi baada ya kukosa soko, leo sasa inaenda kugombaniwa na viwanda kwa kujengewa viwanda vingi sana nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NARCO* imesaini Hati ya Makubaliano ya utekelezaji wa Mradi wa *Integrated Rural Development Project (IRDP)* katika Ranchi ya Ruvu na Kampuni ya *National Egyptian Company for Africa Investment (NECAI)* kwa ajili ya uwekezaji mkubwa utakaogharimu Dola za Marekani milioni 50 sawa na shilingi za Tanzania bilioni 111. Mradi wa ujenzi wa machinjio kubwa na ya kisasa ambao utaweza kuchinja ng'ombe zaidi 1,500, mbuzi na kondoo 4,500 kwa siku na utakuwa unaendeshwa kwa shifti nane. Kiwanda hicho unaingiza ng'ombe asubuhi, jioni unakinga kiatu na makopo ya nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kingine ni kile cha kupitia Mfuko wa Jamii wa *PSSSF,* tumepanua Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Ngozi cha Gereza la Karanga ili kiweze kuongeza uzalishaji kutoka jozi 150 hadi kufikia jozi 400, hii nayo kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vipo viwanda vingi vinavyoendelea kujengwa; uwekezaji huu utaondoa changamoto zilizopo hivi sasa za wafugaji kutangatanga kutafuta masoko ya mifugo, kukosa bei nzuri, kupoteza fedha nyingi za kigeni kuagiza mazao ya mifugo kutoka nje ya nchi, kupoteza ajira na mapato ya Serikali. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuhamasisha na kusimamia uwekezaji katika Sekta ya Mifugo ili waweze kuwekeza na mazao yetu yaendelee upata thamani. Sasa hiyo ilikuwa ni biashara na uchumi wa mifugo, sasa tunaingia Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi; Sekta hii ni miongoni mwa sekta za kiuchumi ambazo ni muhimu sana katika kuondoa umasikini na kukuza uchumi kwa ujumla. Sekta

hii ina mchango mkubwa katika kuwapatia wananchi ajira, chakula, lishe, kipato na fedha za kigeni. Katika mwaka 2018, Sekta ya Uvuvi ilichangia asilimia 1.71 katika Pato la Taifa na imekua kwa asilimia 9.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za tafiti zilizofanyika kwa vipindi tofauti katika mwaka 2018/2019, zinaonesha kwamba, kiasi cha samaki kilichopo katika maji yetu ya Tanzania ni kilo bilioni 2.8 kwa mtawanyiko ufuatao: Ziwa Victoria kilo 2.2; Ziwa Tanganyika kilo milioni 297; na Ziwa Nyasa kilo milioni 168; na maji mengine lakini pia Bahari ya Hindi kilo milioni 100. Kiambatisho kimeonyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya wavuvi wanaoendelea kuvua ni 202,053 ambao wanatumia jumla ya vyombo vya uvuvi 58,930; hao wanashiriki moja kwa moja katika shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguvu hii ya uvuvi imewezesha kuvunwa kwa tani 389,459.4 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 1.18. kwa hiyo kuishia Mei tulikuwa tumefikisha mavuno yenye thamani ya trilioni 1.83. Kati ya tani zilizovunwa mwaka 2018/2019, tani 333,782.32 ambayo ni sawa na asilimia 85.7 ni kutoka maji ya baridi na tani 55,677.08 (asilimia 14.3) ni kutoka maji ya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, wakuzaji viumbe maji 26,474 walishiriki moja kwa moja kwenye shughuli za ukuzaji viumbe maji na kuzalisha jumla ya tani 18,073.6. Kati ya tani hizo tani 16,288 ni za samaki, tani 336.4 ni za kambamiti, tani 1,449 ni za mwani na tani 0.2 ni za kaa pamoja na vipande 395 vya lulu. Aidha, jumla ya vifaranga vya samaki 17,301,076 vilizalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto zilizopo katika Sekta ya Uvuvi, Wizara imeandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo; mapitio ya Sheria ya Uvuvi na kuandaa Sheria mpya ya Kuendeleza Ukuzaji viumbe Maji, Mkakati wa Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi nchini, Mkakati wa Kujenga na Kuboresha

Miundombinu ya Uvuvi, Mkakati wa Kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania *(TAFICO),* Mkakati wa Kuendeleza Tasnia ya Ukuzaji Viumbe Maji; Mkakati wa Kusimamia Samaki Aina ya Jodari; na kuanzishwa kwa Dawati la Sekta Binafsi, Mpango wa Usimamizi wa Samaki Wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji, Usimamizi wa Uvuvi wa Kambamiti na kusimamia rasilimali ya Pweza. Pia, Wizara inafanya mapitio ya Mpango Kabambe wa usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi Tanzania *(Tanzania Fisheries Master Plan).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makusanyo ya Maduhuli Upande wa Sekta ya Uvuvi. Kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara kupitia sekta ya uvuvi ilitarajia kukusanya shilingi bilioni 21.5. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 kabla hata ya mwaka kuisha, Wizara imeshakusanya bilioni 30.3, sawa na asilimia 148.8 ya lengo zilikusanywa kutoka sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchoro unaonesha pale jinsi mgawanyo wa mapato ambavyo ulivyokusanywa katika maeneo mbalimbali. Wako watu wanaweza kusema lakini ukiangalia mchanganuo pale unazungumza vyanzo hivyo vya mapato vimetoka wapi. Katika mwaka ujao huu wa fedha Wizara katika Fungu 64 imepangiwa kukusanya bilioni 32.45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya vipaumbele katika mpango na Bajeti ya Mwaka 2018/2019 na katika Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020. Katika mwaka 2019/2020, Wizara imeainisha maeneo ya vipaumbele katika Mpango na Bajeti ya Wizara kupitia Sekta ya Uvuvi, Fungu 64. Utekelezaji wake utafanyika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha kwamba Sekta ya Uvuvi inachangia kikamilifu katika kuifikisha nchi yetu kwenye uchumi wa viwanda. Maeneo hayo ya vipaumbele yameainishwa katika kitabu cha hotuba yangu ukurasa wa 36.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria. Katika kuhakikisha kwamba Sheria inayosimamia Sekta ya Uvuvi inakidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa, Wizara imeamua kuifumua Sheria ya Uvuvi

Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za Mwaka 2009, ambapo itazaliwa Sheria mpya ya Uvuvi na Sheria Mpya ya Ukuzaji Viumbe Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019, Wizara imefanya marekebisho ya dharura ya baadhi ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 ili kuliwezesha taifa kunufaika na rasilimali za uvuvi. Miongoni mwa marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, matumizi ya nyavu za milimita nane badala ya milimita kumi kwa uvuvi wa dagaa katika ukanda wa bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, matumizi ya nyavu za makila zenye ukubwa wa macho ya kuanzia inchi saba badala ya inchi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, uvunaji wa kaa kutoka gramu 500 hadi gramu 450;

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kuondoa ukomo wa urefu wa sentimita 85 kwa samaki aina ya Sangara;

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, matumizi ya leseni moja kwa kila eneo la maji ya uvuvi badala ya kila Halmashauri kutoa leseni yake.

Marekebisho haya yameainishwa katika *GN* Na. 383 ya tarehe 10 Mei ya mwaka 2019 (Kiambatisho Na. 20 kinaeleza).

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho haya yanaiwezesha Serikali kutekeleza yafuatayo:-

Moja, Serikali kuruhusu kuvua dagaa aina ya mchele kwa kutumia nyavu za milimita nane ambao walikuwa hawawezi kuvuliwa kwa kutumia nyavu za milimita kumi zilizokuwepo kwa mujibu wa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi. Na sasa hivi

ninavyozungumza wavuvi wa Ukanda wa Pwani wanaweza kuanza kuvua kwa kutumia milimita nane sasa kwa sababu kanuni tayari zimekwishakurekebishwa. *(Makofi)*

Pili, Serikali kuruhusu kuvua samaki aina ya Sangara wenye urefu wa zaidi ya sentimita 85 katika Ziwa Victoria. Na sasa hivi wavuvi wanaonisikiliza na wengine ambao wako majini sasa hivi ni ruhusa kuvua samaki aina ya Sangara zaidi ya sentimita 85 na kanuni shakurekebishwa. *(Makofi)*

Tatu, Serikali kuruhusu kuvua Kaa wenye uzito wa gramu 450 badala ya gramu 500 waliokuwepo, kuanzia sasa wanaweza kuendelea.

Nne, Serikali kuondoa usumbufu wa wananchi kusaka leseni ya uvuvi kwa kila halmashauri; sasa hivi watakata leseni kwa eneo la maji husika. Kwa maana ya kama ni Bahari ya Hindi basi unakata ya Bahari ya Hindi utakwenda halmashauri zote, kama ni Ziwa Victoria utakata leseni ya Ziwa Victoria utakwenda halmashauri zote. Na *GN* 383 inayazungumza haya, kwa hiyo endeleeni kutekeleza kuanzia hivi sasa kwa sababu tayari maamuzi yamekwishakufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya marekebisho haya, yataongeza kipato cha wavuvi, yataongezeka malighafi za viwanda, yatavutia uwekezaji mpya, yatadhibiti utoroshaji wa mazao ya uvuvi na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi nchini. Hadi kufikia Machi, 2019, jumla ya tani 389,459.4 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 1.83 zilivunwa ikilinganishwa na tani 376,352.72 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.3 zilizovunwa katika mwaka uliopita wa fedha. Ukiangalia pale mavuno na mapato yetu yamekuwa yakiongezeka kila mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, 2019, tani 38,114.72 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa

mapambo 46,098 wenye thamani ya bilioni 491.19 waliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 34,425.56 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 100,110 wenye thamani ya shilingi bilioni 402.57 waliouzwa katika kipindi cha mwaka 2018. Hadi kufikia Machi 2019 mauzo yameliingizia taifa mrahaba wa bilioni 15.63, hii rekodi haijawahi kufikiwa katika vipindi vyote; ikilinganishwa na kiasi cha bilioni 9.5 tu katika kipindi cha miaka ya nyuma iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2019 jumla ya tani 7,760.12 za samaki zenye thamani ya shilingi bilioni 15.34 zimeingizwa nchini ikilinganishwa na tani 23,000 zenye thamani ya shilingi bilioni 46.98 zilizoingizwa katika miaka iliyopita. Kwa hiyo uingizaji wa samaki kutoka nje hadi sasa umepungua kwa asilimia 67.4 tofauti na ilivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi. Katika mwaka 2018/2019 Wizara imeandaa na kutekeleza Mkakati wa Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi Nchini. Mkakati huu unalenga kuongeza ufanisi katika usimamizi, ulinzi, uendelezaji na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi na mazingira yake pamoja na udhibiti wa uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi. Katika kutekeleza mkakati huu Wizara imeanzisha Kanda kuu tatu za Usimamizi na Udhibiti wa Rasimali za Uvuvi. Kanda ya Ziwa Victoria, Kanda ya Ziwa Tanganyika na Kanda ya Pwani. Aidha, Wizara imeanzisha Kanda ndogo mbili za Ukerewe na Sengerema na kuimarisha vituo vyote 27 vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya operesheni hizo ni kukamatwa kwa zana haramu mbalimbali zikiwemo nyavu za makila 168,708, makokoro 3,715, nyavu za timba 15,915, nyavu za dagaa 9,068, kamba za kokoro zenye urefu wa mita 525,788, ndoano 568,958, mitumbwi/boti 2,291. Pia samaki wazazi kilo 8,958, samaki wachanga/kayabo kilo 110,181, mabondo kilo 634.01, magari 4,489, pikipiki 374, mitungi ya gesi 236 na watuhumiwa 4,713. Kati ya watuhumiwa hao wapo viongozi 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamata jumla ya tani 11 za samaki walioingizwa nchini bila nyaraka, leseni na vibali. Samaki hao walipatikana wakiwa na viambata vya sumu baada ya kufanyiwa uchunguzi ambapo samaki wote waliteketezwa kutokana na kutokukidhi viwango vya ubora, na hapo inaonekana wanateketezwa. Vilevile, jumla ya raia wa kigeni 203 walikamatwa wakijihusisha na shughuli za uvuvi na biashara za mazao ya uvuvi kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Operesheni Sangara ya mwaka 2018 Awamu ya II iliyofanyika mwaka 2017/2018 katika Ukanda wa Ziwa Victoria, mvuvi maarufu ambaye alikamatwa na kikosi cha operesheni Wilayani Sengerema kwa kosa la kukutwa na vipande vya nyavu 24,000, ndoano haramu 1,547,000 na mabunda sita ya makokoro ambapo alipigwa faini ya milioni 40 na Wizara yangu, na yeye kukata rufaa, mahakama ikaenda kumpiga faini ya milioni 306 ambapo alilipa na kuachiwa huru na kuiomba radhi Serikali, na kumuomba radhi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa makosa aliyoyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yamefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale umeoneshwa pale uzalishaji wa vifaranga na vitu vingine; ubora na usalama wa mazao umeoneshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti; baada ya zoezi hili kubwa la operesheni kufanyika, katika kuangalia wingi wa samaki Ziwa Victoria kwa kutumia Teknolojia ya *Hydro-acoustic survey, TAFIRI* kwa kushirikiana na Taasisi za *Kenya Marine and Fisheries Research Institute* (*KMFRI* – Kenya ) na *National Fisheries Resources Research Institute* (*NaFIRRI* – Uganda), utafiti uliofanyika Septemba hadi Oktoba 2018, ulionesha uwepo wa ongezeko la samaki kwenye Ziwa letu Victoria.

Ongezeko la samaki kutoka tani 417,937 mwaka 2016 hadi kufikia tani 553,770 mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sangara wa chini ya sentimita 50 wamepungua kutoka asilimia 96 hadi asilimia 62.8 kwa sasa; sangara wa kuanzia sentimita 50 hadi 85 wameongezeka kutoka asilimia 3.3 mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 32 mwaka 2018; sangara waliokuwa na sentimenta 85 wameongezeka kutoka asilimia 0.4 mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 5.2 mwaka 2018; wastani wa urefu wa Sangara umeongezeka kutoka sentimeta 16 mwaka 2017 hadi kufikia sentimeta 25 mwaka 2018. Kwa hiyo mtaona ongezeko hilo kubwa la mazao yetu ya samaki yalivyoongezeka baada ya kufanya operesheni na usimamizi makini katika maji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi. Kupitia bajeti hii tunategemea kwenda kutekeleza miradi mbalimbali ili kuboresha miundombinu kwa gharama ya bilioni 1.8 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa maabara ya utafiti wa samaki Temeke shilingi milioni 403 zitatumika; ujenzi wa maabara ya *TAFIRI* shilingi bilioni 2.6 zitatumika; ujenzi wa nyumba za watumishi wa *MPRU* na maeneo mengine. P kukarabati Soko letu la Feri zimetengwa shilingi bilioni 1.667, tutalitengeneza kwa kiwango cha juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TAFICO* imeanzishwa na inafanya kazi na sasa jumla ya mali zote tulizozifanyia za *TAFICO* zilizokuwa zinamilikiwa na watu, na zingine watu walitaka kujimilikisha, zimefikia bilioni 118. Pia Shirika letu la *TAFICO* limepata fedha za kuanzia bilioni 4.2 kutoka Serikali ya Japan kwa ajili ya kuanza mipango ya kuanza kuendeleza sekta yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dawati la Sekta Binafsi Ambalo Limeongelea Mafanikio Makubwa. Wizara imeanzisha Dawati la Sekta Binafsi lililozinduliwa rasmi Oktoba, 2018 ili kufuatilia kwa karibu changamoto zinazokabili Sekta Binafsi (Sekta ya Mifugo na Uvuvi) na kuzitafutia ufumbuzi na kuongeza uwekezaji na uchangiaji kwenye Pato la Taifa kwa ajili ya kufikia azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuelekea kwenye Uchumi wa Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya dawati hili ni pamoja na kukirejesha kiwanda cha Azam kilichokuwa sasa kinatarajia kufungwa, sasa kimeweza kuendesha biashara yake baada ya kupewa unafuu wa tozo badala ya 2,000 kuwa shilingi 250; kiwanda hiki kipo Zanzibar. Dawati la Sekta Binafsi limeunganisha wawekezaji mbalimbali nchini na limefanya mambo mengi mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mambo Mtambuka; Gawio la Serikali. Katika mwaka 2018/2019, Taasisi, Bodi na Wakala zilizopo chini ya Wizara zimeshalipa tayari gawio la Serikali la mwaka huu zaidi ya milioni 520; kwa mara ya kwanza; hazijawahi kulipa. Vilevile mchango wa kijamii, taasisi zote za Serikali zilizopo chini ya Wizara hii zimeshatoa jumla ya shilingi milioni 411.79 kama mchango wa jamii, kiwango hiki ni kiwango cha juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu mbalimbali ya kiuchumi inaendelea kuimarsihwa. Wizara inayo faraja kubwa sana katika ujenzi wa miundombinu mikubwa ya kiuchumi inayoendelea kujengwa nchini ikiwemo Reli ya Kisasa ya Mwendokasi *(SGR),* Mradi mkubwa wa Umeme wa Mto Rufiji *(Stiegler's Gorge),* upanuzi wa viwanja vya ndege na ununuzi wa ndege kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboreshwa kwa miundombinu hii, pamoja na mambo mengine utachochea uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi. Kwa muktadha huo Wizara yangu inayo kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kufanya maamuzi mazito haya na sahihi ya kutekeleza miradi hii mikubwa, tena kwa fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchumi na Biashara ya Mifugo. Wizara imeendelea kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa. Katika mwaka 2018/2019 mauzo ya ndani ya nchi katika Sekta za Mifugo na Uvuvi (nyama, samaki, maziwa, mayai, ngozi na vifaranga) yanakadiriwa kufikia

trilioni 6.57. Mauzo ya mazao ya mifugo nje ya nchi yamefikia bilioni 508.97.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwezesha hivyo imewezesha *purchasing power* kwa wananchi kwa kupata nguvu ya kuweza kununua, kulipa kodi mbalimbali za mahitaji yao, aidha, upande mwingine mazao haya yanapouzwa nje ya nchi huliingizia taifa fedha za kigeni, pia kuokoa fedha za kigeni ambazo zingetumika kuagiza mazao hayo nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa nguvu kazi, mifugo inachangia asilimia 27 ya nguvu kazi katika kilimo. Hekta milioni 16 zinazozalishwa nchini, hekta 4.3 zinalimwa na ng'ombe kwa kutumia wanyamakazi. Pia mifugo hii imekuwa ikifanya kazi nyingi ya kusafirisha mazao, kusafirisha vifaa vya ujenzi, vya shule na zahanati, lakini inasafirisha wagonjwa, inasomba maji badala akinamama kujitwisha ndoo kichwani, inabeba mifugo, kubeba mizigo mbalimbali, mifugo kama mbwa imekuwa ikitoa ulinzi. Kwa hiyo haya yote ni mambo lukuki ya faida ya mifugo hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, naomba uende kwenye hitimisho uombe pesa muda nimekuongeza mwingi.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa kusema, katika mwaka wa fedha 2018 Wizara ilipangiwa kukusanya bilioni 40, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 makusanyo yamefikia bilioni 63.3 ambayo ni sawa na asilimia158, lakini pia Halmashauri zimeweza kukusanya mapato yanayotokana na mifugo bilioni 26.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha hotuba yangu naomba sasa kwanamna ya pekee niwapongeze sana wafugaji na wavuvi wote kote nchini kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutunza, kuzalisha na kulinda rasilimali za Taifa. Kazi wanazofanya ni nzuri na za heshima na kwamba Wizara yangu itaendelea kusimamia na kuunga mkono juhudi zao. Pia, niwashukuru wafanyabiashara, wawekezaji na wadau wote wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi kwa dhamira yao njema ya kuendeleza sekta hizi ambao na wengine

wameahidi kutoa mpaka maziwa bure kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Abdallah Hamisi Ulega, Mbunge wa Jimbo la Mkuranga, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa msaada wake wa karibu katika kusimamia kazi za Wizara. Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu kwa Katibu Mkuu, Dkt. Rashid Adam Tamatamah, Katibu Mkuu wa Uvuvi; Profesa Elisante Ole Gabriel, Katibu Mkuu wa Mifugo; Wakurugenzi wote, Watendaji wote wa Wizara na Taasisi kwa kazi nzuri sana wanazozifanya kwa nia thabiti ya kuleta mageuzi makubwa ya Sekta za Mifugo na Uvuvi. Mapambano yanaendelea na kama tulivyokubaliana saa ni namba tu, kamwe hatutafungwa na muda, wala usiku katika kutekeleza wajibu wetu "*Leaders must be willing to sacrifice for the sake of the vision*" .

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani zangu za dhati za kipekee kwa wananchi wangu wa Jimbo la Kisesa ambao wako hapa ambao muda wote wameendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo na kitaifa. Nataka niwahakikishie kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi, bidii, maarifa na ujasiri mkubwa sitajali jua wala mvua katika kuwatumikia. "ni heri punda aumie lakini mzigo wa tajiri ufike".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imepania kuleta mageuzi makubwa katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi ambapo uwekezaji unaoendelea nchini utalindwa kwa nguvu zote, hatutakubali nchi yetu kugeuzwa kuwa dampo...

**MBUNGE FULANI:** Rudia.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imepania kuleta mageuzi makubwa katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi

ambapo uwekezaji unaoendelea nchini utalindwa kwa nguvu zote, hatutakubali nchi yetu kugeuzwa kuwa dampo na kwamba ulinzi wa rasilimali za mifugo na uvuvi utaendelea kuimarishwa. Tunawashukuru sana wadau wote wa maendeleo wa Sekta za Mifugo ambao wamechangia kwa hali na mali katika kutufikisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa heshima kubwa sana katika mwaka 2019/2020, Wizara yangu inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi yenye Jumla shilingi 64,901,756,551. Mgawanyo wake, Fungu la 99 - shilingi 31,774,378,000 - Sekta ya Mifugo; Fungu 64 - Sekta ya Uvuvi ni shilingi 33,127,378,551. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila fungu ni kama ilivyoambatishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchanganuo huu kama nilivyoambatisha kutaja hapa kwamba mishahara ni bilioni 18.87 lakini fedha za kawaida OC bilioni 9.9 na maendeleo bilioni 3.0 ambayo hii ni Fungu 99, ndiyo zinapatikana zile shilingi 31,774,378,000. Sekta ya Uvuvi - Fungu 64 ambapo matumizi ya kawaida; mshahara shilingi 15,584,667,000 lakini matumizi ya kawaida *OC* shilingi 6,847,000,794 na ndiyo inapatikana na fedha za maendeleo ambayo ni shilingi 14,694,917,551 ndipo inapopatikana ile jumla ya shilingi 33,127,378,551.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani zangu za dhati kwako na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba yangu inapatikana pia katika tovuti ya Wizara *www.mifugo.go.tz.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

# HOTUBA YA WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## A: UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji iliyochambua bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99 – Mifugo na Fungu 64 – Uvuvi) Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019. Aidha, naliomba pia Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa namshukuru sana **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kushika wadhifa huu. Pia, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuiongoza nchi yetu kwa uhodari na umahiri mkubwa katika kipindi kifupi tangu aingie madarakani. Katika kipindi cha miaka minne (4) tumeshuhudia mageuzi makubwa ya uchumi na maendeleo na amekuwa Kiongozi wa mfano na wakuigwa Afrika na Dunia. Utendaji wake umewaridhisha wananchi, viongozi na hata taasisi kubwa zinazoaminika kimataifa. Mhe. Rais pamoja na kuwepo na kauli za kukatishwa tamaa zinazotolewa na baadhi ya watu, “**endeleza mapambano ya kusaka maendeleo ya watanzania na sisi wasaidizi wako tupo imara na tutaendelea kufanya kazi usiku na mchana ili matarajio ya watanzania kwa Serikali ya awamu ya tano yafikiwe”.**

3. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, nawapongeza Mheshimiwa **Dkt. Ally Mohamed Shein**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa **Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.),** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiongoza vema nchi yetu kwa hekima na busara.

4. ***Mheshimiwa Spika*,** napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza, Mheshimiwa **Kassim Majaliwa Majaliwa,** Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango (Mb**) Waziri wa Fedha na Mipango, kwa hotuba zao ambazo zimefafanua vizuri mipango na mikakati ya Serikali katika mwaka wa fedha 2019/2020 yenye lengo la kuimarisha na kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii nchini.

5. ***Mheshimiwa Spika*,** napenda pia kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza vizuri Bunge letu Tukufu. Ni imani yangu kuwa, mtaendelea kuliongoza Bunge hili kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo stahiki ili Bunge liweze kuisimamia na kuishauri Serikali.

6. ***Mheshimiwa Spika*,** naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake **Mhe. Mahamoud Hassan Mgimwa**, Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Makamu wake **Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma**, Mbunge wa Viti Maalum Morogoro kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri waliotoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, napenda kuwapongeza **Mhe. Abdallah Ally Mtolea**, Mbunge wa Temeke, **Mhe. Said Maulid Mtulia**, Mbunge wa Kinondoni, **Mhe. James Ole Milya**, Mbunge wa Simanjiro, **Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara** Mbunge wa Ukonga, **Mhe. Julius Kalanga Laizer** Mbunge wa Monduli, **Mhe. Pauline Philipo Gekul**, Mbunge wa Babati Mjini, **Mhe. Ryoba Chacha Marwa,**

Mbunge wa Serengeti, **Mhe. Joseph Michael Mkundi**, Mbunge wa Ukerewe, **Mhe. Mhandisi Christopher Kajolo Chiza** Mbunge wa Buyungu, **Mhe. Timotheo Paul Mnzava** Mbunge wa Korogwe Vijijini, **Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka** Mbunge wa Liwale kwa kuchaguliwa na kisha kuapishwa na Bunge lako Tukufu ili wawatumikie wananchi waliowachagua.

**7.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Mbunge wa Korogwe Vijijini; Marehemu Steven Ngonyani Mbunge mwenzetu. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya marehemu, ndugu na wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi Amina. Aidha, naomba pia, nitumie fursa hii kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge waliopata ajali mbalimbali na waliougua katika kipindi cha Mwaka 2018/2019.

**8.** ***Mheshimiwa Spika*,** pia nichukue nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi **Mhe. Abdallah Hamis Ulega**, Mbunge wa Mkuranga pamoja na Makatibu wakuu **Prof. Elisante Ole Gabriel** (Mifugo) na **Dkt. Rashid Adam Tamatamah** (Uvuvi) kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kuiongoza Wizara.

**9.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kwa mara nyingine tena niwapongeze na kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kisesa kwa kunichagua na kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili Tukufu.

## B: SEKTA YA MIFUGO

### HALI YA SEKTA YA MIFUGO

**10.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2018/2019 idadi ya mifugo hapa nchini inakadiriwa kuongezeka ikilinganishwa na mwaka 2017/2018 ambapo idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka **milioni 30.5** hadi **milioni 32.2,** mbuzi kutoka **milioni 18.8** hadi **milioni 20** na kondoo kutoka **milioni 5.3** hadi **milioni 5.5**.

Aidha, kuku wameongezeka kutoka **milioni 74.8** hadi **milioni 79.1** ikiwa kuku wa asili wameongezeka kutoka **milioni 38.2** hadi **milioni 38.5**, kuku wa kisasa wameongezeka kutoka **milioni 36.6** hadi **milioni 40.6**, nguruwe kutoka **milioni 1.9** hadi **milioni 2** na punda kutoka **595,160** hadi **636,997** (Chanzo: Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania). Aidha, Sekta ya Mifugo katika mwaka 2018 ilikua kwa asilimia **4.9** na kuchangia asilimia **7.6** katika Pato la Taifa.

**11.** ***Mheshimiwa Spika*****,** uzalishaji wa maziwa hapa nchini umeongezeka kutoka lita **bilioni 2.4** mwaka 2017/2018 na kufikia lita **bilioni 2.7** hadi mwezi Aprili Mwaka 2018/2019 **(Kiambatisho Na.1)** ikiwa ni ongezeko la asilimia **12.5**. Ongezeko la uzalishaji limetokana na kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji katika tasnia ya maziwa nchini ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa kiwango cha tozo kutoka shilingi **150** hadi shilingi **2,000** kwa lita/kilo ya maziwa yanayoingizwa nchini.

**12.** ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka hadi kufikia **tani 690,629** mwaka 2018/2019 (Machi, 2019) ikilinganishwa na **tani 679,992** mwaka 2017/2018 (**Kiambatisho Na.1**), ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia **1.6.** Aidha, jumla ya **tani 516.63** za nyama zenye thamani ya Dola za Marekani **2,160,974.33** ziliingizwa nchini mwaka 2018/2019 (Machi, 2019) ikilinganishwa na **tani 1,401.96** za nyama zenye thamani ya Dola za Marekani **4,368,858.07** zilizoingizwa nchini mwaka 2017/2018 sawa na upungufu wa **asilimia 63.15**. Upungufu huu umechangiwa na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji, kuongezeka kwa uzalishaji katika viwanda vya ndani na udhibiti wa uingizaji holela wa nyama kutoka nje ya nchi. Pia, uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai **bilioni 3.2** mwaka 2017/2018 hadi mayai **bilioni 3.6** mwaka 2018/2019 (**Kiambatisho Na. 1**).

**13.** ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya **tani 16,012** za ngozi za ng'ombe, mbuzi na kondoo zenye thamani ya shilingi **bilioni 22.8** zimezalishwa hadi mwezi Aprili Mwaka 2018/2019, ikilinganishwa na **tani 15,389** zenye thamani ya shilingi **bilioni 22** zilizozalishwa katika Mwaka 2017/2018**.**

**14.** ***Mheshimiwa Spika*,** jumla ya marobota ya hei **550,919** yenye wastani wa uzito wa kilo **10** kila moja yalizalishwa mwaka 2018/2019 kutoka kwenye mashamba ya Serikali ikilinganishwa na marobota **482,246.4** yaliyozalishwa mwaka 2017/2018. Ongezeko hilo la asilimia **14.2** limetokana uboreshaji wa mashamba. Vilevile, jumla ya tani **12.1** za mbegu bora za malisho zilizalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali mwaka 2018/2019 ikilinganishwa na tani **10** zilizozalishwa mwaka 2017/2018.

**15.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeandaa na kutekeleza Mkakati wa Kutafuta Ufumbuzi wa Kudumu wa Migogoro ya Wafugaji na Watumiaji Wengine wa Ardhi ambapo Wizara imefanikiwa kutatua migogoro **27** kati ya migogoro **43,** sawa na asilimia **62.8** katika Mikoa Mitano (**5**) ya Kigoma, Katavi, Mbeya, Rukwa na Pwani.

**16.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti magonjwa 11 ya kimkakati kwa kutumia chanjo. Mahitaji ya chanjo kwa magonjwa hayo ni jumla ya dozi **milioni 41.6** kwa ng'ombe, dozi **milioni 30.6** kwa mbuzi na kondoo, dozi **milioni 4** kwa mbwa na paka, dozi **milioni 112.5** kwa kuku wa asili na dozi **milioni 121.8** kwa kuku wa kisasa. Aidha, jumla ya chanjo dozi **301,593,730** ziliingia sokoni kwa ajili ya kukabiliana na magonjwa mbalimbali. Kati ya hizo dozi **39,548,500** zilizalishwa nchini zenye thamani ya **shilingi 1,599,143,000** na dozi **222,496,730** ziliingizwa nchini zenye thamani ya **shilingi 16,350,945,000** ziliagizwa kutoka nje ya nchi. Chanjo zilizozalishwa nchini ni dozi **38,245,800** za Mdondo ($I_2$), dozi **1,114,850** za Kimeta na dozi **187,850** za Chambavu. Kiwango cha chanjo zilizoagizwa nchini ni dozi **26,840,000** za Homa ya Mapafu ya ngómbe (CBPP), dozi **182,000** za Homa ya Mapafu ya Mbuzi (CCPP), dozi **1,074,230** za Kichaa cha Mbwa (Rabies), dozi **122,505,000** za Mdondo, dozi **2,500** za Kutupa Mimba (Brucellosis), dozi **457,000** za Sotoka ya Mbuzi (PPR), dozi **103,984,500** za *Gumboro* na dozi **7,000,000** za *Mareks*.

**17.** ***Mheshimiwa Spika*,** kwa mujibu wa taarifa ya utafiti uliofanywa na Wizara mwaka 2006 na mwaka 2007 ulibaini

kuwa, Magonjwa yaenezwayo na kupe yasipodhibitiwa huchangia asilimia **71.4** ya vifo vyote vya ng'ombe. Magonjwa hayo na asilimia ya uchangiaji kwenye vifo ni Ndigana Kali (**43.5**), Ndigana Baridi (**16.5**), Maji Moyo (**6.3**) na Mkojo Mwekundu (**5.1**). Hasara itokanayo na magonjwa hayo ni takriban Dola za Marekani **milioni 364** sawa na shilingi za Kitanzania **bilioni 815.36** kwa mwaka. Hasara nyingine ni kupungua kwa uzalishaji, kushuka kwa thamani ya ngozi, kupoteza wanyama kazi na udumavu wa ndama.

**18.** ***Mheshimiwa Spika*,** magonjwa yaenezwayo na kupe hudhibitiwa kwa kutumia dawa *(acaricides)* hususan kwa njia ya kuogesha mifugo kwa kutumia majosho, kunyunyiza au kupaka. Uogeshaji huo umekuwa ukizorota kutokana na gharama kubwa ya dawa na usimamizi usioridhisha wa uendeshaji wa majosho na kusababisha magonjwa hayo kuendelea kuwepo na hivyo kuwa tishio kwa mifugo mingi nchini. Wizara inaendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kampeni ya uogeshaji. Kabla ya uzinduzi wa kampeni, kiwango cha uogeshaji kwa mwaka kilikuwa ni **asilimia 10** (Taarifa ya Mtaalamu Mwelekezi: Ujenzi wa Majosho na Matumizi ya dawa za ruzuku-PAPAC, 2017). Baada ya uzinduzi wa Kampeni ya uogeshaji mifugo mwezi Desemba, 2018, wastani wa uogeshaji umefikia jumla ya michovyo **10,145,457** kwa mwezi. Michovyo hiyo ni ya ng'ombe **5,600,042**, Mbuzi **3,209,079** na Kondoo **1,278,917.** Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 uogeshaji mifugo umefikia **asilimia 25** kwa mwezi ambalo ni ongezeko la **asilimia 15**.

**19.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Machi 2019, kuna jumla ya majosho **2,533** nchini ambapo kati ya hayo yanayofanya kazi ni **1,486** na mabovu **1,047**. Mahitaji ya awali ya majosho nchini ni **3,788** na hivyo kufanya upungufu kuwa **1,255.** Hata hivyo, Wizara inaendelea kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya majosho nchini ambapo tathmini hiyo inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2019.

**20.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 jumla ya **lita 518,406** za dawa vimiminika za kuogesha mifugo zenye thamani ya **shilingi 15,939,982,800.00** ziliingizwa kutoka nje ya nchi na nyingine kuzalishwa nchini. Kati ya hizo, **lita 327,530.5** zenye thamani ya **shilingi 8,544,009,500.00** ziliagizwa kutoka nje ya nchi na **lita 190,875.5** zenye thamani ya **shilingi 6,388,580,800.00** zilizalishwa nchini. Aidha, dawa za unga jumla ya **kilo 67,159.5** zenye thamani ya **shilingi 1,007,392,500.00** zinazoua wadudu wasumbufu kwa mifugo zilizalishwa nchini.

**21.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019 biashara ya mifugo nchini imeendelea kuimarika ambapo jumla ya shilingi **trilioni 1.4** zilipatikana kutokana na mauzo ya mifugo katika minada mbalimbali hapa nchini, ikiwa ni mapato ya ng'ombe **2,253,100,** mbuzi **2,003,200** na kondoo **385,500** waliuzwa ikilinganishwa na ng'ombe **1,614,321** mbuzi **1,340,222** na kondoo **315,636** kwa shilingi **trilioni 1.1** waliouzwa katika mwaka 2017/2018.


## MAPITIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2018/2019

### Makusanyo ya Maduhuli

**22.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi **18,467,945,100.** Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 kiasi cha shilingi **33,853,050,919** kimekusanywa na Wizara kutoka Sekta ya Mifugo sawa na asilimia **183.31** ya lengo la makusanyo. Ongezeko hili linatokana na Wizara kuendelea kuimarisha udhibiti wa upotevu wa mapato, marekebisho katika ada na tozo mbalimbali zinazotozwa katika Sekta ya Mifugo.

**23.** ***Mheshimiwa Spika***, Vyanzo vikuu vya fedha hizo ni pamoja na:- Leseni za kusafirisha wanyama na mazao yake nje ya nchi *(export duty license fees);* Ada ya kutoa vibali vya kusafirisha wanyama, nyama, ngozi na mazao mengine nje ya nchi; Ada ya huduma ya vibali vya kusafirisha mifugo ndani ya nchi *(Movement Permits)*; Ushuru wa soko *(Market fee);* Faini: na Mauzo ya chanjo za mifugo, mifugo, mitamba

na mazao ya mifugo (**Kiambatisho Na.2).** Mchango wa kila chanzo kwa mwaka 2018/19 ni kama inavyoonekana hapa chini:




**24.** ***Mheshimiwa Spika*****;** Wizara imefanya tathmini ya utekelezaji wa Waraka wa Rais Na.1 wa Mwaka 2002 unaozitaka Halmashauri zote nchini kuchangia asilimia isiyopungua 15 kwa mapato yatokanayo na mifugo nchini katika mwaka 2017/2018. Tathmini hiyo inaonesha kuwa, Halmashauri **130** kati ya **185** zenye rasilimali ya mifugo nchini zilikusanya kiasi cha shilingi **17,461,690,975.86** ambapo kiasi cha shilingi **1,373,287,346.85** kilitengwa kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Mifugo ambacho ni sawa na asilimia **7.9** ya makusanyo yote. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wakuu wa mikoa ya Tabora, Iringa, Mwanza na Shinyanga kwa kusimamia zoezi hili kwa kiwango cha juu. Vilevile, Wizara yangu imewaandikia barua ya pongezi Wakuu wa Mikoa na Halmashauri zilizofanya vizuri ambazo ni Tarime DC, Magu DC, Kiteto DC, Moshi DC, Same DC, Chato DC, Simanjiro DC na Mbeya Mji. Hata hivyo, baadhi ya Halmashauri hazikufanya vizuri zikiwemo Chunya DC, Njombe DC, Kaliua DC, Morogoro Manispaa, Uvinza DC na Sikonge DC **(Kiambatisho Na.3 ).**

**25.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya tathmini na mapitio ya orodha ya kodi, tozo na ada zinazotozwa na

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Taasisi zake na Wizara nyingine chini ya Sheria mbalimbali za mifugo na kubaini baadhi ya kodi, tozo na ada hizo ni kero kwa wafugaji na maendeleo ya Sekta ya Mifugo kwa ujumla. Katika mwaka 2019/2020 Wizara imetoa mapendekezo ya kuziboresha ili kuondoa usumbufu wa kodi, tozo na ada kwa wafugaji na hivyo kuongeza mapato katika Sekta ya Mifugo na kutoa huduma za mifugo kwa wafugaji. Jumla ya Tozo **10** zimependekezwa kufutwa ikiwa ni pamoja na tozo (**4**) za Maziwa, (**5**) za Nyama na Kuku (**1**) **(Kiambatisho Na. 4).**

### Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

**26.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Sekta ya Mifugo ilitengewa jumla ya shilingi **35,362,663,000.** Kati ya Fedha hizo, shilingi **30,362,663,000.00** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi **5,000,000,000.00** ni fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi **20,458,552,489.00** ni mishahara na shilingi **9,904,110,511.00** ni Matumizi Mengine. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019, jumla ya shilingi **23,291,626,966.48** zilikuwa zimetolewa, ambazo ni sawa na asilimia **76.7** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, shilingi **13,285,693,400.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na shilingi **7,832,745,480.48** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**27.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Sekta ya Mifugo ilitengewa jumla ya **shilingi 5,000,000,000** za Matumizi ya Maendeleo zikiwa ni fedha za ndani. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 kiasi cha shilingi **2,173,188,086.00** (sawa na asilimia **43**) kilikuwa kimetolewa na Wizara ya Fedha na Mipango.

### Maeneo ya Vipaumbele katika Mpango na Bajeti 2018/ 2019

**28.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019 Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Sekta ya Mifugo nchini, iliainisha na kutekeleza maeneo ya vipaumbele

yaliyohusu utekelezaji wa Sekta ya Mifugo. Maeneo hayo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha mashamba ya kuzalisha mitamba na vituo vya uhimilishaji mifugo na kuhamasisha, kusimamia matumizi ya zana, mitambo na teknolojia sahihi katika uzalishaji wa mifugo yenye tija;

(ii) Kuimarisha miundombinu ya uzalishaji mifugo na masoko (minada, majosho na malambo) na kuongeza thamani ya mazao ya mifugo;

(iii) Kudhibiti magonjwa ya milipuko na magonjwa ya kipaumbele;

(iv) Kuongeza upatikanaji na matumizi ya pembejeo na zana za mifugo;

(v) Kuainisha, kupima, kutenga, kumilikisha na kuhamasisha utengaji wa maeneo ya malisho kwa ajili ya mifugo ili kupunguza migogoro ya ardhi kati ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na rasilimali zingine;

(vi) Kuimarisha utafiti, mafunzo na ugani wa mifugo kwa kujenga na kukarabati miundombinu ya vituo vya utafiti na vyuo vya mafunzo ya mifugo kuvipatia watumishi na vitendea kazi;

(vii) Kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya mazao ya mifugo na pembejeo pamoja na kuvifufua viwanda vya zamani;

(viii) Kuhamasisha na kusimamia matumizi ya zana na mitambo na teknolojia sahihi katika uzalishaji wa mifugo yenye tija;

(ix) Kuhamsisha, kuimarisha na kujenga ushirika wa vyama vya wafugaji; na

(x) Kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya kukuza uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta ya mifugo.

**Sera, Mikakati na Programu**

**29.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019 Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 na Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo wa mwaka 2010. Jumla ya wadau **4,800** walipata elimu hiyo kupitia Maonesho ya Sabasaba, Nanenane na Siku ya Chakula Duniani. Aidha, Wizara imesambaza nakala **350** za Sera ya Taifa ya Mifugo na nakala **100** za Fursa za Uwekezaji kwa wadau katika Sekta ya Mifugo.

**30.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019 Wizara ilikamilisha na kuzindua Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania *(Tanzania Livestock Master Plan – TLMP)* hapo tarehe 10 Machi, 2019. Mpango huu umeainisha mahitaji ya jumla ya shilingi **trilioni 1.4** zinahitajika katika utekelezaji wa Mpango ambapo asilimia **64** ya fedha hizi zinatarajiwa zitokane na Sekta binafsi na asilimia **36** zitokane na Serikali. Kupitia Mpango huu, Wizara imeweza kujua hali halisi ya uzalishaji na mahitaji ya mazao yatokanayo na mifugo kwa kuzingatia ongezeko la idadi ya watu, ukuaji wa miji na kipato. Kwa namna ya pekee sana napenda kuwashukuru Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo *(International Livestock Research Institute)* kwa ufadhili wa Taasisi ya Bill & Melinda Gates Foundation (BMGF) tulioshirikiana nao katika kuandaa Mpango. Aidha, Mpango huu umeainisha kanda tatu za mifugo nchini kama ifuatavyo:-

(i) Kanda ya Nyanda za Juu ikijumuisha Kanda ya Kaskasini (Arusha na Kilimanjaro) na Kanda ya Kusini (Iringa, Katavi, Mbeya, Njombe, Rukwa na Songwe), Kanda hii imeainishwa kwa ajili ya uwekezaji na uzalishaji wa maziwa kama zao kuu;

(ii) Kanda ya Kati (Dodoma, Manyara, Morogoro, Simiyu, Singida, Tabora na Shinyanga). Kanda hii imeainishwa kwa ajili ya uwekezaji wa uzalishaji wa nyama; na

(iii) Kanda ya Pwani (Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Pwani na Tanga) na Kanda ya Ziwa (Geita, Kagera, Kigoma, Mara na Mwanza), Kanda ya Pwani na ziwa ni kwa ajili ya uwekezaji

na uzalishaji wa nyama na maziwa kwa upande wa ng'ombe, mbuzi na kondoo.

**31.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania kupitia mfumo wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(Agriculture Sector Development Programme – ASDP II)*. Aidha, Wizara itafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 ili kuboresha mazingira ya biashara.

**32.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka 2018/2019 Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Sekta ya Kilimo pamoja na wadau wengine imeanza kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini Awamu ya Pili (ASDP II). Uzinduzi wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II), ulizinduliwa na **Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 4 Juni, 2018. Lengo la ASDP II ni kufanya mageuzi ya Sekta ya Kilimo (mazao, mifugo na uvuvi) ili kuongeza uzalishaji na tija kwa ajili ya uhakika wa chakula, kuongeza kipato kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na Taifa kwa ujumla.

### Sheria na Kanuni

**33.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019 Wizara imeandaa Waraka wa Mbari za Wanyama *(Animal Breeding Cabinet Paper)* ambao upo katika ngazi ya Sekretariati ya Baraza la Mawaziri. Aidha, Wizara inafanya mapitio ya Sheria Na. 13 ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama ya Mwaka 2010 ili kukidhi mahitaji ya sasa.

**34.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara imekamilisha kuandaa Kanuni za Fedha na Utumishi za Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania, 2017 ambazo zimeidhinishwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali GN No. 27 la Mwaka 2018. Pia, Kanuni zifuatazo za Tasnia ya Mifugo zimeandaliwa na tayari zimeshatangazwa katika Gazeti la Serikali. Kanuni hizo ni:-

*(i) The Animal Diseases (Animals and Animal Products Movement Control) (Amendment) Regulations, 2018 GN No. 475* ambayo imebadilisha viwango vya tozo;

*(ii) The Animal Diseases (Livestock Markets), 2018 GN No. 478;* na

*(iii) The Animal Diseases (Animals and Animal Products Movement Control)*, 2019 GN No. 25.

**35.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara pia, imefanya maandalizi ya Kanuni sita (6) ambazo zitatolewa baada ya marejeo ya Sheria Na. 13 ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama ya Mwaka 2010 kukamilika. Kanuni hizo ni:-

*(i) Import and Export of Animal Feed Resources Regulation;*

*(ii) Detention, Treatment, Disposal and Distruction of Animal Feed Resources, Regulation;*

*(iii) Packing, Branding, Labeling and Sealing of Animal Feed Resources Regulation;*

*(iv) Animal Feed Resources Product Registration Regulation;*

*(v) Fees and Charges of Animal Feed Resources Regulation;* na

*(vi) Varietal Purity Certification of Pasture Seeds Regulation.*

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaandaa kanuni chini ya Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na.17 ya Mwaka 2003 na Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na.19 ya Mwaka 2008. Kanuni zinazoandaliwa ni pamoja na:-

**(i) Kanuni ya Uogeshaji Mifugo.**

Wizara inatunga Kanuni hii ili kukabiliana na kuenea kwa magonjwa yaenezwayo na kupe na wadudu wengine; kukabiliana na tatizo la uogeshaji mifugo usioratibiwa/holela, gharama kubwa za uogeshaji; kutokuwepo kwa takwimu/

taarifa za matumizi ya dawa za kuogesha mifugo; kutofanyika kwa upimaji wa nguvu ya dawa za kuogesha mifugo na maji ya josho; kutokuwepo kwa usajili na ukaguzi wa majosho; kutokuwepo kwa mgawanyo wa dawa kwa maeneo yenye usugu; umiliki usioeleweka wa majosho na hatari ya kuchukuliwa ardhi iliyotengwa kwa ajili ya majosho.

**(ii) Kanuni ya Uzalishaji, Uingizaji, Usambazaji na Uchanjaji wa mifugo**

Wizara inatunga Kanuni hii ili kuondoa changamoto za uzalishaji, uingizaji, usambazaji na utoaji wa chanjo nchini. Kasoro hizo ni kama gharama kubwa za utoaji chanjo; Mwingiliano katika usimamizi; Utunzaji hafifu wa taarifa na takwimu; kiwango kidogo cha uchanjaji na usiofikia maeneo yote kwa magonjwa ya kipaumbele; kutokuwepo kwa udhibiti wa uchanjaji wa mifugo nchini; na utunzaji wa chanjo.

**(iii) Kanuni ya Uhimilishaji, uhawilishaji kiinitete na matumizi ya madume bora.**

Wizara inatunga Kanuni hii ili kutatua changamoto zilizopo katika uzalishaji wa mifugo. Mfano, gharama kubwa ya uhimilishaji na uhawilishaji, Matumizi holela ya madume na mbegu; mapungufu katika utunzaji wa kumbukumbu; mapungufu katika mipango ya utambuzi na uhifadhi wa vinasaba vya mifugo bora; na kutokuwa na vyanzo vya uhakika vya utunzaji wa vinasaba.

**(iv) Kanuni ya Vitotoleshi na Kuku Wazazi *(Hatcheries and Breeding Flock Farms)***

Wizara inatunga Kanuni hii ili kuondoa mwingiliano wa majukumu ya wadau mbalimbali, kuweka bayana mamlaka, vigezo na viwango vya vitotoleshi vya vifaranga; kuweka utaratibu wa uanzishwaji wa vitotoleshi vya vifaranga; mashamba ya kuku wazazi, utunzaji wa mayai, vifaranga vya siku moja *(old day chicks)* na ufuatiliaji wa magonjwa. Pia, kuzingatia viwango vya afya ya wanyama na kuhuisha utoaji wa vibali sawa na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE);

na kuweka viwango tofauti vya teknolojia ya uanzishaji wa vitotoleshi vya vifaranga na mashamba ya kuku wazazi.

**(v) Kanuni ya Ukamataji wa Mifugo**

Wizara inafanya mapitio ya Kanuni za ukamataji mifugo ili kuzuia ukamataji holela wa mifugo. Imejitokeza tabia ya baadhi ya wananchi na watendaji wa Serikali kukamata mifugo bila kuzingatia haki za mifugo ambazo zimeainishwa katika Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya Mwaka 2008 na Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya Mwaka 2003 pamoja na Kanuni zake. Ukiukwaji huu wa Sheria umeleta mateso makubwa kwa wanyama kwa kukosa huduma muhimu kama malisho, dawa, chanjo, na maji. Hali hii inasababisha mifugo mingi kufa ikiwa imeshikiliwa.

**37.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika Mwaka 2019/2020 Wizara itaendelea kukamilisha Sheria na Kanuni zote za Mifugo ili kuboresha huduma za mifugo na mazao yake. Lengo kubwa ni kuhakikisha kuwa chanjo za mifugo zinapatikana kwa bei nzuri kwa ajili ya wafugaji; kuondoa tatizo la dawa zilizoisha muda wake kuendelea kutumika; na kuzuia ukamataji holela wa mifugo.

**UZALISHAJI WA MIFUGO NA MAZAO YAKE**
**Uzalishaji na Usindikaji wa Zao la Maziwa**

**38.** ***Mheshimiwa Spika*****,** uzalishaji wa mifugo na mazao yake hapa nchini umeendelea kuongezeka ambapo idadi ya ng'ombe wa maziwa imeongezeka kutoka **1,100,000** mwaka 2017/2018 hadi **1,294,882** mwaka 2018/2019**.** Pia, katika kipindi cha mwaka 2018/2019, jumla ya mitamba ya ng'ombe wa maziwa **15,097** ilizalishwa na kusambazwa. Kati ya mitamba hiyo, **637** ilizalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali **(Kiambatisho Na. 5)** na **14,460** kutoka Sekta binafsi ikilinganishwa na mitamba **13,735 (**Ikiwa ya Serikali **590** na Binafsi **13,145)** iliyozalishwa na kusambazwa mwaka 2017/2018**.**

**39.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imeanza kutekeleza mkakati wa miaka mitatu (**3**) kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2020/21

unaolenga kuzalisha mitamba **1,000,000** kwa mwaka kutokana na kuhimilisha ng'ombe wa asili **milioni 3** ili kuongeza uzalishaji wa maziwa. Mkakati huu ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Mifugo Tanzania (TLMP) ambao umeainisha kuwa ifikapo mwaka 2021/2022 idadi ya ng'ombe wa maziwa wanatarajiwa kuongezeka mara **3.8** kutoka **789,000** mpaka **2,985,000**.

**40.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza Mkakati huo, Wizara imeendelea kuimarisha kituo cha Uhimilishaji cha Taifa (NAIC) Usa River - Arusha kupitia Mradi wa Ushirikano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika kuboresha Uhimilishaji *(Public Private Partnership for Artificial Insermination Delivery - PAID)* kwa ufadhili wa taasisi ya Bill & Melinda Gates Foundation. Katika mwaka 2018/2019, kituo cha NAIC kimeendelea kuimarishwa kwa kupatiwa kichambuzi cha mbegu (*semen analyzer - CASA)* na madume bora matatu **(3)** aina ya Boran. Pia, mradi wa EU-IBAR umefadhili madume matatu (3) ya Sahiwal na hivyo kufikia madume **31**. Aidha, katika kutekeleza mkakati wa kuzalisha mitamba **1,000,000** kwa njia ya uhimilishaji mradi umenunua mitungi **71** ya kuhifadhi kimiminika cha naitrojeni (lita **35**), pikipiki **46** na vifaa vingine vya uhimilishaji.

**41.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019 Wizara ilitoa mafunzo kwa wataalam **389** wa uhimilishaji ikilinganishwa na Wataalam **204** waliopatiwa mafunzo hayo mwaka 2017/2018, ambalo ni ongezeko la asilimia **90.7.** Aidha, mauzo ya mbegu bora za ng'ombe *(semen)* yameongezeka kutoka shilingi **152,545,250** mwaka 2017/2018 hadi kufikia shilingi **350,218,560** mwaka 2018/2019, sawa na asilimia **129.6.**

**42.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2019/2020 Wizara itaendelea kuimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha NAIC kwa kununua vitendea kazi ikiwa ni pamoja na kukarabati mabanda ya madume, kutengeneza mtambo wa kuzalisha kimiminika cha naitrojeni na kutoa mafunzo kwa wahimilishaji **600** kutoka mikoa ya Lindi, Mtwara, Dodoma, Singida, Simiyu, Shinyanga, Tabora, Kigoma, Katavi, Mwanza na Geita. Pia, Wizara itatoa mafunzo rejea kwa wahimilishaji

**50** na waendesha mitambo saba (**7**). Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha vituo sita vya Kanda vya kuzalisha kimiminika cha Nitrojeni katika Mikoa ya Dodoma, Pwani, Lindi, Mbeya, Mwanza na Katavi kwa kufanya matengenezo na ukarabati wa mitambo.

**43.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kuratibu Mradi wa Uendelezaji wa Sekta ya Maziwa Afrika Mashariki (East Africa Dairy Development - EADD II) unaotekelezwa na Shirika la Heifer International. Mradi umetoa mafunzo ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa katika nyanja za uzalishaji mifugo, ulishaji, afya ya mifugo na elimu ya ushirika kwa wafugaji **40,498** kutoka katika Mikoa ya Iringa, Mbeya na Njombe. Aidha, mradi umewezesha wafugaji wa Halmashauri za Rungwe, Busokelo, Iringa na Njombe kuunda na kuimarisha vyama vya Msingi vya Ushirika **35.** Kati ya hivyo, vyama **23** vya kutoka Rungwe vimeunda Chama Kikuu cha Ushirika kiitwacho Maziwa Cooperative Union (MCU). Vilevile, mradi umevijengea uwezo vyama vya Msingi vya Ushirika **26** kutoka Mkoa wa Songwe vinavyounda mtandao *(Songwe Dairy Cooperative Joint Entreprises).*

**44.** ***Mheshimiwa Spika*,** Mradi wa EADD II umeendelea kutekeleza Programu ya miaka mitano (2014 hadi 2019) ya Unywaji Maziwa Shuleni (*School Milk Feeding Program*) kwa lengo la kuwafikia wanafunzi **15,000** wa shule za awali na msingi ili kuboresha lishe na afya, kupunguza utoro, kuongeza ufaulu na kujenga utamaduni wa unywaji wa maziwa. Hadi kufikia Machi 2019, wanafunzi **16,849** kutoka katika shule **25** za Wilaya za Njombe, Mbeya na Wanging'ombe wanakunywa maziwa kwa ujazo wa mililita **200** kwa mtoto kwa siku kwa siku nne **(4)** za wiki. Program hii imechangia kuongeza udahili na mahudhurio ya wanafunzi katika shule husika yameongezeka kutoka asilimia **89.04** mwaka 2017/2018 hadi kufikia asilimia **95.6** mwezi Machi, 2019. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia **6.56**.

**45.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/2020 Wizara kwa kushirikina na mradi wa EADD II itaendelea kupanua wigo wa masoko ya maziwa kwa kuanzisha na kuendeleza vituo

**10** vya ukusanyaji wa maziwa vyenye uwezo wa lita **34,000** kwa siku ili kusogeza soko la maziwa karibu na wafugaji wengi zaidi. Pia, mradi utaendelea kutekeleza program ya unywaji maziwa shuleni kwa kuongeza shule ili kuwafikia wanafunzi wengi zaidi katika maeneo ya mradi.

**46.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu uzalishaji wa maziwa hapa nchini ambapo katika mwaka 2018/2019 kiasi cha lita **bilioni 2.7** kimezalishwa ikilinganishwa na lita **bilioni 2.4** zilizozalishwa mwaka 2017/2018 sawa na ongezeko la asilimia **12.5**. Kati ya hizo, lita **bilioni 1.8** zilitokana na ng'ombe wa asili na lita **milioni 900** zilitokana na ng'ombe wa kisasa. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa idadi ya ng'ombe wa maziwa kutoka **1,100,000** hadi kufikia ng'ombe **1,294,882,** matumizi ya uhimilishaji na hali nzuri ya upatikanaji wa malisho na maji.

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania imeendelea kuratibu na kusimamia usindikaji na biashara ya maziwa nchini. Katika Mwaka 2018/2019 usindikaji umeongezeka kutoka lita **milioni 56** Mwaka 2017/ 2018 hadi lita **milioni 66.9** Mwaka 2018/2019, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia **19.4.** Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa uwekezaji wa Sekta binafsi katika ujenzi wa viwanda vya kusindika maziwa ambapo viwanda vipya **14** vya Maziwa vimejengwa na kufanya jumla ya viwanda vya kusindika maziwa vinavyofanya kazi kote nchini kuwa **91** (**Kiambatisho Na.6**) ikilinganishwa na viwanda **76** vilivyokuwa vinafanya kazi Mwaka 2017/2018. Pia, vituo vya kukusanyia maziwa vimeongezeka kutoka vituo **184** mwaka 2017/2018 hadi vituo **195** mwaka 2018/2019.

**48.** ***Mheshimiwa Spika*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuhamasisha Sekta binafsi kuimarisha ukusanyaji na usindikaji wa maziwa kufikia **lita 284,500** kutoka **lita 154,100** kwa siku. Aidha, Wizara imeingia makubaliano (MoU) ya uwekezaji katika usindikaji kupitia Dawati la Sekta binafsi ili kuongeza usindikaji wa maziwa nchini.

**Uzalishaji na Usindikaji wa Zao la Nyama na Mayai**

**49.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia tasnia ya nyama nchini. Katika Mwaka 2018/2019, uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kutoka tani **679,992** mwaka 2017/2018 hadi kufikia tani **690,629** Mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia **1.54**. Aidha, katika Mwaka 2018/2019 ng'ombe **449,120** wamenenepeshwa ikilinganishwa na ng'ombe **322,030** walionenepeshwa Mwaka 2017/2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia **39.47**. Ongezeko hilo limetokana na Wizara kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu unenepeshaji ili kutoa nyama nyingi na bora inayokidhi mahitaji ya soko. Hadi mwezi Machi, 2019 wafugaji **86** kutoka katika Halmashauri **17** za Wilaya mwaka 2018/2019 wamepatiwa mafunzo ya unenepeshaji.

**50.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuhamasisha wadau wa tasnia ya nyama kupitia mashamba darasa ya unenepeshaji ili kuwekeza kwenye ufugaji wa kisasa ukiwemo wa ranchi na unenepeshaji wa mifugo ili kufikia ng'ombe **550,000** kwa mwaka.

**51.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania imeendelea kufuatilia biashara ya nyama ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 jumla ya **tani 1,759.12** za nyama zenye thamani ya **Shilingi 9,498,468,816 (Dola za Marekani 3,957,695.34)** ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na kiasi cha **tani 2,608.93** zenye thamani ya **Dola za Marekani 5,679,217.28** zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2017/2018 ikiwa ni pungufu kwa asilimia **48.3**.

**52.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, jumla ya **tani 516.63** za nyama zenye thamani ya Dola za Marekani **2,160,974.33** ziliingizwa kutoka nje ya nchi ikilinganishwa na **tani 1,401.96** za nyama zenye thamani ya Dola za Marekani **4,368,858.07** zilizoingizwa nchini katika Mwaka 2017/2018 sawa na upungufu wa **asilimia 63.15**. Upungufu huu umetokana na sababu mbalimbali ikiwemo Wizara kubadilisha Kanuni na Taratibu za usimamizi wa uingizaji na uuzaji wa bidhaa za mifugo kutoka nje ya nchi ili kuweka uwiano wa

ushindani katika soko. Kiasi hicho cha nyama kiliingizwa kutoka nchini Kenya, Afrika Kusini, Ubelgiji na Uingereza. Katika mwaka 2019/20, Wizara itaendelea kusimamia Sheria, Kanuni na Miongozo ili wawekezaji waweze kuzalisha nyama yenye ubora wa kukidhi viwango na mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

**53.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, Wizara imejenga na kukarabati minada kwa kujenga ukuta katika Mnada wa Mpakani wa Kirumi ulioko Butiama uliofunguliwa rasmi tarehe 16 Oktoba, 2018. Aidha, ujenzi wa jengo la ofisi ya mnada wa Kirumi litakalokuwa na huduma za kibenki unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2019. Kazi ya ujenzi wa sakafu katika mnada wa mpakani uliopo Wilaya ya Longido unaendelea na upo katika hatua za mwisho. Vilevile, ujenzi wa kituo cha Polisi na uzio katika mnada wa mpakani wa Buhigwe na uzio katika minada ya Kasesya na Nyamatala unaendelea na utakamilika mwezi Mei, 2019.

## Operesheni Nzagamba II

**54.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Mambo ya Ndani, Viwanda na Biashara (TBS), Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee, Walemavu na Watoto (TFDA), Ofisi ya Rais (TISS) na TAMISEMI imeendesha doria maalum (Operesheni Nzagamba Awamu ya II) ikiwa na lengo la:-

(i) Kudhibiti ukwepaji wa kulipa maduhuli ya Serikali kwenye biashara ya mifugo na mazao yake unaofanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu;

(ii) Kulinda viwanda vya ndani kwa kudhibiti uingizaji holela wa bidhaa mbalimbali zinazoingizwa nchini kinyume cha Sheria, Kanuni na Taratibu; na

(iii) Kuwalinda wananchi/walaji kwa kudhibiti uuzwaji wa bidhaa zisizokidhi viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania na TFDA.

**55. *Mheshimiwa Spika*,** pamoja na kuelimisha wananchi, Operesheni Nzagamba Awamu ya II, 2018 imekuwa na mafanikio makubwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kudhibiti utoroshaji wa Mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi;

(ii) Kulinda afya ya watumiaji wa mazao ya mifugo na bidhaa zake;

(iii) Kuongeza Pato la Taifa (kutokana na utii wa kibiashara);

(iv) Kulinda ajira za watanzania;

(v) Kuvutia wawekezaji kwenye Sekta ya Mifugo; na

(vi) Kulinda raslimali za nchi.

**56. *Mheshimiwa Spika*,** katika awamu hii, zoezi lililenga maeneo ya viwandani, minadani, mipakani, *supermarkets,* maeneo ya kupumzishia mifugo na vituo vya ukaguzi wa mifugo na maeneo mengine ya kimkakati. Operesheni hii ilifanyika nchi nzima kuanzia tarehe 9 Oktoba, 2018 hadi Machi, 2019. Aidha, ufuatiliaji huu umekuwa na mafanikio yafuatayo:-

(i) Jumla ya ngómbe **207,906,** mbuzi/kondoo **268,048**, nguruwe **1,356**, ngamia **10**, farasi **9**, punda **193** na sungura **102**; ngozi vipande **162** na mbwa **5** walikaguliwa na wamiliki kubainika kuwa na makosa mbalimbali (**Kiambatisho Na. 7**);

(ii) Jumla ya ngómbe **40,944**, mbuzi na kondoo **165,115** walikamatwa wakiwa wanatoroshwa kwenda nje ya nchi bila kulipiwa vibali na ushuru stahiki. Aidha, tani **26.3** za nyama na maziwa zilikamatwa zikiwa zimeingizwa nchini bila vibali, zilizokwisha muda wa matumizi na kuwa na ubora hafifu ambapo zote ziliteketezwa. Vilevile, vifaranga **27,600** na mayai **21,500** vilivyoingizwa nchini bila vibali vilikamatwa na kuharibiwa kwa mujibu wa Sheria;

(iii) Tani **12,555** za mashudu, tani **2,223** za pumba na tani **45** za dagaa (malighafi ya chakula cha mifugo) zilikaguliwa zikisafirishwa kwenda nje ya nchi kwa kupitia maeneo mbalimbali. Aidha, tani **25,425** za vyakula vya mifugo zilikamatwa zikisafirishwa kwenda nje ya nchi bila vibali. Pia, jumla ya katoni **118** za madawa ya mifugo zilikamatwa zikiuzwa katika maeneo yasiyosajiliwa na bila kuzingatia utaalam katika mikoa ya Kigoma, Tabora na Arusha zikiuzwa katika maeneo yasiyosajiliwa na bila kuzingatia utaalam.

**57.** ***Mheshimiwa Spika***, kabla ya Operesheni Nzagamba II makusanyo ya Wizara kwa mwezi Julai hadi Septemba, 2018 yalikuwa ni wastani wa shilingi **1,147,592,640.47** kwa mwezi. Aidha, wakati wa kipindi cha Operesheni, mwezi Oktoba hadi Desemba, 2018 mapato yaliongezeka na kufikia wastani wa shilingi **3,139,309,528** kwa mwezi. Hii ina maana kuwa bila udhibiti huu, Serikali inapoteza wastani wa shilingi **bilioni 2** kwa mwezi**.**

**58.** ***Mheshimiwa Spika*****,** faida za operesheni Nzagamba ni kuongezeka kwa mapato ya Serikali, kulinda viwanda na wazalishaji wa ndani na kuleta ushindani ulio sawa, kulinda afya za walaji, kuchochea uwekezaji katika Sekta ya Mifugo ambapo viwanda vingi hivi sasa vinajengwa, upatikanaji wa bei nzuri, soko la uhakika, kuongezeka kwa uelewa na utii wa Sheria bila shuruti.

**59.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kusimamia na kudhibiti uingizaji holela wa mazao na pembejeo za mifugo kutoka nje ya nchi, kuelimisha wafanyabiashara kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za uendeshaji wa biashara ya mazao ya mifugo, kudhibiti matumizi ya bidhaa zisizokuwa na ubora, kuzuia utoroshaji wa malighafi za mifugo, kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali na kuweka mifumo thabiti ya kusimamia biashara ya mifugo na mazao yake.

**Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)**

**60.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) imetekeleza

majukumu yake ikiwa ni pamoja na kutunza jumla ya ng'ombe **14,590**, mbuzi **2,829**, kondoo **2,477**, nguruwe **144** na farasi **27**. Aidha, Kampuni ilizalisha na kukuza ndama **4,606** kutokana na ng'ombe wazazi **5,703** ikilinganishwa na ndama **4,269** waliozalishwa na kukuzwa mwaka 2017/2018.

**61.** ***Mheshimiwa Spika*****,** NARCO imenunua ng'ombe **1,343** wenye thamani ya shilingi **bilioni 1.05** kati ya hao ng'ombe **313** ni wazazi walionunuliwa kutoka Mzalishaji wa nyama 'Overland' na kupelekwa West Kilimanjaro na ng'ombe **1,030** kwa ajili ya kunenepesha kwa kutumia vyakula vya ziada kwa ajili ya nyama bora na hivyo kuwa sehemu ya soko la uhakika kwa wafugaji nchini ikilinganishwa na ng'ombe **1,175** walionunuliwa mwaka 2017/2018.

**62.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, NARCO imeuza ng'ombe **3,598** wenye thamani ya shilingi **bilioni 2.572** ikilinganishwa na ng'ombe **3,149** wenye thamani ya shilingi **bilioni 2.078** waliouzwa katika mwaka 2017/2018. Vilevile, uuzaji wa nyama bora (Kongwa Beef) kiasi cha **Tani 305.097** umefanyika hivyo kujipatia mapato ya jumla ya shilingi **1,983,135,170.**

**63.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Kampuni imetoa ushauri wa kitaalam kwa wafugaji **439** katika vijiji **52** vinavyozunguka ranchi za Kampuni katika ranchi za Kongwa (vijiji **10**), Ruvu (vijiji **12**), West Kilimanjaro (vijiji **7**), Kagoma (vijiji **6**), Kalambo (vijiji **8**), Missenyi (vijiji **7**) na Mkata (vijiji **2**).

**64.** ***Mheshimiwa Spika*****,** ili kupunguza changamoto ya upatikanaji wa malisho na kuboresha uhusiano kati ya Kampuni na jamii za wafugaji wanaozunguka maeneo ya ranchi, Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) imetenga vitalu **122** vyenye ukubwa wa hekta **59,290** vitakavyopangishwa kwa muda mfupi**.** Hadi kufikia Aprili, 2019 vitalu **92** vimeshapangishwa ambapo ng'ombe **31,356** wanalishwa. Aidha, Kampuni inawakaribisha wafugaji kupangisha vitalu **30** vilivyobaki vyenye uwezo wa kulisha ng'ombe **8,780**.

**65.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza azma ya kuendeleza ufugaji wenye tija, Kampuni ilitangaza vitalu **122** kwa ajili ya uwekezaji wa mifugo wa muda mrefu. Vitalu hivi vina jumla ya hekta **59,290.** Hadi sasa, jumla ya vitalu **92** vyenye **ng'ombe 31,356** vimepangishwa kwa muda mfupi. Aidha, jumla ya vitalu **30** bado havijapata wawekezaji (**Kiambatisho Na. 8**).

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Kampuni imetenga jumla ya shilingi **95,000,000** kwa ajili ya kuchangia huduma za kijamii katika vijiji vinavyozunguka ranchi. Kati ya fedha hizo shilingi **50,000,000** zitajenga na kukarabati majosho na shilingi **45,000,000** zitajenga miundombinu ya maji katika maeneo hayo. Katika mwaka 2019/2020, Kampuni ya NARCO imepanga kuzalisha ng'ombe **4,791** na mbuzi/kondoo **1,399** na kuzalisha na kuuza nyama tani **323.6**.

**Uzalishaji wa Kuku**

**67.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara inaendelea kuratibu na kusimamia uzalishaji wa nyama na mayai kutokana na kuku wa asili na wa kisasa, ambapo vituo vya kutotolesha vifaranga vimeongezeka kutoka vituo **10** mwaka 2017/2018 hadi kufikia vituo **19** mwezi Aprili, 2019. Vituo hivyo **19** viko katika mikoa ya Dar es Salaam (**4**), Iringa (**2**), Njombe (**1**), Pwani (**6**), Kilimanjaro (**3**), Arusha (**1**) na Mwanza (**2**). Aidha, mashamba ya kuku wazazi nchini yameongezeka kutoka **6** hadi **16** katika kipindi hicho yenye uwezo wa kutunza zaidi ya kuku wazazi **1,000,000**. Katika mwaka 2018/2019, jumla ya vifaranga **50,928,000** vimezalishwa na kusambazwa nchini, ambapo vifaranga **47,328,000** ni wa nyama, vifaranga **1,896,000** ni vya kuku chotara hususan *Sasso* na *Kroiler* na vifaranga **1,704,000** ni vya kuku wa mayai. Aidha, Wizara ilitoa vibali maalum kwa Kampuni **13** kuingiza vifaranga vya kuku wazazi **556,616** wa nyama na mayai kutoka nchi za Uholanzi, Uingereza, Ufaransa, Zambia na India. Pia, jumla ya mayai ya kutotolesha vifaranga vya nyama **360,000** yaliingizwa nchini kutoka Zambia. Katika mwaka 2019/2020 Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia uzalishaji wa kuku vifaranga na mayai.

## Uzalishaji wa Nguruwe

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019 Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ufugaji na biashara ya nguruwe. Hadi mwezi Aprili, 2019 jumla ya tani **37,773** za nyama ya nguruwe zimezalishwa ikilinganishwa na tani **37,191** zilizozalishwa mwaka 2017/2018. Ongezeko hilo limetokana na kukua kwa soko na wafugaji kuendelea kuwekeza katika ufugaji wa nguruwe.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji, usindikaji na biashara ya nguruwe. Aidha, Wizara itahimiza sekta binafsi kuzalisha na kusambaza mbegu bora za nguruwe kwa wafugaji ili kuongeza uzalishaji wa nguruwe na bidhaa zake. Pia, Wizara itaendelea kuimarisha Chama cha Wazalishaji Nguruwe nchini TAPIFA kwa lengo la kuboresha kosaafu za nguruwe. Vilevile, Wizara itaendelea kuimarisha shamba lake la nguruwe la Ngerengere ili liweze kuendelea kuzalisha mbegu bora za nguruwe.

## Zao la Ngozi

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia uendelezaji wa tasnia ya ngozi hapa nchini. Katika mwaka 2018/19 jumla ya kilo **5,384,735.79** za ngozi **ghafi,** zilizosindikwa kufikia hatua ya kati (*wet blue*) na bidhaa za ngozi zenye thamani ya **shilingi 8,165,356,495.28** zimesafirishwa kwenda katika nchi za Ethiopia, China, Pakistani, Kenya na India. Kati ya hizo, **kilo 935,286.50** zilizosindikwa (wet blue) zenye thamani ya **shilingi 1,808,412,620.41** ni za ngozi ya ng'ombe, **kilo 386,135** zilizosindikwa (wet blue) zenye thamani ya **shilingi 788,964,283.46** ni ngozi za mbuzi na kondoo kilo 16,594.00 ni ngozi zilizochakatwa (crust leather) zenye thamani ya shilingi **40,185,479** na kilo **20,985.54** ni bidhaa za ngozi zenye thamani ya shilingi **146,177,818.00** zilizosafirishwa kwenda nje ya nchi.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, ngozi ghafi za ngo'mbe zenye uzito wa kilo **3,636,700.06** zikiwa na thamani ya shilingi

**4,687,562,544.21** na mbuzi/kondoo **kilo 274,234.96** zenye thamani ya shilingi **535,552,749.70** zimeuzwa katika nchi za Nigeria na Ghana Pia, jumla ya **kilo 114,800** za ngozi zilizosindikwa za punda zenye thamani ya shilingi **157,201,000** zimeuzwa China na Vietnam**.** (**Kiambatisho Na. 9a).**

**72.** ***Mheshimiwa Spika*,** tathmini inaonesha kuwa uwezo wa uzalishaji wa viatu vya ngozi nchini ni takriban **jozi 1,200,000** kwa mwaka kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 9c** ukilinganisha na mahitaji ya viatu takriban jozi **milioni 54.2** kwa sasa. Kutokana na takwimu hizo uwekezaji mkubwa unahitajika katika tasnia ya ngozi kwa kuwa kuna fursa nyingi. Hata hivyo, tasnia hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

(i) Ubora hafifu wa ngozi ghafi zinazozalishwa nchini;

(ii) Ushindani wa soko la ndani kwa bidhaa za ngozi zinazozalishwa nchini unaotokana na wingi wa uingizwaji wa bidhaa za ngozi zinazozalishwa nje ya nchi kama mitumba na ngozi-ghushi *(synthetic leather);*

(iii) Utoroshwaji wa ngozi ghafi kwenda nje ya nchi kupitia njia zisizo halali;

(iv) Udanganyifu wa thamani halisi ya ngozi ghafi na zilizosindikwa *(Wet Blue)* unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu; na

(v) Uhaba wa wataalam katika sekta ya ngozi hivyo kuathiri usindikaji na ubora wa bidhaa za ngozi.

**73.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019 Wizara kupitia mfuko wa ngozi (LDF) imetekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ngozi (*Leather Sector Development Strategy 2016 - 2020)* kwa kufanya kikao cha wadau **25** wa tasnia ya ngozi kujadili changamoto zinazoikabili tasnia ya ngozi. Pia, Wizara imeendesha mafunzo ya ubora wa ngozi kwa wakaguzi wa ngozi **26** kutoka mikoa yote ya Tanzania bara.

## MATUMIZI YA RASILIMALI ZA ARDHI, MAJI NA MALISHO KWA MIFUGO

**74.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imeandaa mkakati wa upatikanaji wa uhakika wa malisho na maji na inakamilisha maandalizi ya miongozo ya usimamizi wa rasilimali hizo. Aidha, Wizara inaendelea kuhamasisha na kuwezesha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji. Katika mwaka 2018/2019 Wizara inaendelea kukamilisha ujenzi wa bwawa la Mbangala (Songwe), lambo katika Kijiji cha Chamakweza (Bagamoyo) na Visima virefu katika Vijiji vya Mpapa (Manyoni) na Nsolanga-Ismani (Iringa). Pia, Wizara imekamilisha ukarabati wa bwawa la Nyakanga (Butiama) na inaendelea na ukarabati wa lambo katika Kijiji cha Wami -Dakawa (Mvomero) na hivyo kufanya idadi ya mabwawa/ malambo kufikia **1,384** na visima virefu **103.**

**75.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuimarisha upatikanaji wa maji kwa mifugo kwa kufanya ukarabati wa malambo sita (6) katika mikoa ya Manyara, Pwani, Simiyu, Arusha, Geita na Tabora na kuchimba visima virefu 50.

**76.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kuboresha lishe na upatikanaji wa uhakika wa malisho, Wizara inaendelea kutoa elimu kwa wafugaji na wadau wengine kuhusu uzalishaji na uhifadhi wa malisho. Katika mwaka 2018/2019, jumla ya marobota **550,919** ya hei yalizalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali ikilinganishwa na marobota **482,246** yaliyozalishwa mwaka 2017/2018 (**Kiambatisho Na. 10**). Ongezeko hilo la asilimia **14.2** limetokana na uboreshaji wa mashamba.

**77.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019 jumla ya tani **12.1** za mbegu bora za malisho zilizalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali ikilinganishwa na tani **10** zilizozalishwa mwaka 2017/2018. Aidha, jumla ya hekta **730** za mbegu za nyasi na hekta **245** za mbegu za mikunde kutoka mashamba ya TALIRI, LMUs – Sao Hill na Mabuki zimestawishwa;

Mashamba ya Malisho Vikuge na Langwira pia yameimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi. Aidha, wafugaji na wawekezaji wenye mashamba binafsi wamehamasishwa na wamestawisha hekta **197** za nyasi na hekta **35** za mikunde katika mashamba yao. Vilevile, mashamba ya malisho **208** yameendelezwa katika Halmashauri **32**. Katika mwaka 2018/ 2019, mashamba darasa ya malisho **67** yamestawishwa kwa kupanda malisho aina ya nyasi ekari **72,** mikunde ekari **16** na malisho mchanganyiko ekari **48** katika Halmashauri 17 za Mpanda, Nsimbo, Nkasi, Tunduru, Mbarali, Lushoto, Maswa, Itilima, Meatu, Chato, Muleba, Butiama, Bunda, Morogoro, Rungwe, Njombe na Mufindi, ambapo wafugaji **1,756** wamefikiwa na kupatiwa mafunzo.

**78.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za malisho kwa kuimarisha na kupanua mashamba saba **(7**) ya Serikali. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa mbegu bora za malisho na kusimamia urasimishaji wa mbegu aina tano (5) kupitia vituo vya Utafiti na Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu *(Tanzania Official Seed Certification Institute – TOSCI).* Mbegu hizo ni Buffel, Rhodes, Lucerne, Lablab na Blue pea.

**79.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, Wizara ilifanya ukaguzi wa maeneo ya kuzalisha, kuhifadhi na kuuza vyakula vya mifugo ambapo viwanda **22** vilikidhi vigezo na kusajiliwa hivyo kufanya viwanda vilivyosajiliwa kote nchini kuongezeka kutoka **72** mwaka 2017/2018 hadi viwanda **94 (Kiambatisho Na. 11).** Katika kipindi hicho, wakaguzi **15** kutoka Mikoa ya Mwanza, Simiyu na Mara walijengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya ukaguzi wa vyakula vya mifugo. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kusimamia na kudhibiti ubora wa vyakula vya mifugo kwa kufanya ukaguzi wa viwanda, maeneo ya kuuzia na kutoa mafunzo kwa wakaguzi **50** na watengenezaji **20.** Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu uzalishaji na uhifadhi wa vyakula vya mifugo.

**Utatuzi wa Migogoro baina ya Wafugaji na Watumiaji wengine wa Ardhi**

**80.** ***Mheshimiwa Spika*,** migogoro baina ya wafugaji na wakulima, wafugaji na wahifadhi, wafugaji na mashamba ya Serikali na watumiaji wengine wa ardhi imekuwepo kwa muda mrefu katika mikoa mbalimbali hapa nchini. Migogoro hiyo imekuwa ikisababisha madhara mbalimbali ikiwemo vifo vya binadamu na mifugo, uharibifu wa mali na uvunjifu wa amani, wafugaji kukamatwa na wakati mwingine mifugo yao kutaifishwa na kuuzwa. Hadi kufikia Oktoba, 2017 kulikuwa na migogoro **428** iliyowahusisha wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

**81.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutatua migogoro hiyo, Wizara yangu imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(i) Kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Kutafuta Ufumbuzi wa Kudumu wa Migogoro ya Wafugaji na Watumiaji wengine wa Ardhi,

(ii) Kuunda timu ya Wataalam kutoka OR-TAMISEMI; OR – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Wizara za Mambo ya Ndani; Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na Chama cha Wafugaji Tanzania kwa lengo la kutatua migogoro katika mikoa mbalimbali nchini. Timu ilifanya kazi katika Mikoa mitano (5) katika Wilaya za Uvinza, Kasulu na Kibondo (Kigoma); Tanganyika na Mlele (Katavi); Kalambo, Nkasi na Sumbawanga (Rukwa); Chunya na Mbarali (Mbeya); na Mkuranga, Kibiti, Rufiji na Kisarawe (Pwani), ambapo migogoro **27** kati ya **43** sawa na asilimia **59.26** ilitatuliwa. Kazi hii inaendelea katika maeneo mengine yaliyobainika kuwa na migogoro.

(iii) Kutafuta na kuainisha maeneo kwa ajili ya malisho ya mifugo ambapo Wizara imetenga jumla ya hekta **350,576.05 (Kiambatisho Na. 12)** kutoka katika maeneo yake ya vituo vya kupumzishia mifugo, Ranchi za Taifa, Mashamba ya TALIRI na Mashamba ya Kuzalisha Mifugo (LMUs) ili

yatumiwe na wafugaji kwa utaratibu maalum. Pia, Halmashauri tano (**5**) za Tunduru, Mpanda, Biharamulo, Muleba na Kyerwa zimetenga jumla ya hekta **199,827.3 (Kiambatisho Na. 13)** kwa ajili ya malisho ya mifugo na hivyo kupunguza migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini.

(iv) Wizara pia imeanzisha Kurugenzi kwa lengo la kuendeleza na kusimamia maeneo ya malisho, vyanzo vya maji kwa mifugo na rasilimali za vyakula vya mifugo na hivyo kusaidia katika utatuzi wa migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa Ardhi.

**82.** ***Mheshimiwa Spika****,* Wizara yangu inatoa shukrani za dhati kwa **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Agizo alilolitoa tarehe 15 Januari, 2019 kwa Mawaziri nane (8). Agizo hilo lilihusisha OR – TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mifugo na Uvuvi; Kilimo; Maliasili na Utalii; Maji; na Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kushirikiana kwa pamoja kufuatilia migogoro iliyopo na kuitafutia ufumbuzi.

**83.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imeendelea kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Asasi zisizo za Kiserikali kwa kutoa elimu ya uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Wizara kupitia mradi wa Usimamizi Endelevu wa Nyanda za Malisho *(Sustainable Range Management Project-SRMP)* imetenga hekta **172,218.87** za maeneo ya malisho ya pamoja *(Joint Village Land Use Plans)* katika Halmashauri za Chemba, Kiteto na Chalinze. Aidha, katika Mwaka 2018/2019 jumla ya Vijiji **42** vimetenga hekta **80,823.26** kwa ajili ya malisho katika Wilaya **9 (Kiambatisho Na. 14).** Hadi sasa Vijiji **1,852** vimeandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kati ya Vijiji **12,545** vilivyopo nchini ambapo maeneo ya malisho hekta **2,788,901.17** yametengwa kwa ajili ya ufugaji katika Mikoa **22.**

**84.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, wadau na Mamlaka nyingine za Serikali kuendelea kutenga na kupima maeneo ya malisho. Pia, itaandaa miongozo ya utumiaji na usimamizi wa maeneo hayo.

## UDHIBITI WA MAGONJWA YA MIFUGO

**85.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara iliandaa na kuanza kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti Magonjwa ya Mifugo, Matumizi ya Dawa, Chanjo na Viuatilifu vya Mifugo nchini. Ili kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe nchini Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutoa elimu na hamasa. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili 2019, jumla ya michovyo **40,352,228** imefanyika. Kati ya michovyo hiyo, ng'ombe ni **22,400,170**, Mbuzi ni **12,836,389** na Kondoo ni **5,115,669**. Ili kuchochea zoezi la uogeshaji nchini Wizara ilitoa dawa lita **8,823.53 aina ya Paranex (Alphacypermethrin) yenye thamani ya shilingi 300,000,000 na kuzigawa katika majosho 1,486** yanayofanya kazi katika Mikoa **24**. Vilevile, ili kudhibiti ubora wa dawa za kuogeshea nchini Wizara kupitia TVLA imenunua kifaa cha kupima ubora wa dawa ya kuogeshea mifugo (HPLC) kwa shilingi **120,000,000.** Katika Mwaka 2019/2020 Wizara **itaendelea kuhamasisha uogeshaji na kutoa dawa ya kuogesha mifugo kwa majosho yote yatakayokuwa yanafanya kazi kila baada ya miezi sita.**

**86.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019 Wizara inakarabati majosho **161** kwa gharama ya shilingi **235,113,200** katika mikoa 21 nchini **(Kiambatisho Na.15a)**. Aidha, Wizara imehamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kukarabati majosho ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 jumla ya majosho **151** yalikuwa yamekarabatiwa. Pia, Wizara inazitaka Halmashauri zote nchini kutekeleza **Agizo la Chato** la kukarabati majosho yote nchini ifikapo mwezi Juni, 2019. Halmashauri zote nchini ambazo hazitatekeleza agizo hili zitanyang'anywa mamlaka ya kukusanya mapato yatokanayo na mifugo na mazao yake (**Kiambatisho Na. 15b)**.

Vilevile, jumla ya Kamati **847** za kusimamia majosho zimeundwa na kufungua akaunti za uendeshaji **(Kiambatisho Na.15c**). Katika mwaka 2019/2020 Wizara itaendelea kuhamasisha uogeshaji na kutoa dawa yenye ruzuku ya kuogesha mifugo kwa majosho yote yatakayokuwa yanafanya kazi kila baada ya miezi sita **(6)** kuanzia Desemba, 2018.

**87.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa kutokomeza magonjwa mbalimbali yenye athari kijamii na kiuchumi. Magonjwa hayo ni pamoja na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo, Homa ya Mapafu ya Ng'ombe, Mafua Makali ya Ndege, Mdondo, Homa ya Nguruwe, Chambavu, magonjwa yaenezwayo na Kupe (Ndigana Kali, Ndigana Baridi, Maji Moyo na Mkojo Mwekundu), Kimeta, Ugonjwa wa Kutupa Mimba na ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa. Aidha, kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, Sekta binafsi na Washirika wa Maendeleo Wizara inahamasisha na kutekeleza uchanjaji wa mifugo. Kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 jumla ya ng'ombe **milioni 3.9 (9.6%),** mbuzi **milioni 2.3 (7.8%)** na mbwa **milioni 0.3 (7.5%)** wamechanjwa dhidi ya magonjwa mbalimbali. Vilevile, dozi **milioni 46.9 (41.7%)** zilitolewa kwa kuku wa asili dhidi ya mdondo na kuku wa kisasa dozi **milioni 121.8** dhidi ya Mdondo, **milioni 75 (57%)** Gumboro na **milioni 1.8 (100%)** Mareks **(Kiambatisho Na.**16). Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuhamasisha, kuratibu na kusimamia uchanjaji wa mifugo dhidi ya magonjwa mbalimbali.

**88.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Washirika wa Maendeleo imeendelea kutekeleza Mikakati ya kutokomeza magonjwa yanayoambukiza binadamu kutoka kwa wanyama kwa dhana ya Afya Moja. Magonjwa hayo ni pamoja na Malale, Mafua Makali ya Ndege, Kimeta, Ugonjwa wa Kutupa Mimba, Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa na Homa ya Bonde la Ufa. Aidha, kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, Sekta binafsi na Washirika wa Maendeleo Wizara inahamasisha na kutekeleza uchanjaji wa mifugo.

**89.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaweka utaratibu wa manunuzi ya pamoja ya chanjo pamoja na dawa za kuogesha mifugo ili kupunguza gharama za manunuzi. Pia, itakijengea uwezo Kiwanda cha Chanjo za Mifugo cha Serikali kilichopo Kibaha (Tanzania Vaccine Institute - TVI) ili kiweze kuzalisha aina saba **(7)** za chanjo za magonjwa kutoka aina tano **(5)** za chanjo zinazozalishwa. Aina saba za chanjo ni pamoja na M*dondo (New Casttle Disease)*, Kimeta *(Anthrax)*, Chambavu *(Black Quarter),* Ugonjwa wa Kutupa Mimba *(Brucellosis)*, Homa ya Mapafu ya Ng'ombe *(CBPP),* Homa ya Mapafu ya Mbuzi *(CCPP)* na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo *(PPR).* Vilevile, Wizara itaendelea kusimamia na kufuatilia Usalama wa Chakula ili kulinda afya za walaji wa mazao ya mifugo na kukuza biashara ya mazao ya mifugo Kimataifa. Aidha, ili kurahisisha biashara hii, Wizara imekusudia kutengeneza mfumo wa kuomba vibali kwa njia ya kielektroniki na kuhuisha Sheria na Kanuni za ukaguzi na usafirishaji wa mifugo na mazao yake nchini na nje ya nchi.

**90.** ***Mheshimiwa Spika****,* Wizara kupitia Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) imezalisha dozi **39,548,000** za chanjo za magonjwa ya mifugo kati ya lengo la kuzalisha dozi **100,000,000** kwa mwaka ikilinganishwa na dozi **28,427,100** zilizozalishwa na kusambazwa mwaka 2017/2018. Kati ya dozi hizo, **38,245,800** ni za Mdondo ($1_2$), **1,114,850** ni za Kimeta na **187,850** ni za Chambavu ambapo zote zimesambazwa kupitia vituo saba (**7)** vya TVLA katika kanda ambapo Halmashauri tatu **(3)** za Mkalama, Kondoa na Longido na wasambazaji binafsi **599** wananunua katika vituo hivyo na kuwahudumia wafugaji. Kiwango cha chanjo zilizoagizwa kutoka nje ya nchi ni dozi **26,840,000** za Homa ya Mapafu ya ngómbe (CBPP), dozi **182,000** za Homa ya mapafu ya mbuzi (CCPP), dozi **1,074,230** za Kichaa cha Mbwa (Rabies), dozi **122,505,000** za Mdondo, dozi **2,500** za Kutupa mimba (Brucellosis), dozi **457,000** za Sotoka ya Mbuzi (PPR), dozi **103,984,500** za *Gumboro* na dozi **7,000,000** za *Mareks.*

**91.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara kupitia Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) imeanza usajili wa chanjo

mchanganyiko wa Kimeta na Chambavu (TECOBLAX) baada ya kufaulu vipimo vya ubora kutoka Maabara ya PANVAC Ethiopia. Aidha, majaribio ya chanjo ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP) yamekamilka na sampuli za chanjo zimepelekwa PANVAC kwa ajili ya kupimwa ubora ili hatimaye chanjo hii isajiliwe na ianze kuzalishwa. Pia, maandalizi ya kutengeneza chanjo ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Mbuzi (CCPP) na Ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi (PPR) ikiwa ni pamoja na kufundisha wataalam na kununua vifaa yameanza. Lengo ni kuanza kufanya majaribio ya uzalishaji wa chanjo hizo ifikapo mwezi Mei, 2019. Vilevile, ujenzi wa jengo la kuzalisha chanjo za Bakteria unaendelea katika kituo cha kuzalisha chanjo cha Kibaha (TVI) ambapo umekamilika kwa asilimia **45.**

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia TVLA imefanya uchunguzi wa sampuli **8,016** kutoka kwa mifugo**.** Uchunguzi wa sampuli hizo ulibaini uwepo wa magonjwa ya Kimeta, Ndigana Kali, Ndigana Baridi, Homa ya Nguruwe, Mdondo, Gumboro, na Homa ya Mapafu ya Ng'ombe**.** Aidha, jumla ya sampuli **2,861** za vyakula vya mifugo na malighafi zilifanyiwa uchambuzi ambapo asilimia **75** ya sampuli hizo zilionekana kuwa na ubora unaotakiwa. Pia, Wafugaji na watengenezaji wa vyakula vya mifugo walipewa ushauri wa namna ya kudhibiti magonjwa na kuboresha vyakula vya mifugo. Vilevile, Wizara kupitia TVLA imeendelea kufanya tafiti za namna ya kudhibiti magonjwa na teknolojia za kuangamiza mbun'go waenezao magonjwa ya Nagana na Malale.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, TVLA inapanga kuzalisha dozi **milioni 111** za chanjo za mifugo ikiwa ni pamoja na dozi **100,000,000** za chanjo ya Mdondo ya TEMEVAC I2; 5,000,000 za chanjo ya CBPP; **3,000,000** za chanjo ya Kimeta na **3,000,000** za chanjo ya Chambavu. Aidha, Wakala inapanga kuanza majaribio ya kuzalisha chanjo dhidi ya ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (CCPP), chanjo dhidi ya Kichaa cha Mbwa na Chanjo ya Mapele Ngozi (LSD).

## UTAFITI, MAFUNZO NA UGANI WA MIFUGO

### Utafiti wa Mifugo

**94.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) imefanya tafiti nane (**8)** vituoni na kwa wafugaji. Tafiti hizo zimefanyika katika Mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mwanza, Simiyu, Dodoma, Pwani, Morogoro, Singida, Lindi Mtwara na Kigoma kwa lengo la kuboresha mbari za ng'ombe wa maziwa na nyama, kuku, mbuzi na kondoo, uzalishaji wa punda, malisho bora na vyakula vya mifugo. Aidha, utaratibu wa ununuzi wa vifaa vya maabara ya viinitete iliyopo TALIRI Mpwapwa vyenye thamani ya shilingi **milioni 189** kupitia Mradi wa Uhawilishaji wa Viinitete *Multiple Ovulation and Embryo Transfer, (MOET*) unaofadhiliwa na Serikali ya Tanzania kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) unaendelea. Manufaa ya teknolojia hii ni:-

(i) Kuwezesha ng'ombe jike kuzalisha viinitete **8** mpaka **450** kwa mwaka;

(ii) Kuzalisha, kuhifadhi na kufungasha viinitete kwa ajili ya uhimilishaji na uhawilishaji; na

(iii) Kuongeza kasi ya uzalishaji wa mifugo nchini hasa mitamba na madume kwa ajili ya maziwa na nyama (ndama **50** kwa mwaka kwa ng'ombe mmoja).

**95.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia TALIRI, kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), imeendelea kufanya ufuatiliaji wa tija ya ng'ombe wa maziwa ambapo Halmashauri **24** nchini zimeendelea kutekeleza Mradi wa Kuboresha Mbari za Ng'ombe wa Maziwa (*African Dairy Genetic Gain, ADGG*). Halmashauri hizo ni Tanga Jiji, Muheza, Korogwe Mji, Moshi, Rombo, Hai, Siha, Arusha Jiji, Meru, Arusha, Iringa Manispaa, Mufindi, Mafinga Mji, Njombe Mji, Makambako Mji, Mbeya Jiji, Mbeya, Mbozi, Iringa, Rungwe, Lushoto na Bumbuli. Kupitia mradi huu,

wafugaji **8,347** wamepata elimu ya ufugaji bora na wanatembelewa kila mwezi. **(Kiambatisho Na. 17).**

**96.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Wizara kupitia TALIRI kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la PASS trust (*Private Agricultural Sector Support*) imeanzisha mkakati wa kuwajengea uwezo vijana na kuwavutia kuingia katika ufugaji wa kibiashara. Aidha, ujenzi wa miundombinu yenye uwezo wa kuweka mbuzi **4,000** kwa ajili ya kunenepesha kwa mwaka umekamilika. Pia, mradi huu utawajengea uwezo vijana **20** kwa mwaka kufuga kibiashara.

**97.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia TALIRI kwa kushirikiana na mradi wa Kuboresha Mbari za Kuku (*African Chicken Genetic Gain, ACGG*), ilisambaza kuku **468** na mayai **720** kwa wafugaji **1,801**. TALIRI kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo katika maeneo k*ame (International Centre for Agricultural Research in Dry land Areas, ICARDA*) imeendelea kuimarisha tafiti za kuainisha vinasaba vya kuongeza uzalishaji wa nyama katika mbuzi wa asili kwa kuimarisha maabara ya uhimilishaji wa mbuzi katika Kituo cha West Kilimanjaro. Aidha, Mafunzo ya uhimilishaji wa mbuzi kwa wataalamu 18 yametolewa. Vilevile, kupitia Mpango wa Huduma za Jamii na Uhusiano (*Corporate Social Responsibility*) TALIRI ilisambaza teknolojia mbalimbali **27** katika Halmashauri **41** nchini na kuwafikia wadau **23,659** wakiwemo wataalam wa ugani **127**, wanafunzi **346** wa vyuo vya LITA, SUA, Visele na MATI; na wafugaji **23,186** walioko vijiji vya jirani na vituo vya TALIRI kupitia semina za mafunzo.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia TALIRI itaendelea kuibua, kutathmini na kuendeleza utafiti wa mifugo na malisho ikiwa ni pamoja na kuendeleza kosaafu bora za mifugo ili kuongeza tija katika uzalishaji wa maziwa, nyama, mayai na ngozi kuendana na mnyororo wa thamani na uchumi wa viwanda. Aidha, miundombinu ya mashamba ya Utafiti katika vituo saba **(7)** ikiwemo ujenzi wa Makao Makuu ya TALIRI utafanyika. Pia, uzalishaji wa mbuzi wa nyama na maziwa kupitia uhimilishaji hadi kufikia mbuzi **1,500** na unenepeshaji wa mbuzi **4,000** kwa kushirikiana na

PASS utafanyika. Vilevile, TALIRI itashirikiana na Kiwanda cha Maziwa cha Tanga Fresh kuzalisha malisho kwa njia ya umwagiliaji. Aidha, TALIRI ina upungufu wa watumishi **221** ambapo katika Mwaka 2019/2020, imeomba ajira ya watumishi **74** ili kukabiliana na upungufu mkubwa wa Rasilimali Watu.

**Mafunzo ya Mifugo**

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (Livestock Training Agency – LITA) imefanya udahili wa wanachuo **2,536.** Aidha, wanafunzi **580** kutoka vyuo vya Serikali na **398** kutoka vyuo binafsi wanatarajia kuhitimu mafunzo ya Stashahada na Astashahada mwezi Juni, 2019. Vilevile, wafugaji **156** walipatiwa mafunzo katika Kampasi za Wakala juu ya uzalishaji bora wa mifugo na malisho. Pia, Wizara kupitia LITA kwa ushirikiano na Wizara ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Poland imekarabati mabweni manne **(4)** na Kiwanda kidogo cha kusindika maziwa katika Kampasi ya Tengeru. Aidha, jumla ya mitamba **15** ya maziwa yenye thamani ya Shilingi **22,000,000** imenunuliwa kwa ajili ya Kampasi ya Madaba ili kuongeza uzalishaji wa maziwa na mafunzo. Katika Mwaka 2019/2020 LITA imeomba ajira ya watumishi **239** ili kukabiliana na upungufu mkubwa wa Rasilimali Watu.

**Huduma za Ugani wa Mifugo**

**100.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na sekta binafsi ilitoa elimu kwa Maafisa Ugani na **wafugaji 19,839** kupitia mafunzo rejea, ziara za mafunzo, mikutano ya uhamasishaji na semina zilizoendeshwa wakati wa maonesho ya Nanenane, Sabasaba na Siku ya Chakula Duniani. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa wadau juu ya ufugaji bora kwa njia ya vitabu **9,396**, vipeperushi **29,350**, mabango **1,850**, vipindi **52** vya redio na 12 runinga.

**101.** ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za Wizara kutekeleza mikakati yake, ilibainisha uhitaji mkubwa wa maarifa na stadi mpya za ufugaji bora kwa wataalam na wafugaji nchini ili

kuongeza na kuboresha uzalishaji wa mazao ya mifugo sambamba na falsafa ya uchumi wa viwanda nchini. Wizara imeanza kutoa Mafunzo Rejea kwa Wafugaji na Maafisa Ugani kutoka katika Halmashauri **185** nchini. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wataalam walioko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuamsha ari ya uwajibikaji na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma bora za ugani kwa wafugaji.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo hayo pia yanalenga kuwaongezea wafugaji maarifa kwa kuwapatia teknolojia mpya ili kuhamasisha Ufugaji wa Kisasa na Kibiashara nchini. Mpango huu unalenga kuongeza uzalishaji wa malighafi zitokanazo na mifugo zenye viwango bora ili kukidhi mahitaji ya Viwanda vya nyama, maziwa na ngozi vinavyoendelea kujengwa nchini. Mafunzo haya yalizinduliwa mwezi Aprili, 2019 katika Wilaya za Simanjiro na Kaliua ambapo wafugaji **1,840** na Maafisa ugani **65** walipatiwa mafunzo na hivi sasa mafunzo yanaendelea nchi nzima.

**103.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma za ugani na kusambaza teknolojia sahihi za ufugaji bora kupitia mashamba darasa, mafunzo rejea, pamoja na maonesho ya Nanenane, Sabasaba na Siku ya Chakula duniani. Aidha, Wizara itatoa mafunzo rejea ya ufugaji wa Kisasa na Kibiashara kwa Maafisa Ugani **1,500** na Wafugaji **80,000** kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Pia, Wizara itaanzisha na kusimamia mashamba darasa **90** ya malisho katika Halmashauri **30** nchini. Vilevile, Wizara itaendelea kuhamasisha wafugaji kuanzisha na kusimamia vyama vya ushirika vya wafugaji ili kuwa na sauti moja na kutetea haki zao.

### Usimamizi wa Uzalishaji wa Mazao ya Mifugo Bodi ya Maziwa

**104.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa imefanya Ukaguzi katika Mikoa ya

Songwe, Tanga, Mbeya, Morogoro na Dar es Salaam. Ukaguzi umefanyika katika vituo **42** vya kukusanyia maziwa, viwanda **20** vya kusindika maziwa, Vioski vya maziwa **19** na maghala **12** ya kuhifadhi maziwa kutoka nje ya nchi. Aidha, Bodi imesajili wadau wapya 63 (wazalishaji wa maziwa **25**, wakala wa masoko **23**, waingizaji maziwa kutoka nje ya nchi **7** na wasindikaji wa maziwa **8**). Wadau hao ni kutoka katika Mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa, Pwani, Kilimanjaro, Shinyanga, Arusha,Tanga, Dodoma na Dar es Salaam. Pia, Bodi imefanya marekebisho ya Kanuni za Maziwa chini ya usimamizi wa Wizara ili kuongeza ufanisi na kuondoa muingiliano wa Kisheria na Kanuni na Taasisi za Serikali zinazosimamia tasnia ya maziwa.

**105. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Bodi ya Maziwa, imetoa mafunzo kwa wadau 148 katika Mikoa ya Mbeya, Songwe, Morogoro, Tanga na Dar es Salaam yaliyohusisha wazalishaji **88**, wakusanyaji na wasafirishaji **56** na wasindikaji wanne (**4**) wa maziwa. Pia, kwa kipindi cha Julai 2018 hadi Machi, 2019, Bodi ya Maziwa imetoa vibali **692** na kuingiza maziwa lita **18,617,659.07** zenye thamani ya shilingi **26,224,025,033.80** ikilinganishwa na maziwa lita **20,920,537.59** zenye thamani ya shilingi **30,290,485,222** zilizoingizwa kipindi kama hiki kwa mwaka 2017/2018 sawa na upungufu wa asilimia 11.01. Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa imeendelea kuimarisha vyama vya ushirika **18** vya maziwa katika Mikoa ya Tanga, Morogoro, Pwani, Mbeya na Dar es Salaam kwa lengo la kuvijengea uwezo wa ukusanyaji maziwa ili kuongeza upatikanaji wa maziwa kwenye viwanda vilivyopo.

**106. *Mheshimiwa*** Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa itaendelea kuimarisha na kuongeza vituo **50** vya kukusanyia maziwa katika maeneo yanayozalisha maziwa mengi katika Mikoa ya Geita (Bukombe na Chato); Iringa (Mufindi na Mafinga); Mara (Bunda); Mbeya (Rungwe na Busokelo); Morogoro (Mvomero); Njombe (Makete na Ludewa); Pwani (Chalinze na Mkuranga); Rukwa (Kalambo); Ruvuma (Mbinga na Madaba); Simiyu (Meatu); Shinyanga (Kahama) na Tanga

(Kilindi). Aidha, kituo cha kukusanyia maziwa cha mfano kinatarajiwa kujengwa Mkuranga na Bodi ya maziwa itasimamia ujenzi wa mabanda bora kwa wafugaji watakaokopeshwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB).

## Bodi ya Nyama

**107.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Bodi ya Nyama imetambua na kusajili wadau **179** kutoka katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kagera, Dodoma, Mwanza, Lindi, Kilimanjaro na Arusha. Pia, minada tisa (**9**) ya mifugo kutoka katika Mkoa wa Singida imetambuliwa na kusajiliwa. Aidha, watumishi **12** wa Bodi wamepewa mafunzo ya kutumia mfumo wa usajili na kutafuta masoko kielektroniki ambapo taarifa za usajili za wadau **404** kutoka Mikoa ya Dar es Salaam (**137**), Iringa (**57**), Morogoro (**31**), Singida (**142**), Tabora **(7)** na Mtwara (**1**) zimeingizwa kwenye mfumo huo. Vilevile, Wizara kupitia Bodi imeendelea kutoa mafunzo ya kutumia mfumo wa usajili na kutafuta masoko kielektroniki katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ambapo wadau **50** walipatiwa mafunzo. Aidha, machinjio/viwanda **15**, Karo **25** na Bucha **203** katika Mikoa ya Dodoma (Dodoma Jiji, Dodoma MC na Chamwino); Arusha (Arusha Jiji na Arusha DC); Mwanza (Mwanza Jiji, Ilemela na Magu); Shinyanga (Shinyanga MC) na Kilimanjaro (Moshi MC) zimekaguliwa na wamiliki wamehamasishwa kuboresha miundombinu.

**108.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Nyama itatoa mafunzo ya kutumia mfumo wa usajili wa wadau kielektroniki kwa watumishi **52** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Mara na Mwanza. Aidha, mafunzo ya uzalishaji na uuzaji wa nyama kwa kuzingatia taratibu za usafi yatatolewa kwa wadau wa tasnia ya nyama **150** kutoka Mikoa ya Simiyu, Singida, Manyara, Tabora, Songwe na Njombe. Pia, mafunzo ya Kilimo Biashara na teknolojia ya uzalishaji wa mifugo kwa wafugaji **180** wa ng'ombe, mbuzi, nguruwe, kuku, kondoo na punda yatatolewa. Vilevile, wadau **1,000** wa tasnia ya nyama na vyama vyao watatambuliwa na kusajiliwa.

## Usimamizi wa Viwango vya Huduma ya Afya ya Mifugo na Maadili ya Wataalam

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Baraza la Veterinari imefanya ukaguzi katika Mikoa **24**. Katika ukaguzi huo vituo vya kutoa huduma ya afya ya mifugo **800** vilikaguliwa**.** Aidha, Baraza lilifanya kaguzi katika minada minane **(8)** ya mifugo ambapo wauzaji holela **21** wa dawa za mifugo walikamatwa, kutozwa faini kwa mujibu wa Sheria na kupewa elimu ya namna bora ya utoaji wa huduma ya afya ya mifugo. Pia, Baraza limesajili madaktari wa mifugo 42 kati ya madaktari **60** waliotarajiwa kusajiliwa. Idadi ya madaktari wa mifugo waliosajiliwa sasa imefikia **900.** Vilevile, wataalam wasaidizi wa afya ya mifugo **337** wenye Stashahada na Astashahada waliandikishwa na kuorodheshwa katika kipindi hicho na kufanya idadi ya wataalam wasaidizi walioandikishwa na kuorodheshwa kufikia **3,218.**

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Baraza la Veterinari imetoa leseni za kutoa huduma kwa wakaguzi wa nyama **54,** wataalam wa maabara za veterinari watano **(5)** na wahimilishaji tisa **(9)**. Aidha, vituo **111** vya kutolea huduma ya afya ya mifugo vimesajiliwa kati ya vituo **400** vinavyotarajiwa kusajiliwa hadi kufikia mwezi Juni, 2019. Pia, vyuo vitatu **(3)** vya kutolea mafunzo ya mifugo vya *Tanzania Research and Career Development Institute* (*TRACDI*), Dodoma; *Institute of Development and Entrepreneurship Studies* (DIDES), Dodoma na *Mahinya College of Sustainable Agriculture* (Ruvuma) vilikaguliwa kwa lengo la kutambuliwa. Hata hivyo, vyuo hivyo vimetakiwa kukamilisha taratibu kabla ya kutambuliwa.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Baraza la Veterinari itasajili madaktari wa mifugo **70,** vituo vya huduma za mifugo **400,** kuorodhesha wataalam wasaidizi **500** na kuandikisha wasaidizi wa wataalam 5**00.** Aidha, Baraza litatoa leseni kwa wakaguzi wa nyama, wahimilishaji na wataalam wa maabara za veterinari **210** na litafanya ukaguzi wa maadili na viwango vya utoaji huduma

kwa kushirikiana na Halmashauri **185** nchini. Pia, Baraza kwa kushirikiana na Baraza la Veterinari la Afrika Kusini na Shirika la Afya ya Wanyama Ulimwenguni litaendelea na mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji wake katika kusimamia utoaji wa huduma ya afya ya mifugo nchini. Vilevile, kwa kushirikiana na Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Jamii ya Chuo Kikuu cha Sokoine Cha Kilimo, Baraza litatoa mafunzo ya kujiendeleza ya miezi mitatu **(3**) kwa watoa huduma wa afya ya mifugo **300.**

## UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MIFUGO

**112.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, Serikali kupitia Wizara imeweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji katika ujenzi wa viwanda vya utengenezaji wa chanjo na uchakataji wa mifugo na mazao yake nchini. Uwekezaji huo umefanywa katika miradi ifuatayo:-

(i) Ujenzi wa jengo la kuzalishia chanjo za aina ya bakteria katika Kiwanda cha Serikali cha uzalishaji Chanjo cha Kibaha (TVI). Gharama ya jengo hilo ni shilingi **milioni 667**. Jengo hilo linatarajia kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2019.

(ii) Ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kuzalisha chanjo za mifugo cha *Hester Bioscience Africa Limited* cha Kibaha. Kiwanda hicho kitazalisha chanjo 27 zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Gharama za uwekezaji wa Kiwanda hicho ni **Dola za Marekani milioni 18** sawa na shilingi **bilioni 41**. Kiwanda hiki kinatarajiwa kuanza kuzalisha chanjo ifikapo Februari 2020.

(iii) Kiwanja cha TAN CHOICE (Kibaha-Pwani) chenye uwezo wa kuchakata ngómbe **1,000** na mbuzi/kondoo **4,500** kwa siku na uwekezaji wake ni **Dola za Marekani milioni 5.5** sawa na shilingi **bilioni 12.5** na kinatarajiwa kuanza kazi mwezi Septemba, 2019. Kiwanda hicho pia kinatarajia kutoa ajira zaidi ya wafanyakazi 500.

(iv) Kiwanda cha *Elia Food and Overseas Ltd* (Longido) chenye uwezo wa kuchakata ng'ombe **400** na mbuzi/kondoo **2,000** kwa siku ujenzi wake ni Dola za Marekani **milioni 5** sawa

na shilingi **bilioni 11.3** kitaanza kufanya kazi mwezi Septemba, 2019. Kiwanda hicho kinategemea kutoa ajira zaidi ya wafanyakazi 200.

(v) Kiwanda cha *Galaxy Food and Beverage Limited* (Jijini Arusha) cha kusindika maziwa, kina uwezo wa kusindika lita **75,000** kwa siku na kimeajiri jumla ya wafanyakazi 30 kwa kuanzia. Gharama za uwekezaji wa kiwanda hicho ni Dola za Marekani **milioni 2.5** sawa na shilingi **bilioni 5.7.** Kiwanda hicho tayari kimeshaanza kuzalisha maziwa (Kilimanjaro Fresh) kwa kiwango cha *UHT* tangu mwezi Machi, 2019.

(vi) Viwanda vya nyama vya SAAFI (Rukwa), Tanganyika Parkers (Shinyanga na Mbeya) na Kiwanda cha maziwa cha Utegi na Musoma Dairy. Serikali inatafuta Wawekezaji mahiri wa kuvifufua na kuviendesha viwanda hivyo.

**113.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia NARCO imesaini Hati ya Makubaliano ya utekelezaji wa Mradi wa *Integrated Rural Development Project (IRDP)* katika Ranchi ya Ruvu na Kampuni ya *National Egyptian Company for Africa Investment (NECAI)* kwa ajili ya uwekezaji mkubwa utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 50** sawa na shilingi za Tanzania **bilioni 111**. Mradi wa ujenzi wa machinjio kubwa na ya kisasa utaweza kuchinja ng'ombe **1,500** na mbuzi/ kondoo **4,500** kwa shifti moja ya saa nane. Viwanda vingine vitakavyojengwa kwenye mnyororo mzima wa mifugo ni pamoja na Kiwanda cha Ngozi kitakachoweza kusindika ngozi hadi kupata bidhaa zake.

**114.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Jamii wa PSSSF imepanua Kiwanda cha kuzalisha bidhaa za ngozi cha Gereza la Karanga ili kiweze kuongeza uzalishaji kutoka jozi **150** hadi kufikia jozi **400** za viatu kwa siku. Uboreshaji huu umekamilika mwezi Septemba, 2018 na kiwanda kimeanza kufanya kazi.

**115.** ***Mheshimiwa Spika*,** uwekezaji huu utaondoa changamoto zilizopo hivi sasa za wafugaji kutangatanga kutafuta masoko ya mifugo, kukosa bei nzuri, kupoteza fedha

nyingi za kigeni kuagiza mazao ya mifugo kutoka nje ya nchi, kupoteza ajira na mapato ya Serikali. Katika mwaka 2019/20 Wizara itaendelea kuhamasisha na kusimamia uwekezaji katika Sekta ya Mifugo kwa kuendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji nchini.

## C: SEKTA YA UVUVI

### HALI YA SEKTA YA UVUVI

**116.** ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Uvuvi ni miongoni mwa sekta za kiuchumi ambazo ni muhimu katika kuondoa umasikini na kukuza uchumi wa Taifa kwa ujumla. Sekta hii ina mchango mkubwa katika kuwapatia wananchi ajira, chakula, lishe, kipato na fedha za kigeni. Katika mwaka 2018, Sekta ya Uvuvi ilichangia asilimia **1.71** katika pato la Taifa na imekua kwa asilimia **9.2.**

**117.** ***Mheshimiwa Spika*,** zaidi ya watanzania **milioni 4.5** wameendelea kupata kipato cha kila siku kutokana na shughuli zinazohusiana na Sekta ya Uvuvi ikiwemo kuunda na kutengeneza boti, kushona nyavu, ukuzaji viumbe maji, biashara ya samaki na mazao yake na mama lishe. Kwa upande wa lishe, samaki huchangia takriban asilimia **30** ya protini inayotokana na wanyama. Aidha, ulaji wa samaki kwa sasa katika nchi yetu kwa mtu kwa mwaka ni kilo **8.2** ikilinganishwa na kilo **20.3** zinazopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO, 2018), hali hii inaonesha bado kuna uhitaji mkubwa wa kitoweo aina ya samaki.

**118.** ***Mheshimiwa Spika*,** taarifa za tafiti zilizofanyika kwa vipindi tofauti katika mwaka 2018/2019 zinaonesha kwamba, kiasi cha samaki kilichopo katika maji yetu ni tani **2,803,000** kwa mtawanyiko ufuatao: Ziwa Victoria tani **2,210,000**, Ziwa Tanganyika tani **295,000** na Ziwa Nyasa tani **168,000**, Maji madogo (maziwa madogo ya kati, mito na mabwawa) tani **30,000** na Maji ya Kitaifa ya Bahari ya Hindi tani **100,000** (**Kiambatisho Na. 18**).

**119.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, jumla ya wavuvi **202,053** wanaotumia vyombo vya uvuvi **58,930** walishiriki moja kwa moja kwenye shughuli za uvuvi. Nguvu hii ya uvuvi iliwezesha kuvunwa kwa tani **389,459.40** za samaki zenye thamani ya shilingi **trilioni 1.83.** Kati ya tani zilizovunwa katika mwaka 2018/2019, tani **333,782.32** (asilimia **85.70)** ni kutoka maji baridi na tani **55,677.08** (asilimia **14.30)** ni kutoka maji bahari (**Kiambatisho Na. 19).**

**120.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, wakuzaji viumbe maji **26,474** walishiriki moja kwa moja kwenye shughuli za ukuzaji viumbe maji na kuzalisha jumla ya tani **18,073.6**. Kati ya tani hizo, tani **16,288** ni za samaki, tani **336.4** ni za kambamiti, tani **1,449** ni za mwani na tani **0.2** ni za kaa pamoja na vipande **395** vya lulu. Aidha, jumla ya vifaranga vya samaki **17,301,076** vilizalishwa.

**121.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Sekta ya Uvuvi imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi, ukosefu na uchakavu wa miundombinu ya uvuvi, uwekezaji mdogo katika uvuvi wa Bahari Kuu, Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 kutokidhi mahitaji ya sasa, upatikanaji wa vifaranga na vyakula vya samaki vyenye ubora, uhaba wa wataalam katika ngazi mbalimbali za utumishi na upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

**122.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kukabiliana na changamoto hizi Wizara imeandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo: mapitio ya Sheria ya Uvuvi na kuandaa Sheria mpya ya kuendeleza Ukuzaji viumbe Maji; Mkakati wa Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi Nchini; Mkakati wa Kujenga na Kuboresha Miundombinu ya Uvuvi; Mkakati wa Kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO 2018); Mkakati wa kuendeleza tasnia ya ukuzaji viumbe maji; Mkakati wa Kusimamia Samaki aina ya Jodari; na Kuanzishwa kwa Dawati la Sekta Binafsi; Mpango wa Usimamizi wa Samaki wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji, Usimamizi wa Uvuvi wa Kambamiti; na kusimamia rasilimali ya Pweza. Pia,

Wizara inafanya mapitio ya Mpango Kabambe wa usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi Tanzania (Tanzania Fisheries Master Plan).


## MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/2019

### Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2018/2019

**123.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara kupitia sekta ya uvuvi ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi **21,534,305,600.00**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 kiasi cha shilingi **30,330,063,743.25** sawa na asilimia **140.8** ya lengo zilikuwa zimekusanywa kutoka Sekta ya Uvuvi.

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** fedha hizi zimekusanywa kutoka vyanzo vifuatavyo: leseni za kusafirisha samaki na mazao yake (Export Licences); leseni za uingizaji mazao ya uvuvi (Import Licences); ushuru wa mrabaha (Export Royalty); Mrabaha wa kuingiza mazao ya uvuvi nchini (Import Royalty), leseni za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa bahari Kuu, Tozo ya Maabara; leseni za uvuvi wa kambamiti, mauzo ya vifaranga vya samaki na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria za uvuvi.

**MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19**




**019/**

**125.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Fungu 64 inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi **32,301,458,400.** Vyanzo vikuu vya fedha hizo ni pamoja na; leseni za kusafirisha samaki na mazao yake (Export Licences); leseni za uingizaji mazao ya uvuvi (Import Licences); ushuru wa mrabaha (Export Royalty); Tozo ya Maabara; mauzo ya vifaranga vya samaki; mauzo ya mazao ya uvuvi na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria za uvuvi.

**Fedha Zilizoidhinishwa**

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/2019***,*** Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Fungu 64 ilitengewa jumla ya Shilingi **21,093,086,000.00**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **13,966,406,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **7,126,680,000.00** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.Matumizi ya Bajeti ya Kawaida.

**127.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, Fungu 64 lilitengewa jumla ya shilingi **13,966,406,000**. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019, jumla ya shilingi **11,135,859,951** zilikuwa zimetolewa, sawa na asilimia **79.7** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi **6,794,398,181** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Wizara (PE) na shilingi **4,341,461,770** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo**

**128.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka wa 2018/2019, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa kiasi cha shilingi **7,126,680,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwa ni fedha za ndani na nje. Kati ya fedha hizo Shilingi **3,000,000,000.00** ilikuwa ni fedha za ndani na shilingi **4,126,680,000.00** ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019, jumla ya shilingi **4,012,643,853.20** kutoka vyanzo vya nje zilitolewa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

## MAENEO YA VIPAUMBELE KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2018/2019 NA KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**129.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara imeainisha maeneo ya vipaumbele katika Mpango na Bajeti ya Wizara kupitia Sekta ya Uvuvi Fungu 64. Utekelezaji wake utafanyika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha kwamba Sekta ya Uvuvi inachangia kikamilifu katika kuifikisha nchi yetu kwenye uchumi wa viwanda. Vipaumbele hivyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha usimamizi, udhibiti na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi pamoja na kutunza mazingira;

(ii) Kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali yatokanayo na Sekta ya Uvuvi;

(iii) Kuimarisha usimamizi wa rasilimali katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari na Bahari Kuu;

(iv) Kuimarisha usimamizi na uthibiti wa ubora, usalama na viwango vya samaki na mazao ya uvuvi;

(v) Kuimarisha Miundombinu na kukuza biashara ya Mazao ya Uvuvi;

(vi) Kuboresha upatikanaji wa taarifa sahihi za Uvuvi;

(vii) Kuongeza upatikanaji wa vifaranga vya samaki;

(viii) Kuandaa kanda za ufugaji wa samaki;

(ix) Kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi; na

(x) Kuimarisha Utafiti, Huduma za Ugani na Mafunzo ya Uvuvi.

## UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KATIKA MWAKA 2018/2019 NA MIPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

### SERA NA SHERIA

**130.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2015 kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uendelezaji, uhifadhi, matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na utunzaji wa mazingira nchini. Katika mwaka 2018/2019, Wizara imechapisha nakala **2,000** za Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 katika lugha ya Kiswahili na jumla ya nakala **1,702** zimesambazwa kwa wadau.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni mbalimbali za uvuvi zikiwemo Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009; Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994; Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Na. 1 ya Mwaka 1998 na Marekebisho yake ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009 na Marekebisho yake ya Mwaka 2016; na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Na. 11 ya mwaka 2016.

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kwamba Sheria inayosimamia Sekta ya Uvuvi inakidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa, Wizara imeamua kuifumua Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009, ambapo itazaliwa Sheria mpya ya Uvuvi na Sheria Mpya ya Ukuzaji Viumbe Maji. Hivi sasa timu ya wataalam wa Wizara imekusanya maoni ya wadau na taasisi mbalimbali nchi nzima ambapo jumla ya wadau **2,156** (watu Binafsi **56,** Vikundi **2,088.** Wizara **6** na Taasisi **8**) wameshiriki kutoa maoni yao. Vilevile, Wizara imeendelea kufanya mapitio ya Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya Mwaka 1994 ili kupanua maeneo ya hifadhi hadi kwenye maji baridi. Pia, imeendelea kufanya maboresho ya Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu Na. 1 ya Mwaka 1998 na marekebisho yake ya Mwaka 2007.


**133.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara imefanya marekebisho ya dharura ya baadhi ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 ili kuliwezesha Taifa kunufaika na rasilimali za uvuvi. Miongoni mwa marekebisho hayo ni kuruhusu matumizi ya nyavu za milimita nane (**8**) badala ya kumi (**10**) kwa uvuvi wa dagaa katika ukanda wa bahari, matumizi ya nyavu za makila zenye ukubwa wa macho ya kuanzia inchi saba (**7**) badala ya inchi sita (**6**), uvunaji wa kaa kutoka gramu 500 hadi gramu 450, kuondoa ukomo wa urefu wa sentimita **85** kwa samaki aina ya Sangara, na pia matumizi ya leseni moja kwa kila eneo la maji ya uvuvi badala ya kila Halmashauri kutoa leseni yake. Marekebisho haya yamefanywa chini ya GN Na. 383 ya tarehe 10 Mei ya mwaka 2019 **(Kiambatisho Na. 20).**

**134.** ***Mheshimiwa Spika***, marekebisho haya yatawezesha wananchi wa Ukanda wa Pwani kuvua dagaa aina ya mchele kwa kutumia nyavu za milimita nane (8) ambao walikuwa hawawezi kuvuliwa kwa kutumia nyavu za milimita kumi (10) zilizokuwepo kwa mujibu wa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009, kuwezesha kuvua samaki aina ya Sangara wenye urefu wa zaidi ya sentimita 85 na kuondoa usumbufu wa kukata leseni kwa kila Halmashauri. Matokeo ya marekebisho haya ni pamoja na kuongeza kipato cha wavuvi, kuongezeka malighafi viwandani, kuvutia uwekezaji mpya, kudhibiti utoroshaji wa mazao ya uvuvi na kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, Wizara imefanya marekebisho haya baada ya utafiti wa kina na ushirikishwaji wa wadau kwa lengo la kuondoa kasoro zilizokuwepo.

**135.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itakamilisha mapitio ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003, Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya Mwaka 1994, Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu Na. 1 ya Mwaka 1998 na marekebisho yake ya Mwaka 2007 na kuandaa Muswada wa Sheria mpya ya Uendelezaji Ukuzaji Viumbe Maji. Aidha, Wizara itaandaa kanuni za kutekeleza Sheria hizi.

## MWENENDO WA UVUNAJI WA RASILIMALI ZA UVUVI

**136.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi nchini. Hadi kufikia mwezi Machi 2019 jumla ya tani **389,459.40** za samaki zenye thamani ya shilingi **trilioni 1.83** zilivunwa ikilinganishwa na tani **376,352.72** zenye thamani ya shilingi **trilioni 1.77** zilizovunwa katika kipindi kama hiki mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia **3 (Kiambatisho Na. 21).** Aidha, kutokana na juhudi kubwa iliyofanywa na Wizara katika kudhibiti matumizi ya zana na uvuvi haramu, katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2019 kumekuwa na ongezeko la samaki wanaovunwa ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2018 (**Kielelezo Na.1).**




**Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi 2019**

**137.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imeendelea kusimamia biashara ya samaki na mazao ya uvuvi ndani na nje ya nchi kwa kuzingatia viwango vya kitaifa, kikanda, kimataifa na mahitaji ya soko. Aidha, hadi kufikia mwezi Machi 2019, tani **38,114.72** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **46,098** wenye thamani ya shilingi **bilioni 491.15** waliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani **34,425.56** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **100,110** wenye thamani ya shilingi **bilioni 402.57** waliouzwa nje ya nchi katika kipindi kama hiki mwaka 2018. Aidha, hadi kufikia Machi 2019 mauzo haya yameliingizia Taifa mrahaba wa shilingi **bilioni 15.63**

ikilinganishwa na kiasi cha shilingi **bilioni 9.5** katika kipindi kama hiki mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia **64.5 (Kiambatisho Na. 22 na Kiambatisho Na.23).** Ongezeko hili limetokana na kuimarishwa kwa udhibiti na usimamizi wa biashara ya samaki na mazao ya uvuvi uliofanyika kupitia operesheni mbalimbali dhidi ya uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi.

**138.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019**,** kati ya tani **38,114.72** za mazao ya uvuvi zilizouzwa nje ya nchi, tani **36,670.93** ambazo ni sawa na **asilimia 96.21** zilitoka Ziwa Victoria. Sehemu kubwa ya mchango huu inatokana na biashara ya samaki aina ya sangara na mazao yake (tani **28,975.08** zenye thamani ya shilingi **bilioni 346.56**) ambayo ni sawa na asilimia **76.02** ya mauzo yote **(Kiambatisho Na. 24a na 24b)**. Aidha, tani **1,138.27** zenye thamani ya shilingi **bilioni 14.98** kutoka Ukanda wa Bahari ya Hindi ziliuzwa nje ya nchi (**Kiambatisho Na. 25**). Pia, mauzo ya samaki na mazao yake kutoka maziwa ya Tanganyika, Nyasa, na Rukwa ambayo yaliuzwa nje ya nchi ni kiasi cha tani **284.44** zenye thamani ya shilingi **bilioni 2.15** sawa na asilimia **1** ya mauzo yote**.**

**139.** ***Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2019, jumla ya tani **7,760.12** za samaki zenye thamani ya shilingi **bilioni 15.34** zimeingizwa nchini ikilinganishwa na tani **23,806.11** zenye thamani ya shilingi **bilioni 46.98** zilizoingizwa nchini katika kipindi kama hiki mwaka 2018 **(Kiambatisho Na 26).** Uingizaji wa samaki kutoka nje umepungua kwa asilimia **67.4** ikilinganishwa na mwaka 2017/2018. Hii imetokana na kuongezeka kwa uvunaji wa samaki katika maji ya asili, ufugaji wa samaki na udhibiti wa uingizaji holela wa samaki kutoka nje ya nchi.

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa takwimu za Uvuvi kwa kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa takwimu kwa njia ya kielectroniki ikiwemo matumizi ya simu za viganjani. Katika mwaka 2018/2019 Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Uvuvi ya Ziwa Victoria (LVFO) imeandaa mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za Uvuvi kwa njia ya simu ujulikanao kama e-CAS (electronic catch

Assessment Survey). Katika majaribio ya kutumia mfumo huo jumla ya simu **108** zimetolewa kwa maafisa Uvuvi kutoka Halmashauri za Wilaya zenye maeneo ya Uvuvi katika Ziwa Victoria, Ukanda wa Bahari ya Hindi na Ziwa Tanganyika. Ugawaji wa simu ulifanyika sambamba na kutoa mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu za Uvuvi kwa kutumia simu.

**141.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kusimamia uvunaji endelevu wa rasilimali za uvuvi na biashara ya mazao ya uvuvi nchini. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na nchi jirani ikiwemo nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, SADC na IOC - IOTC kutekeleza mikakati mbalimbali ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika maji ya pamoja.

**USIMAMIZI NA UDHIBITI WA RASILIMALI ZA UVUVI**

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeandaa na kutekeleza Mkakati wa Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi Nchini. Mkakati huu unalenga kuongeza ufanisi katika usimamizi, ulinzi, uendelezaji na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi na mazingira yake pamoja na udhibiti wa uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi. Katika kutekeleza mkakati huu, Wizara imeanzisha Kanda kuu tatu (**3**) za Usimamizi na Udhibiti wa Rasimali za Uvuvi katika Ukanda wa Ziwa Victoria (**1**), Tanganyika (**1**) na Ukanda wa Pwani (**1**). Aidha, Wizara imeanzisha kanda ndogo mbili (**2**) za Ukerewe na Sengerema na kuimarisha Vituo **27** vilivyopo vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi kote nchini.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mkakati huu, katika mwaka 2018/2019 Wizara imeendesha operesheni mbalimbali zenye siku kazi **10,914** zenye lengo la kuimarisha usimamizi na udhibiti wa uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi. Operesheni hizo ni pamoja na Sangara 2018 Awamu ya III ilifanyika katika Ukanda wa Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Bwawa la Mtera na Nyumba ya Mungu yenye sikukazi **4,170**, MATT iliyofanyika Bahari ya Hindi yenye sikukazi **1,500** na doria za kawaida zilizofanyika nchi nzima zenye sikukazi **5,244**.

**144.** ***Mheshimiwa Spika***, Matokeo ya Operesheni hizo ni kukamatwa kwa zana haramu mbalimbali zikiwemo nyavu za makila **168,708**, makokoro **3,715**, nyavu za timba **15,915**, nyavu za dagaa **9,068**, kamba za kokoro zenye urefu wa mita **525,784**, ndoano **568,958**, mitumbwi/boti **2,291**. Pia, samaki wazazi kilo **8,958**, samaki wachanga/kayabo kilo **110,181**, mabondo kilo **634.01**, magari **4,489**, Pikipiki **374**, mitungi ya gesi **236** na watuhumiwa **4,713**. Kati ya watuhumiwa hao wapo Viongozi **17.** (**Kiambatisho Na.27**).


**145.** ***Mheshimiwa Spika***, aidha, Wizara ilikamata jumla ya tani **15.53** za samaki walioingizwa nchini bila nyaraka, leseni na vibali. Samaki hao walipatikana na viambata vya sumu baada ya kufanyiwa uchunguzi ambapo samaki wote waliteketezwa kwa kutokukidhi viwango vya ubora na usalama. Vilevile, jumla ya raia wa kigeni **203** walikamatwa wakijihusisha na shughuli za uvuvi na biashara za mazao ya uvuvi kinyume cha sheria.

**146.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Operesheni Sangara 2018 Awamu ya II iliyofanyika mwaka 2017/2018 katika Ukanda wa Ziwa Victoria, mvuvi maarufu, ambaye alikamatwa na kikosi cha operesheni wilayani Sengerema kwa kosa la kukutwa na nyavu haramu za uvuvi vipande **24,000,** ndoano haramu **1,547,000** na mabunda **6** ya makokoro ambapo alitakiwa kulipa faini ya shilingi **milioni 240,** alikaidi kulipa na hivyo kupelekwa mahakamani. Mahakama ya Hakimu Mkazi Mwanza ilimtia hatiani na kumhukumu kifungo cha miaka mitano au kulipa faini ya shilingi **milioni 306** ambayo aliilipa. Baada ya kulipa faini, mvuvi huyo aliandika barua ya kukiri kosa na kuomba msamaha kwa makosa aliyotenda na kuahidi kuacha vitendo vya uvuvi haramu na kutoa ushirikiano katika kukomesha vitendo hivyo. Aidha, jumla ya watuhumiwa **110** walifungwa kutokana na kupatikana na makosa mbalimbali ya uvuvi na biashara haramu wakati wa kutekeleza Operesheni Sangara na doria.

**147.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Sea Shepherd Global mwaka 2017/2018, iliendesha operesheni

Jodari katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu. Katika operesheni hiyo, meli iitwayo Buah Naga Na. 1 ya Malaysia ilikamatwa kwa kosa la kukutwa na kilo **90** za mapezi ya papa bila miili na kutozwa faini ya shilingi **milioni 770** ambapo alikaidi na kufikishwa mahakamani. Aidha, Mwezi Desemba, 2018 Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara iliwatia hatiani watuhumiwa wakiwemo mmiliki, nahodha na wakala wa meli na kuwahukumu kulipa faini ya jumla shilingi **bilioni 1** au kutumikia kifungo cha **miaka 20** kila mmoja. Watuhumiwa wote wanatumikia kifungo baada ya kushindwa kulipa faini.

**148.** ***Mheshimiwa Spika***, zana haramu zilizokamatwa katika maeneo yote ziliteketezwa kwa amri ya mahakama. Zana hizo haramu kama zingeendelea kutumika zingeathiri uendelevu wa rasilimali za uvuvi na hivyo kuathiri upatikanaji wa malighafi kwenye viwanda vya kuchakata samaki. Samaki wachanga na wazazi waliokamatwa waligawiwa kwa taasisi za umma, vituo vya kulelea watoto yatima na wenye mahitaji maalum na mabondo yalitaifishwa na kupigwa mnada. Aidha, injini na mitumbwi iliyokamatwa ilikabidhiwa kwa wahusika baada ya kulipa faini. Operesheni na doria hizi zimewezesha kuleta matokeo chanya yakiwemo kuongezeka kwa upatikanaji wa samaki wakubwa ambao siku za nyuma hawakuwa wanapatikana. Kutokana na juhudi hizi uvuvi haramu umepungua kwa asilimia **75** kwa maji baridi na kupungua kwa milipuko katika uvuvi kwa asilimia **99** katika mwambao wa Bahari.



**149.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019 Wizara ilishiriki katika Kikao cha Baraza la Mawaziri la Kisekta la Uvuvi la Jumuiya ya Afrika Mashariki kilichofanyika Arusha tarehe 1 Machi, 2019 ambapo baadhi ya maamuzi yaliyofikiwa ni pamoja na nchi wanachama:-

(i) Kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi za kupambana na uvuvi haramu katika Ziwa Victoria kupitia Operesheni Sangara 2018 ambapo kumepelekea kuongezeka kwa wingi na ukubwa wa samaki;

(ii) Kutekeleza Operesheni Okoa Sangara (Operation Save Nile Perch -OSNP);

(iii)Kuendelea na utafiti kuhusu matumizi ya nyavu zilizounganishwa; na

(iv)Kushirikiana katika juhudi za kudhibiti utoroshaji wa mazao ya uvuvi katika maeneo ya mipakani.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa kufanya doria za kawaida zenye sikukazi **6,500**. Aidha, Wizara itafanya Operesheni Maalum kila robo mwaka na kuiwezesha MATT kutekeleza majukumu yake kwa kufanya Operesheni **12**. Vilevile, Wizara itaimarisha vituo **27** na kuanzisha Kanda tano **(5)** za usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Pia, Wizara itaanzisha vituo vipya **10** vya ukusanyaji wa maduhuli katika Ziwa Victoria **(7)** na Ziwa Tanganyika **(3)** na kufanya kaguzi katika maeneo ya mipaka, vizuizi, masoko na kwenye mialo.

### Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu

**151.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) iliendelea kusimamia hifadhi za bahari na maeneo tengefu kwa kufanya doria zenye sikukazi **677** katika maeneo yote **18** yaliyohifadhiwa ambayo ni Hifadhi za Bahari tatu **(3)** na Maeneo Tengefu **15**. Matokeo ya doria hizo ni pamoja na

kukamatwa kwa boti tano **(5),** injini tatu **(3)**, seti tatu **(3)** za vifaa vya kuogelea, magogo kumi **(10),** fito **117** za mikoko na nyavu haramu vipande **58.**

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo yaliyohifadhiwa katika bahari huwa ni kivutio kikubwa cha utalii kwa wageni wa kutoka ndani na nje ya nchi. Vivutio hivyo ni pamoja na fukwe nzuri zenye mchanga laini na mweupe, magofu yenye historia za kusisimua, uoto wa asili, nyasi za bahari za aina mbalimbali, matumbawe laini na magumu yenye rangi mbalimbali, samaki aina ya potwe, silikanti, kasa, kaa wanaokwea minazi waitwao tuyuyu (coconut crab) na samaki wa mapambo. Viumbe hivi vinapatikana katika maeneo machache sana hapa duniani na hivyo kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache zenye vivutio vya aina hii na viwango bora vya utalii wa bahari na pwani ambapo kwa mwaka 2018/ 2019 jumla ya watalii **46,304** walitembelea hifadhi hizo ikilinganishwa na Watalii **45,091** katika kipindi kama hiki mwaka 2017/2018.

**153.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, MPRU iliendelea kutoa gawio la maduhuli kwa Halmashauri na Vijiji vilivyomo ndani ya maeneo ya Hifadhi, ambazo maduhuli hukusanywa. Jumla ya shilingi **153,793,383** zilitengwa na kutolewa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia kwa ajili ya kugharamia shughuli za uhifadhi na miradi ya maendeleo katika vijiji **17** vilivyomo ndani ya Hifadhi ya Kisiwa cha Mafia. Aidha, kiasi cha shilingi **47,599,141** kimetengwa kwa ajili ya kuwakopesha wananchi wanaoishi katika vijiji vilivyomo ndani ya Hifadhi ya Bahari ya Mafia.

**154.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia MPRU itaendelea kusimamia rasilimali za Bahari na Pwani zilizoko katika maeneo Tengefu kwa kufanya doria zenye sikukazi **700**. Aidha, itaendelea kukiimarisha Kitengo kwa kutekeleza Mkakati wa Kuongeza Mapato kwa kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo katika maeneo ya hifadhi na kuboresha miundombinu iliyopo ili kuvutia watalii na kuendeleza taratibu za kutangaza maeneo ya visiwa vya Ukuza, Nyuni, Fanjove na Simaya kuwa Maeneo Tengefu. Pia,

Wizara imejipanga kuongeza idadi ya watalii wa ndani na nje ili kufikia **60,000** kwa mwaka 2020/2021.

**Uvuvi katika Bahari Kuu**

**155.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika 2018/2019, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu iliendelea kuboresha zaidi mfumo wa Kanzidata (Web Based Database) wa ukusanyaji takwimu za meli za uvuvi na uvuvi wa samaki aina ya Jodari na jamii zake katika Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari (EEZ) kwa kuongeza moduli moja ya ukusanyaji wa takwimu za urefu wa samaki kwa kutumia simu ya kiganjani (*mobile phone data collection module*). Aidha, Mamlaka iliendesha mafunzo maalum ya Ukaguzi wa shughuli za uvuvi katika meli zinazopewa leseni ya kuvua katika EEZ ya Tanzania kwa Maafisa Uvuvi **22** kutoka SMT (**9**), SMZ (**8**) na Mamlaka (**5**) yatawezesha Wakaguzi na wachukua takwimu kutekeleza vyema majukumu yao wawapo kwenye meli za uvuvi.

**156.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Mamlaka kwa kushirikiana na Wadau imefanya doria za kawaida za anga na baharini zenye jumla ya saa **24** ili kupambana na uvuvi haramu na kufuatilia mienendo ya meli za uvuvi kwenye eneo la Ukanda wa Kiuchumi wa Bahari ya Tanzania. Aidha, wakati wa doria hizo hakuna meli ya uvuvi iliyoonekana katika maji ya Tanzania.

**157.** ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka imeandaa Mapendekezo ya Sera (Policy briefs) ili kuhamasisha Watanzania kuhusu vivutio vya uwekezaji vinavyopatikana katika uvuvi wa Bahari Kuu. Maandiko haya yatachochea wazawa kuwekeza katika uvuvi wa Bahari Kuu, kuwa na vyombo vya uvuvi wa Bahari Kuu vya kitanzania (*Development of National Fishing Fleet for Sustainable EEZ Fisheries*) ili kuchangia katika uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, Sera ya Uchumi wa Viwanda na kuondokana na mwenendo usioridhisha wa meli za kigeni katika kukata leseni za uvuvi katika EEZ ya Tanzania kama ilivyo hivi sasa. Aidha, makampuni ya uvuvi ya Serikali ya TAFICO na ZAFICO yako kwenye maandalizi ya kuanza uvuvi wa Bahari Kuu.

**UKUZAJI VIUMBE MAJI**

**158. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeandaa na kutekeleza Mpango Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji yaani *National Aquaculture Development Strategic Plan* (NADSP) 2018-2025. Mpango huo unalenga kuongeza uzalishaji, ulaji na masoko ya mazao yatokanayo na viumbe maji kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira.

**159. *Mheshimiwa Spika***, katika kujenga uwezo wa kukabiliana na magonjwa ya viumbe maji, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE) iliandaa Mafunzo ya Kimataifa ya Afya ya Viumbe Maji (Aquatic Animal Health) yaliyofanyika nchini na kushirikisha wataalam **61** kutoka nchi **41** za Afrika na nje ya Afrika.

**160. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, jumla ya vifaranga **17,301,076** (samaki **6,221,076** na kambamiti **11,080,000**) vimezalishwa katika vituo vya Serikali na sekta binafsi ikilinganishwa na vifaranga **15,119,757** vilivyozalishwa mwaka 2017/2018. (**Kiambatisho Na. 28**)**.** Pia, idadi ya mabwawa ya samaki imeongezeka kutoka **24,302** mwaka 2017/2018 hadi **26,445**. Vilevile, Wizara inaendelea kuhamasisha uwekezaji na matumizi ya teknolojia stahiki katika kuzalisha viumbe maji. Miongoni mwa teknolojia hizo ni matumizi ya vizimba (Fish cage) ambapo hadi sasa jumla ya vizimba **408** vimewekwa: Ziwa Victoria (**346)**; Ziwa Tanganyika (**9)**; na malambo (**53)**. Aidha, teknolojia ya *Recirculation Aquaculture System* ambayo hutumia maji kidogo katika ufugaji na inawezesha uzalishaji wa samaki wengi katika eneo dogo imeanza kutumika katika mikoa ya Arusha na Dar es Salaam.

**161. *Mheshimiwa Spika*,** ongezeko la mabwawa na vizimba limeenda sambamba na ongezeko la uzalishaji ambapo katika mwaka 2018/2019, uzalishaji wa viumbe maji umefikia tani **18,081.6** ikilinganishwa na tani **16,129.6** za mwaka 2017/2018. Vipande **395** vya lulu vilizalishwa mwaka 2018/2019 ikilinganishwa na vipande **180** mwaka 2017/2018.

**162.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, Wizara katika juhudi za kuongeza upatikanaji wa samaki nchini hususan kwa wananchi wanaoishi maeneo yaliyo mbali na shughuli za uvuvi, imepandikiza jumla ya vifaranga **18,700** vya samaki aina ya sato katika malambo mawili ya Mwamapalala - Itilima (**7,000**) na Mwanjolo - Meatu (**11,700**) mkoani Simiyu.

**163.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara imefanya makadirio na mchanganuo wa gharama za ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vituo vya Kingolwira (Morogoro), Ruhila (Songea), Mwamapuli (Igunga) na kujenga upya kituo cha Nyamirembe (Chato) ili kuimarisha uzalishaji wa vifaranga. Pia, Wizara imeendelea na kazi ya kuboresha kituo cha Machui (Tanga) ikiwa ni pamoja na kukiunganisha na umeme wa Tanesco.

**164.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuimarisha vituo vyake vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji ili viweze kutoa huduma bora za ugani na kuzalisha vifaranga **milioni 18** kwa kushirikiana na sekta binafsi. Wizara itakarabati miundombinu ya vituo vya Ruhila (Songea) Kingolwira (Morogoro), Mwamapuli (Igunga), Nyamirembe (Chato) na Machui (Tanga) ili kuboresha mifumo ya maji na miundombinu ya utotoleshaji wa vifaranga vya samaki.

**165.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaandaa miongozo sita (**6**) ya kuimarisha na kusimamia tasnia ya ukuzaji viumbe maji. Aidha, Wizara itafanya kaguzi kwa kila robo mwaka katika mashamba yote ya kuzalisha vifaranga vya samaki, viwanda vya vyakula na mashamba ya uzalishaji samaki nchini. Vilevile, Mpango wa Kudhibiti Magonjwa ya Samaki utaandaliwa ikiwa ni pamoja na kufanya mafunzo kwa mashamba **20** ya ufugaji samaki. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na sekta binafsi itaainisha, kufanya tathmini ya athari ya mazingira na kuingiza kwenye ramani maeneo yanayofaa kwa ajili ya kuunda kanda **3** za ukuzaji viumbe maji kwenye vizimba katika Ziwa Victoria na kanda **2** za ukuzaji viumbe maji bahari katika Mikoa ya Pwani na Mtwara.

**166. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia mradi wa SWIOFish itasimika kanzidata kwa ajili ya kutunza taarifa mbalimbali ikiwemo za mazao yatokanayo na ukuzaji viumbe maji na kutoa mafunzo kwa watumiaji. Kanzidata hii itaimarisha utendaji kazi wa Wizara na wadau wengine kwa kutoa taarifa zenye tija katika kuendeleza tasnia. Vilevile, Wizara itaanza ujenzi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari kitakachojengwa Kunduchi, Dar es Salaam.

## UBORA NA USALAMA WA MAZAO YA UVUVI

**167. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, jumla ya viwanda vikubwa **12** vikiwemo viwanda **(8)** Ziwa Victoria na **(4)** Ukanda wa Pwani vilichakata mazao yenye viwango vya kuuzwa katika Soko la nchi za nje hususan nchi za Jumuia ya Umoja wa nchi za Ulaya. Vilevile, viwanda vya kati vinne **(4)** vilichakata mazao ya uvuvi ambayo yaliuzwa katika soko la kikanda la nchi zingine zisizo za Jumuiya ya Ulaya zikiwemo za Bara la Asia na Marekani. Aidha, kuna viwanda vidogo **34** vya kupokelea samaki hai na maghala **52** kwa ajili ya mazao ya uvuvi yaliyokaushwa.

**168. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imefanya kaguzi **3,155** za kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi yanayosafirishwa nje ya nchi. Kaguzi hizo zilifanyika mipakani, viwanja vya ndege na bandarini. Vilevile, vibali **3,108** vilitolewa kwa ajili ya kusafirisha tani **41.2** za samaki kwa ajili ya soko la ndani na vibali **47** vilitolewa kuruhusu mazao ya uvuvi kuingizwa nchini. Aidha, kufuatia doria na Operesheni zinazoendelea nchini, hali ya upatikanaji wa samaki hususan samaki aina ya sangara imeimarika na viwanda kuongeza uzalishaji, ambapo wastani wa tani **180** zinazochakatwa kwa siku katika mwaka 2018/2019 ikilinganishwa na tani **165** za mwaka 2017/2018. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kufuatilia mifumo ya uzalishaji katika viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, masoko na maghala kwa kufanya kaguzi za kina **120**.

**169.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imefanya kaguzi katika mialo **125** ikiwemo mialo ya kisasa **13** katika ukanda wa Ziwa Victoria **(6)**, ukanda wa Ziwa Tanganyika (**4**) na ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi **(3)** ili kuthibiti ubora na usalama wa mazao ya uvuvi. Aidha, Wizara imefanya tathmini katika maeneo ya vijijini **10** vya Marehe na Katembe (Kagera) Kibuyi, Busekela, Bukima na Kisorya (Mara), Kayenze, Chifunfu na Kijiweni (Mwanza), na Nyamikoma (Simiyu) ili kutambua changamoto katika usimamizi na uendelezaji wa mialo na masoko ya mazao ya uvuvi, usalama na miundombinu iliyopo. Pia, katika kutatua changamoto za miundombinu ya masoko ya uvuvi, Wizara inaendelea na ujenzi wa matundu **12** ya choo na mabafu manne **(4)** katika Soko la Samaki la Feri ambao unatarajia kukamilika katika mwaka huu wa fedha.

**170.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itashirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta binafsi katika kujenga, kukagua na kuendeleza miundombinu ya uvuvi nchini. Vilevile, kaguzi **7,200** za kuhakiki ubora na usalama wa samaki na mazao ya uvuvi kabla ya kusafirishwa nje ya nchi zitafanyika. Pia, Wizara itaimarisha na kuviwezesha vituo **27** vya Uthibiti Ubora na Viwango vya mazao kwa kuvipatia vitendea kazi ili viweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Wizara itaimarisha upatikanaji wa taarifa ya masoko ya mazao ya uvuvi kwa kuanzisha utafiti na ushauri wa masoko (Marketing Intelligence Unit-MIU) kupitia Dawati la Sekta Binafsi la Wizara.

**171.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imeendelea kuimarisha Maabara ya Uvuvi - Nyegezi kwa kuipatia vitendea kazi na mafunzo kwa watalaam ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Katika mwaka 2018/2019, wataalam tisa **(9)** wa Maabara walipata mafunzo kuhusu mbinu za ukaguzi, uhakiki wa njia na vifaa vya kupimia na usimamizi wa Maabara. Aidha, Maabara imefanya chunguzi za kimaabara kwa sampuli **3,238** za minofu ya samaki, maji na udongo ili kubaini uwepo wa vimelea, masalia ya madawa ya mimea, kemikali na madini tembo. Vilevile, Maabara imeendelea kukidhi vigezo vya ithibati kutoka Taasisi ya Ithibati ya Nchi

za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Africa-SADC (SADCAS) kwa vipimo **13** vya maikrobaiolojia kwa maji na chakula. Pia, mwezi Juni, 2018 Maabara hii upande wa kemikali ilipata ithibati katika aina nne **(4)** za vipimo (parameters) ambavyo ni vya madini tembo, unyevunyevu (Moisture content), pH na *Conductivity*.

**172. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuimarisha Maabara kwa kuipatia vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuiwezesha kupanua wigo wa vipimo vyenye ithibati upande wa maikrobaiolojia na kemikali.

## USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA KATIKA SEKTA YA UVUVI

**173. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kuimarisha mashirikiano ya kikanda na kimataifa ili kusimamia rasilimali za uvuvi katika maji yanayomilikiwa kwa pamoja na nchi husika. Miongoni mwa maji hayo ni maziwa makuu ya Victoria (LVFO), Tanganyika (LTA), Nyasa na Ukanda wa Bahari ya Hindi (IOTC, WIOMSA, SWIOFC, IORA). Kupitia mashirikiano hayo, nchi yetu inapata fursa ya kushiriki na kutekeleza sheria, miongozo, mikataba, itifaki na taratibu mbalimbali za kikanda na kimataifa zenye lengo la kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa kuzingatia kwamba samaki hawana mipaka. Aidha, nchi yetu ni mwanachama wa mashirika na Taasisi mbalimbali za Kimataifa.

**174. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kushiriki kwenye **mikutano**, makongamano na warsha mbalimbali zenye lengo la kujadili na kuweka mikakati ya pamoja ya kusimamia rasilimali za uvuvi. Miongoni mwa mikakati hiyo ni ya kuendesha operesheni za pamoja dhidi ya uvuvi haramu usioratibiwa na usiotolewa taarifa katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. Aidha, ushirikiano huo umewezesha nchi yetu kushiriki kwenye operesheni katika Ukanda wa Bahari ya Hindi.

**175.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi za kikanda na kimataifa katika sekta ya uvuvi ili kuboresha usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi. Vilevile, Wizara itaendelea kushiriki katika masuala ya kikanda, kimataifa na kutekeleza mikataba na itifaki mbalimbali za kikanda na kimataifa ambazo nchi yetu ni mwanachama.

**UTAFITI, MAFUNZO NA UGANI**
**Utafiti wa Uvuvi**

**176.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia TAFIRI imefanya tafiti mbalimbali kwa nyakati tofauti zenye lengo la kujua mwenendo wa rasilimali za uvuvi. Matokeo ya tafiti hizi yanasaidia kuandaa mipango ya uvuvi endelevu ili kuleta tija na kusaidia ukuaji wa sekta katika kuchangia pato la Taifa. Tafiti hizo ni pamoja na:-

**Ziwa Victoria**
**Utafiti wa Rasilimali za Uvuvi katika Ziwa Victoria**

**177.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuangalia uwingi wa samaki Ziwa Victoria kwa kutumia Teknolojia ya *Hydro-acoustic survey*, TAFIRI kwa kushirikiana na Taasisi za *Kenya Marine and Fisheries Research Institute (KMFRI-Kenya )* na *National Fisheries Resources Research Institute (NaFIRRI-Uganda),* utafiti uliofanyika mwezi Septemba hadi Oktoba 2018, ulionesha uwepo wa tani **2,210,000** za aina mbalimbali za samaki. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwepo kwa ongezeko la Sangara kutoka tani **417,936** mwaka 2016 hadi kufikia tani **553,770** mwaka 2018. Vilevile, Sangara wa chini ya sentimita **50** wamepungua kutoka asilimia **96.6** mwaka 2017 hadi kufikia asilimia **62.8** mwaka 2018; wale wa kuanzia sentimita **50** hadi **85** wameongezeka kutoka asilimia **3.3** mwaka 2017 hadi kufikia asilimia **32.0** mwaka 2018; na walio juu ya sentimenta **85** wameongezeka kutoka asilimia **0.4** mwaka 2017 hadi kufikia asilimia **5.2** mwaka 2018. Aidha, Takwimu zinaonesha kuwa wastani wa urefu wa Sangara umeongezeka kutoka sentimeta **16** mwaka 2017 hadi kufikia sentimeta **25.2** mwaka 2018.

**178.** ***Mheshimiwa Spika***, matokeo haya yanaonesha kuongezeka kwa Sangara ziwani sambamba na kuongezeka kwa Sangara wazazi na kupungua kwa Sangara wachanga ikilinganishwa na mwaka 2017. Ongezeko hili ni matokeo ya doria na operesheni dhidi ya uvuvi haramu katika Ziwa Victoria zilizofanyika katika vipindi tofauti. Aidha, ongezeko hili la Sangara wakubwa litawanufaisha wavuvi, wenye viwanda na wafanyabiashara ya mabondo kwa vile sangara wenye urefu wa zaidi ya sentimita 85 hutoa minofu na mabondo makubwa ambayo yana thamani ya juu katika soko.

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kushamiri kwa biashara ya mabondo hivi karibuni, ambapo uzalishaji na mauzo nje ya nchi hadi kufikia mwezi Machi, 2019 umefikia tani **884.30** zenye thamani ya shilingi **bilioni 178.31** na kuingiza mrabaha wa shilingi **bilioni 2.87** (**Kiambatisho Na.29**). Aidha, Wizara imefanya tathmini ya kina ili kuangalia mnyororo mzima wa zao hili la uvuvi na utafiti wa kuangalia urefu na uzito wa mabondo ya sangara wa Ziwa Victoria unaofaa kibiashara bila kuathiri rasilimali. Utafiti huu umeonesha kuwa mabondo ya kuanzia sentimita **12** /gramu **13** kwa mabondo mabichi, na sentimita **8** /gramu **4** kwa mabondo makavu ndiyo yanayofaa kuingizwa sokoni.

**Bahari ya Hindi**

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, TAFIRI kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (Deep Sea Fishing Authority - DSFA) imeendelea na utafiti wa vifaa vya kuvutia samaki FADs (Fish Aggregating Devices) ambao unafanyika katika maeneo ya Bagamoyo na Nungwi Zanzibar, ambapo wavuvi wadogo watasogezwa taratibu kutoka maji mafupi hadi kufikia maji marefu. Aidha, tafiti hizi zimeonesha kuwa mapato ya wavuvi walioshiriki kwenye utafiti huu yaliongezeka na kuwa na uhakika wa kupata wastani wa shilingi **20,000** hadi shilingi **35,000** kwa siku na muda wa kuvua umepungua kutoka saa **12** kabla ya FADs na kuwa saa tano (**5**) baada ya FADS. Aidha, katika mwaka 2019/2020, TAFIRI itaendelea kufanya ufuatiliaji wa ufanisi wa FADs katika kukusanya samaki kwa maeneo ya Bagamojo na Nungwi.

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, TAFIRI imeendelea na utafiti wa kujua wingi na biolojia ya Kambamiti katika pwani ya Tanzania. Hali ya rasilimali ya Kambamiti imeendelea kuimarika ambapo Kambamiti wameongezeka katika eneo la Bagamoyo hadi Pangani ambapo utafiti ulionyesha kuongezeka kwa mavuno kutoka kilo **26.16** kwa saa mwaka 2015/2016 hadi kilo **58.45** kwa saa mwaka 2018/2019. Aidha, katika maeneo ya Mkuranga hadi Kilwa mavuno yaliongezeka kutoka kilo **29.58** kwa saa mwaka 2015/2016 hadi kilo **61.38** kwa saa mwaka 2018/2019. Ongezeko hili ni matokeo ya kufunga kwa msimu wa uvuvi wa kambamiti kwa kipindi cha miezi sita **(6)** kila mwaka.

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI kwa kushirikiana na kikundi cha ufugaji samaki cha Barikiwa, Liwale, Lindi inaendelea kufanya utafiti wa kupata samaki wazazi (brood stock) bora wa sato kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora (local fish strain) ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa mbegu bora za samaki katika mikoa ya kusini.

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, utafiti wa kuzalisha mbegu bora ya samaki inayofaa kufugwa katika maeneo ya Liwale utaendelea ikiwa ni pamoja na upanuzi wa mabwawa na ujenzi wa vitotoleshi vipya ili kuongeza uzalishaji vifaranga vya sato na vya kambale. Aidha, TAFIRI itaendelea na utafiti wa ufugaji wa samaki kwenye vizimba katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa pamoja na Bahari ya Hindi. Pia, TAFIRI itafanya tafiti za kubaini uwepo, aina na mtawanyiko wa rasilimali za uvuvi nchini.

**184.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/2020**,** Wizara kupitia TAFIRI itafanya tafiti za kuchunguza uhusiano wa vinasaba kati ya makundi ya samaki aina ya Jodari na jamii zake na kuchunguza mazingira ya Bahari yanayovutia uwepo wa samaki hao wanaopatikana Bahari ya Hindi. Tafiti hizi zitaimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi, kupunguza gharama za uvuvi hususan wavuvi wadogo ili kuwanufaisha na rasilimali za uvuvi na kuongeza mchango wa Sekta ya Uvuvi katika pato la Taifa.

### Elimu na Mafunzo ya Uvuvi

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) imeendelea kutoa mafunzo ya teknolojia za uvuvi kwa vijana nchini kama Sera ya Uvuvi inavyoagiza. Jumla ya wanafunzi **1,088** walidahiliwa katika masomo ya ngazi za Astashahada na Stashahada kwenye Kampasi zake za Mbegani, Nyegezi na Kigoma. Kwa upande wa kozi fupi, jumla ya wananchi **1,300** wamepatiwa mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo na mbinu za kuvua na ukuzaji viumbe maji.

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, FETA kwa kushirikiana na NORGES VEL (Asasi isiyo ya Kiserikali ya nchini Norway) na Chama cha Wakuzaji Viumbe Maji Nchini (Aquaculture Association of Tanzania - AAT) walipata ufadhili wa shilingi **bilioni 4.6** kutoka Shirika la Misaada la nchini Norway (NORAD) kutekeleza Mradi wa Uzalishaji wa Samaki aina ya Sato na Kufundisha Stadi za Ufugaji na Biashara. Fedha hizi zitatumika kuanzisha yafuatayo katika Wilaya ya Kibaha**,** Pwani: shamba la ufugaji samaki litakalokuwa na mabwawa **20** na vitotoleshi vya vifaranga vya samaki, kituo cha mafunzo kwa vitendo kitakacholenga umahiri na weledi katika usimamizi wa tasnia ya ufugaji samaki, na kituo atamizi (*Incubation Centre*), kutoa fursa kwa wahitimu kuanzisha mashamba madogo ya ufugaji na kupatiwa pembejeo (vifaranga na chakula) na ushauri ili kuimarisha weledi. Atamizi italenga kufundisha stadi za ufugaji na biashara kwa vijana na wanawake **120** kila mwaka.

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia FETA imeandaa rasimu ya mitaala ya kutoa mafunzo ya rasilimali watu kwa ajili ya uwekezaji katika uvuvi wa Bahari Kuu (Deep Sea Fishing). Hadi sasa, Mitaala hiyo imefikia hatua za mwisho za uhakiki (*validation*). Aidha, Wizara inaendelea na hatua za kuomba ridhaa ya kuridhiwa kwa Itifaki ya *Standards of Training, Certification and Watch keeping for Fishing Vessel Personnel* (STCW – F), 1995. Kuridhiwa kwa Itifaki hii kutasaidia mafunzo hayo kutambulika kimataifa na

wahitimu kuwa na sifa ya kufanya kazi katika meli za uvuvi wa bahari kuu.

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara imepanga kuhakikisha kwamba Vituo vya FETA vya Gabimori (Rorya), Mwanza South (Mwanza), na Mikindani (Mtwara) vinaanza utoaji wa mafunzo na elimu ya ufugaji samaki, ikiwa ni pamoja na kuzalisha vifaranga vya samaki na huduma za ugani katika Kanda husika.

**Huduma za Ugani wa Uvuvi**

**189.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kutoa Huduma za Ugani kwa kutoa miongozo inayotumiwa na Halmashauri mbalimbali na watoa huduma wengine wanaotoa huduma hii kwa wavuvi na wakuzaji viumbe maji. Vilevile, Sekta ya Uvuvi ina hitaji la wagani **16,000** ikilinganishwa na wagani 671 waliopo kwa sasa. Kati ya hao, Wagani **419** ni kutoka Halmashauri na wagani 252 wapo chini ya Wizara. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika mafunzo ya uvuvi kwa lengo la kuongeza wataalam hao. Pia, Wizara inaendelea kushauriana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga nafasi na kuomba kibali cha kuajiri Maafisa Ugani ili kupunguza pengo hilo. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI inafanya tathmini ili kutambua maeneo yenye upungufu na maeneo yenye ziada ya watumishi/wagani waweze kuhamishimiwa kwenye maeneo yenye uhitaji mkubwa.

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kutoa elimu ya uvuvi endelevu na ukuzaji viumbe maji kwa umma kupitia vipindi **15** vya radio na vipindi vitano (**5**) vya luninga. Aidha, nakala **4,000** za machapisho mbalimbali zimesambazwa kwa wadau. Wizara imeendelea kuhamasisha ukuzaji viumbe maji ambapo idadi ya wadau waliopatiwa elimu ya ufugaji bora wa samaki imeongezeka kutoka **5,229** mwaka 2017/2018 hadi kufikia **7,047** mwaka 2018/2019. Vilevile, elimu ya kuongeza thamani ya zao la mwani imetolewa kwa wadau **492** kutoka vikundi **31** na kuwawezesha kutengeneza bidhaa mbalimbali kama

shampoo, sabuni na mafuta ya ngozi. Vilevile, wadau **7,586** walipata elimu ya uvuvi endelevu na ukuzaji viumbe maji kupitia maonesho mbalimbali yakiwemo ya Nanenane, Sabasaba na Siku ya Chakula Duniani.

**191.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kutokana na changamoto nyingi zinazowakabili wavuvi na Sekta ya Uvuvi kwa ujumla, Wizara imeamua kuendesha mafunzo Rejea kwa wavuvi na maafisa ugani nchi nzima ili kuleta uelewa wa pamoja wa sheria, matumizi ya zana halali za uvuvi, ufugaji viumbe maji, kupunguza uharibifu wa mazao ya uvuvi (Post harvest loss), kuunda ushirika wa wavuvi na urahisi wa upatikanaji mikopo na elimu ya ujasiriamali. Mafunzo haya yamezinduliwa tarehe 14 Aprili, 2019 katika mwalo wa Kilindoni ulioko Wilayani Mafia katika Mkoa wa Pwani. Lengo la Mafunzo hayo ni kubadili mtazamo na fikra za wavuvi juu ya ulinzi, uhifadhi na kuendelea kuvua na kutumia rasilimali za uvuvi ili kuhakikisha rasilimali hizi zinakuwa endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Mafunzo haya yanatolewa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza imeanza katika Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani. Jumla ya wavuvi **6,911** kutoka katika mialo ya Kilindoni, Jibondo, Chole, Juani, Nganje, Boza, Kisiju Pwani, Koma, Buyuni, Kimbiji, Minazimikinda, Tandavamba, Ununio, Mbweni, Kwale na Kunduchi wamepata mafunzo.

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara itarusha hewani vipindi **30** vya radio na **10** vya runinga kuhusu uvuvi endelevu na ukuzaji viumbe maji. Vilevile, itahamasisha wagani **200** na wadau **8,000** kuhusu shughuli mbadala ili kupunguza nguvu ya uvuvi katika maji ya asili. Pia, Wizara itaendelea kusimamia na kufuatilia uanzishwaji wa mashamba darasa ya ukuzaji viumbe maji na kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi na kutangaza bidhaa mbalimbali zinazotokana na Sekta kupitia maonesho mbalimbali.

## MIRADI YA SEKTA YA UVUVI

**193.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi

(SWIOFish)". Lengo kuu la mradi huu ni kuimarisha usimamizi madhubuti wa uvuvi katika ngazi ya kijamii, kitaifa na kikanda.

**194.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Mradi wa SWIOFish umeiwezesha TAFIRI kufanya tafiti mbalimbali katika ukanda wa Bahari ya Hindi; Doria na Operesheni MATT; mafunzo kwa vikundi **50** vya BMUs; uandaaji wa mitaala ya FETA; tathmini ya matumbawe katika maeneo yaliyohifadhiwa na mazao ya uvuvi; mafunzo kwa watumishi wa sekta ya uvuvi na semina kuhusu madhara ya uvuvi haramu kwa wadau.

**195.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Mradi itafanya kazi zifuatazo:- Kuwezesha TAFIRI kufanya tafiti za mavuvi ya kipaumbele; Kuimarisha ushiriki wa jamii za wavuvi katika usimamizi na ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi; Kuwezesha Doria katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi katika mavuvi ya kipaumbele; Kuiwezesha Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU); Kuimarisha Mfumo wa Taarifa zinazohusu Uvuvi kulingana na matakwa ya kikanda. Kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Samaki wanaopatikana katika tabaka la juu la maji ifikapo Juni 2020; na kuzijengea uwezo Taasisi za Uvuvi pamoja na Taasisi za Umma.

**196.** ***Mheshimiwa Spika*****,** pia, mradi huu utaboresha miundombinu kwa gharama ya shilingi **8,191,312,294.20** kama ifuatavyo: ujenzi wa maabara ya utafiti wa samaki Temeke shilingi **403,053,600.00**; ujenzi wa maabara ya TAFIRI shilingi **2,609,491,754.20**; ujenzi wa nyumba za watumishi wa MPRU Tanga shilingi **962,918,940.00;** ujenzi wa jengo la ofisi MPRU - Mafia shilingi **926,560,000.00;** ukarabati mkubwa wa miundombinu ya soko la Feri - Dar es Salaam shilingi **1,667,808,000.00**; na ujenzi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari (Mariculture Centre) Kunduchi, Dar es Salaam shilingi **1,621,480,000.00.**

**KUWEZESHA WAVUVI WADOGO NA WAKUZAJI VIUMBE MAJI**

**197.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, jumla ya vikundi **50** vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) katika

Wilaya tano (**5**) za Pangani (**12**), Mkinga (**14**), Jiji la Tanga (**5**) Bagamoyo (**9**) na Lindi Vijijini (**10**) vimeimarishwa kwa kupatiwa mafunzo ya uvuvi endelevu. Vilevile, mafunzo juu ya kuendeleza Maeneo ya Usimamizi wa pamoja yamefanyika kwa maafisa uvuvi **10** wa Halmashauri na watano (**5**) wa Serikali Kuu.

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, kupitia Mradi wa Kupunguza Uharibifu wa Samaki baada ya Mavuno unaotekelezwa katika Ziwa Tanganyika, majiko banifu **100** yamesambazwa katika Vijiji/mialo ya uvuvi **16** katika Mkoa wa Kigoma. Vilevile, wachakataji wa samaki **640** katika vijiji **16** wamefundishwa jinsi ya kutumia majiko na kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi katika Ziwa Tanganyika. Pia, Wizara imewezesha vikundi vya ushirika vya wavuvi vya Igombe – Mwanza, Ikumba itale – Chato, Nkasi (Ziwa Tanganyika), Migoli - Mtera na vikundi viwili vya ushirika wa ufugaji samaki Peramiho (Ruvuma) kwa kupatiwa fedha na vifaa.

## UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI

**199.** ***Mheshimiwa Spika*, **Wizara imeendelea kuhamasisha Sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvi kwa kuweka mazingira mazuri ikiwemo uwepo wa malighafi kwa viwanda vya kusindika mazao ya uvuvi hususan viwanda vya kuchakata samaki aina ya Sangara. Aidha, kiwanda kimoja (**1**) kimejengwa wilaya ya Mkuranga katika mkoa wa Pwani.

**200.** ***Mheshimiwa Spika*, **Wizara inaendelea kuchukua hatua ya kuhakikisha kuwa viwanda vilivyofungwa vya *Prime Catch* cha Musoma, *Supreme Perch* (zamani VicFish) na *TanPerch* vya Mwanza vinafufuliwa. Aidha, Serikali inahamasisha ujenzi wa viwanda vipya vya kuchakata samaki katika ukanda wa bahari na maziwa makuu. Kwa sasa, mazungumzo yanaendelea na wawekezaji kutoka nchi za Japan, Mauritius, Korea kusini na Misri ili waweze kujenga viwanda hivyo.

**201.** ***Mheshimiwa Spika*, **katika mwaka 2018/2019, Wizara inafanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari ya uvuvi

kupitia Mshauri Mwelekezi Kampuni ya *Sering Ingegneria* ya nchini Italia kwa gharama ya shilingi **bilioni 1.4**. Mkataba wa kazi hiyo ulisainiwa tarehe 2 Julai, 2018 na kazi hiyo ilianza tarehe 2 Agosti, 2018. Kukamilika kwa upembuzi yakinifu kutaiwezesha Serikali kutambua maeneo yanayofaa kwa ujenzi wa bandari ya uvuvi na kujua gharama za ujenzi wa bandari hiyo. Aidha, uwepo wa bandari ya uvuvi utawezesha meli za uvuvi zinazovua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari ya Tanzania na Bahari Kuu kutia nanga, kushusha na kupakia mazao ya uvuvi.

**202.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Bahari na Uvuvi (Ministry of Oceans and Fisheries – MOF) ya Jamhuri ya Korea ya Kusini inafanya mazungumzo kwa ajili ya kufadhili ujenzi wa Bandari ya Uvuvi kupitia *Exim Bank* ya Korea baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu. Mkataba wa Makubaliano (MoU) wa ujenzi wa Bandari hiyo ya uvuvi utasainiwa mwishoni mwa mwezi Mei 2019.

**203.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara inaendelea na juhudi za kufufua lililokuwa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) ili kuimarisha uwekezaji katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari, na Bahari Kuu. Katika mwaka 2018/2019, Wizara imezindua Menejimenti ya kusimamia ufufuaji wa TAFICO. Aidha, Wizara imeandaa na kutekeleza Mkakati wa kufufua TAFICO. Katika kutekeleza mkakati huo, menejimenti ya TAFICO inaendelea kutambua mali za lililokuwa shirika la Uvuvi ambapo hadi sasa mali zenye thamani ya shilingi bilioni **118** zimetambuliwa.

**204.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara inaendelea kuwasiliana na wadau mbalimbali wa maendeleo ili kupata fedha za kuendesha Shirika ikiwemo kununua meli mbili **(2)** za uvuvi, kukarabati majengo na miundombinu ya TAFICO inayojumuisha mitambo ya kuzalisha barafu, gati, vyumba vya ubaridi na kuzuia mmomonyoko wa ardhi.

**205.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kupitia Serikali ya Japan zimepatikana jumla ya Yen za Japan **milioni 200** sawa na takriban shilingi **bilioni 4.2** kwa ajili ya ununuzi wa meli ya uvuvi kwenye maji ya Kitaifa, ukarabati wa chumba na ununuzi

wa mtambo wa barafu na gari maalum la kubebea samaki. Hadi sasa Serikali ya Japan kupitia *Japan Tuna Fisheries Cooperative Association* (JTFCA) wameonesha nia ya kuyarejesha makampuni ya meli ya Japan kukata leseni za uvuvi katika maji ya Bahari Kuu ya Tanzania. Hii itasaidia kuongeza mapato ya Serikali yanayotokana na tozo za leseni kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA).

**206.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2019/2020, Wizara itakamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari ya uvuvi na kuendelea kutekeleza mkakati wa kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) na kuweka mazingira mazuri kwa wananchi kuwekeza katika tasnia ya ukuzaji viumbe maji.

## D: MASUALA MTAMBUKA YA MIFUGO NA UVUVI

### Dawati la Sekta Binafsi

**207.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/2019, Wizara ilianzisha Dawati la Sekta Binafsi lililozinduliwa rasmi tarehe 01 Oktoba, 2018. Lengo la kuanzishwa kwa Dawati la Sekta Binafsi ni kufuatilia kwa karibu changamoto zinazoikabili Sekta Binafsi (Sekta ya Mifugo na Uvuvi), kuzitafutia ufumbuzi na kuongeza uwekezaji na uchangiaji kwenye Pato la Taifa ili kufikia azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuelekea kwenye Uchumi wa Viwanda.

**208.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Dawati la Sekta Binafsi limesaidia kutatua migogoro ya kampuni za Sekta Binafsi na Taasisi za Serikali pamoja na kuharakisha upatikanaji wa huduma zilizokuwa zinachelewesha ufanisi wa kampuni hizo. Baadhi ya kampuni zilizowasilisha changamoto zao dhidi ya Taasisi za Serikali na kutatuliwa kwa wakati ni Kiwanda cha nyavu za samaki Sun flag na TBS, Kiwanda cha chakula cha mifugo na samaki-Marenga Milers na TBS, Kampuni ya kutengeneza madawa mifugo-Farm Base na TRA, kiwanda cha kuzalisha maziwa cha AZAM na Wizara, Viwanda vya kusindika minofu ya samaki na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC - kuanzisha Ofisi Mwanza), Kiwanda cha kusindika nyama za kuku (Kuku Poa) na Bodi ya Nyama.

**209.** ***Mheshimiwa Spika,*** Dawati la Sekta Binafsi limesaidia kuunganisha kampuni zinazohitaji huduma ya mikopo hususan kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kusaidia utayarishaji wa Andiko la Biashara (*Bankable business Plan*). Jumla ya kampuni tano (5) zimefaidika na huduma ya Dawati la Sekta Binafsi kwenye huduma ya Maandiko ya Biashara. Hadi kufikia mwezi Aprili 2019, Dawati la Sekta Binafsi limewezesha mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni **17.3.** Aidha, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni **55** inategemewa kutolewa wakati wowote (Mifugo bilioni **26** na Uvuvi bilioni **29**).

**210.** ***Mheshimiwa Spika***, Dawati limewezesha Wizara kuingia katika Makubaliano (MoU) na Viwanda Vinne vya kimkakati vinavyosindika maziwa yanayokaa muda mrefu bila kuharibika *(Ultra Heat Treatment – UHT)* ambavyo ni ASAS LTD, Tanga Fresh Ltd, MilkCom Ltd na AZAM Dairy Products. Lengo ni kuongeza usindikaji wa Maziwa kutoka lita **154,100** hadi lita **284,500** kwa siku, sawa na ongezeko la lita **130,500** kwa viwanda vyote kufikia Desemba 2019.

**211.** ***Mheshimiwa Spika***, Dawati limesaidia kurejesha uzalishaji wa Kiwanda cha AZAM kilichopo Zanzibar baada ya Wizara kuwezesha unafuu wa tozo wa shilingi **250** kwa lita badala ya shilingi **2,000** kwa lita kwa maziwa yaliyozalishwa kwa malighafi kutoka nje ya nchi. Vilevile, kusamehe tozo zote za maziwa yanayozalishwa na kusindikwa Zanzibar yanapoingizwa Tanzania Bara, pia maziwa ghafi yanayosafirishwa kwenda Zanzibar na baadaye kusindikwa na kuuzwa katika soko la Tanzania Bara.

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** Dawati limetembelea na kukutana na wadau **213** wa Sekta za Mifugo na Uvuvi na kutoa ushauri wa kitaalam. Wadau waliotembelewa ni pamoja na viwanda vya kusindika samaki, nyama, ngozi, maziwa, kuku pamoja na wafugaji wa samaki katika vizimba na mabwawa (**Kiambatisho Na. 30).**

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi inaendelea kuunganisha vyama vya Ushirika **86**

vya Wavuvi na taasisi za kifedha ili waweze kupata mikopo. Pia, Dawati limewezesha kuanzishwa kwa vyama vya Ushirika vipya vitatu (3) vya Wavuvi vya Kikumba Itale katika Wilaya ya Chato, Igombe katika Wilaya Ilemela na Kasera cha Tanga Mjini. Vilevile, Dawati limewezesha vyama vya ushirika viwili (**2**) vya wafugaji kupatiwa mkopo wa ng'ombe bora wa maziwa **73** kati ya vyama saba (**7**) vilivyoomba kukopeshwa ng'ombe **350**.

**214.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina dhamira ya dhati ya kuimarisha ushirikiano na Sekta Binafsi na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na wadau wa maendeleo (World Bank, DALBERG, ANSAF, ASPIRE, TADB, PASS, TPSF na SAGCOT) kwa lengo la kukuza mchango wa Sekta Binafsi katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**215.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Dawati la Sekta Binafsi litaendelea kuainisha, kuratibu na kufuatilia changamoto na kuzitafutia ufumbuzi kwa haraka ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara katika Sekta za Mifugo na Uvuvi. Aidha, Dawati litaendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi ikiwemo: uwekezaji katika viwanda vya kusindika mazao ya mifugo (maziwa, ngozi na nyama), vyakula vya mifugo, ufugaji samaki katika vizimba, mabwawa, uzalishaji wa vifaranga na vyakula bora vya samaki; kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika mashirika ya NARCO na TAFICO; na kuwaunganisha wadau wa mifugo na uvuvi na taasisi za kifedha.

## Utawala Bora, Jinsia na UKIMWI

**216.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara imehamasisha watumishi **420** kupima afya zao kwa hiari na watumishi watatu (**3**) wanaoishi na Virusi vya UKIMWI wamepatiwa huduma ya lishe. Aidha, Wizara imeendelea kuwaelimisha watumishi kuhusu kuzingatia maadili, haki na wajibu katika Utumishi wa Umma. Vilevile, Wizara imewezesha viongozi kutimiza majukumu yao katika Wizara, Majimbo pamoja na kusimamia ujenzi wa jengo la Ofisi za Wizara kwenye eneo la Mji wa Serikali Jijini Dodoma.

**217.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019 Wizara imeajiri watumishi wapya watatu (**3**) wakiwemo Madereva wawili (**2**) na Mkemia mmoja (**1**), vikao viwili (**2**) vya Kamati ya Ajira vimefanyika ambapo watumishi **50** wa kada mbalimbali walithibitishwa kazini baada ya kumaliza vizuri muda wa majaribio. Aidha, watumishi wamehamasishwa kushiriki michezo na kuwezeshwa kushiriki kwenye maonesho mbalimbali ya kitaifa. Pia, watumishi **19** wamewezeshwa kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na **11** kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi. Vilevile, Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Utumishi na Mishahara (HCMIS) na wa Malipo ya Mishahara kwa watumishi (GSPP) imeendelea kusimamiwa ipasavyo.

**218.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara iliandaa mahitaji ya kazi pamoja na maelezo ya kazi kwa kila nafasi ambapo katika kipindi cha miaka mitatu ijayo watumishi **1,893** watahitajika wakiwemo **1,001** wa Sekta ya Mifugo na **892** wa Sekta ya Uvuvi ikilinganishwa na watumishi **824** waliopo sasa kwa Sekta zote. Kati ya hao, watumishi **465** ni wa Sekta ya Mifugo na watumishi **359** ni wa Sekta ya Uvuvi, hivyo kuwa na upungufu wa watumishi **1,069**. Kati ya upungufu huo watumishi **536** ni wa Mifugo na **533** ni wa Uvuvi. Aidha, Wizara imepata kibali cha UTUMISHI cha kuwahamisha watumishi **224** kwenda kwenye Wakala ya Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA). Vilevile, Wizara imeendelea kushirikisha watumishi kupitia Baraza la Wafanyakazi ambapo kikao kimoja cha Baraza kilifanyika kwa ajili ya kujadili bajeti pendekezwa ya Wizara kwa mwaka 2019/2020. Pamoja na watumishi waliopo Wizarani pia katika Serikali za Mitaa kuna jumla ya watumishi **3,795** wa Sekta ya Mifugo **(Kiambatisho Na. 31)** na watumishi **419** wa Sekta ya Uvuvi katika Halmashauri **(Kiambatisho Na.32).** Katika mwaka 2019/20 Wizara itaendelea kuwatembelea watumishi katika maeneo yao ya kazi ili kubaini changamoto zinazowakabili na kuzitafutia ufumbuzi.

**219.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Rais Menejimenti ya

Utumishi wa Umma na Utawala Bora inafanya tathmini ili kutambua maeneo yenye upungufu na maeneo yenye ziada ya watumishi/wagani waweze kuhamishimiwa kwenye maeneo yenye uhitaji mkubwa.

**220.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itatekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa na kuelimisha watumishi kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya kazi katika Utumishi wa Umma. Pia, Mkataba wa Huduma kwa Mteja utatekelezwa, mafunzo kwa watumishi kuhusu Mfumo wa Wazi wa Upimaji wa Utendaji Kazi (OPRAS) yatatolewa. Aidha, Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Utumishi na Mishahara (HCMIS) na Mfumo wa Malipo ya Mishahara ya watumishi (GSPP) itawezeshwa na kusimamiwa ipasavyo. Vilevile, Wizara itasimamia utekelezaji wa Waraka Na.2 wa Mwaka 2006 pamoja na mwongozo wake wa mwaka 2014 unaohusu VVU, UKIMWI na magonjwa Sugu yasiyoambukiza. Aidha, Wizara itahamasisha watumishi kupima afya zao ili wale watakaobainika kuathirika wajitokeze na kupatiwa huduma zinazostahili.

**221.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaajiri watumishi **295** wakiwemo **176** wa Sekta ya Mifugo na **119** Sekta ya Uvuvi na watumishi **10** watathibitishwa kazini. Aidha, Wizara itaendelea kufanya uhakiki wa watumishi **824**. Vilevile, vikao vinne (**4**) vikiwemo viwili (**2**) vya Kamati ya Ajira na viwili (**2**) vya Baraza la Wafanyakazi vitawezeshwa. Pia, majukumu ya Vyama vya Wafanyakazi yatawezeshwa.

### Mwingiliano wa Majukumu, Sheria na Tozo

**222.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kumekuwepo na mwingiliano wa majukumu, sheria, kanuni na tozo kati ya Wizara yangu na wizara nyingine hali ambayo imesababisha urasimu katika utoaji vibali na leseni katika ujenzi wa viwanda na uanzishaji wa biashara. Aidha, utitiri wa kodi na tozo umesababisha ongezeko la gharama za uwekezaji na uendeshaji wa biashara na hivyo kuwepo kwa malalamiko makubwa kutoka kwa wawekezaji na wafanyabiashara.

**223.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kutokana na mwingiliano huu Waziri Mkuu **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)** alitoa agizo la kuzitaka Wizara tano (5) na Taasisi zake kutatua changamoto hizi. Wizara yangu imeshiriki katika majadiliano na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; Viwanda na Biashara; Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Elimu, Sayansi na Teknolojia na Kilimo. Aidha, katika majadiliano hayo Taasisi zilizohusika ni pamoja na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA); Shirika la Viwango Tanzania (TBS); Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC); Wakala wa Barabara (TANROADS) na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA). Majadiliano yanaendelea kwa kuzingatia vigezo muhimu vilivyoainishwa kwenye Majukumu ya Wizara (*Instrument),* Muundo, Sera, Sheria, *Blueprint*, weledi, viwango na utendaji bora wa kimataifa, jukumu la kiutendaji, kiusimamizi na kiuangalizi kwa lengo la kuondoa kasoro zilizopo na kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu katika Sekta husika.

**224.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Utatuzi wa changamoto hizi utapunguza urasimu wa upatikanaji wa vibali na leseni, kupunguza gharama za uwekezaji na uendeshaji biashara, kuvutia uwekezaji na kupanuka kwa Sekta Binafsi, Ajira na ukuaji wa Uchumi nchini.

**Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

**225.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara imetoa mafunzo na kusambaza vifaa maalum vya kukusanyia maduhuli kwa njia ya kielekroniki (PoS) kwenye vituo vyote vya ukusanyaji nchi nzima. Kwa upande wa Sekta ya Mifugo vifaa vimesambazwa kwenye Minada yote ya Upili na ya mipakani ambayo ni Pugu, Igunga, Ipuli, Nyamatala, Mhunze, Korogwe, Meserani, Themi, Weruweru, Kirumi, Lumecha, Longido, Waso, Murusagamba, Buhigwe na Kasesya. Aidha, kwa upande wa Sekta ya Uvuvi vifaa vimepelekwa katika vituo vya Mtukula, Simiyu, Rusumo, Murusagamba, Sirari, Sota, Kanyigo, Kabanga, Mganza, Bukoba, Ikola, Kasanga, Kipili, Tunduma, Kasumulu, Horohoro, Mbeya, Kilwa, Mwanza, Geita,

Musoma, Mtwara na Mbamba-bay. Pia, Wizara imesimika mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji maduhuli ambayo imeunganishwa na mfumo wa malipo ya Serikali (*Government Electronic Payment Gateway*) katika Taasisi na Wakala zake za FETA, LITA TALIRI, TAFIRI, TVLA, LMU na MPRU. Lengo likiwa ni kuongeza tija na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na kupunguza mianya ya upotevu wa mapato.

**226.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuboresha na kusimika mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji maduhuli ya Mifugo kwenye minada yote ya awali hususan katika ukusanyaji wa Tozo za vibali vya kusafirisha Mifugo *"Animal Movement Permit''*. Pia, kuboresha Mfumo wa Uvuvi ili kuwezesha wafanyabiashara wanaosafirisha mazao ya uvuvi ndani na nje ya nchi kuomba leseni zao kwa kupitia mfumo wa kielektroniki *"Fisheries Licence Online Application*" tofauti na ilivyokuwa ikifanyika awali.

**Hifadhi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

**227.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeanzisha Kitengo cha Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi katika Sekta za Mifugo na Uvuvi. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na Utekelezaji wa Azimio la Kilimo na Ufugaji Linazozingatia Tahadhari ya Mabadiliko ya Tabianchi (*Climate Smart Agriculture* – CSA). Azimio hilo liliandaliwa kwa pamoja kwa ushirikiano na Wizara ya Kilimo, na utekelezaji wake unafanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs). Aidha, tathmini ya athari ya Mazingira *(Environmental Impact Assessment – EIA)* za Miradi mitano (**5**) na *Environmental Audit – EA* kwa miradi miwili (**2**) zilifanyika katika utekelezaji wa Miradi inayohusu Sekta ya Mifugo kama ujenzi wa machinjio, viwanda vya kuchakata nyama, viwanda vya vyakula vya mifugo na maziwa. Katika tathmini hizo, Wizara imetoa maelekezo ya kimaandishi kuhusu miradi hiyo ili kulinda maslahi ya Sekta ya Mifugo bila kuathiri Mazingira.

**228.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kufuatilia athari za mabadiliko ya tabia nchi

katika Ziwa Tanganyika. Matokeo yanaonesha kwamba mabadiliko ya tabia nchi yamesababisha ongezeko la joto katika Ziwa hali inayoathiri uzalishaji wa viumbe wa awali kwenye Ziwa (*Primary Productivity*) ambao ni chakula cha samaki. Pia, Wizara imeendelea kufuatilia na kufanya tathmini ya mifumo ya ikolojia hususan matumbawe, majani bahari na mikoko. Matokeo ya ufuatiliaji huu yatatoa hali halisi ya mifumo ikolojia katika maeneo yaliyohifadhiwa na kusaidia katika maamuzi ya usimamizi endelevu wa rasilimali hizo.

Aidha, Wizara inaendelea kufuatilia hali ya mmomonyoko wa fukwe pamoja na kiasi cha taka zinazotupwa kwenye maeneo ya hifadhi kwani taka hizo ni hatari kwa mazingira.

**229.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Wizara imedhibiti uvuvi haramu wa nyavu, mabomu na sumu ambapo uvuvi haramu umepungua kwa asilimia kubwa na kusababisha ukuaji wa bioanuai na viumbe hai. Aidha, wizara imetoa elimu kwa wagani wa mifugo na uvuvi pamoja na wadau wa sekta hizi juu ya kuzuia na kuhimili mabadiliko ya tabia nchi (Mitigation and Adaptation measures).

**230.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendesha mafunzo kwa wawezeshaji (TOT) kuhusu Azimio la Kilimo na Ufugaji linalozingatia Tahadhari ya Mabadiliko ya Tabianchi (*Climate Smart Agriculture* – CSA) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Jiji la Dodoma, Chamwino, Bahi, Kongwa, Chemba, Dodoma Vijijini, Mpwapwa, Ikungi, Iramba na Manyoni**.** Pia, Mradi wa miaka mitano (2018-2022) wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Maeneo ya Vijijini (*Ecosystem Based Adaptation for Rural Resilience* in Tanzania - EBARR) unaotekelezwa kwa pamoja na Wizara za Maji, Kilimo na Ofisi ya Rais - TAMISEMI utatekelezwa katika Halmashauri za Mvomero, Mpwapwa, Kishapu, Simanjiro na Wilaya ya Kaskazini A Unguja. Aidha, Wizara itaendelea kufuatilia athari za mabadiliko ya tabia nchi katika Ziwa Tanganyika na maziwa mengine.

## E: HITIMISHO

### MAMBO YA KIUJUMLA

### Gawio la Serikali

**231.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019, Taasisi, Bodi na Wakala zilizopo chini ya Wizara ikijumuisha Sekta ya Mifugo (NARCO, LITA, TALIRI, TVLA, Bodi ya Nyama na Bodi ya Maziwa) na Sekta ya Uvuvi (TAFIRI, FETA na MPRU) zimetoa gawio kwa Serikali kwa mara ya kwanza lenye jumla ya shilingi **milioni 520** ikilinganishwa na miaka iliyopita ambapo hapakuwa na gawio (**Kiambatisho Na. 33).**

### Michango katika shughuli za Kijamii

**232.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2018/19, Taasisi, Bodi na Wakala zilizopo chini ya Wizara zimetoa mchango wa shilingi **411,793,383** kwa jamii kwa ajili ya kuchangia shughuli za maendeleo na kukarabati miundombinu muhimu ikiwemo ukarabati wa majosho; kuchimba visima vya maji kwa matumizi ya binadamu na mifugo; kujenga kituo bora cha kukusanyia maziwa; ununuzi wa zana za uvuvi; ukarabati wa masoko na mialo; na kusaidia vyama vya ushirika vya wafugaji na wavuvi (**Kiambatisho Na. 34).**

### Miundombinu ya Kiuchumi

**233.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara yangu inayo faraja kubwa kuhusu ujenzi wa miundombinu mikubwa ya kiuchumi inayoendelea kujengwa nchini ikiwemo Reli ya Kisasa ya Mwendokasi (SGR), Mradi mkubwa wa Umeme wa Mto Rufiji (Stieglers' Gorge), upanuzi wa viwanja vya ndege na ununuzi wa ndege kubwa. Kuboreshwa kwa miundombinu hii, pamoja na mambo mengine utachochea uwekezaji mkubwa katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, kurahisisha usafirishaji wa mifugo, samaki na mazao yatokanayo na mifugo na uvuvi, kupunguza gharama za uzalishaji na hivyo kuwezesha viwanda vya ndani kushindana kibiashara na bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya nje ya nchi. Kwa muktadha

huo, Wizara yangu inayo kila sababu ya kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya maamuzi mazito na sahihi ya kutekeleza miradi hii mikubwa tena kwa fedha za ndani.

**234.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaendelea kufanya tathmini ya ubora wa miundombinu muhimu katika uhifadhi na usafirishaji wa mazao ya mifugo na uvuvi. Hatua hii itawezesha kuondoa kasoro zilizopo kwa kujenga na kufanya ukarabati wa miundombinu muhimu kama *refrigerated facilities* katika maeneo ya viwanja vya ndege na bandari. Ninamshukuru Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, **Mhe. Mhandisi Isack Aloyce Kamwelwe (Mb)** kwa kufanya ziara ya kubaini mahitaji ya utunzaji, usafirishaji wa mazao ya mifugo na uvuvi kwa masoko ya ndani na kimataifa.

**Uchumi na Biashara ya Mifugo na Uvuvi**

**235.** ***Mheshimiwa Spika**,* Wizara hii imeendelea kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa. Katika mwaka 2018/2019 mauzo ya ndani ya nchi katika Sekta za Mifugo na Uvuvi (nyama, samaki, maziwa, mayai, ngozi na vifaranga) yanakadiriwa kuwa shilingi **trilioni 6.57**. Pia, mauzo ya mazao ya mifugo na nje ya nchi yalifikia jumla ya **shilingi 508,973,674,981.** Uzalishaji huu umechangia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa chakula nchini (kitoweo). Vilevile, mapato haya yanawezesha nguvu ya manunuzi (**Purchasing Power**) kwa wananchi na kuwezesha kulipwa kwa kodi mbalimbali wanaponunua mahitaji yao. Aidha, kwa upande mwingine mazao haya yanapouzwa nje ya nchi huliingizia Taifa fedha za kigeni, pia kuokoa fedha za kigeni ambazo zingetumika kuagiza mazao hayo nje ya nchi.

**236.** ***Mheshimiwa Spika**,* kwa upande wa nguvu kazi, mifugo inachangia asilimia 27 ya nguvu kazi katika kilimo (Kati ya Hekta milioni 16 zinazolimwa nchini hekta milioni 4.3 hulimwa kwa kutumia wanyama kazi) Chanzo: Wizara ya Kilimo**),**

mifugo imekuwa ikifanya kazi nyingi ikiwemo usafirishaji wa mazao, usafirishaji wa vifaa vya ujenzi katika shule na zahanati, usafirishaji wa wagonjwa, kusomba maji na mizigo mingine. Mifugo kama mbwa na paka inatoa ulinzi kwa raia na mali zao. Vilevile, mifugo inazalisha nishati na mbolea ya samadi.

**237.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta za Mifugo na Uvuvi pamoja na masuala mengine zimeajiri Watanzania wengi na wawekezaji kutoka nchi za nje. Pia, kwa mujibu wa *National Panel Survey of 2015/16* iliyofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) mwaka 2015/16 ilionesha kuwa jumla ya Kaya **4,493,600** zinajihusisha na ufugaji sawa na asilimia **49.8** ya kaya **9,026,785** zote nchini. Vilevile, kwa mwaka 2018/19 Sekta ya Uvuvi ina jumla ya Watanzania zaidi ya **milioni 4** walioajiriwa katika shughuli zinazohusiana na uvuvi.

**238.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara ilipangiwa kukusanya shilingi **bilioni 40**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 makusanyo yalikuwa yamefikia shilingi **bilioni 63.3** ambayo ni sawa na asilimia **158** ya lengo ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2017/18 ya shilingi **bilioni 39.1** na mwaka 2016/17 shilingi **bilioni 25.9** kwa kipindi kama hiki sawia.

**239.** ***Mheshimiwa Spika,*** licha ya maduhuli yaliyokusanywa na Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi kufikia mwezi Machi, 2019 zimekusanya jumla ya shilingi **26,131,556,564** sawa na asilimia **84** ya lengo la shilingi **31,261,047,057 (Kiambatisho Na. 35).**

**240.** ***Mheshimiwa Spika,*** mapato mengine yanakusanywa kupitia mamlaka nyingine za Serikali ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) hukusanya kodi na tozo mbalimbali zikiwemo *Value Added Tax, Import Duty, Corporate Tax*, *Service Levy* na *Skills Development Levy*.

**F: SHUKRANI**

**241.** ***Mheshimiwa Spika*,** kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka uliopita yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, taasisi za fedha za kitaifa na kimataifa, taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini bila kusahau hamasa na ushiriki wa wananchi wakiongozwa na wawakilishi wao Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

**242.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua fursa hii kuzitambua na kuzishukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), na Umoja wa Nchiza Ulaya (EU), Serikali za Australia, Austria, Brazil, Canada, Jamhuri ya Czech, Hispania, Iceland, Ireland, Japan, Israel, Korea Kusini, Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Misri, Norway, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi pamoja na mashirika ya Umoja wa Mataifa ya FAO, IAEA, UNICEF, UNDP, UNIDO, SIDA, ILRI, CIAT na WHO. Pia, natoa shukrani kwa Mifuko ya Kimataifa ya GEF na IFAD kwa kuchangia katika maendeleo ya Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**243.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda pia kutambua na kuzishukuru taasisi za kimataifa ambazo ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea (KOICA) Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Japan (JICA), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DfID), Taasisi ya Raslimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika (AU/IBAR), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Maendeleo ya Uswisi (SDC), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GTZ), United Nations University

(UNU), Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA) kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**244.** ***Mheshimiwa Spika***, pia, napenda kushukuru Mashirika na Taasisi za hiari za Bill and Melinda Gates Foundation, Association for Agricultural Reseach in East and Central Africa (ASARECA), International Livestock Research Institute (ILRI), World Wide Fund for Nature (WWF), Indian Ocean Commission (IOC), South West Indian Ocean Fisheries Commission (SWIOFC), Heifer Project Tanzania (HPT), Overseas Fisheries Cooperation Foundation of Japan (OFCF), Vetaid, Care International, OXFARM, Welcome Trust, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, Building Resources Across Communities (BRAC), World Society for Protection of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute of Social Studies (ISS), International Land Coalition (ILC), British Gas International, Sea Sense, Indian Ocean Tuna Commission (IOTC), International Whaling Commission (IWC), SmartFish, Marine Stewardship Council (MSC), Mashirika na Taasisi mbalimbali za humu nchini zinazojihusisha na uendelezaji wa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**245.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya pekee niwapongeze sana Wafugaji na Wavuvi kote nchini kwa kazi nzuri wanazofanya za kutunza, kuzalisha na kulinda rasilimali za Taifa. Kazi wanazofanya ni nzuri na za heshima na kwamba Wizara yangu itaendelea kusimamia na kuunga mkono juhudi zao. Pia, niwashukuru wafanyabiashara, wawekezaji na wadau wote wa Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa dhamira yao njema ya kuendeleza sekta hizi muhimu.

**246.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mheshimiwa Abdalah Hamisi Ulega**, Mbunge wa Jimbo la Mkuranga, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa msaada wake wa karibu katika kusimamia kazi za Wizara. Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu kwa Katibu Mkuu Uvuvi, **Dkt. Rashid Adam Tamatamah** na Katibu Mkuu Mifugo, **Profesa Elisante Ole Gabriel**, Wakurugenzi pamoja na

Watendaji wote wa Wizara na Taasisi kwa kazi nzuri sana wanazofanya kwa nia thabiti ya kuleta mageuzi makubwa katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, mapambano yanaendelea na kama tulivyokubaliana saa ni namba tu, kamwe hatutafungwa na muda, wala usiku katika kutekeleza wajibu na majukumu yetu "***Leaders must be willing to sacrifice for the sake of the vision"*** .

**247.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa shukrani zangu za dhati na za kipekee kwa wananchi wangu wa Jimbo la Kisesa ambao muda wote wameendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo na kitaifa nataka niwahakikishie kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi, bidii, maarifa na ujasiri mkubwa sitajali jua wala mvua katika kuwatumikia. "***ni heri punda aumie lakini mzigo wa tajiri ufike"***.

**248.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na **Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** imepania kuleta mapinduzi makubwa katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi ambapo uwekezaji unaoendelea nchini utalindwa kwa nguvu zote na hatutakubali nchi yetu kugeuzwa kuwa dampo na kwamba ulinzi wa rasilimali za mifugo na uvuvi utaendelea kuimarishwa.

## G: MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA

**249.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2019/2020, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya **shilingi 64,901,756,551.00.** Kati ya fedha hizo, **shilingi 31,774,378,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Mifugo na **shilingi 33,127,378,551.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Uvuvi. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:-

### Fungu 99: Sekta ya Mifugo

**250.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara inaomba kutumia jumla ya shilingi **31,774,378,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Mifugo. Kati ya Fedha hizo, **shilingi 28,774,378,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 3,000,000,000.00**

ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo**.** Mgawanyiko wake ni kama ifuatavyo:-

**(i) Fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 28,774,378,000.**

- Mishahara: Shilingi **18,870,267,000;** na
- Matumizi Mengine (OC): Shilingi **9,904,111,000.**

(ii) **Fedha za Matumizi ya Maendeleo shilingi 3,000,000,000.**

- Fedha za Ndani: Shilingi **3,000,000,000**; na
- Fedha za Nje: Shilingi - **Sifuri.**

**Fungu 64: Sekta ya Uvuvi**

**251.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/2020, Wizara inaomba jumla ya shilingi **33,127,378,551.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Uvuvi. Kati ya fedha hizo, **shilingi 18,432,461,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **14,694,917,551.00** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mgawanyiko wake ni kama ifuatavyo:-

**(i) Fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 18,432,461,000.00**

- Mishahara: **shilingi 11,584,667,000.00;** na
- Matumizi Mengine (OC): **shilingi 6,847,794,000.00.**

**(ii) Fedha za Matumizi ya Maendeleo shilingi 14,694,917,551.00**

- Fedha za Ndani: **shilingi 3,000,000,000.00**, na
- Fedha za Nje : **shilingi 11,694,917,551.00.**

**252.** ***Mheshimiwa Spika*****,** naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara: www.mifugouvuvi.go.tz.

**253.** ***Mheshimiwa Spika*****,** naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imeungwa mkono. Sasa nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Nitakupa mwisho, acha tumalize kwanza taarifa, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, karibu.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru *Allah* aliyeniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa na maoni ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha mwaka 2018/2019 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwatakia kila la kheri Waislam kote ulimwenguni katika mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, *Ramadhan Kareem. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mufindi Kaskazini kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kazi zangu za Kibunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, maoni yetu naomba yaingie katika *Hansard* kama yalivyo katika vitabu vya taarifa vilivyogawiwa hivi punde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo cha 7 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni ya Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo,

Mifugo na Maji pamoja na majukumu mengine jukumu la kushughulikia bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 98 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inataka Kamati kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kwa madhumuni ya taarifa hii Wizara ya Mifugo inajumuisha mafungu mawili ambayo ni Fungu 64 - Sekta ya Uvuvi na Fungu 99 - Sekta ya Mifugo. Taarifa inafafanua mambo matano yanayohusu:-

(1) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019;

(2) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019;

(3) Mapitio ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019;

(4) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020; na

(5) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo tisa kama ilivyoorodhesha katika taarifa mliyogawiwa kipengele (a) mpaka (i). Kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati haujatekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha kutokana na sababu kubwa mbili:-

(i) Serikali bado haitumii kikamilifu fursa muhimu zilizopo kwenye Sekta za Uvuvi na Mifugo kwa kuchangia pato la Taifa kwa maendeleo ya uchumi na kwa pato la wavuvi na wafugaji kwa ujumla. Hii inadhihirisha kuwa sekta hizo sio sekta za vipaumbele kwa Serikali kutokana na bajeti ndogo inayotengwa pamoja na kuwa dhana ya uchumi wa viwanda, sehemu kubwa ya malighafi za viwanda zitapatikana kutoka kwenye sekta hizi.

(ii) Majibu yaliyotolewa na Wizara kwenye ushauri wa Kamati kuhusu malalamiko mbalimbali ya wavuvi na wafugaji yanasisitiza kuwa Wizara inatekeleza matakwa ya sera na sheria zilizopo. Kamati imebaini kuwa sera na sheria zilizopo zimepitwa na wakati na haziwezi kutatua changamoto zilizopo ili kuendana na kasi ya sasa ya uchumi wa viwanda. Hivyo kuna umuhimu wa Serikali kuharakisha mchakato wa marekebisho ya Sheria za Uvuvi na Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa bajeti wa mwaka wa fedha 2018/2019; kiasi cha fedha kilichotengwa na kutolewa; Sekta ya Mifugo - Fungu 99. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara kupitia Fungu 99 iliidhinisha jumla ya Sh.35,362,663,000 kati ya fedha hizo Sh.30,362,663,000 ni fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.5,000,000,000 ni fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni kutoka katika fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 jumla ya Sh.23,291,626,096 zilikuwa zimetolewa sawa na asilimia 76.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya hizo Sh.13,285,693,400 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Sh.7,832,745,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo hadi kufikia Aprili, 2019 jumla ya Sh.2,173,188,000 zilikuwa zimetolewa sawa na asilimia 43 ya fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi – Fungu 64; katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa jumla ya shilingi 21,093,086,000. Kati ya Fedha hizo, shilingi 13,966,406,000 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 7,126,680,000 ni fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019, jumla ya Sh.10,688,944,000 zilikuwa zimeshatolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 76.5. Kati ya fedha hizo shilingi 6,000,347,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara

na shilingi 4,341,000,000 ni kwa ajili ya matumizi mengine. Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 zilikuwa Sh.4,012,643,853 sawa na asilimia 56 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli; Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2018/2019, ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 40,002,250,700 ambazo Sekta ya Mifugo ilipanga kukusanya shilingi 18,467,945,100 sawa na asilimia 46 ya lengo lililowekwa na Sekta ya Uvuvi ilipanga kukusanya shilingi 21,534,305,600 sawa na asilimia 54 ya matarajio ya lengo lililowekwa. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019, Wizara iliweza kukusanya jumla ya shilingi 59,605,579,562.15 ikiwa ni asilimia 149 ya malengo ya ukusanyaji ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na tathmnini kuhusu mwenendo wa utoaji fedha za miradi ya maendeleo na makusanyo ya maduhuli; uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba kwa miaka mitatu mfululizo, fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge hazijatolewa kama ilivyoainishwa na hivyo kuchangia kutokufikiwa kwa malengo yaliyopangwa ikiwa ni pamoja na kutofanyiwa kazi kama ushauri wa Kamati na maeneo mengi kama ilivyoelezwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imesikitishwa na kiasi kidogo cha fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa Sh.6,185,831,939.2 ambazo ni asilimia 51 ya kiasi cha Sh.12,126,680,000 zilizotengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019. Kamati ina maoni kuwa ni vema Serikali ikatambua fursa zilizopo katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi katika kuinua pato la wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya mapato ya wastani wa asilimia 149 ya malengo na makadirio ya makusanyo. Kamati imeridhishwa kwa namna ambayo sekta hizi zimeweza kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 59 hadi Aprili, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, Kamati ilitaka kufahamu ni kwa namna gani makusanyo haya yanashabihiana na ukuaji na uimarishaji wa sekta hizi. Msingi wa hoja hii ni kutokana na ukweli kwamba hali ya ukuaji wa sekta hiyo siyo ya kuridhisha kiasi cha kuweza kukusanya makusanyo ya wastani ya asilimia 149.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huu, Kamati inatoa angalizo kwa Wizara kuwa ni vema makusanyo ya kiasi kikubwa yasitokane na faini na adhabu wanazotozwa wadau wa mifugo na uvuvi, bali yatokane na mapato ya juhudi zilizowekwa na Serikali katika kuimarisha sekta hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2018/2019; Kamati haikuweza kukagua kikamilifu miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kutokana na miradi ya maendeleo kutokupewa fedha za kuiwezesha kuanza kutekelezwa na baadhi ya miradi kuwa katika hatua za awali za uratibu. Hata hivyo Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua shughuli zinazotekelezwa na Wizara kupitia programu ya miradi mbalimbali, ilipata fursa katika miaka ya nyuma na inaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ziara ya ukaguzi na vikao vilivyofanywa, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto na malalamiko kadhaa kutoka kwa wadau kuhusu mwenendo wa Sekta za Mifugo na Uvuvi na namna ambayo changamoto hizo zinaathiri tija katika ukuaji wa sekta hizo. Aidha, pamoja na ahadi na maelezo ya Serikali katika nyakati tofauti ya kushughulikia changamoto hizo, bado hakuna hatua zinazoonekana kutekelezwa na kuleta mafanikio tarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa, changamoto zilizoko kwenye Sekta ya Uvuvi zimegawanyika katika maeneo makubwa matatu yanayohusu:-

(i) Changamoto zinazowakabili wavuvi wa samaki;

(ii) Changamoto zinazowakabili wafanyabiashara na mawakala wa samaki na zana za uvuvi; na

(iii) Changamoto zinazowakabili wenye viwanda vya kuchakata samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa changamoto kwa kila eneo umefafanuliwa kama ilivyo katika taarifa iliyogawiwa, kipengele (a) hadi (c).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa upande wa Sekta ya Mifugo, changamoto mbalimbali zilibainika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa bajeti na uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Tarehe 18 - 24 Machi, 2019, Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2019/2020, mpango ambao umeandaliwa kwa kuzingatia miongozo iliyopo kama ilivyoainishwa katika taarifa ya Kamati mliyopewa, kipengele (a) hadi (i).

(1) Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/2020;

(2) Dira ya Taifa ya Maendeleo 2020/2025; na

(3) Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kwa ujumla kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Mifugo na Uvuvi Fungu 64 na Fungu 99 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 64,901,756,551. Aidha, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi 82,301,458,400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 64 - Sekta ya Uvuvi. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara kupitia Fungu 64 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 33,127,378,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 18,432,000,000 ni kwa ajili ya matumizi

ya kawaida na shilingi 14,694,000,000 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za miradi ya maendeleo shilingi 3,000,000,000ni fedha za ndani na shilingi 11,694,000,000 ni fedha za nje. Aidha kwa upande wa maduhuli Wizara kupitia Fungu 64 imepanga kukusanya jumla ya shilingi 32,301,458,000 zitakazopatikana kutokana na mapato yatokanayo na leseni za kusafirisha samaki na mazao *(export licenses),* leseni za uingizaji mazao ya samaki *(import royalty),* ushuru wa mrahaba *(export royalty*), tozo za maabara na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa Sheria za Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 99. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara kupitia Fungu 99 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 31,774,000,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 28,774,300,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 3,000,000,000 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, kwa upande wa maduhuli Wizara kupitia Fungu 99 imepanga kukusanya jumla ya shilingi 50,000,000,000 zitakazopatikana kutokana na leseni za kusafirisha wanyama na mazao yake nje ya nchi *(exporty duty license),* ada mbalimbali, ushuru wa soko, mauzo ya chanjo na kodi za pango la nyumba za serikali na mauzo ya zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya Utekelezaji na Vipaumbele kwa Sekta ya Mifungo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Malengo yaliyokusudiwa ni kama ilivyoorodheshwa katika taarifa mliyogawiwa kipengele (a) mpaka (j).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tathimini ya Malengo kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kamati imepitia, kuchambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na kuridhishwa nayo. Hata hivyo, changamoto kubwa imekuwa ni kasi ndogo ya utekelezaji wa vipaumbele vinavyopangwa kutokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa na kutolewa. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha iliyotengwa kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza malengo na vipaumbele ilivyojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini mambo yafuatayo:-

(1) Makadirio ya matumizi ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Fungu 64 na Fungu 99 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 imeongezeka kwa asilimia 15 ikilinganishwa na bajeti inayomalizika ya mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa Wizara hii yanatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 106 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 ikilinganishwa na makisio ya bajeti inayomalizika ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatilia shaka tija ya sekta za mifugo na uvuvi kwa uwiano huu uliopo kati ya ongezeko la asilimia 15 ya fedha inayoombwa katika Bajeti ya Wizara ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 106 la makadirio ya makusanyo ya maduhuli. Kamati ina maoni kuwa makusudio ya kuwa na makusanyo makubwa yasiyoendana na uwekezaji katika sekta yanaweza kusababisha athari hasi na changamoto ya tija ndogo katika sekta hii.

(2) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande bajeti ya miradi ya maendeleo, Wizara kupitia Fungu 64, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 kuna ongezeko la asilimia 106 ya fedha inayoombwa. Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hili. Hata hivyo Kamati ina maoni kuwa pamoja na ongezeko hili la bajeti la asilimia 106, ambayo ni sawa na jumla ya shilingi 14,694,000,000, bado kiasi hiki ni kidogo na hakikidhi mahitaji ya kuwezesha mabadiliko ya kweli katika Sekta ya Uvuvi.

(3) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bajeti ya miradi ya maendeleo, Wizara kupitia Fungu 99 Sekta ya Mifugo; katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 kiasi kilichotengwa ni pungufu kwa asilimia 40 ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imesikitishwa na kupungua kwa kiasi cha fedha za miradi ya maendeleo kwa

Sekta ya Mifugo kutoka shilingi bilioni tano katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufukia shilingi bilioni tatu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu wa makisio makubwa ya makusanyo ya maduhuli bila ya kufanya uwekezaji wa kutosha katika Sekta ya Mifugo hauna tija katika kuimarisha sekta hii, kwani Sekta ya Mifugo inakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo za kukosekana kwa miundombinu, masoko ya uhakika, minada na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Mapendekezo ya Kamati. Uwiano wa Bajeti Inayotengwa na Makusanyo ya Maduhuli. Kamati haijaridhishwa na kukosekana uwiano stahiki kati ya bajeti inayotengwa kwa ajili ya Sekta za Mifugo na Uvuvi na makisio ya makusanyo kutoka katika sekta hii, ambapo makadirio ya matumizi ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha imeongezeka kwa asilimia 15 ikilinganishwa na bajeti.

Mheshimiwa mwenyekiti, Kuimarisha Tija na Changamoto katika Sekta Ndogo ya Maziwa ili Kuinua Uchumi wa Wafugaji na Pato la Taifa. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa nchini Tanzania uzalishaji wa maziwa umefikia lita bilioni 2.4, na kwamba kati ya kiasi kinachozalishwa ni asilimia mbili tu, sawa na lita milioni 37.5 kinasindikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa kutoimarika kwa usindikaji maziwa nchini kunatokana kukosekana kwa mazingira rafiki ya uwekezaji wenye tija. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na wingi wa tozo na kodi zipatazo ishirini na nane, wingi wa taasisi za udhibiti na ukaguzi, miundombinu duni, ushindani usio sawia baina ya wasindikaji nchini ambapo wachakataji wa maziwa ya unga wamepewa punguzo la asilimia 87.5 kuingiza maziwa ya unga nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkanganyiko wa Kisheria Kuhusu Aina za Nyavu za Uvuvi Zinazopaswa Kutumika Wakati wa Kuvua Samaki. Katika utekelezaji wa majukumu yake Kamati imebaini kuwa kwa muda mrefu kumekuwepo na

matamko yanayokinzana kutoka kwa Watendaji Wakuu wa Wizara kuhusu aina za nyavu zinazofaa kwa kuvua samaki aina ya dagaa. Haya yanayokinzana na yasiyozingatia Sheria ya Uvuvi kumepelekea matukio ya mara kwa mara ya wavuvi kuchomewa nyavu zao na kuvulia samaki ambazo ni moja ya dhana muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mlundikano wa Ngozi Ghafi Uliopo Kwenye Maghala Nchini. Serikali ilianzisha tozo ya ushuru wa asilimia 80 ya ushuru wa ngozi ghafi kwa nia ya kulinda viwanda vya ndani ili visikose malighafi za viwanda. Nia ya Serikali ilikuwa nzuri na ni ya kupongezwa. Hata hivyo hali imekuwa tofauti kutokana na ukweli kwamba viwanda vingi vya kuzalisha bidhaa za ngozi havizalishi na vingine vimeuzwa na kubadilisha matumizi na hivyo kupelekea mlundikano wa ngozi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi hivi sasa kuna mlundikano wa ngozi zitokanazo na ng'ombe kwa wastani wa vipande zaidi ya milioni moja na nusu na vipande milioni mbili vya ngozi itokanayo na mbuzi na kondoo ambavyo vimehifadhiwa na wazalishaji na wakusanyaji ngozi nchi nzima na vimeendelea kuharibika na kusababisha hasara kwa wakusanyaji, wazalishaji na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uwezo mdogo wa viwanda vya ndani kuzalisha bidhaa za ngozi na kwa kuwa soko la uhakika la ngozi linapatikana katika Bara la Ulaya na Asia, Kamati inaishauri Serikali kuwa wakati ikiendelea na mchakato wa kufufua viwanda vya bidhaa za ngozi nchini, ipunguze ushuru wa ngozi ghafi kutoka asilimia 80 hadi asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, Maboresho ya Sera na Sheria ya Uvuvi. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha mchakato wa maboresho ya Sera na Sheria ya Uvuvi. Pamoja na pongezi hizo Kamati inaishauri Wizara kuharakisha mapema iwezekanavyo mchakato wa maboresho ya Sera na Sheria ya Uvuvi ili ziweze kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwekezaji Katika Uvuvi wa Bahari Kuu. Kamati inaamini kuwa Serikali inatambua fursa kubwa ya rasilimali zinazopatikana katika Ukanda wa Bahari Kuu na kwamba ipo nia na dhamira ya Serikali kuweka mazingira bora ili kuwezesha uwekezaji wenye tija na kulinufaisha taifa na mapata ya rasilimali zilizopo.

Kamati ina maoni kuwa kutotekeleza nia na dhamira hii njema kunatoa fursa kwa nchi nyingine kuzitumia rasilimali zilizopo kwenye ukanda wa eneo la bahari kuu ambalo hatuwezi kuwazuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu na kuchukua hatua mahsusi za kuweka mazingira wezeshi na kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuimarisha Ufugaji wa Viumbe Kwenye Maji na Ukuzaji wa Samaki Katika Vizimba *(aquaculture).* Kufuatia changamoto hizo, Kamati ina kuwa ni vyema Serikali ikapata takwimu za uhakika kuhusu wingi wa samaki katika vyanzo mbalimbali nchini, mahitaji ya samaki na upungufu uliopo.

Aidha, Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa kuanzisha Mfuko wa *Aquaculture Fund* kwa ajili ya kuimarisha miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho. Napenda kukushukuru kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

# TAARIFA YA MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/ 2020 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

---

## 1.0 MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na majukumu mengine jukumu la kushughulikia bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inataka Kamati kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa madhumuni ya Taarifa hii, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inajumuisha mafungu mawili (2) ambayo ni:-

a) Fungu 64- Sekta ya Uvuvi; na
b) Fungu 99 –Sekta ya Mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inafafanua mambo matano (5) yanayohusu:-
a) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

b) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

c) Mapitio ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; na

e) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MASWALA MBALIMBALI

### 2.1 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo tisa (9) yafuatayo:-

a) Mtiririko usioridhisha wa Fedha za Miradi ya Maendeleo;

b) Uwekezaji mdogo katika Sekta ya Uvuvi;

c) Udhibiti wa Uvuvi Haramu Nchini;

d) Ufugaji wa Viumbe kwenye Maji na Ukuzaji wa Samaki katika Vizimba (*Aquaculture*);

e) Mabadiliko kuhusu taratibu za uingizaji na usambazaji samaki nchini;

f) Bajeti Ndogo ya Sekta ya Mifugo isiyowiana na mchango wa Sekta katika Pato la Taifa;
g) Uwekezaji usioridhisha katika Ranchi za Taifa;

h) Uwekezaji mdogo katika Tasnia ya Maziwa Nchini; na

i) Mikakati ya Serikali kuweka mazingira bora ya biashara ili kuchochea Sekta Binafsi kushiriki kikamilifu katika mnyororo wa thamani kwa mazao yatokanayo na Mifugo na Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati haujatekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha kutokana na sababu kubwa mbili: -

I. Serikali bado haitumii kikamilifu fursa muhimu zilizopo kwenye Sekta za Uvuvi na Mifugo kwa kuchangia Pato la Taifa kwa Maendeleo ya Uchumi na kwa pato la wavuvi na wafugaji kwa ujumla. Hii inadhihirisha kuwa sekta hizi sio sekta za vipaumbele kwa Serikali kutokana na bajeti ndogo inayotengwa. Pamoja na kuwa dhana ya Uchumi wa Viwanda sehemu kubwa ya malighafi za viwanda zitapatikana kutoka kwenye sekta hizi.

II. Majibu yaliyotolewa na Wizara kwenye ushauri wa Kamati kuhusu malalamiko mbalimbali ya Wavuvi na Wafugaji yanasisitiza kuwa Wizara inatekeleza matakwa ya Sera na Sheria zilizopo. Kamati imebaini kuwa Sera na Sheria zilizopo zimepitwa na wakati na haziwezi kutatua changamoto zilizopo ili kuendana na kasi ya sasa ya Uchumi wa viwanda. Hivyo kuna umuhimu wa Serikali kuharakisha mchakato wa marekebisho ya Sheria za Uvuvi na Mifugo.

## 2.2 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ulijikita katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika hadi mwezi Aprili, 2019 na eneo la ukusanywaji maduhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi Aprili, 2019.

### 2.2.1 Kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa na kutolewa

#### a) Sekta ya Mifugo - Fungu 99

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara kupitia Fungu 99 iliidhinishiwa jumla ya shilingi

**35,362,663,000.00**. Kati ya Fedha hizo shilingi **30,362,663,000.00** ni Fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi **5,000,000,000.00** ni Fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kutoka Fedha za Ndani.

Hadi kufikia mwezi Aprili 2019, jumla ya shilingi **23,291,626,966.48** zilikuwa zimetolewa sawa na **asilimia 76.7** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, shilingi **13,285,693,400** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na shilingi **7,832,745,480.48** ni kwa ajili ya Matumizi Mengine. Kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia mwezi Aprili 2019, jumla ya shilingi **2,173,188,086.00** zilikuwa zimetolewa, sawa na **asilimia 43** ya Fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa.

**b) Sekta ya Uvuvi - Fungu 64**

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa jumla ya shilingi **21,093,086,000:00**. Kati ya Fedha hizo, shilingi **13,966,406,000:00** ni Fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi **7,126,680,000:00** ni Fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019, jumla ya shilingi **10,688,944,731.20** zilikuwazimetolewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, sawa na **asilimia 76.5.** Kati ya fedha hizo, shilingi **6,347,482,961.20** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na shilingi **4,341,461,770.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengine. Aidha, Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 zilikuwa shilingi **4,012,643,853.20** sawa na **asilimia 56** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

**c) Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ilipanga kukusanya jumla ya shilingi **40,002,250,700.00**, ambapo Sekta ya Mifugo ilipanga kukusanya shilingi **18,467,945,100.00** sawa na asilimia **46%** ya lengo lililowekwa na Sekta ya Uvuvi ilipanga kukusanya shilingi **21,534,305,600.00** sawa na asilimia **54%** ya matarajio ya lengo lililowekwa.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Kufikia Mwezi Aprili, 2019, Wizara imeweza kukusanya jumla ya shilingi **59,605,579,562.15** ikiwa ni **asilimia 149%** ya malengo ya ukusanyaji ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**.** Kati ya kiasi hicho, shilingi **31,872,312,040.00** sawa na **asilimia 173%** ya lengo lililowekwa zimetokana na ukusanyaji wa maduhuli katika Sekta ya Mifugo. Aidha, shilingi **27,733,267,521.15** sawa na **asilimia 129** zimetokana na makusanyo ya Sekta ya Uvuvi.

**d) Maoni na Tathmnini kuhusu Mwenendo wa Utoaji Fedha za Miradi ya Maendeleo na Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba kwa miaka mitatu mfululizo, Fedha za Miradi ya Maendeleo zinazoidhinishwa na Bunge hazitolewi kama zilivyoidhinishwa na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa ikiwa ni pamoja na kutofanyiwa kazi ushauri wa Kamati katika maeneo mengi kama ilivyoelezwa hapo juu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imesikitishwa na kiasi kidogo cha Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa shilingi **6,185,831,939.2** ambazo ni **asilimia 51** ya kiasi cha shilingi **12,126,680,000** zilizotengwa katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019. Kamati ina maoni kuwa, ni vema Serikali ikatambua fursa kubwa zilizopo katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi katika kuinua Pato la Wananchi na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya Mapato ya wastani wa **asilimia 149%** ya malengo ya makadirio ya makusanyo. Kamati imeridhishwa kwa namna ambayo sekta hizi zimeweza kukusanya Maduhuli ya shilingi **59,605,579,562.15** hadi Aprili, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na pongezi hizi, Kamati ilitaka kufahamu ni kwa namna gani makusanyo haya yanashabihiana na ukuaji na uimarishaji wa sekta hizi. Msingi wa hoja hii ni kutokana na ukweli kwamba, hali ya ukuaji wa sekta hizi siyo ya kuridhisha hadi kuweza kukusanya makusanyo ya wastani wa **asilimia 149.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huu, Kamati inatoa angalizo kwa Wizara kuwa, ni vema makusanyo ya kiasi kikubwa yasitokane na faini na adhabu wanazotozwa wenye viwanda vya kusindika samaki, wafanyabiashara, wavuvi na wafugaji bali yatokane na mapato ya juhudi zilizowekwa na Serikali katika kuimarisha sekta hizi.

**2.3 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa Kamati kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ni kufanya ukaguzi na ulinganifu wa Tathimini ya Fedha iliyotumika (*Value for Money*) katika miradi iliyotekelezwa, ili kuweza kuishauri Serikali ipasavyo juu ya namna ya kuimarisha utekelezaji miradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuweza kukagua kikamilifu Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kutokana na Miradi ya Maendeleo kutopelekewa fedha za kuiwezesha kuanza kutekelezwa na baadhi ya miradi kuwa katika hatua za awali za uratibu. Hata hivyo, Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua shughuli zinazotekelezwa na Wizara kupitia programu na miradi mbalimbali ambayo ilipata fedha katika miaka ya nyuma na inaendelea kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya miradi na shughuli zilizotembelewa na kukaguliwa na Kamati ni pamoja na: -

a) Mradi wa Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo ASDP II), Uzalishaji wa Mifugo na Masoko mkoani Mwanza.

b) Kufanya kikao cha pamoja na wadau wa Uvuvi Mkoani Mwanza kuhusu changamoto na mafanikio ya Sekta ya Uvuvi na namna bora ya kuimarisha sekta hii.

c) Mradi wa Uhamilishaji Mifugo na Masoko, Vituo vya Uhamilishaji.

d) Mradi wa Ujenzi wa Minada miwili ya mpakani katika Wilaya ya Longido.

e) Kutembelea Kampuni ya Shan Zain - Arusha inayoshughulika na uzalishaji samaki kwenye mitungi.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia Ziara, Ukaguzi na Vikao vilivyofanyika, Kamati ilibaini kuwepo changamoto na malalamiko kadhaa kutoka kwa wadau kuhusu mwenendo wa Sekta za Mifugo na Uvuvi na namna ambayo changamoto hizo zinaathiri tija katika ukuaji wa sekta hizo. Aidha, pamoja na ahadi na maelezo ya Serikali katika nyakati tofauti ya kushughulikia changamoto hizi, bado hakuna hatua zinazoonekana kutekelezwa na kuleta mafanikio tarajiwa.
**Mheshimiwa spika,** Kamati ilibaini kuwa, changamoto zilizoko kwenye Sekta ya Uvuvi zimegawanyika katika maeneo makuu matatu yanayohusu: -

i. Changamoto zinazowakabili Wavuvi wa Samaki;

ii. Changamoto zinazowakabili Wafanyabiashara na Mawakala wa Samaki na zana za uvuvi; na

iii. Changamoto zinazowakabili wenye Viwanda vya Kuchakata Samaki.

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa changamoto kwa kila eneo umefafanuliwa kama ifuatavyo: -

**a) Changamoto zinazowakabili Wavuvi wa Samaki**

i. Tozo nyingi na ushuru mkubwa wanaotozwa Wavuvi ambazo zinajumuisha Ushuru wa Maegesho ya Chombo, Usajili wa Mitumbwi, Leseni ya Uvuvi, Leseni ya Wavuvi, Leseni ya SUMATRA, Kodi ya Mapato, Vibali vya BMU, Leseni ya Zimamoto, Ushuru wa Mazao ya Samaki na Leseni ya Uvuvi katika kila Halmashauri ambayo Mvuvi ataenda kuvua;

ii. Usalama wa Wavuvi na mali zao wawapo ziwani. Pamoja na wavuvi kulipa kodi na tozo mbalimbali, bado vyombo vya

Serikali vyenye dhamana ya usalama havifanyi doria za mara kwa mara kwenye maeneo ya Ziwa na hivyo kuhatarisha maisha ya Wavuvi na mali zao na mara nyingine kuporwa mali na majangili;

iii. Uhaba wa zana za uvuvi na upatikanaji wa zana za uvuvi kwa gharama kubwa hali inayochangia Wavuvi kutumia zana duni za Uvuvi zisizokubalika kisheria kwa ajili ya uvuvi endelevu;

iv. Ukosefu wa mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya Wavuvi kutokana ukweli kwamba Sheria za Fedha hazitambui kutumia zana za Uvuvi kama dhamana;

v. Ushirikishwaji hafifu wa Wavuvi katika utungwaji wa Sheria Ndogo Ndogo za Halmashauri ambazo kwa kiasi kikubwa zinagusa shughuli za kila siku za wavuvi;

vi. Faini zisizozingatia Sheria ikiwa ni pamoja na faini kandamizi kwa wavuvi na wafanyabiashara;

vii. Wenye viwanda kupanga bei ya samaki bila kuwashirikisha Wavuvi na bila ya kuzingatia bei elekezi ya samaki iliyopangwa na kukubaliwa;

viii. Ukosefu wa Huduma za Kijamii katika maeneo ya Visiwani ambapo kwenye maeneo mengi hakuna Vyoo, Hospitali, Umeme na Vituo vya Polisi; na

ix. Kutofautiana kwa faini inayotozwa kwa makosa ya aina moja na hivyo kupelekea kushamiri mazingira na viashiria vya rushwa.

**b) Changamoto zinazowakabili wenye Viwanda (Wachakataji wa Samaki)**

i. Kukosekana kwa uwiano wa Utekelezaji wa Sheria ya Uvuvi katika nchi za Afrika Mashariki. Kwa mfano; nchi za Kenye na Uganda zinatekeleza Sheria ya **Sentimeta 50** bila kuweka ukomo, wakati Tanzania Sheria ya Uvuvi imeweka ukomo wa **Sentimeta 85** ha hivyo kunufaisha nchi za Kenya na

Uganda kwa kuuza Nje ya Nchi samaki zenye minofu mikubwa. Hali hii pia inachochea ongezeko la vitendo vya magendo kwa Wavuvi wa Tanzania kuwauzia samaki wakubwa kwa Wafanya Biashara na wenye Viwanda kwa nchi za jirani.

ii. Kuongezeka kwa gharama za kuzalisha minofu ya samaki nchini Tanzania kutokana na utitiri wa tozo za Idara na Mamlaka mbalimbali za Serikali pamoja na tozo kubwa za mrahaba zinazotozwa nchini.

iii. Kukosekana kwa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa mkoani Mwanza sehemu ambako ni kiunganishi kikubwa cha mikoa inayopitiwa na Ziwa Victoria kwa ajili ya kusafirisha minofu ya samaki Nje ya Nchi. Nchini Tanzania Wafanyabiashara wa samaki wanaouza Nje ya Nchi hulazimika kusafirisha samaki ghafi kwa magari kutoka Mwanza hadi Dar es salaam ili kupata Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa ambako ni mbali na hivyo kuongeza gharama mara dufu.

iv. Ongezeko kubwa la ushuru na tozo kwa wenye Viwanda vya uchakataji na uuzaji wa mabondo. Tozo hizi zinajumuisha ushuru wa ukusanyaji mabondo unaolipwa Manispaa wa shilingi **1,000,000:00** kila mwezi bila ya kujali kama mwenye kiwanda ameuza mabondo au la, Ushuru wa Huduma **$ 0.03 %** kwa kila kilo, Tozo ya Atomiki **$ 0.02%** ya kila kilo, na Mrahaba wa shilingi **7,500** kwa kila kilo inayouzwa Nje ya Nchi.

**c) Changamoto zinazowakabili mawakala na wafanya biashara wa samaki**

i. Ukaguzi wa samaki wa mara kwa mara na katika vituo vingi wakati wa usafirishaji samaki na hivyo kupelekea uharibifu wa mazao ya samaki kabla ya kumfikia mlaji na kusababisha hasara kubwa. Kamati ilibaini ukaguzi huu unahusisha Maafisa Uvuvi, Polisi, Wakuu wa Wilaya, Mgambo n.k.

ii. Wafanyabiashara kutozwa Tozo ya Samaki za Chumvi (Kayabo) na Dagaa katika Soko la Samaki la Kimataifa –

Mwaloni lililoko mkoani Mwanza na kwamba tangu mwezi Januari, 2018 wafanya biashara wa samaki katika soko hili wamekuwa wakilipa Tozo ya kusafirisha bidhaa nje (*Export Royality)*, kwa samaki za chumvi na dagaa ambao wanasafirishwa katika maeneo mbalimbali ya Nchi, tozo ambayo hutozwa kwa bidhaa zinazouzwa nje ya nchi ambapo tani moja hulipiwa **shilingi 1,149, 500:00** kwa sasa.

iii. Samaki zinazokataliwa na wenye Viwanda vya Samaki kutorudishwa kwa Wafanya Biashara wa samaki, badala yake kutakiwa kuwauzia Wenye viwanda kwa bei ya hasara ambapo hulipwa sehemu ya asilimia ya thamani ya shehena inayodaiwa kuharibika.

iv. Zana za uvuvi zinazoingizwa Nchini kisheria na zinazoweza kutumika sehemu moja ya nchi kuharibiwa, kutaifishwa au kupigwa faini kubwa isiyoendana na thamani ya zana bila ya uhalali kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Mifugo, changamato mbalimbali zilibainika ambazo zinajumuisha: -

**a) Kituo cha Uhamilishaji Mifugo USA RIVER.**

Kamati imebaini kuwepo kwa muitikio mdogo wa wafugaji katika kutumia huduma ya kuhimilisha mifugo yao, ili kuwa na uzalishaji wenye tija. Aidha Kituo kinakabiliwa na ufinyu wa bajeti na hivyo kukosa vitendea kazi muhimu ikiwa ni pamoja na ukosefu wa gesi ya haijrojeni kwa ajili ya hifadhi salama ya mbegu zinazozalishwa na kusambazwa katika maeneo mbalimbali. Kamati iltaka kufahamu mikakati ya Wizara kuhamasisha wafugaji waweze kutumia teknolojia hii ili waweze kufuga kibiashara na kwa tija.

**b) Mnada wa Kimataifa wa mifugo katika Mpaka wa Longido.**

Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya ushuru mkubwa kwa mifugo ambayo imechochea baadhi wafanyabiashara /wafugaji kuuza mifugo kwa njia za magendo nchi za jirani. Kaika mnada wa Longodo kila mbuzi

hutozwa ushuru wa **shilingi 9,000** na ng'ombe hutozwa kiasi cha **shilingi 35,000.** Aidha, kuna mgawanyo usiowiana wa mapato yanayokusanywa kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**c) Thamani ya fedha zilizotumika katika ujenzi wa awamu ya kwanza na ya pili ya mnada wa Mpakani Longido.**

Kiasi cha **shilingi 782,000,000:00** zilizotumika katika ujenzi wa mnada wa Longido awamu ya kwanza nay a pili hauwiani na thamani ya hali halisi ya miundombinu iliyojengwa katika awamu husika.

**d) Kiwanda cha kuchakata mazao ya mifugo kinchojengwa karibu na mnada wa Longido**

Kiwanda hiki kinajengwa huku hakuna eneo la kuhifadhi (*Holding Ground*) wanyama watakaokua wanasubiri kuchinjwa, ili pamoja na mambo mengine kufika viwango stahiki vya kuweza kuuza nyama Nchi za Nje.

## 2.4 MPANGO WA BAJETI NA UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 28 - 29 Machi, 2019 Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mpango ambao umeandaliwa kwa kuzingatia: -

a) Maelekezo yaliyoko kwenye Mwongozo wa Mpango wa Bajeti ya Serikali wa Mwaka 2019/2020;

b) Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025) Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (*Five Year Development Plan Phase* II – FYDP II);

c) Malengo Endelevu ya Maendeleo (Sustanable Development Goals – SDGs);

d) Mpango wa Uwekezaji katika Kilimo na Usalama wa Chakula Tanzania (*Tanzania Agriculture and Food Security* Investment Plan – TAFSIP);

e) Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015;

f) Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006;

g) Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II);

h) Mpango kabambe wa Mifugo Tanzania (*Tanzania Livestock Master Plan*- TLMP); na

i) Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka 2015.

### 2.4.1 Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/2020 vinatokana na maeneo manne ya kipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17- 2020/21 ambapo katika eneo la ukuzaji Uchumi pamoja na Sekta zingine msisitizo pia umewekwa katika Viwanda vya Uzalishaji wa bidhaa kwa kutumia malighafi kutoka nchini ambazo kwa kiasi kikubwa zinatokana na Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

### 2.4.2 Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imechambua Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kulinganisha na vipengele Kumi na Mbili (12) vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo ya Bajeti wa Taifa wa Mwaka 2019/2020 kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo lengo lake kuu ni kuiwezesha Tanzania kufikia hadhi ya nchi zenye kipato cha kati na kuondokana na umaskini uliokithiri ifikapo 2025.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mambo mengine inatazamiwa ifikapo Mwaka 2025 nchi yetu itakuwa imepitia

katika marekebisho ya kiuchumi kwa kujenga viwanda vya kisasa zaidi ambavyo vitatumia malighafi zinazopatikana ndani na zinazotokana na mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na hivyo kuondoa umasikini kwa kuongeza ajira, vitaongeza masoko ya thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi yanayozalishwa hapa nchini na wananchi wengi waishio vijijini. Aidha, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/2020 ambao umezingatiwa katika uandaaji wa Bajeti umebeba dhima ya **"Kujenga Uchumi wa Viwanda ili kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu ".**[1]

### 2.4.3 Sera ya Taifa ya Mifugo, 2006

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Taifa ya Mifugo inatanabahisha kuwa, Sekta ya Mifugo ina nafasi kubwa katika kujenga Uchumi imara wa Taifa, kuongeza kipato kwa Watanzania wanaotegemea Mifugo, na kutoa fursa za ajira sanjari na kuhifadhi rasilimali za Taifa. Sera hii inaeleza nia ya Serikali na wadau wengine katika kukabiliana na changamoto zinazokabili Sekta ya Mifugo. Jukumu kubwa ni kujenga mazingira mazuri yatakayotoa fursa za kuongeza kipato na ajira kwa wafugaji wadogo, kufuga kibiashara na kuongeza ajira. Ili kufikia haya, malengo makuu matatu ya kisera yatatekelezwa kama ifuatavyo: -

a) Kuendeleza Sekta ya Mifugo itakayokuwa na mwelekeo wa kibiashara, yenye ufanisi na itakayohimili ushindani wa kimataifa;

b) Kuibua mifumo bora ya uzalishaji itakayoongeza tija miongoni mwa wafugaji wadogo; na

c) Kuhifadhi rasilimali za mifugo na kuunda sera na taasisi zitakazosimamia maendeleo na matumizi endelevu ya rasilimali hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Dira ya Sekta ya Mifugo kama ilivyokubaliwa na wadau wa Sekta mwezi Aprili, 2001 inatamka, "**Kuwe na sekta ya mifugo ambayo ifikapo mwaka 2025 kwa sehemu kubwa, itakua na ufugaji wa kisasa na**

**endelevu, yenye mifugo bora yenye uzalishaji mzuri, inayoendeshwa kibiashara na yenye kuboresha lishe ya Mtanzania, kuinua kipato cha mfugaji na Taifa na kuhifadhi mazingira''** Kwa misingi ya Sera hii na Dira ya Sekta ya Mifugo, Kamati inasisitiza juu ya kuongeza kasi ya kufikia malengo yaliyopo, ikiwa ni pamoja na kuwa na uhakika wa chakula, kupunguza umaskini, kuchangia katika uchumi wa nchi na hivyo kuongeza mchango wa Sekta ya Mifugo katika pato la Taifa.

## 2.5 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Mifugo na Uvuvi Fungu 64 na Fungu 99 inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 64,901,756,551:00**. Aidha, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli kiasi cha **shilingi 82,301,458,400:00**.

### 2.5.1 FUNGU 64: SEKTA YA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara kupitia Fungu 64 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi **33,127,378,551:00**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 18,432,461,000:00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **14,694,917,551** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Miradi ya Maendeleo shilingi **3,000,000,000:00** ni Fedha za Ndani na shilingi **11,694,917,551:00** ni Fedha za Nje. Aidha, kwa upande wa maduhuli Wizara kupitia Fungu 64 imepanga kukusanya jumla ya **shilingi 32,301,458,400:00** zitakazopatikana kutokana na mapato yatokanayo na Leseni za kusafirisha samaki na mazao yake (*Export Licenses*), Leseni za uingizaji mazazo ya samaki (*Import Royalty*), Ushuru wa Mrahaba (Export Royalty), Tozo za Maabara na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa Sheria za Uvuvi.

### 2.5.2 FUNGU 99: MIFUGO

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara kupitia Fungu 99 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 31,774,378,000:00**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 28,774,378,000:00**

ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 3,000,000,000:00** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo. Aidha, kwa upande wa Maduhuli Wizara kupitia Fungu 99 imepanga kukusanya jumla ya **shilingi 50,000,000,000:00** zitakazopatikana kutokana na Leseni za kusafirisha wanyama na mazao yake nje ya nchi (*Exporty Duty License fees*), Ada mbalimbali, Ushuru wa Soko (*Market Fee*), Mauzo ya Chanjo na Kodi za Pango la Nyumba za Serikali na Mauzo ya Zabuni.

## 2.6 MALENGO YA UTEKELEZAJI NA VIPAUMBELE KWA SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, fedha zinazoombwa zimepangwa kutekeleza Malengo na Vipaumbele katika Bajeti ya Wizara kupitia Idara Kuu ya Uvuvi Fungu - 64 na Idara Kuu ya Mifugo - Fungu 99.

Kwa upande wa Sekta ya Uvuvi malengo yatakayotekelezwa ni pamoja na: -

a) Kuimarisha usimamizi, Udhibiti na Matumizi Endelevu ya Rasilimali za Uvuvi pamoja na Kutunza Mazingira;

b) Kudhibiti Upotevu wa Mapato ya Serikali yatokanayo na Sekta ya Uvuvi;

c) Kuimarisha Usimamizi wa Rasilimali katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari na Bahari Kuu;

d) Kuimarisha Usimamizi na Udhibiti wa Ubora, Usalama na Viwango vya Samaki na Mazao ya Uvuvi;

e) Kuimarisha Miundombinu na Kukuza Biashara ya Mazao ya Uvuvi;

f) Kuboresha Upatikanaji wa Taarifa Sahihi za Uvuvi;

g) Kuimarisha na Kuongeza Upatikanaji wa Vifaranga vya Samaki;

h) Kuandaa Kanda za Ufugaji wa Samaki katika Maji;

i) Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi; na

j) Kuimarisha Utafiti, Huduma za Ugani na Mafunzo ya Uvuvi;

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Mifugo, Malengo yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na: -

a) Kuimarisha Vituo vya Uhimilishaji Kitaifa na Kikanda;

b) Kuimarisha Usimamizi wa Ardhi kwa Kutenga Maeneo ya Malisho;

c) Kuimarisha upatikanaji wa Maji na Malisho ya Mifugo;

d) Kuimarisha Huduma za Utafiti, Ugani na Mafunzo ya Uzalishaji Bora wa Mifugo ili kupata Bidhaa za Mifugo zenye ubora (Nyama, Maziwa na Ngozi);

e) Kuboresha Masoko na Miundombinu ya Uzalishaji Mifugo na Kuongeza Thamani bidhaa za Mifugo; na

f) Kuimarisha Tiba na Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo.

## 2.7 TATHIMINI YA MALENGO KWA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepitia, kuchambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2019/2020 na kuridhishwa nayo. Hata hivyo, changamoto kubwa imekuwa ni kasi ndogo ya Utekelezaji wa Vipaumbele vinavyopangwa kutokana na ufinyu wa Bajeti inayotengwa na kutolewa. Kamati inaishauri Serikali kutoa Fedha iliyotengwa kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza Malengo na Vipaumbele ilivyojiwekea kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini mambo yafuatayo: -

a) Makadirio ya Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 64 na Fungu 99) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 imeongezeka kwa **asilimia 15** ikilinganishwa na Bajeti inayomalizika ya Mwaka wa Fedha 2018/2019. Aidha, Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Wizara hii yanatarajiwa kuongezeka kwa **asilimia 106** katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 ikilinganishwa na Makisio ya Bajeti inayomalizika ya Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatilia shaka tija ya sekta za mifugo na uvuvi kwa uwiano huu uliopo kati ya ongezeko la **asilimia 15** ya fedha inayoombwa katika Bajeti ya Wizara ikilinganishwa na ongezeko la **asilimia 106** la Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli. Kamati ina maoni kuwa, makusudio ya kuwa na makusanyo makubwa yasiyoendana na uwekezaji katika sekta yanaweza kusababisha athari hasi na changamoto ya tija ndogo katika sekta hizi.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuwa na Sekta ya Mifugo na Uvuvi yenye tija katika Uzalishaji na Kuinua Pato la Wavuvi na Wafugaji ni lazima pawepo na uwiano sahihi ambao utaimarisha Sekta na hivyo kuimarisha uzalishaji na mapato kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande Bajeti ya Miradi ya Maendeleo, Wizara kupitia Fungu 64, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 kuna ongezeko la **asilimia 106** ya fedha inayoombwa. Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hili. Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa, pamoja na ongezeko hili la Bajeti la **asilimia 106,** ambayo ni sawa na jumla ya **shilingi 14,694,917,551,** bado kiasi hiki ni kidogo na hakikidhi mahitaji ya kuwezesha mabadiliko ya kweli katika Sekta ya Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika.** Maoni hayo ya Kamati yanazingatia uhalisia na ukweli kuwa nchi yetu ina rasilimali nyingi za uvuvi, hivyo uwekezaji katika sekta hii unahitaji fedha ya kutosha kuweza kuratibu, kusimamia na kuwekeza katika miundombinu ya msingi ya kuwezesha nchi kunufaika na Rasilimali za Uvuvi zilizopo katika Bahari, Maziwa na Mito, ambapo tafiti zinaonyesha kiwango cha rasilimali za uvuvi kinachoweza kuvuliwa bila kuathiri uwepo wa rasilimali hii ni

**tani za kimetriki 750,000** wakati wastani wa uvunaji wa samaki kwa mwaka ni **tani 350,000** ili hali mahitaji ya samaki kwa mwaka yanakadiriwa kuwa **tani 378,352**.

b) Kwa upande wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo, Wizara kupitia Fungu 99 - Sekta Kuu Mifugo, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020, kiasi kilichotengwa ni pungufu kwa **asilimia 40** kikilinganishwa na kiasi kilichotengwa katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imesikitishwa na kupungua kwa kiasi cha Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Sekta ya Mifugo kutoka **shilingi bilioni 5** katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi kufukia **shilingi bilioni 3,** katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020, ilihali Makisio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Fungu 99, Sekta ya Mifugo ikiongezeka kwa **asilimia 171** kutoka **shilingi 18,467,945,100:00** katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi **shilingi 50,000,000,000:00** katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu wa Makisio Makubwa ya Makusanyo ya Maduhuli bila ya kufanya Uwekezaji wa kutosha katika Sekta ya Mifugo hauna tija katika kuimarisha sekta hii, kwani Sekta ya Mifugo inakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo za Kukosekana kwa Miundombinu ya Msingi kama Malisho, Majosho, Masoko ya Uhakika, Minada na Viwanda vya Usindikaji ili kuwezesha Wafugaji kunufaika ipasavyo na ufugaji na kuweza kuinua kipato cha Wafugaji pamoja na kuchangia katika Pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza kuwa, Mipango na Vipaumbele vilivyopo havinabudi kuwa na uwiano stahiki kati ya Uwekezaji, Kuongezeka tija katika uzalishaji hivyo kuimarika kwa Sekta. Hivyo, ni vema Serikali ikatekeleza dhamira hii kwa kutenga fedha za kutosha kutekeleza mipango iliyopo.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na Maombi ya Fedha kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020. Naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo Tisa (9) yafuatayo : -

### 1. UWIANO WA BAJETI INAYOTENGWA NA MAKUSANYO YA MADUHULI

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Mifugo na Uvuvi ni mojawapo ya sekta zinazochangia ukuaji wa Uchumi wa Taifa kwa kuuza mazao ya mifugo na samaki ndani na nje ya nchi hivyo husaidia nchi kupata Fedha za Kigeni. Aidha, Sekta hizi zina mchango mkubwa katika kuwapatia Wananchi ajira, lishe bora, na kipato. Pamoja na wingi wa Rasilimali za Mifugo na Uvuvi na manufaa yake kwa wananchi na Taifa, changamoto kubwa imekuwa ni ufinyu wa Bajeti kwa ajili ya kutekeleza mipango na vipaumbele katika sekta hizi ili kuziimarisha na kuzifanya kuwa na tija inayostahili na kuchangia ipasavyo katika Pato la Wananchi na Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haijaridhishwa na kukosekana uwiano stahiki kati ya Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Sekta za Mifugo na Uvuvi na makisio ya makusanyo kutoka katika sekta hizi, ambapo Makadirio ya Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 64 na Fungu 99) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 imeongezeka kwa **asilimia 15** ikilinganishwa na Bajeti inayomalizika.

**Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Wizara hii yameongezeka kwa **asilimia 106** kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 ikilinganishwa na makisio ya Bajeti inayomalizika ya Mwaka wa Fedha 2018/2019. Aidha, Bajeti ya Maendeleo kwa ajili ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi **shilingi 17,694,917,551:00,** inayoombwa ni kidogo na hakikidhi

mahitaji ya kuweza kufanya mabadiliko ya kweli katika Sekta ya Uvuvi na Mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa, makusudio ya kuwa na makusanyo makubwa yasiyoendana na uwekezaji katika sekta yanaweza kusababisha athari hasi na changamoto ya tija ndogo katika sekta hizi. Hivyo, ili kuwa na Sekta za Mifugo na Uvuvi yenye tija katika uzalishaji na kuinua Pato la Wavuvi na Wafugaji ni lazima pawepo na uwiano sahihi ambao utaimarisha sekta na matokeo yake kuimarisha uzalishaji na mapato kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza kuwa, mipango na vipaumbele vilivyopo havinabudi kuwa na uwiano stahiki kati ya uwekezaji, kuongezeka tija katika uzalishaji hivyo kuimarika kwa sekta hizi ili ziweze kuchangia katika uchumi ipasavyo. Hivyo ni vema Serikali ikatekeleza dhamira hii kwa kutenga fedha za kukidhi kutekeleza mipango iliyopo kikamilifu na kuongeza mchango wa Sekta katika Pato la Wafugaji na kukuza uchumi kwa ujumla.

## 2. TAHADHARI KUHUSU ATHARI ZA MABADILIKO YA TABIANCHI KWA SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,** athari za Mabadiliko ya Tabianchi zinazoendelea Duniani kote zinaathiri kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa Sekta za Mifugo na Sekta za Uvuvi. Nchini Tanzania aina ya ufugaji unaofanyika ni wa asili na unategemea upatikanaji wa malisho na maji kulingana na misimu ya mvua ambayo umeathiriwa na Mabadiliko ya Tabia Nchi. Aidha, utafiti unaonyesha kuwa shughuli za uvuvi baharini na hasa katika Nchi maskini zaidi Duniani ikiwemo Tanzania zitaathirika sana sanjari na kupungua kwa kiwango cha maji baridi ifikapo mwaka 2050[2] ambayo hutegemewa kwa kiasi kikubwa na shughuli za uvuvi wa baharini na ziwani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huu Mabadiliko ya Tabia ya Nchi yanaathiri jamii ya Wafugaji hususan katika upatikanaji wa malisho na maji ambayo ni mahitaji muhimu katika ufugaji. Kwa upande mwingine kumekuwa na punguzo

la kina katika vyanzo vya maji baridi hususan kwenye mito na maziwa ambayo kwa kiasi kikubwa hutegemewa na Wavuvi wadogo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto ya Mabadiliko ya Tabia Nchi, bado Serikali haijaweka mkazo kwa kuchukua hatua za kukabiliana nazo. Kamati inaishauri Serikali kuweka mkazo kwenye uongezaji wa nyanda za malisho na mabwawa kwa ajili ya mifugo kwani ongezeko la idadi ya mifugo halina uwiano na ongezeko la maeneo ya malisho na maji ya kunyweshea mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Kamati inaishauri Serikali kuweka na kuanza kutekeleza Mikakati ya kuimarisha Teknolojia za Ufugaji wa Samaki katika Vizimba, Mabwawa, Mito na Matanki ili kuongeza uzalishaji wa samaki. Aidha, ili kuweka mazingira wezeshi Serikali ione namna ya kupunguza kodi kwa baadhi ya teknolojia, vifaa na nyenzo za kuchimba mabwawa na kufuga samaki ambao matumizi yake yameendelea kuongezeka kutokana na umuhimu wa samaki kwenye mwili wa binadamu.

## 3. KUIMARISHA TIJA NA MCHANGO WA SEKTA NDOGO YA MAZIWA ILI KUINUA UCHUMI WA WAFUGAJI NA PATO LA TAIFA

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, nchini Tanzania, uzalishaji wa maziwa umefikia lita billion 2.4. Na kwamba, kati ya kiasi kinachozalishwa ni asilimia 2 tu, sawa na lita milioni 37.5 ndicho kinasindikwa katika viwanda 62 vya usindikaji maziwa vilivyopo nchini.  Uhaba wa viwanda vya kusindika maziwa kunakosesha Wafugaji fursa ya soko la uhakika, ajira, na kupelekea Nchi kutonufaika na mauzo ya maziwa Nje ya Nchi na hivyo kukosa Fedha za Kigeni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa, kutoimarika kwa usindikaji maziwa nchini kunatokana kukosekana kwa mazingira rafiki ya uwekezaji wenye tija. Baadhi ya changamoto za msingi ni pamoja na: -

a) Wingi wa Tozo na Kodi zipatazo Ishirini na Nane (28);

b) Wingi wa Taasisi za Udhibiti na Ukaguzi zipatazo Kumi na Moja (11);

c) Miundombinu duni maeneo yanakozalishwa maziwa kwa wingi;

d) Ushindani usio sawa baina ya Wasindikaji nchini ambapo Wachakataji wa Maziwa ya Unga wamepewa Punguzo la Kodi la **asilimia 87.5** kuingiza maziwa ya unga nchini.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto hizi kwa kiasi kikubwa zinasababisha kuongezeka gharama za uwekezaji katika usindikaji na hivyo Wawekezaji wa ndani kushindwa kumudu ushindani wa bidhaa za maziwa zinazotoka Nje ya Nchi au kushindana na maziwa yanayozalishwa kutokana na maziwa ya unga yaliyopewa punguzo la kodi.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia changamoto hizo, Kamati inaishauri Serikali: -

a) Kutathimini upya uamuzi wa kuweka kodi kwenye maziwa na bidhaa zitokanazo na maziwa ili kuondoa kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT Exempt*) kama ilivyokuwa kwenye Sheria ya Kodi ya mwaka 2012.

b) Kutekeleza mwongozo wa maboresho ya Taasisi simamizi (*Blue Print*) ambayo inalenga kupunguza kero za wingi wa Taasisi za Usimamizi na Udhibiti.

c) Kuboresha miundombinu kwa kuboresha barabara unganishi kufika maeneo ya uzalishaji malighafi zitokanazo na mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

d) Kulinda viwanda vya ndani vya kusindika maziwa ambavyo vinatumia maziwa ghafi (fresh milk) pamoja na kuweka mazingira sawia katika ushindani wa soko. **kwa kuondoa punguzo la kodi ya asilimia 87.5** kwa bidhaa ya maziwa ya unga yanayoingizwa nchini.

e) Kuweka na kutekelza mikakati ya kupunguza kodi ya vifaa vinavyotumika katika mnyororo wa kuhifadhi mazao ya mifugo na uvuvi *(cold storage facilities and chillers).*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini kwa kufanya hivyo kutachochea uwekezaji na hivyo kukuza sekta ndogo ya maziwa, kuinua kipato cha Wafugaji na kuchochea ushindani ulio sawa; na

## 4. MKANGANYIKO WA KISHERIA KUHUSU AINA ZA NYAVU ZA UVUVI ZINAZOPASWA KUTUMIKA WAKATI WA KUVUA SAMAKI

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati imebaini kuwa, kwa muda mrefu kumekuwepo na matamko yanayokinzana kutoka kwa Watendaji Wakuu wa Wizara kuhusu aina za nyavu zinazofaa kwa kuvua samaki aina ya dagaa, haya yanayokinzana na yasiyozingatia Sheria ya Uvuvi kumepelekea matukio ya mara kwa mara ya Wavuvi kuchomewa nyavu zao za kuvulia samaki ambazo ni moja ya dhana muhimu katika shughuli za uvuvi na hivyo kuwaletea wavuvi hasara kubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilitoa agizo la kuwataka Wavuvi kuvua dagaa kwa kutumia nyavu zenye ukubwa wa tundu la mm 8, hata hivyo utekelezaji wa katazo hili umekuwa na mkanganyiko kwani kuna baadhi ya maeneo nyavu hizo zinachomwa moto na baadhi ya maeneo nyavu zenye ukubwa huo huo zinaruhusiwa. Kwa mfano; eneo la Kilwa Nyavu za **mm 8** zimeruhusiwa kuvua dagaa, ilihali wavuvi kutoka eneo la Kojani mkoani Tanga nyavu za aina hiyo hiyo zimeteketezwa kwa moto.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Taarifa za Kitaalamu zinaonyesha kuwa kuna baadhi ya samaki walioko Baharini na Ziwani ambao hata wasipovuliwa kwa miaka Kati ya 10 - 20 hawawezi kuwa wakubwa kama dagaa kutokana na uhalisia wa maumbo yao ya kibailojia. Kamati inashauri samaki wa aina hii na dagaa waruhusiwe kuvuliwa na nyavu zenye matundu ya ukubwa wa **mm 8 - 10.**

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Kamati inashauri Wataalamu wa Uvuvi wafanye Utafiti ili kubaini ukubwa wa dagaa na samaki kulingana na maeneo ili makatazo yanayotolewa yaweze kuendana na hali halisi ya eneo husika badala ya kuwa ni

makatazo ya ujumla kwa Nchi nzima. Kwa mfano; katazo lililotolewa la kuzuia kutumia matundu ya nyavu zenye ukubwa wa **mm 8** utekelezaji wake umekuwa mgumu kwa upande wa wavuvi wa Visiwa vya Ukerewe kutokana na ukweli kwamba ukubwa wa dagaa wanaopatikana Ukanda wa Ziwa Victoria hawajakua na kufikia ukubwa wa **mm 8**.

## 5. MLUNDIKANO WA NGOZI GHAFI ULIOPO KWENYE MAGHALA NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilianzisha Tozo ya Ushuru wa 80% ya ushuru wa ngozi ghafi (*Export Levy*) kwa nia ya kulinda viwanda vya ndani ili visikose malighafi za viwanda. Nia ya Serikali ilikuwa nzuri na ni ya kupongezwa, hata hivyo hali imekuwa tofauti kutokana na ukweli kwamba viwanda vingi vya kuzalisha bidhaa za ngozi havizalishi na vingine vimefungwa, vimeuzwa na kubadilisha matumizi na hivyo kupelekea mlundikano wa ngozi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** hadi hivi sasa kuna mlundikano wa ngozi zitokanazo na **ng'ombe** kwa wastani wa vipande zaidi ya **milioni moja na nusu** na vipande **milioni mbili** vya ngozi itokanayo na **mbuzi na kondoo** ambazo zimehifadhiwa kwa wazalishaji na wakusanyaji ngozi nchi nzima, ambazo zimeendelea kuharibika na kusababisha hasara kwa wakusanyaji, wazalishaji na wafugaji kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uwezo mdogo wa viwanda vya ndani kuzalisha bidhaa za ngozi, na kwa kuwa soko la uhakika la ngozi linapatikana katika Bara la Ulaya na Asia, Kamati inaishauri Serikali kuwa, wakati ikiendelea na mchakato wa kufufua viwanda vya bidhaa za ngozi nchini, ipunguze ushuru wa ngozi ghafi wa **asilimia 80** hadi kufikia **asilimia 20** ili kuwasaidia wazalishaji na wakusanyaji ngozi kuuza ngozi ghafi Nchi za Nje na hivyo kupunguza mlundikano wa ngozi uliopo, hatua ambayo itawasaidia Wafugaji kuongeza kipato.

## 6. KUIMARISHA TIJA KATIKA SHUGHULI ZA UVUVI, BIASHARA NA UCHAKATAJI SAMAKI

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia malalamiko ya wadau mbalimbali wa Sekta ya Uvuvi, ikijumuisha Wavuvi wenyewe, Wafanyabiashara wa samaki na Mawakala pamoja na wenye Viwanda vya kuchakata samaki, Kamati imebaini kuwa, msingi wa malalamiko yaliyopo ni kukosekana mazingira bora na yenye tija katika shughuli za uvuvi kibiashara. Kamati inaishauri Serikali kushughulikia changamoto zilizopo kwa kufanya yafuatayo: -

a) Kutekeleza kwa vitendo Mwongozo wa Maboresho ya Taasisi Simamizi (*Blue Print),* hatua hii itapunguza wingi wa kodi, ada na tozo mbalimbali ambazo kwa sasa ni kikwazo katika kuleta tija kwenye shughuli na uwekezaji nchini;

b) Kupanua na kuimarisha kiwanja cha Ndege cha Mwanza kufikia Viwango vya Kimataifa kwa ajili ya kuwezesha urahisi wa usafirishaji minofu ya samaki Nje ya Nchi;

c) Kuongeza na kusimamia kikamilifu doria katika ziwa Victoria kwa ajili ya kuimarisha usalama wa Wavuvi na mali zao awapo ziwani dhidi ya vitendo vya unyang'anyi na ujangili;

d) Kuimarisha Usimamizi na Upatikanaji wa Zana Bora za Uvuvi nchini;

e) Kusimamia ipasavyo miongozo na nidhamu ya Watendaji wa Serikali wanatekeleza operesheni na doria mbalimbali.

## 7. MABORESHO YA SERA NA SHERIA YA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha mchakato wa maboresho ya Sera na Sheria ya Uvuvi, pamoja na pongezi hizo Kamati inaishauri Wizara kuharakisha mapema iwezekanavyo mchakato wa maboresho ya Sera na Sheria ya Uvuvi ili ziweze kutatua changamoto mbalimbali zinazokwamisha ufanisi hii. Hatua

hii itaimarisha ufanisi wa Sekta ya Uvuvi, tija na mchango katika mapato ya wadau na Pato la Taifa kwa ujumla.

## 8. UWEKEZAJI KATIKA UVUVI WA BAHARI KUU

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini kuwa Serikali inatambua fursa kubwa ya rasilimali zilizopo katika Ukanda wa Bahari Kuu. Na kwamba ipo nia na dhamira ya Serikali kuweka mazingira bora ili kuwezesha uwekezaji wenye tija na kulinufaisha Taifa na mapata ya rasilimali zilizopo. Kamati ina maoni kuwa, kutotekeleza nia na dhamira hii njema, kunatoa fursa kwa nchi nyingine kuzitumia rasilimali zilizopo kwenye ukanda wa eneo la bahari kuu ambalo hatuwezi kuwazuia. Zipo taarifa kuwa **asilimia 67** ya samaki aina ya Jodari.

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonyesha samai aina ya Jodari waliouzwa Duniani kwa kipindi cha mwaka 2018 wanatoka katika eneo la Ukanda wa Bahari Kuu –Tanzania. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu na kuchukua hatua mahsusi za kuweka mazingira wezeshi na kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu kwa: -

a) Ujenzi wa viwanda vya kuchakata samaki aina ya Jodari kwenye Ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi

b) Ununuzi wa meli za kufanya uvuvi katika Bahari Kuu ya eneo la Tanzania na

c) Ujenzi wa maeneo ya kuhifadhia samaki na mazo yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza Serikali kujiridhisha na mikataba iliyopo kuhusu ujenzi wa bandari ya uvuvi, na endapo zitabainika kasoro, basi hatua madhubuti zichukuliwe kuzimaliza kasoro hizo ili kutoa nafasi ya utekelezaji wa ujenzi kuanza.

### 9. KUIMARISHA UFUGAJI WA VIUMBE KWENYE MAJI NA UKUZAJI WA SAMAKI KATIKA VIZIMBA (AQUACULTURE)

**Mheshimiwa Spika,** ufugaji wa viumbe kwenye maji na ukuzaji wa samaki katika vizimba ndio njia mbadala ya kuongeza uzalishaji wa samaki hivyo kuwezesha upatikanaji wa samaki endelevu. Hata hivyo, ufugaji wa samaki kwenye vizimba unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile Ufinyu wa Bajeti, Ukosefu wa Takwimu za uhakika za Sekta, uhaba wa Maafisa Ugani, Ukosefu wa Elimu na Mitaji, pamoja na Ukosefu wa Teknolojia na Nyenzo za Kisasa.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia changamoto hizo, Kamati ina maoni kuwa ni vyema Serikali ikapata takwimu za uhakika kuhusu wingi wa samaki katika vyanzo mbalimbali nchini, mahitaji ya samaki na upungufu uliopo. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa kuanzisha mfuko maalum (*Aquaculture Fund*) kwa ajili ya kugharamia miradi ya ufugaji samaki ili kuwezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika kilimo/ ufugaji wa samaki.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga J. Mpina, (Mb), na Naibu Waziri Mhe. Abdallah Hamis Ulega (Mb), Katibu Mkuu – Uvuvi Dkt. Rashid Tamatamah na Katibu Mkuu - Mifugo Prof. Elisante Ole Gabriel pamoja na Wataalamu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati Kamati ikichambua na kujadili Bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake.

Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa , Mb | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Dkt. Christine G.Ishengoma, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Emmanuel Papian John, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe.Eng. Edwin A. Ngonyani , Mb | “ |
| 5. Mhe. Justine Joseph Monko, Mb | “ |
| 6. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga , Mb | “ |
| 7. Mhe. Katani Ahmad Katani, Mb | “ |
| 8. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb | “ |
| 9. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb | “ |
| 10. Mhe. Haroon Mullah Pirmohamed, Mb | “ |
| 11. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb | “ |
| 12. Mhe. Lucy Saimon Magereli , Mb | “ |
| 13. Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo, Mb | “ |
| 14. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb | “ |
| 15. Mhe. Omar Abdallah Kigoda, Mb | “ |
| 16. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb | “ |
| 17. Mhe. Devotha Mathew Minja, Mb | “ |
| 18. Mhe. Pascal Yohana Haonga, Mb | “ |
| 19. Mhe. Haji Khatibu Khai, Mb | “ |
| 20. Mhe. Sikudhani Yasin Chikambo, Mb | “ |
| 21. Mhe. Mbaraka Salim Bawazir, Mb | “ |
| 22. Mhe. Juma Ali Juma, Mb | “ |
| 23. Mhe. Anthony Calist Komu, Mb | “ |
| 24. Mhe. Haji Ameir Haji, Mb | “ |
| 25. Mhe. Mattar Alli Salum, Mb | “ |
| 26. Mhe Jivu Vrajlal Soni, Mb | “ |

**Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi – Sehemu ya Kamati za Huduma za Jamii Ndg. Dickson Bisile pamoja na Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Virgil Mtui na Ndg. Rachel Nyega pamoja na msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John kwa kuihudumia Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita na naomba kuwasilisha.

Mahmoud Hassan Mgimwa, (Mb)
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO,**
**MIFUGO NA MAJI**
21 MEI, 2018

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Mheshimiwa Mahmoud. Sasa tunaendelea na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi karibu.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nitoe shukrani kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuniamini na kunipa madaraka ya kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii. Pia niwashukuru wadau wa Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Sekretarieti ya Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano ambao wanautoa kwangu na

Wabunge wetu katika kutupatia uzoefu na uhalisia wa sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umuhimu wa Sekta za Mifugo na Uvuvi. Mifugo na Uvuvi ni sekta muhimu sana kwa uchumi na maendeleo ya nchi na Watanzania kiujumla. Sekta ndogo ya mifugo inaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa katika uchumi wa nchi kama uwekezaji utafanyika inavyotakiwa. Sekta hii inaajiri takribani asilimia 50 ya Watanzania ambayo ni watu takribani milioni 27 na inachangia asilimia 6.9 kwenye Pato la Taifa. Shughuli za Uvuvi zinachangia asilimia 2.2 ya pato la taifa. Baadhi ya maeneo ya nchi yetu uvuvi ndio shughuli kuu ya uchumi. Kwa mfano asilimia 30 ya wakazi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji wanaishi kwa kutegemea shughuli za uvuvi. Hali ni hiyo hiyo kwa mifugo kwa maeneo ya wafugaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia na Sekta ya Mifugo; katika mwaka wa fedha 2017/2018 Tanzania ilikuwa na ng'ombe takriban milioni 30.5. Idadi hiyo inaifanya Tanzania kuwa nchi ya tatu kuwa na ng'ombe wengi Barani Afrika baada ya Ethiopia na Sudani. Katika mwaka huo huo idadi ya mifugo mingine kama kondoo na mbuzi ilikuwa ni milioni 23.8. Hata hivyo Tanzania iliuza nje nyama tani 3,162 tu na kuagiza kutoka nje nyama tani 900 katika mwaka wa fedha 2017/2018. Uzalishaji wa nyama nchini ulipungua kutoka tani 650,000 mwaka 2016 mpaka tani 560,000 mwaka 2017/2018. Kwa hali hii ni dhahiri kuwa, wingi wa mifugo nchini haumsaidii Mtanzania kuondokana na umasikini. Upungufu wa uzalishaji wa nyama uliendana na upungufu wa uzalishaji wa bidhaa nyingine kama vile maziwa.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Sekta ya Mifugo iliipatia Serikali mapato ya shilingi bilioni 20.876 na hadi kufikia mwezi Februari kwa mwaka wa fedha 2018/2019 fedha ambazo zilikuwa zimeshakusanywa kutoka katika sekta hiyo, zilikuwa shilingi bilioni 22.885. Hiki ni kiwango kidogo mno cha mapato kutoka kwenye sekta inayochangia pato ghafi la taifa kwa takribani asilimia saba. Mwaka huo mapato ya ndani ya Serikali yalitarajiwa kuwa shilingi trilioni 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mifugo inayochangia asilimia saba ya shughuli za uchumi nchini na kuingiza mapato kwa chini ya asilimia 0.05 ya mapato yote ya ndani ya Serikali, hii ni changamoto kubwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuwekeza zaidi katika Sekta hii ya Mifugo na kuweka mazingira mazuri kwa Sekta Binafsi kuwekeza, ili kuendelea kupata mavuno ya kutosha na kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 sekta ya uvuvi imeipatia Serikali shilingi 25.7 na hadi kufikia mwezi Machi kwa mwaka wa fedha 2018/19, Serikali imejipatia shilingi 23.9. Takwimu za hali ya uchumi za mwaka 2017 zinaonesha kuwa mapato yaliyotokana na shughuli za uvuvi hapa nchini huchangia asilimia 2.2 ya Pato Ghafi la Taifa, na tasnia nzima ya uvuvi inachangia asilimia 10 ya mauzo nje ya nchi. Sekta hii ya Uvuvi inaweza kufanya vizuri zaidi na kuivusha Serikali katika hali ya umasikini kama ikipewa kipaumbele inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya nje kwa mwaka kwa bidhaa za uvuvi huchangiwa kwa kiasi kikubwa kutoka maji ya baridi, ambapo inachangia asilimia 75; kati ya hii asilimia 65 ni kutoka Ziwa Victoria. Uvuvi kutoka bahari ya ndani umechangia asilimia 13 na asilimia moja tu kutoka kwa wafugaji wa samaki yaani *Aquaculture*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani mauzo ya nje ya bidhaa za uvuvi yanazidi kushuka mwaka hadi mwaka. Kwa Mfano mwaka 2015 Tanzania iliuza nje mazao ya uvuvi ya thamani ya USD 259 milioni lakini mwaka 2016 mauzo yalishuka mpaka USD 257 milioni na mwaka 2017 ikashuka zaidi mpaka USD 182 milioni, ikilinganisha na mauzo ya USD 832 milioni mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya mchango wenye matumaini kwa Sekta ya Uvuvi katika uchumi wa nchi yetu bado Serikali haijafanya uwekezaji wa kutosha ili kuifanya sekta hii kuwa chanzo cha uhakika cha mapato ya Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kubadili

fikra, na kujipanga upya na kuichukulia Sekta ya Uvuvi kama maliasili inayohitaji ushauri wa kisayansi kwa maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Sekta ya Mifugo. Wafugaji wengi wa Tanzania wanatumia mfumo wa ufugaji huria, mfumo ambao unategemea upatikanaji wa malisho na maji kwa msimu na matokeo yake husababisha wafugaji kuhamahama. Aina hii ya ufugaji ndiyo unaozalisha nyama takribani asilimia 95 kwa matumizi ya ndani na takribani asilimia 5 kwa ajili ya kuuza nje, sambamba na uuzwaji wa ng'ombe wazima kwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zinaonesha kuwa ufugaji wa asili unachangia 7.4% tu ya pato la Taifa na ongezeko la ukuaji wa 2.2% kila mwaka. Ufugaji wa asili unategemewa na idadi kubwa ya Watanzania kwa kuendesha maisha yao na huchangia maendeleo kwa mapana yake. Mchango wa sekta hii ya mifugo katika uchumi upo zaidi kupitia kodi na tozo mbalimbali katika masoko ya mifugo, usafirishaji wa mifugo, ukaguzi wa mifugo, na upatikanaji wa malighafi kwa matumizi ya viwanda mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kwamba ufugaji wa asili unaajiri takribani Watanzania 5,000,000 na unachangia 97% ya mifugo yote nchini na kuwapatia 98% ya Watanzania nyama na maziwa. Ufugaji wa asili pia unachangia 30% ya uzalishaji wa sekta ya kilimo na 18% ya pato ghafi la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa sekta hizi mbili za uvuvi na mifugo ni muhimu sana katika maendeleo ya jamii na nchi kwa ujumla, kuna maeneo kadhaa yakitatuliwa na kuwekeza katika rasilimali watu, teknolojia na fedha, basi sekta hii inaweza kulikwamua Taifa letu kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ndogo ya maziwa; Sekta hii ni kitovu kikubwa cha uchumi hasa kwa wafugaji wadogo wadogo hapa nchini. Uzalishaji wa maziwa hapa

nchini umefika lita bilioni 2.4 kwa mwaka na hii inatokana na idadi ya mifugo iliyopo ambayo kwa sasa inakadiriwa kuwa takribani mifugo milioni 28.4. Pamoja na uzalishaji huo mkubwa wa maziwa; viwanda vyetu vya maziwa vinaweza kuchakata na kusindika asilimia mbili tu ya maziwa yote yanayozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo huo mdogo wa viwanda vyetu kuchakata na kusindika maziwa umesababisha asilimia 98 ya maziwa yanayozalishwa kukosa soko na hivyo kusababisha wafugaji wetu kuendelea kuwa maskini licha ya kuwa na rasilimali nyingi za mifugo pamoja na mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilidhani kwamba, Serikali ingejikita kwenye ujenzi wa maboresho ya viwanda vya maziwa ili kuweza kuwapatia wafugaji wetu soko la uhakika la maziwa, lakini kinyume na matarajio hayo Serikali inanunua maziwa kutoka nje kwa wastani wa lita milioni 13 kila mwaka yenye thamani ya zaidi ya shilingi billioni 17.958, jambo ambalo linakwenda kuua kabisa uchumi wa wafugaji wanaotegemea soko la maziwa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia randama ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya mwaka wa fedha 2018/2019, utaona kwamba, kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2017, bodi ya maziwa ilitoa vibali 417 vya kuingiza maziwa ndani ya nchi yenye thamani ya shilingi bilioni 22.81. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba; fedha hizi zingelipwa kwa wafugaji wanaozalisha maziwa hapa nchini na maziwa hayo kununuliwa ndani ya nchi. Uamuzi wa Serikali kununua maziwa nje ya nchi kwa shilingi bilioni 22.81; ni kujinyima fursa ya kukuza soko la ndani na kuwakosesha wafugaji wanaozalisha maziwa kiasi hicho cha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta Ndogo ya Nyama; takwimu za Serikali zinaonesha kuwa Tanzania tuna viwanda na machinjio ya nyama 25 na vina uwezo wa kuzalisha tani 626,992 za nyama kwa mwaka, lakini uzalishaji kwa sasa ni

tani 81,220 tu kwa mwaka na uzalishaji huu ni chini ya uwezo kwa asilimia 87.05. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za randama ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2018/2019 zinaonesha kuwa jumla ya tani 1,207.93 za nyama ziliuzwa nje ya nchi ikiwa ni pungufu kwa asilimia 44.23 ikilinganishwa na kiasi cha tani 2,165.95 zilizouzwa kwa mwaka 2017/2018. Aidha, tani 472.62 za nyama ziliingizwa nchini kutoka nchi za Afrika ya Kusini, Ubelgiji na Uingereza. Idadi hii ya uingizaji nyama ni pungufu kwa asilimia 61.4 ikilinganishwa na kiasi cha tani 1,224.55 zilizoingizwa nchini kwa mwaka 2017/2018. Jambo hili la upungufu linaweza kuwa ni dalili njema kuwa sasa wafugaji wetu wanaanza kufuga kwa kuzingatia viwango na mahitaji ya soko ama ni kutokana na mahitaji ya soko kubadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Tanzania pamoja na kuwa na ng'ombe wengi bado inaagiza nyama kutoka nje ya nchi na viwanda vya nyama vilivyopo havizalishi kama inavyotakiwa. Tanzania inaagiza tani 2,000 za nyama kila mwaka na wakati huo huo inauza nje tani 2,000 za nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni dhahiri kuwa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi anatamani kuona uwekezaji katika sekta hii ya nyama, lakini kuna upungufu wa viwanda na viwanda vilivyopo vinafanya kazi zake chini ya uwezo wake halisi. Swali la msingi la kuuliza tatizo ni nini katika sekta hiyo hadi viwanda vinashindwa kuwa katika *full production capacity*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ndogo ya Ngozi; ngozi katika sekta ya mifugo ina uwezo mkubwa wa kuchangia maendeleo ya uchumi wa Tanzania. Tanzania ina uwezo wa kuzalisha vipande vya ngozi ya ng'ombe milioni 3.4, vipande milioni 2.0 ya ngozi ya kondoo na vipande milioni 4.4 vya ngozi ya mbuzi. Hata hivyo, sababu zinazofanya ngozi nyingi kuwa na ubora wa chini ni ufugaji usiozingatia kanuni bora za ufugaji ikiwa ni pamoja upigaji chapa ovyo mifugo hususan katika

maeneo muhimu ya ngozi, hali mbaya ya miundombinu ya machinjio, makaro, mabanda ya kukaushia na kuhifadhia ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa nchi yetu ina utajiri mkubwa wa mifugo ambayo ingezalisha ngozi kama malighafi za viwandani na kuongeza pato la Taifa, lakini bado sekta hii ndogo ina mapungufu mengi. Zao la ngozi ambalo linaweza kutuimarishia uchumi kwa kuuzwa nje, soko lake limekuwa likishuka. Mfano, ulinganifu wa mwaka 2016/2017 na 2017/2018 inaonesha upungufu wa shilingi bilioni 31.5 katika mauzo ya ngozi katika hatua ya *wet blue,* kwani mwaka 2017/2018 zao hili liliingiza shilingi bilioni 3.255 badala ya shilingi bilioni 34.7 iliyopatikana mwaka 2016/2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa zaidi ya asilimia 50 ya ngozi zinazozalishwa hapa nchini hutoroshwa nje kwa njia ya magendo, hususan kwenda nchi za Kenya na Uganda na pia kusafirishwa nje kupitia Bandari ya Dar es Salaam. Ni mara chache sana wafanyabiashara wanaofanya magendo hukamatwa na vyombo vya dola. Taifa linapoteza fedha nyingi sana ambazo zingetokana na ushuru wa usafirishaji wa ngozi ghafi nje ya nchi. Aidha, ngozi zinazotoroshwa ni zenye ubora nafuu, hali inayosababisha viwanda vya ndani kupata ngozi zenye ubora wa chini na hivyo kukosa bei nzuri kwenye masoko ikilinganishwa na nchi jirani za Kenya na Uganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu iliyopelekea kushuka kwa biashara ya zao hili ni kutokana na Tanzania pekee kutoza tozo za asilimia 10 kwa bidhaa za ngozi zinazouzwa nje. Tozo hii inapelekea kupunguza uwezo wake wa kushindana kwenye soko la kimataifa na kuwa na bei kubwa ukilinganisha na nchi zingine za jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Takwimu ya Taifa pamoja na Mamlaka ya Mapato *(TRA)* zinaonesha kuna uingizaji mkubwa wa bidhaa za ngozi kuliko bidhaa zinazotengenezwa nchini, hivyo

kutumia fedha nyingi za kigeni, ambapo kwa mwaka 2017 kiasi cha dola za kimarekani 51,216,732 zilitumika kuagiza bidhaa za ngozi na wakati kuna fursa ya kuviendeleza viwanda vyetu kwa kuwa na mikakati ya kujipanua kwenye soko la ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa *TRA* kwa mwaka 2017 takribani vipande 2,913,386 vya ngozi ghafi za ng'ombe na mbuzi na kondoo viliripotiwa; aidha kuuzwa nje ya nchi ama kuingiziwa viwandani kwa ajili ya kusindikwa. Idadi ya uzalishaji wetu wa ngozi ghafi kwa mwaka, kiasi cha ngozi za ng'ombe na mbuzi, kondoo 6,786,033 hupotea au kutoroshwa kwenda nje ya nchi na hivyo kulipotezea Taifa zaidi ya bilioni 52 kwa mwaka iwapo ngozi hizo zingepelekwa nje kwa kufuata taratibu na kulipiwa ushuru stahiki na takriban shilingi bilioni 87.5 kwa mwaka iwapo ngozi hizo zingebakizwa nchini na zote kutumika katika viwanda vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuiangalia sekta hii kwa umuhimu wake; kuwekeza na kuimarisha zao la ngozi sambamba na kuboresha na kudhibiti biashara yake nje na ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto katika Sekta ya Mifugo; huduma za Mifugo kupitia majosho; huduma ya majosho ni hitaji la msingi kwa maendeleo ya mifugo. Hata hivyo, huduma hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo upungufu wa majosho yenyewe lakini pia majosho yaliyopo kuwa katika hali duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za Wizara ya Mifugo na Uvuvi zinaonesha kuna majosho 1,409 yanayofanya kazi huku majosho mengine 1,019 yasiyofanya kazi na hivyo kufanya jumla kuu kuwa majosho 2,428. Aidha, inaelezwa kwamba kuna majosho mengi ambayo yanashindwa kufanya kazi ya kuogeshea mifugo kutokana na wananchi kufanya shughuli za kibinadamu karibu na majosho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na takwimu hizo Wilaya moja tu, mfano ya Kishapu yenye mifugo takribani 775,907 kwa mwaka 2017 ilikuwa na majosho 23, lakini yanayofanya kazi ni majosho manne tu. Kwa upande wa Wilaya ya Hanang, kwa mfano pia zaidi ya mifugo 5,000 huugua na 600 kati ya hiyo mifugo hufa kila mwaka kutokana na maradhi yaletwayo na kupe. Wilaya hiyo ina jumla ya majosho 21, lakini ni majosho sita yaliyokuwa yanafanya kazi, majosho 10 yanahitaji matengezo na mengine manne yanahitaji kujengwa kwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia idadi ya mifugo tuliyonayo kwa takwimu za Mwaka 2017, ng'ombe walikuwa milioni 28.4, mbuzi milioni 17.7 na kondoo milioni 5.1 kulinganisha na majosho tuliyonayo 1,409 tu ni dhahiri kuwa bado hatujakuwa makini katika kuhakikisha huduma kwa mifugo tunaipa kipaumbele. Hata hayo majosho tuliyo nayo bado hatujakuwa na mfumo thabiti wa upatikanaji wa madawa ya kuoshea hiyo mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kiasi gani cha majosho kinahitajika kwa kila Wilaya ili kuwa na ufugaji wenye tija na endelevu kwa manufaa ya jamii husika na kwa nchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maeneo ya Malisho na Migogoro baina ya Wafugaji na Watumiaji wengine wa Ardhi; changamoto nyingine inayoikabili sekta ya mifugo ni upungufu wa maeneo ya malisho. Kutokana na kukosekana kwa mpango madhubuti wa matumizi ya ardhi hapa nchini kumekuwa na mwingiliano wa matumizi ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima na pia Hifadhi za Taifa. Mwingiliano huo umesababisha migogoro kati ya wafugaji na wakulima na pia wahifadhi wa mapori na maeneo tengefu ya Hifadhi za Taifa. Kutokana na tatizo hilo, wafugaji ndio wamekuwa wahanga wakubwa kwani mara zote huonekana kama wavamizi wa maeneo mengine kwa ajili ya malisho ya mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hisia hizo kwamba wafugaji ni wavamizi, kumekuwa na ukatili mkubwa kwa mifugo kutoka kwa wahifadhi dhidi ya mifugo inayokamatwa hifadhini. Askari wa wanyamapori wamekuwa wakiua mifugo na kuwajeruhi wamiliki wa mifugo hiyo kwa sababu ya kulisha mifugo hiyo katika Hifadhi za Taifa. Kwa mfano, mapema mwezi huu Mei, 2019 katika Kijiji cha Buger, kama nimepatia, Karatu, askari wa *TANAPA* wa *Lake* Manyara wameuwa ng'ombe watatu na kuwajeruhi wengine watano kwa kuwapiga risasi na pia kumpiga risasi na kumjeruhi mwenye ng'ombe mguuni. Matukio kama haya yametokea maeneo mengi hapa nchini na kwa idadi kubwa zaidi ya mifugo kuuawa kwa kupigwa risasi na au kukatwakatwa mapanga na wanaodai kuingiliwa katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi; mabadiliko ya tabia nchi yanaathiri sana jamii za wafugaji hususan katika upatikanaji wa malisho ya maji na kusababisha kuongezeka kwa magonjwa mapya kwa mifugo na pia kuwa kichocheo cha migogoro na maeneo ya hifadhi kwa wakulima katika kutafuta malisho hayo. Ni dhahiri na ni muhimu pia, Serikali kuliangalia tatizo hili la mabadiliko ya tabia nchi, ili kujipanga vyema ili kuikabili hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine katika sekta ya mifugo ni kama zifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wadogo wadogo na wale walio katika mnyororo wa uongezaji thamani bidhaa za mifugo wameendelea kuwa kwenye lindi la umaskini kutokana na kukosa fursa na mikakati ambayo itazinufaisha jamii za wafugaji wadogo kutoka Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, mtazamo hasi dhidi ya wafugaji unaotokana na changamoto na matatizo yanayotokana na maeneo ya malisho na mfumo mzima wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mgawo mdogo wa bajeti kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, uwekezaji mdogo wa sekta binafsi kwenye sekta hii kutokana na mazingira yasiyo rafiki kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, vikwazo katika mfumo rasmi wa kupatiwa mikopo ya kifedha kwa wafugaji wadogo wadogo na wa asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, gharama za pembejeo kuwa juu, huduma za dawa za utabibu wa mifugo pamoja na kukosekana kwa teknolojia za kisasa za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, tozo na kodi mbalimbali, mfano; ushuru wa asilimia 10 kwa ngozi zinazosindikwa zinazouzwa nje ya nchi, Uwepo wa kodi na tozo nyingi katika usindikaji wa bidhaa za ngozi nchini, ushuru, kodi na ongezeko la thamani, katika vipuri, vifaa na viatilifu vyote vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi na nane, upungufu wa rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa Sekta ya Mifugo na mchango wake katika uchumi na katika mkakati wa kupambana na changamoto zinazoikabili sekta ya mifugo nchini, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupitia CHADEMA imeeleza kwa ufasaha katika Sera yake ya Kilimo, namna itakavyoboresha sekta ya mifugo pindi itakapopewa ridhaa ya kuongoza Serikali, ili sekta hiyo iweze kuwa na tija kwa wafugaji na pia katika uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Sekta ya Uvuvi; sekta ndogo ya uvuvi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware, muda umeenda naomba uende kwenye hitimisho na mapendekezo ya Kambi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, basi naomba masuala yote yanayogusa, Sekta ya Uvuvi na hotuba hii yaingie katika *Hansard*. Nitaenda kwenye changamoto za Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi, inakabiliwa na changamoto kadhaa inazosababishwa na upungufu katika Sera na Sheria uharibifu wa mazingira; Elimu duni ya shughuli za uvuvi katika jamii; Upotevu na uharibifu mkubwa wa samaki waliokwishavuliwa kutokana na kutokuwepo kwa njia nzuri za uhifadhi; Upungufu katika ufatiliaji wa Sheria ya Uvuvi; Uharibifu mkubwa wa mazalia ya samaki unaosababishwa na aina au njia mbovu za uvuvi; Kutopata pesa za kutosha katika sekta hii kupitia Wizara husika na kwa wakati ili kutekeleza majukumu yanayoainishwa kwenye Mpango kazi wa Wizara na kutokupatikana kwa mikopo ya kutosha na yenye masharti nafuu kwa wafugaji wa samaki na wavuvi; Gharama za zana za uvuvi; na uhaba wa Maafisa Ugani wa Uvuvi ikilinganishwa na mahitaji. Hizi ni baadhi tu ya changamoto katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako naomba nigusie tu kidogo kuhusu suala la nyavu za uvuvi. Kumekuwa na mwendelezo wa wavuvi kuchomewa nyavu zao za kuvulia kila mara na pia kumekuwa na matamko kinzani, kutoka Wizara husika juu ya matumizi ya nyavu sahihi za kuvulia mfano iko mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tu mdogo Wavuvi wa Kilwa, kwa mfano wamechomewa nyavu zao 116 zenye thamani ya shilingi milioni 928 na kutozwa kila mmoja wa hawa wavuvi milioni moja, ilhali wavuvi hao wako kwa mujibu wa Sheria na wamekata leseni husika na wana leseni za uvuvi na leseni za vyombo vya wanaovua zinazotumia nyavu zinazoruhusiwa. Sasa tungependa kupata majibu kutoka kwa Serikali, je, Serikali imejipangaje kuwarudishia fedha waathirika hao waliochomewa nyavu zao ili wavuvi hawa waweze kuendelea na shughuli zao za uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho na mapendekezo ya Kambi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa mapendekezo yake katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kwa kuwa Tanzania ina fursa kubwa zinazopatikana katika Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini katika maeneo kama usindikaji, uongezaji wa thamani, kuboresha masoko, kuboresha njia bora na za kisasa za ufugaji, kuna umuhimu mkubwa wa kuimarisha tafiti katika kupata mbegu na vyakula bora na utengenezaji wa vifaa vya uvuvi, ujenzi wa bandari za uvuvi na bandari kavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, kwa kuwa tayari tumeanza kuziishi athari za mabadiliko ya tabia nchi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuanza kuiona hali hiyo na kuwekea mikakati na utekelekezaji mapema na siyo kusubiri hadi janga la usalama wa chakula kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuna umuhimu wa kutathmini kwa upya kodi, tozo na ushuru mbalimbali katika Sekta hizi mbili za Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kuwepo na uwekezaji mahsusi kwa wajasiriamali wa uvuvi hasa katika ufugaji wa samaki, kaa, lulu kulima wa mwani na uzalishaji wa vyakula mbegu na vifaranga vya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kwa kuwa kuna fursa kubwa kwenye Sekta ya uvuvi ni vyema sasa kuweka mazingira rafiki ili kuwekeza zaidi katika ufugaji wa samaki katika vizimba kwenye maziwa na kwenye mwambao wa bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, kwa kuwa Serikali inalazimika kuagiza samaki kutoka nje kwa fedha za kigeni kila mwaka na ni fedha nyingi kweli kweli, jambo ambalo linazidi kupunguza akiba yetu chache ya fedha za kigeni, hivyo ni muhimu kuwekeza zaidi ili kukuza uzalishaji nchini na kuweza kukabiliana na tatizo hilo katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, Serikali itafute suluhisho la kudumu kuhusu nyavu za kuvulia na kutafuta njia mbadala ambazo ni rafiki kwa mazingira katika kuteketeza nyavu haramu za uvuvi. Ni vyema pia Serikali ikadhibiti vyanzo vya nyavu hizo kabla ya kufika sokoni na kutoa elimu kuhusu uvuvi ambao si endelevu ambao unatumia vifaa haribifu katika maeneo ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, ni vyema Serikali ikapitia Sera ya CHADEMA ili kuboresha utendaji kazi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI, MHESHIMIWA DR. SWARE I.SEMESI (MB), KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19 NA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Yanatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016*

---

## I. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu hoja iliyo mbele yetu.

2. **Mheshimiwa Spika**, aidha, nitoe shukrani kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuniamini na kunipa madaraka ya kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii. Pia niwashukuru wadau wa sekta hii ya mifugo na uvuvi pamoja na secretariat ya Kambi ya

Upinzani kwa ushirikiano ambao wanautoa kwangu na Wabunge wetu katika kutupatia uzoefu na uhalisia wa sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Tanzania kwa ujumla.

## II. UMUHIMU WA SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI

3. **Mheshimiwa Spika**, Mifugo na Uvuvi ni sekta muhimu sana kwa uchumi na maendeleo ya nchi na Watanzania kiujumla. Sekta ndogo ya mifugo inaweza kuchangia kwa kiwango kikubwa katika uchumi wa nchi kama uwekezaji utafanyika inavyotakiwa. Sekta hii inaajiri **takribani 50 %[1] ya watanzania ambayo ni watu takribani milioni 27 na inachangia 6.9 % kwenye pato la Taifa[2].** Shughuli za Uvuvi zinachangia 2.2 % ya pato la taifa. Baadhi ya maeneo ya nchi yetu Uvuvi ndio shughuli kuu ya uchumi, kwa Mfano asilimia 30 ya wakazi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji wanaishi kwa kutegemea shughuli za uvuvi. Hali ni hiyo hiyo kwa mifugo kwa maeneo ya wafugaji hapa nchini.

4. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuanzia na sekta ya mifugo; katika mwaka wa fedha 2017/18; Tanzania ilikuwa na ng'ombe takriban milioni 30.5. Idadi hiyo inaifanya Tanzania kuwa nchi ya tatu kuwa na ng'ombe wengi Barani Afrika baada ya Ethiopia na Sudani. Katika mwaka huo huo idadi ya mifugo mingine kama kondoo na mbuzi ilikuwa ni milioni 23.8, hata hivyo Tanzania iliuza nje nyama tani 3,162 tu na kuagiza kutoka nje nyama tani 900 katika mwaka wa fedha 2017/18. Uzalishaji wa nyama nchini ulipungua kutoka tani 650,000 mwaka 2016 mpaka tani 560,000 mwaka 2017/18. Ni dhahiri kuwa, wingi wa mifugo nchini haumsaidii Mtanzania kuondokana na umasikini. Upungufu wa uzalishaji wa nyama uliendana na upungufu wa uzalishaji wa bidhaa nyingine kama vile maziwa.

5. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2017/18, sekta ya mifugo iliipatia Serikali mapato ya shilingi bilioni 20.876

---
[1]Ministry of Livestock and Fisheries Development-Livestock modernization initiative-2015

[2] Kitabu cha Hali ya Uchumi- 2017

na hadi kufikia mwezi Februari kwa mwaka wa fedha 2018/19 fedha ambazo zilikuwa zimeshakusanywa kutoka katika sekta hiyo, zilikuwa shilingi bilioni 22.885. Hiki ni kiwango kidogo mno cha mapato kutoka kwenye sekta inayochangia pato ghafi la taifa (GDP) kwa takribani 7%. Mwaka huo mapato ya ndani ya Serikali yalitarajiwa kuwa shilingi 19 trilioni.

**6.** **Mheshimiwa Spika,** sekta ya mifugo inayochangia 7% ya shughuli za uchumi nchini na kuingiza mapato kwa chini ya 0.05% ya mapato yote ya ndani ya Serikali, hii ni changamoto kubwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuwekeza zaidi katika Sekta hii ya mifugo na kuweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi kuwekeza, ili kuendelea kupata mavuno ya kutosha na kukuza uchumi wetu.

**7.** **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2017/18 sekta ya uvuvi imeipatia Serikali shilingi 25,727,659,157.00 na hadi kufikia mwezi Machi kwa mwaka wa fedha 2018/19, Serikali imejipatia shilingi 23,901,862,510.79. Takwimu za hali ya uchumi za mwaka 2017 zinaonesha kuwa, mapato yaliyotokana na shughuli za uvuvi hapa nchini huchangia 2.2% ya pato ghafi la Taifa (GDP), na tasnia nzima ya uvuvi inachangia 10% ya mauzo nje ya nchi (Annual fisheries statistics report 2014). Sekta hii ya uvuvi inaweza kufanya vizuri zaidi kwa kuivusha Serikali katika hali ya umasikini kama ikipewa kipaumbele inayostahili.

**8.** **Mheshimiwa Spika**, mauzo ya nje kwa mwaka kwa bidhaa za uvuvi huchangiwa kwa kiasi kikubwa kutoka maji ya baridi, ambapo inachangia 75%, kati ya hii, 65% ni kutoka Ziwa Victoria. Uvuvi kutoka bahari ya ndani umechangia 13% na asilimia moja tu kutoka kwa wafugaji wa samaki (Aquaculture). Tangu Serikali ya awamu ya tano iingie madarakani, mauzo ya nje ya bidhaa za uvuvi yanazidi kushuka mwaka hadi mwaka. Kwa Mfano mwaka 2015 Tanzania iliuza nje mazao ya uvuvi ya thamani ya USD 259 milioni lakini mwaka 2016 mauzo yalishuka mpaka USD 257 milioni na mwaka 2017 ikashuka zaidi mpaka USD 182 milioni, ikilinganisha na mauzo ya USD 832 milioni mwaka 2014.

**Jedwali: Jumla ya Mapato Vs Mapato ya samaki na bidhaa za samaki**

| Mwaka | Jumala ya Mapao ya Serikali | Mapato toka uvuvi na bidhaa zake | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 2017/18 | 27,712,376,692,431.00 | 25,727,659,157.00 | 0.0928 |
| 2018/19 | 32,475,949,753,000.00 | 23,901,862,510.79 | 0.0736 |
| 2019/20 | 33,105,409,726,000.00 | 32,301,458,400.00 | 0.0976 |

Takwimu ni kwa mujibu wa Randama ya Uvuvi fungu 64 ya Machi, 2019 na kitabu cha mapato-volume I

9. **Mheshimiwa Spika,** licha ya mchango wenye matumaini kwa sekta ya uvuvi katika uchumi wa nchi yetu; bado Serikali haijafanya uwekezaji wa kutosha ili kuifanya sekta hii kuwa chanzo cha uhakika cha mapato ya Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kubadili fikra, na kujipanga upya na kuichukulia sekta ya uvuvi kama mali asili inayohitaji ushauri wa kisayansi kwa maendeleo endelevu.

10. **Mheshimiwa Spika**, ulaji wa samaki Tanzania unachangia kwa asilimia 30 tu ya protini inayotokana na nyama, hivyo kutokana na kukua kwa idadi ya watu ni muhimu sana kuongeza upatikanaji wa samaki ili kuhakikisha mchango wa protini ya samaki katika vyakula unaongezeka.

## III. HALI YA SEKTA YA MIFUGO

11. **Mheshimiwa Spika,** wafugaji wengi wa Tanzania wanatumia mfumo wa ufugaji huria, mfumo ambao unategemea upatikanaji wa malisho na maji kwa msimu na matokeo yake husababisha wafugaji kuhamahama. Aina hii ya ufugaji ndio unaozalisha nyama takribani 95% kwa matumizi ya ndani na takribani 5% kwa ajili ya kuuza nje, sambamba na uuzwaji wa ng'ombe wazima kwenda nje ya nchi.

12. **Mheshimiwa Spika,** tafiti zinaonesha kuwa ufugaji wa asili unachangia 7.4% ya pato la Taifa na ongezeko la ukuaji la 2.2% kila mwaka. Ufugaji wa asili unategemewa na idadi

kubwa ya watanzania kwa kuendesha maisha yao na huchangia maendeleo kwa mapana yake. Mchango wa sekta hii ya mifugo katika uchumi ni upo zaidi kupitia kodi na tozo mbalimbali katika masoko ya mifugo, usafirishaji wa mifugo, ukaguzi wa mifugo, na upatikanaji wa malighafi kwa matumizi ya viwanda mbalimbali.

**13.** **Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonesha kwamba ufugaji wa asili unaajiri takriban watanzania 5,000,000 na unachangia 97%[3] ya mifugo yote nchini na kuwapatia 98% ya Watanzania nyama na maziwa. Mifugo ya ufugaji wa asili pia inachangia 30% ya uzalishaji wa sekta ya kilimo na 18% pato ghafi la taifa[4].

**14.** **Mheshimiwa Spika**, japokuwa sekta hizi mbili za uvuvi na mifugo ni muhimu sana katika maendeleo ya jamii na nchi kwa ujumla, kuna maeneo kadhaa yakitatuliwa na kuwekeza katika rasimali watu, teknolojia na fedha, basi sekta hii ina weza kulikwamua taifa letu kiuchumi.

***(a) Sekta Ndogo ya Maziwa***

**15.** **Mheshimiwa Spika,** sekta ndogo ya maziwa ni kitovu kikubwa cha uchumi hasa kwa wafugaji wadogo hapa nchini. Uzalishaji wa maziwa hapa nchini umefikia lita bilioni 2.4 kwa mwaka; na hii ni kutokana na idadi ya mifugo iliyopo ambayo kwa sasa inakadiriwa kuwa takriban milioni 28.4. Pamoja na uzalishaji huo mkubwa wa maziwa; viwanda vyetu vya maziwa vinaweza kuchakata na kusindika asilimia 2 tu ya maziwa yote yanayozalishwa nchini.

**16.** **Mheshimiwa Spika,** uwezo huo mdogo wa viwanda vyetu kuchakata na kusindika maziwa umesababisha asilimia 98 ya maziwa yanayozalishwa kukosa soko, na hivyo kusababisha wafugaji wetu kuendelea kuwa maskini licha ya kuwa na rasilimali nyingi za mifugo pamoja na mazao yake.

---

[3] http://41.73.194.134/xmlui/handle/123/320 -**Ufugaji bora wa ng'ombe**: Desemba -2016

[4]Taarifa ya asasi zinazofanya kazi na wafugaji wa asili kuhusu migogoro ya ardhi tanzania

**17.** **Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilidhani kwamba, Serikali ingejikita kwenye ujenzi na maboresho ya viwanda vya maziwa ili kuweza kuwapatia wafugaji wetu soko la uhakika la maziwa lakini kinyume na matarajio hayo Serikali inanunua maziwa kutoka nje kwa wastani wa lita milioni 13 kila mwaka yenye thamani ya zaidi ya shilingi billion 17.958, jambo ambalo linakwenda kuuwa kabisa uchumi wa wafugaji unaotegemea soko la maziwa (Rejea randama fungu 99 ya machi 2019 aya 4.4.4 uk 18 & 19).

**18.** **Mheshimiwa Spika**, ukiangalia randama ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya mwaka wa fedha 2018/19(uk.27) utaona kwamba, kuwa kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2017, bodi ya maziwa ilitoa vibali 417 vya kuingiza maziwa ndani ya nchi vyenye thamani ya shilingi bilioni 22.81. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba; fedha hizi zingelipwa kwa wafugaji wanaozalisha maziwa hapa nchini, na maziwa hayo kununuliwa ndani ya nchi. Uamuzi wa Serikali kununua maziwa nje ya nchi kwa shilingi bilioni 22.81; ni kujinyima fursa ya kukuza soko la ndani na kuwakosesha wafugaji wanaozalisha maziwa kiasi hicho cha fedha.

***(b) Sekta Ndogo ya Nyama***

**19.** **Mheshimiwa Spika,** takwimu za Serikali zinaonesha kuwa Tanzania tuna viwanda/machinjio ya nyama 25 na vinauwezo wa kuzalisha tani 626,992 za nyama kwa mwaka, lakini uzalishaji kwa sasa ni tani 81,220 kwa mwaka. Uzalishaji huu ni chini ya uwezo kwa asilimia 87.05 (*operating under capacity for 87.05 %)*

**20.** **Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa tani 2,165.95 za nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo na punda ziliuzwa nje ya nchi, wakati huo huo jumla ya tani 1,224.55 za nyama ziliagizwa toka nje ya nchi, ikiwa tani 506.05 nyama ya nguruwe, tani 711.03 nyama ya ng'ombe na tani 7.47 nyama ya kondoo. Uagizaji huo uliongezeka kwa asilimia 37.5 mwaka 2017/18 kwa kulinganisha na kipindi kama hicho mwaka 2016/17 cha uagizaji wa tani 890.66; ongezeko hili ni kutokana na kuongezeka kwa soko maalum.

**21.** **Mheshimiwa Spika**, takwimu za randama wizara ya mifugo na uvuvi ya mwaka 2018/19 inaonesha kuwa jumla ya tani 1,207.93 za nyama ziliuzwa nje ya nchi ikiwa ni pungufu kwa asilimia 44.23 ikilinganishwa na kiasi cha tani 2,165.95 zilizouzwa kwa mwaka 2017/18. Aidha, tani 472.62 za nyama ziliingizwa nchini kutoka nchi za Afrika ya Kusini, Ubelgiji na Uingereza. Idadi hii ya uingizaji nyama ni pungufu kwa asilimia 61.4 ikilinganishwa na kiasi cha tani 1,224.55 zilizoingizwa nchini kwa mwaka 2017/18. Jambo hili la upungufu linaweza kuwa ni dalili njema kuwa sasa wafugaji wetu wanaanza kufuga kwa kuzingatia viwango na mahitaji ya soko.

**22.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Tanzania pamoja na kuwa na ng'ombe wengi bado inaagiza nyama kutoka nje ya nchi, na viwanda vya nyama vilivyopo havizalishi kama inavyotakiwa. Tanzania inaagiza tani 2,000 za nyama kila mwaka na wakati huo huo inauza nje tani 2,000 za nyama. *"Utaona kuwa kiasi cha nyama tunachouza nje kwa bei rahisi kabisa, ndio kiasi hicho hicho tunachoagiza kutoka nje kwa bei ya juu, natamani kuona wawekezaji wengi wakiwekeza katika sekta hii kwa sababu fursa zilizopo ni kubwa".*

**23.** **Mheshimiwa Spika,** hapa ni dhahiri kuwa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi anatamani kuona uwekezaji katika sekta hii ya nyama lakini kuna upungufu wa viwanda na viwanda vilivyopo vinafanyakazi zake chini ya uwezo wake halisi. Swali la msingi la kuuliza tatizo ni nini katika sekta hiyo hadi viwanda vinashindwa kuwa katika "*full production capacity*"?

### (e) Sekta ndogo ya Ngozi

**24.** **Mheshimiwa Spika,** ngozi katika sekta ya mifugo ina uwezo mkubwa wa kuchangia maendeleo ya uchumi wa Tanzania. Tanzania ina uwezo wa kuzalisha vipande vya ngozi ya ng'ombe milioni 3.4, vipande milioni 2.0 vya ngozi ya kondoo na vipande milioni 4.4 vya ngozi ya mbuzi. Hata hivyo, sababu zinazofanya ngozi nyingi kuwa na ubora wa chini ni ufugaji usiozingatia kanuni bora za ufugaji ikiwa ni pamoja

upigaji chapa ovyo mifugo hususan katika maeneo muhimu ya ngozi, hali mbaya ya miundombinu ya machinjio, makaro, mabanda ya kukaushia na kuhifadhia ngozi.

**25.** **Mheshimiwa Spika,** japokuwa nchi yetu inautajiri mkubwa wa mifugo ambayo ingezalisha ngozi kama malighafi za viwandani na kuongeza pato la Taifa, lakini bado sekta hii ndogo ina mapungufu mengi. Zao la ngozi ambalo linaweza kutuimarishia uchumi kwa kuuzwa nje, soko lake limekuwa likishuka. Mfano, ulinganifu wa mwaka 2016/2017 na 2017/18 inaonesha upungufu wa shilingi bilioni 31.5 katika mauzo(kwa ngozi hatua ya *wet blue*), kwani mwaka 2017/18 zao hili liliingiza shilingi bilioni 3.255 badala ya shilingi bilioni 34.7 iliyopatikana mwaka 2016/17.

**26.** **Mheshimiwa Spika,** ni kweli kuwa zaidi ya asilimia 50 ya ngozi zinazozalishwa hapa nchini hutoroshwa nje kwa njia ya magendo, hususan kwenda Kenya na Uganda, na pia kusafirishwa nje kupitia bandari ya Dar es Salaam. Ni mara chache sana wafanyabiashara wanaofanya magendo hukamatwa na vyombo vya dola. Taifa linapoteza fedha nyingi sana ambazo zingetokana na ushuru wa usafirishaji wa ngozi ghafi nje ya nchi. Aidha, ngozi zinazotoroshwa ni zenye ubora nafuu, hali inayosababisha viwanda vya ndani kusindika ngozi zenye ubora wa chini na hivyo kukosa bei nzuri kwenye masoko ikilinganishwa na nchi jirani za Kenya na Uganda.

**27.** **Mheshimiwa Spika,** moja ya sababu iliyopelekea kushuka kwa biashara ya zao hili ni kunatokana na Tanzania pekee kutoza tozo ya asilimia 10 kwa bidhaa za ngozi zinazouzwa nje katika nchi wanachama wa Afrika Mashariki. Tozo hii inapelekea kupunguza uwezo wake wa kushindana kwenye soko la kimataifa kwa kuwa na bei kubwa ukilinganisha na nchi zingine za jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

**28.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) pamoja na mamla ya mapato Tanzania (TRA) zinaonesha kuna uingizaji mkubwa wa bidhaa za ngozi kuliko bidhaa

zinazotengenezwa nchini hivyo kutumia fedha nyingi za kigeni, ambapo kwa mwaka 2017 kiasi cha dola za kimarekani (USD) 51,216,732 zilitumika kuagiza bidhaa za ngozi na wakati tuna fursa ya kuviendeleza viwanda vyetu kwa kuwa na mikakati ya kujipanua kwenye soko la ndani.

**29.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa TRA kwa mwaka 2017 takribani vipande 2,913,386 vya ngozi ghafi za ng'ombe na mbuzi/kondoo viliripotiwa; aidha kuuzwa nje ya nchi ama kuingizwa viwandani kwa ajili ya kusindikwa. Kwa idadi ya uzalishaji wetu wa ngozi ghafi kwa mwaka, kiasi cha ngozi za ng'ombe na mbuzi/kondoo 6,786,033 hupotea ama kutoroshwa kwenda nje ya nchi na hivyo kulipotezea taifa zaidi ya bilioni 52 kwa mwaka iwapo ngozi hizo zingepelekwa nje kwa kufuata taratibu na kulipiwa shuru, na takriban shilingi bilioni 87.5 kwa mwaka iwapo ngozi hizo zingebakizwa nchini na zote kutumika katika viwanda vya ndani. Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuiangalia sekta hii kwa umuhimu wake; kuwekeza na kuimarisha zao la ngozi sambamba na kuboresha na kudhibiti biashara yake nje na ndani ya nchi.

## IV. CHANGAMOTO KATIKA SEKTA YA MIFUGO

### *a. Huduma za Mifugo-Majosho*

**30.** **Mheshimiwa Spika,** huduma ya majosho ni hitaji la msingi kwa maedeleo ya mifugo. Hata hivyo, huduma hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo upungufu wa majosho yenyewe lakini pia majosho yaliyopo kuwa katika hali duni.

**31.** **Mheshimiwa Spika,** takwimu za Wizara ya mifugo na uvuvi zinaonesha kuna majosho 1,409 yanayofanya kazi huku majosho mengine 1,019 yasiyofanya kazi na hivyo kufanya jumla kuu kuwa 2,428. Aidha, inaelezwa kwamba kuna majosho mengi ambayo yanashindwa kufanya kazi ya kuogeshea mifugo kutokana na wananchi kufanya shughuli za kibinaadamu karibu na majosho hayo (*kwa mujibu wa daktari mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Kanda ya Ziwa*).

32. **Mheshimiwa Spika,** sambamba na takwimu hizo wilaya moja tu ya Kishapu kwa mfano, yenye mifugo takribani 775,907 (ng'ombe 394,371, mbuzi 248,219, kondoo 133,035 na punda 282) kwa mwaka 2017 ilikuwa na majosho 23 lakini yanayofanya kazi ni majosho 4 tu. Kwa upande wa Wilaya ya Hanang**,** zaidi ya mifugo 5,000 huugua na 600 kati ya hiyo hufa kila mwaka kutokana na maradhi yaletwayo na kupe. Wilaya hiyo inajumla ya majosho 21, lakini ni majosho 6 yaliyokuwa yanafanyakazi, majosho 10 yanahitaji matengezo na mengine 4 yanahitaji kujengwa upya (*taarifa ya madiwani kwenye warsha iliyoandaliwa na Asasi isiyo ya Kiserikali ya SNV pamoja na TAMISEMI).*

33. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuangalia idadi ya mifugo tuliyo nayo kwa takwimu za Mwaka 2017, ng'ombe walikuwa milioni 28.4, mbuzi milioni 17.7 na kondoo milioni 5.1 kulinganisha na majosho tuliyo nayo 1,409 ni dhahiri kuwa bado hatujakuwa makini katika kuhakikisha huduma kwa mifugo tunaipa kipaumbele. Na hata hayo majosho tuliyo nayo bado hatujakuwa na mfumo thabiti ya upatikanaji wa madawa ya kuoshea mifugo.

34. **Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kiasi gani cha majosho kinahitajika kwa kila wilaya ili kuwa na ufugaji wenye tija na endelevu kwa manufaa ya jamii husika na kwa nchi kwa ujumla.

### b. Maeneo ya Malisho na Migogoro baina ya Wafugaji na Watumiaji wengine wa Ardhi

35. **Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine inayoikabili sekta ya mifugo ni upungufu wa maeneo ya malisho. Kutokana na kukosekana kwa mpango madhubuti wa matumizi ya ardhi hapa nchini kumekuwa na mwingiliano wa matumizi ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima na pia hifadhi za taifa. Mwingiliano huo umesababisha migogoro kati ya wafugaji na wakulima na pia wahifadhi wa mapori na maeneo tengefu ya hifadhi za taifa.

**36. Mheshimiwa Spika,** kutokana na tatizo hilo, wafugaji ndio wamekuwa wahanga wakubwa kwani mara zote huonekana kama wavamizi wa maeneo mengine kwa ajili ya malisho ya mifugo yao. Kutokana na hisia hizo kwamba wafugaji ni wavamizi, kumekuwa na ukatili mkubwa kwa mifugo kutoka kwa wahifadhi (askari wanyama pori) dhidi ya mifugo inayokamatwa hifadhini. Askari wa wanyamapori wamekuwa wakiuwa mifugo na kuwajeruhi wamiliki wa mifugo hiyo kwa sababu ya kulisha mifugo hiyo katika hifadhi za taifa. Kwa mfano, mapema mwezi huu wa tano 2019 katika kijiji cha Buger, Karatu, askari wa TANAPA wa Lake Manyara wameuwa ng'ombe watatu na kuwajeruhi wengine watano kwa kuwapiga risasa na pia kumpiga risasi na kumjeruhi mwenye ng'ombe mguuni (ambaye kwasasa anapatiwa matibabu Hospitali ya Selian). Matukio kama haya yametokea maeneo mengi hapa nchini na kwa idadi kubwa zaidi ya mifugo kuuwawa kwa kupigwa risasi na au kukatwakatwa mapanga na wanaodai kuingiliwa katika maeneo yao.

**37. Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa migogoro baina ya wafugaji na wakulima na baina ya wafugaji na wahifadhi inaendelea na kusababisha mauaji ya mifugo na kusababisha uvunjifu wa amani na vifo kwa wahusika; na kwa kuwa sekta ya mifugo ndio tegemeo la mapato ya kiuchumi kwa jamii za kifugaji; na kwa kuwa sekta ya mifugo ina mchango mkubwa katika maendeleo ya uchumi wa taifa; hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imefikia hatua gani katika mgawanyo wa matumizi ya ardhi, ili wafugaji wawe na maeneo maalum ya kutosha kwa malisho ili kupunguza migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na wakulima na baina ya wafugaji na wahifadhi.

### c. Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi

**38. Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabia nchi yanaathiri sana jamii za wafugaji hususan katika upatikanaji wa malisho na maji, na kusababisha kuongezeka kwa magonjwa ya mapya kwa mifugo, na pia kuwa kichocheo

cha migogoro na maeneo ya hifadhi na wakulima katika kutafuta malisho na maji.

**39. Mheshimiwa Spika,** taarifa kutoka Mamlaka ya Maendeleo ya Mataifa ya *IGAD* kwenye kituo chake cha *(ICPAC)* zinasema kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kutokea ukame ambao hautakuwa wa kawaida kwa mikoa yote ya mwambao wa Tanzania, Magharibi ya Kenya, Kusini na Kusini Mashariki mwa Ethiopia, Ukanda wa Kati na Kaskazini Mashariki mwa Somalia, Uganda na Sudani ya Kusini. Maeneo hayo yaliyotajwa kwenye mataifa hayo yatakuwa na kipindi cha ukame na joto kuwa la juu kuliko kawaida na hivyo kuwa na athari kwenye malisho, upatikanaji wa maji kwa matumizi ya binadamu, mifugo na wanyamapori.

**40. Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine katika sekta ya mifugo ni kama ifuatavyo:-

i. Wafugaji wadogo wadogo na wale walio katika mnyororo wa uongezaji thamani bidhaa za mifugo wameendelea kuwa kwenye lindi la umasikini kutokana na kukosa fursa na mikakati ambayo itazinufaisha jamii za wafugaji wadogo kutoka Serikalini.

ii. Mtazamo hasi dhidi ya wafugali unaotokana na changamoto na matatizo yanayotokana na maeneo ya malisho na mfumo mzima wa matumizi ya ardhi.

iii. Mgawo mdogo wa bajeti kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya mifugo

iv. Uwekezaji mdogo wa sekta binafsi kwenye sekta hii kutokana na mazingira yasiyo rafiki ya kibiashara.

v. Vikwazo katika mfumo rasmi wa kupatiwa mikopo ya kifedha kwa wafugaji wadogo na wa asili

vi. Gharama za pembejeo kuwa juu, huduma na dawa za utabibu wa mifugo pamoja na kukosekana kwa teknolojia ya kisasa ya uzalishaji.

vii. Tozo na kodi mbalimbali, mfano; (a) ushuru wa asilimia 10 (export tax)kwa ngozi zilizosindikwa (wet blue) zinazouzwa nje ya nchi, (b) Uwepo wa kodi/tozo nyingi katika usindikaji wa bidhaa za ngozi nchini, (c) Kuondoa ushuru, kodi ya ongezeko la thamani, "*withholding tax*" katika vipuri, vifaa na viatilifu vyote vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi.

viii. Upungufu wa rasilimali watu (wataalam). Hali ya upungufu wa rasilimali watu katika sekta ya Mifugo na Uvuvi ni kama ilivyo kwenye sekta ya kilimo. Watumishi wenye taaluma ya kuanzia shahada na kuendelea wanaohitajika ni 1,936 waliopo kwa sasa ni 867 sawa na asilimia 44.8. Ngazi ya cheti na Diploma wanaohitajika ni 15,000 waliopo ni 3,904 sawa na asilimia 26. Kwa ujumla sekta inahitaji watumishi wataalam 16,936 lakini waliopo ni 4,771 sawa na asilimia 28.1

**41. Mheshimwa Spika**, kwa kutambua uhuhimu wa sekta ya mifugo na mchango wake katika uchumi; na katika mkakati wa kupambana na changamoto zinazoikabili sekta ya mifugo nchini, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupitia CHADEMA imeeleza kwa ufasaha katika Sera yake ya Kilimo, Sura ya 9.4 (Sekta ya Mifugo) namna itakavyoboresha sekta ya mifugo pindi itakapopewa ridhaa ya kuongoza Serikali, ili sekta hiyo iweze kuwa na tija kwa wafugaji na pia katika uchumi wa taifa. Sera inatamka kuwa:-

*"Chadema itapanua wigo na kuboresha ufugaji ili kuwa na bidhaa bora za mifugo pamoja na kuishirikisha sekta binafsi katika kusindika mazao ya mifugo kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Chadema itahakikisha kwamba kuna wataalamu wa mifugo wa kutosha vijijini ili kuleta tija katika ufugaji. Aidha, Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itatoa mafunzo ya ufugaji bora tofauti na uchungaji holela wa mifugo mijini. Hali kadhalika, chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itahakikisha kwamba kuna madawa na chanjo za kutosha kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya mifugo".*

## IV. HALI YA SEKTA YA UVUVI

**42. Mheshimiwa Spika,** sekta ndogo ya uvuvi hapa nchini inaongozwa na Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2015 ambayo inatoa mwelekeo wa sekta katika kukuza na

kuchangia katika uchumi wa Taifa kwa kuweka dira na dhamira ya sekta.

**43.** **Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwa na utajiri wa eneo kubwa la maji lenye fursa kubwa ya uvuvi, Tanzania bado haijaweza kutumia ipasavyo rasilimali hii. Wavuvi wadogo (baharini na maziwa) wanachangia 98% ya sekta nzima ya uvuvi. Sekta hii hutegemea wavuvi wadogo wanaotumia zana duni ambazo ni vigumu kwenda katika maeneo ya kina kirefu cha maji. Pamoja na Tanzania kuwa na Ukanda wa Pwani ya Bahari wenye urefu wa kilomita 1,424 na eneo la maji ya kitaifa (*Territorial Sea)* lenye ukubwa wa kilomita za mraba 64,000 na eneo la bahari kuu lenye ukubwa wa kilomita za mraba 223,000, tumeshindwa kuwa bandari mahususi za uvuvi, na viwanda vikubwa vya uchakataji na usindikaji wa samaki na mazao yake.

**44.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uvuvi wa samaki ya mwaka 2016 inaonesha kuwa kiwango cha raslimali kinachoweza kuvuliwa bila kuleta madhara ya upatikanaji wa rasilimali hiyo ni tani 750,000; na wastani wa uvunaji wa samaki kwa mwaka ni tani 350,000. Aidha, taarifa hiyo inaonesha kuwa tani hizo zinavuliwa na wavuvi wapatao 200,579 ambao hutumia vyombo vya uvuvi vipatavyo 59,338. Aidha, taarifa inaonesha kuwa nchi inaagiza samaki takribani tani 24,000 kila mwezi zenye thamani ya shilingi bilioni 56 (USD 25 milioni) kutoka China, Vietnam na mataifa mengine yaliyozungukwa na bahari ya India.

**45.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeteketeza tani 11 za samaki zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 60 zilizotoka China baada ya kubainika kuwa na kemikali za zebaki zenye madhara ya kiafya kwa jamii na zenye uwezo kusababisha saratani.[5] Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza wananchi, hiyo hasara iliyosababishwa na uzembe itafidiwa na nani? Na Serikali imejipangaje katika kudhibiti uingizaji haramu wa samaki nchini?

[5]Azam TV 11 March 2019

**46.** **Mheshimiwa Spika**, uagizaji wa samaki nchini kwa mwezi ni dola za kimarekani milioni 25 na kwa mwaka ni dola za kimarekani milioni 300. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa kama kweli tungekuwa na dhamira njema ni dhahiri fedha hizo zinazotumia kuagiza samaki kwa mwaka zinatosha kabisa kuufanya uvuvi kuwa wa kisasa na endelevu.

**47.** **Mheshimiwa Spika,** aidha, kwa mujibu wa takwimu za mapato kama yalivyotolewa na "*kundi la Fungamano la vyama na vikundi vya sekta ya uvuvi"* katika soko la samaki Magogoni/Ferry na maeneo mengine, wastani wa mapato yanayochangiwa na wadau wa sekta ya uvuvi kwa taifa kwa soko la samaki Magogoni/Feri kwa mwaka mmoja ni shilingi 8,663,294,000/-, hizi ni stahiki za Serikali peke yake bado mzunguko wa biashara kwa wananchi. Vyombo vya uvuvi vikubwa vinavyotumika katika mwambao wa Dar es Salaam na Pwani ni 3,000 na vyombo vidogo 650, lakini wamiliki wanashindwa kufanyakazi kutokana na mazingira magumu wanayowekewa na watendaji na hivyo kupelekea Halmashauri husika na Serikali kukosa stahiki za mapato kwa maendeleo ya nchi.

**48.** **Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuiangalia vizuri sekta hii ya uvuvi hususan wavuvi wadogo ili wasiendelee kukandamizwa na waweze kuzalisha kwa kuwekewa mazingira rafiki na kufanya shughuli zao kwa kuzingatia sheria na kanuni husika.

**(a) Uvuvi (maziwa, mabwawa na mito)**

**49.** **Mheshimiwa Spika**, takwimu za uvuvi kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, inasema mwaka 2016, sekta ya uvuvi ilikua kwa asilimia 4.2 ikilinganishwa na asilimia 2.5 ya mwaka 2015. Aidha, utumiaji wa mazao ya uvuvi kwa mtu kwa mwaka ni kilo 8.0 ikilinganishwa na kilo 16.7 zinazopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO, 2011). Mwaka 2016 jumla ya tani 362,595 za samaki zilivunwa ikilinganishwa na tani 362,645 zilizovunwa mwaka 2015[6].

[6] *Rejea kitabu cha Hali ya Uchumi 2016 uk.180 aya 29*

**50. Mheshimiwa Spika,** Mwaka 2017 jumla ya tani 387,543 za samaki zilivunwa ikilinganishwa na tani 362,452 zilizovunwa mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 16.6. Kati ya kiasi hicho, tani 332,373 zilivunwa katika maji baridi na tani 55,170 zilivunwa baharini. Aidha, mazao ya uvuvi tani 36,063.2 na samaki hai wa mapambo 101,110 waliuzwa nje ya nchi na kuipatia Serikali ushuru wa mapato kiasi cha shilingi bilioni 10.4 ikilinganishwa na mazao ya uvuvi tani 39,691.46 na samaki hai wa mapambo 65,841 waliouzwa nje ya nchi na kuipatia Serikali ushuru wa mapato kiasi cha shilingi bilioni 14.3 mwaka 2016. Upungufu huu ulisababishwa na kupungua kwa mahitaji na bei katika masoko ya nje[7].

**51. Mheshimiwa Spika,** takwimu hizo za samaki waliovuliwa kwa vipindi hivyo hazihusishi samaki wanaolimwa (aquaculture) na wafugaji wadogo wadogo na wakubwa kama wapo. Ufugaji samaki hutoa fursa mbadala na endelevu, hivyo kupunguza pengo kubwa lililopo la upatikanaji na mahitaji ya samaki. Hivyo, kuna haja kubwa ya kuwekeza kwenye utafiti na uzalishaji katika tasnia ya ufugaji samaki.

**52. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kukosekana kwa takwimu za uvunaji wa samaki wanaofugwa sio bahati mbaya bali ni kutokana na ukweli kuwa uhamasishaji uliofanyika ulikuwa ni kuwaletea hasara wafugaji kutokana na ukweli kwamba Serikali haijajiandaa au kuruhusu sekta binafsi kuwekeza kwenye utafiti wa vifaranga bora (*fingerlings*) kama vile kuku wa nyama au mayai ambavyo vina uhakika wa kutoa mazao bora kama mahitaji yote ya utunzaji yatazingatiwa na hivyo kumletea mfugaji faida na taifa kwa ujumla.

---

[7] (Rejea kitabu cha Hali ya Uchumi 2017 Uk.159 aya 229)

**(b) Uvuvi (bahari kuu)**

53. **Mheshimiwa Spika,** Tanzania ina ukanda wa kilometa 1,424 ambao umegawanyika katika eneo la maji ya kitaifa (territorial sea) lenye ukubwa wa kilometa za mraba 64,000 na eneo la ukanda wa uchumi wa bahari lenye ukubwa wa kilometa za mraba 223,000.

54. **Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kuwa eneo letu lina kina kikubwa na samaki wengi, lakini watanzania hawanufaiki ipasavyo na rasilimali hiyo na badala yake meli za kigeni hufika na kuwavua samaki hao, wengi wakiwa wa aina ya Jodari, samaki wenye gharama kubwa katika masoko ya kimataifa.

55. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ilizindua ndege ya kisasa novemba 2017 itakayofanya kazi ya ulinzi wa rasilimali bahari kuu kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar ili kuchunguza meli za uvuvi zinazovua katika maji yetu ili kuhakikisha rasilimali zilizo katika ukanda wa kiuchumi wa bahari unawanufaisha watanzania.

56. **Mheshimiwa Spika,** katika muendelezo huo wa kuhakikisha rasilimali zinawanufaisha watanzania, Julai, 2018, Waziri alisema kuwa Serikali imenunua meli tano za kisasa ili zifanye kazi kwenye ukanda wa maji ya kitaifa na ukanda wa uchumi wa bahari. Uwekezaji huu uliofanywa ni dhahiri kuwa suala la uanzishwaji wa bandari ya uvuvi na kiwanda cha samaki linatakiwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata maelezo ya kina, kipi hasa kinatakiwa kitangulie kati ya ujenzi wa bandari ya uvuvi, viwanda vya uchakataji samaki ama uwekezaji wa meli za uvuvi? Aidha, tunaomba tupatiwe mchanganuo wa mapato tokea uwekezaji wa ndege na meli ulipofanyika hadi sasa.

57. **Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iondoe mkanganyiko uliopo kati ya wafanyabiashara wa dagaa wanaovuliwa baharini na wanaovuliwa kwenye maziwa katika utozaji wa ushuru *(Export Loyalty)* wa kusafirisha dagaa nje ya nchi. Maana dagaa wanaotoka ukanda wa

pwani tozo yake ni dola za kimarekani 1.5 kwa kilo moja sawa na shilingi 3,400 kwa kilo 1, wakati huo tozo ya dagaa wanaotoka kwenye maziwa ni dola za kimarekani 0.16 kwa kilo moja sawa na shilingi 360 kwa kilo 1. Zamani ushuru wa kusafirisha nje ya nchi dagaa hao hao wa pwani ulikuwa shilingi 300 kwa kilo lakini Serikali imepandisha hadi shilingi 3,400. Ni muhimu sana kama wadau wangefahamishwa sababu hasa za kupandisha tozo kwa zaidi ya asilimia 900.

58. **Mheshimiwa Spika,** mkanganyiko wa tozo kwa wafanyabiashara hasa wa dagaa wa baharini kumewaumiza sana na wengine kushindwa kuendelea na biashara hii. Bei ya kununulia dagaa kwa ndoo moja yenye ujazo wa wastani wa kilo saba ni Tsh. 18,000 hii inamaana kwamba, kiwango cha ushuru kinakaribiana sana na bei ya manunuzi kwa kilo moja. Hali hii imewakatisha tamaa wanunuzi wa dagaa wanaosafirisha nje ya nchi ambako ndiko kwenye soko tegemeo kwa wavuvi na wachuuzi. Hivi sasa wafanyabiashara hao wamepotea kabisa na hawaji tena kununua dagaa jambo ambalo limezorotesha sana uchumi wa maeneo ya uvuvi ukanda wa pwani.

59. **Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali ipitie upya tozo hizi za dagaa hususan kwa upande wa pwani angalau ifikie katika kiwango kinachotozwa kwa dagaa wanaovuliwa kwenye maziwa ili kuweka uwiano mzuri na hivyo kunufaisha wavuvi wa dagaa watokao maeneo ya pwani.

### (c) Ufugaji wa Samaki

60. **Mheshimiwa Spika,** shughuli za ufugaji wa samaki nchini unafanywa na wafugaji wadogo wadogo kwa asilimia kubwa. Ufugaji wa samaki hukabiliwa na matatizo na changamoto kadhaa kama ukosefu wa sera thabiti ya ufugaji samaki; mabadiliko katika sera za uchumi; ukosefu wa teknolojia bora; upungufu wa vifaranga bora; miundombinu ya usafiri kuwa duni; utafiti usiokidhi mahitaji; ukosefu wa takwimu za uzalishaji na upungufu wa taarifa sahihi za utunzaji wa bwawa la samaki.

**61. Mheshimiwa Spika,** kuna uhaba wa idadi ya wataalam wa uvuvi walioajiriwa katika ngazi zote za Serikali, kutoka wilayani hadi taifa. Shughuli za ugani wa ufugaji wa samaki kwa kiasi kikubwa hazifanyiki. Wataalam waliopo ni watu wenye utaalam mkubwa sana na ni hazina kubwa kama kweli wataachwa watoe mwelekeo wa sekta hii bila kuingiliwa na maamuzi ya kisiasa na kuwezeshwa kwa rasilimali fedha.

**(d) Changamoto katika Sekta ya Uvuvi**

**62. Mheshimiwa Spika,** sekta ya uvuvi inakabiliwa na changamoto kadhaa inazosababishwa na;

i. Mapungufu katika sera na sharia

ii. Uharibifu wa mazingira

iii. Elimu duni juu ya shughuli za uvuvi katika jamii

iv. Upotevu/uharibifu mkubwa wa samaki waliokwishavuliwa kutokana na kutokuwepo kwa njia nzuri za uhifadhi wa samaki.

v. Uvuvi uliopitiliza na hivyo kuathiri rasilimali za uvuvi.

vi. Mapungufu katika ufuatiliaji wa sheria ya uvuvi.

vii. Uharibifu mkubwa wa mazaria ya samaki unaosababishwa na aina au njia mbovu za uvuvi.

viii. kutopata fedha za kutosha na kwa wakati ili kutekeleza majukumu yanayoainishwa kwenye mpango kazi wa Wizara

ix. Uwekezaji mdogo katika sekta hii

x. Kutopatikana kwa mikopo ya kutosha na yenye masharti nafuu kwa wafugaji wa samaki na wavuvi; gharama kubwa za zana za uvuvi na uhaba wa maafisa ugani wa uvuvi

ikilinganishwa na mahitaji. Hii ni baadhi tu ya changamoto katika sekta ya uvuvi.

**(e) Nyavu za Uvuvi**

**63. Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na muendelezo wa wavuvi kuchomewa nyavu zao za kuvulia kila mara, na pia kumekuwa na matamko kinzani kutoka wizara husika juu ya matumizi ya nyavu sahihi za kuvulia. Wavuvi kutoka Kojani walioko Tanga wameeleza kuwa, Wizara iliagiza wenye nyavu za mm 8 na 10 ziteketezwe kwa moto, lakini zilizoteketezwa ni mpaka nyavu za mm 15 na 16.

**64. Mheshimiwa Spika**, wavuvi wa Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa, na mwambao wa bahari mpaka sasa wameshachomewa kwa moto nyavu nyingi mno, na kuwaletea hasara kubwa sana wavuvi ambao wamenunua nyavu hizo kwa gharam kubwa, na kuwanyima nyenzo zao za kufanyika kazi za kuwaletea mapato. Nyavu hizi huchomwa na mamlaka husika tena katika mazingira ya wazi, hali ambayo pia inachangia katika uharibifu wa mazingira.

**65. Mheshimiwa Spika,** wavuvi wa Kilwa wamechomewa nyavu zao 116 zenye thamani shilingi 928,000,000/- na kutozwa faini Tshs. 1,000,000/- kila mmoja, wavuvi ambao wapo kwa mujibu wa taratibu; wana leseni za uvuvi na leseni za vyombo na wanavua sehemu zinazoruhusiwa.

**66. Mheshimiwa Spika,** wavuvi wa Tanga waliandika barua ya tarehe 23/03/2019 yenye Kumb. Na. MV/B/4/19 ikielekezwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Tanga wakiomba kurejeshewa nyavu zao zenye gharama ya shilingi 238,000,000/- zilizokamatwa kinyume na sheria; kwani nyavu hizo ni za mm16. Majibu ya barua hii Mheshimiwa Spika bado hayajarejeshwa kwa wahusika, na huu ni mmoja tu wa mifano ya changamoto wanazopata wavuvi juu ya nyavu zao.

**67. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu, Serikali inayojipambanua kuwa ni ya wanyonge

mbona inawafukarisha? hao wanyonge? Aidha, tunahitaji maelezo hizo fedha za nyavu zilizochomwa wakati ni Serikali hiyo hiyo iliyotoa leseni za kutumia nyavu hizo, itawalipa lini au itawasaidiaje waathirika walioharibiwa/kuchomewa vitendekea kazi vyao?

**68.** **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa baharini na ziwani kuna samaki ambao hata wakikaa miaka 10 au 20 bila kuvuliwa hawawezi kuwa wakubwa kama walivyo dagaa na dagaa mchele. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaomba kupewa ufafanuzi dagaa na dagaa mchele wanavuliwa na nyavu za size gani?

**69.** Kinyume na sheria **Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuondoa unyanyasaji usioleta tija kwa watanzania, kwani madhira haya yanazidi kuifanya Tanzania kuwa mbali na uchumi wa kati na kipato cha kati kwa watanzania wote.

## V. UTEKELEZAJI WA BAJETI 2018/19 NA MPANGO WA MAENDELEO 2019/2020

**70.** **Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa haiipi kipaumbele kinachohitajika wizara hii licha ya mchango mkubwa katika kutoa ajira kwa watanzania wengi, na ndio wizara ambayo takriban watanzania wa kariba tofauti katika jamii wanashiriki.

**Jedwali la fedha kwa wizara ya mifugo na Uvuvi kwa fedha za maendeleo**

| Mwaka | Mifugo | | | Uvuvi | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idhinishwa | Tolewa hadi April 2019 | % | Idhinishwa | Tolewa hadi April 2019 | % |
| 2018/19 | 5,000,000,000 | 2,173,188,086.00 | 43 | 7,126,680,000.00 | 4,012,643,853.20 | 56.3 |
| 2019/20 | 3,000,000,000 | | | 14,694,917,551.00 | | |

Chanzo; Taarifa za utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa wizara zilizotolewa Machi, 2019

**71. Mheshimiwa Spika,** ukiangalia fedha zilizotolewa kwa sekta ya uvuvi Fungu 64, inaonesha fedha zote zilizotolewa kwa ajili maendeleo ni fedha za nje na hakuna hata shilingi kutoka fedha za ndani. Hii maana yake ni kuwa Serikali bado haijaona umuhimu wa sekta katika kukuza uchumi wa nchi sambamba na kuongeza kipato kwa watanzania.

## VI. HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA KAMBI

**72. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa mapendekezo yake katika sekta za mifugo na uvuvi katika maeneo yafuatayo:

i. Kwa kuwa Tanzania ina fursa kubwa zinazopatikana katika sekta za mifugo na uvuvi nchini katika maeneo kama; usindikaji, uongezaji wa thamani, kuboresha masoko, kuboresha njia bora na za kisasa za ufugaji, kuna umuhimu mkubwa wa kuimarisha tafiti katika kupata mbegu na vyakula bora na utengenezaji wa vifaa vya uvuvi, ujenzi wa bandari za uvuvi na bandari kavu.

ii. Kwakuwa tayari tumeanza kuziishi athari za mabadiliko ya tabia nchi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuanza kuiona hali hiyo na kuiwekea mikakati wa utekelezaji mapema na sio kusubiri hadi janga la usalama wa chakula kutokea.

iii. Kuna umuhimu kwa kutathimini kwa upya kodi, tozo na ushuru mbalimbali katika sekta hizi mbili za mifugo na uvuvi. Mfano; (a) Kuondolewa tozo ya asilimia 10 kwa usafirishaji wa ngozi (wet blue). Hii itawezesha viwanda vya ndani kuongeza uwekezaji na kuweza kushindana katika soko (b) Tozo katika minada, hii imekuwa ni kero kubwa kwa wafugaji kwani kila mfugo unaoingizwa mnadani hulipiwa (c) kufanya tathimini ya tozo za madawa ya kusindika ngozi

iv. Kuwepo na uwekezaji mahususi kwa wajasiriamali wa uvuvi hasa katika ufugaji wa samaki, kaa, lulu, ukulima wa mwani na uzalishaji wa vyakula, mbegu na vifaranga vya samaki

v. Kwakuwa kuna fursa kubwa kwenye sekta ya uvuvi, vyema sasa kuweka mazingira rafiki ili kuwezkeza zaidi katika ufugaji wa samaki katika vizimba kwenye maziwa, na kwenye mwambao wa bahari

vi. Kwa kuwa Serikali inalazimika kuagiza samaki toka nje kwa fedha za kigeni kila mwaka, jambo ambalo linazidi kupunguza akiba yetu chache ya fedha za kigeni, hivyo ni muhimu kuwekeza zaidi ili kukuza uzalishaji nchini na kuweza kukabiliana na tatizo hilo.

vii. Serikali itafute suluhisho la kudumu kuhusu nyavu za kuvulia, na kutafuta njia mbadala ambazo ni rafiki kwa mazingira katika kuteketeza nyavu haramu za uvuvi. Ni vyema pia Serikali ikadhibiti vyanzo vya nyavu hizo kabla ya kufika sokoni, na kutoa elimu kuhusu uvuvi ambao si endelevu ambao unatumia vifaa haribifu maeneo ya uvuvi.

viii. Ni vyema pia Serikali ikapitia sera ya CHADEMA kuhusu sekta ya Uvuvi ili kubuni na kuboresha shughuli za kibiashara za masuala la uvuvi ambazo zitalenga kuhakikisha kwamba kuna usambazaji wa kutosha wa samaki na bidhaa nyingine za baharini kwa ajili ya matumizi ya wananchi na matumizi ya viwandani ili kukuza pato la Taifa na kuboresha uchumi.

**73.** **Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**...........................**

Dkt. Sware I. Semesi, (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

21.05.2019

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Sware kwa uwasilishaji huo na mapendekezo hayo kwa Serikali. *(Makofi)*

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mmasi dakika moja.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68(7) hasa nikirejea maneno ambayo Mheshimiwa Selasini, Mbunge wa Rombo aliyesimama hapa kunitaja kwa majina yangu mawili, akisema kwamba Ester Mmasi, Mbunge anayewakilisha vijana amekosa adabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirejea maana pana ya neno kukosa adabu; mtu aliyekosa adabu ni mtu asiyekuwa na maana, ni mtu mpumbavu, ni mtu ambaye hana maana wala hana heshima katika nchi yake. Sifa hizi zote mimi sina, kwa sababu sio tu kufundishwa kwa mama yangu, lakini hata chama changu, hakikuwahi kunifundisha tabia hizi mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Selasini kwa kauli aliyoitoa hapo, sio tu amedhamiria kunitusi mimi au kunidhihaki mimi kama Esther, lakini amedhamiria kutukana wanawake wote wa nchi hii kwa sababu mimi nimechaguliwa na wanawake wa Chama cha Mapinduzi wote wa nchi ya Tanzania. nimechaguliwa Pemba na Zanzibar, lakini sio tu hivyo, kwa matusi na kejeli alizozitoa Mheshimiwa Selasini, Mbunge wa Rombo amedhamiria kutukana Jimbo langu kwa wanafunzi ninaowawakilisha wa nchi hii, wanafunzi hao ni wasomi, wamefundishwa katika utu, uadilifu na heshima katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kuomba Mwongozo wa Kiti wa chako, suala hili linaruhusiwa hapa Bungeni na kama haliruhusiwi nini kifanyike? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ahsante sana Mheshimiwa Mmasi, umeeleka na Kanuni yako ya 68(7), tutarudi kwenye *Hansard* tuangalie maneno hayo kama

ameyazungumza kwa namna hiyo tutamtaka ayafute na kuomba radhi.

Waheshimiwa Wabunge kabla ya kumaliza tuna tangazo dogo lilikuwa limechelewa kuja, Mheshimiwa Anna Lupembe anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa Imani ya Kikristo kwamba wanaitwa kuhudhuria katika Kikao kule *basement* hapo sasa hivi baada ya kusitisha shughuli za Bunge na kwamba Askofu Oscar John atakuwepo pamoja na Wahudumu wake katika sehemu hiyo.

Baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10. 00 Jioni)*

*(Saa 10:00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano. Tunaanza na Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Zitto na baadae Mheshimiwa Maftaha anaendelea.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu

Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia mawili; la Kwanza ni Kuhusu Mifugo. Tanzania tuna mifugo mingi sana, kama 32,000,000 lakini mifugo hii inachangia Pato la Taifa asilimia 7.6, ni kidogo sana, kwa sababu mifugo yetu haikuboreshwa. Sasa na suala la kuboresha mifugo ni suala la elimu. Muwaelimishe wafugaji jinsi ya kuboresha mifugo yao na si suala la kusema kwamba punguzeni mifugo, punguzeni mifugo. Tupunguze tuipeleke wapi? Kwa hiyo suala wale maafisa ugani wafanye kazi ya kuelimisha wafugaji jinsi ya kuboresha mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile mifugo inahitaji maji, mabwawa ni shida. Kwa hiyo mimi nilikuwa na shauri kwamba maeneo yote mabwawa yachimbwe ili wafugaji wapate mahali pa kunywesha mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri nimewahi kutembelea Botswana na Namibia. Botswana watu wachache, asilimia ndogo sana lakini wana mifugo haifiki hata 3,000,000 lakini mifugo kwa nchi ya Botswana inachangia takriban asilimia 40 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nasema badala ya kuhimiza watu wapunguze mifugo, mboreshe, muelimishe wananchi ufugaji bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nizungumzie suala la Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania. Niliuliza swali hapa, hata Mheshimiwa Waziri ulikuwepo, ulikuwa Mbunge mwenzangu hapa; kwamba ni lini Serikali itaanzisha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo; na niliomba Makao Makuu yawe Mpwapwa. Kweli Serikali ilitoa jibu kwamba basi tutafanya mpango tuhakikishe kwamba tunaanzisha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania. Hiyo Taasisi imeshaanzishwa lakini jambo la kushangaza Mheshimiwa Waziri kwakweli mimi Mbunge wa Mpwapwa mnanionea. Mmehamisha kituo cha uchunguzi wa magonjwa, *VIC* Mpwapwa mmeleta Dodoma, Dodoma

hakuna vifaa ni majengo yale! Lakini sasahivi majengo ya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo yale yaliyopo majengo yako Mpwapwa yanaharibika, yanachakaa hayana kazi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini mnahamisha vituo vyote? Sasa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ilianzia Mpwapwa leo mnahamishia kwenye maghorofa *NBC* pale, pale ghorofa la *NBC* kuna mifugo? Hivi wageni wakiwatembelea kutoka nje mtakuja kuwaonesha yale maghorofa? Maana kituo cha utafiti ama taasisi inatakiwa Makao Makuu yawe pale ambapo kuna mifugo, hata wageni wakija mnawatembeza kwenye mashamba ya mifugo. Sasa kila kitu mnahamishia Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania Makao Makuu yarudishwe Mpwapwa pale. Jengeni majengo maofisa wote wawe pale. Haiwezekani kabisa! Mifugo iko Mpwapwa Taasisi Makao Makuu kwenye maghorofa ya *NBC,* haiwezekani! Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, umehamisha *VIC,* umehamisha Makao Makuu ya Taasisi ya *TARIRI,* kuja Mpwapwa kuja Dodoma, hapana! Ni kweli Dodoma ni Makao Makuu ya nchi lakini Mpwapwa vilevile iko Dodoma. Kwa hiyo nakuomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliojenga Chuo cha Uchunguzi wa Magonjwa *VIC* wenzenu waliona mbali. Pale kuna Kituo cha Utafiti wa Mifugo, kuna Chuo cha Mifugo na Taasisi ya Uchunguzi wa Mifugo. Hii ilikuwa inasaidia wale wanafunzi walikuwa wanajifunza pale *practicals,* sasa wanasafiri kutoka Mpwapwa kuja Dodoma, gharama gani hii? Gharama kubwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni kuhusu Kituo cha Uchunguzi au Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa. Kile kituo kimeanzishwa mwaka 1905, mimi naanza kusoma darasa la kwanza mwaka 1958, kile kituo n a baba yangu mzazi mimi ndiye alieanzisha kile kituo. Sasa Mheshimiwa Waziri, kituo kina mahitaji mengi sana. Zamani kulikuwa kuna matrekta,

kulikuwa na magari mengi, kulikuwa na vitendea kazi vingi sana; na pale unaposikia Kituo cha Utafiti wa Mifugo kuna mifugo, na ile mifugo inahitaji chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kinahitaji vitendea kazi vya kutosha; wanahitaji mashamba ya kulima majani ili mifugo ipate chakula. Sasa kuna trekta moja tu, hakuna hata jembe moja la kulimia. Hicho ni kituo cha Uchunguzi Mpwapwa, Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakuomba sana katika bajeti yako; nashukuru kwamba umeelezea hapa lakini nakuomba kile kituo ndicho cha kwanza Tanzania, Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa, ndicho cha kwanza. Kwa hiyo naomba ukiboreshe. Tunaomba vitendea kazi vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linguine, Serikali ilipunguza watumishi wahudumu wote pale waliondoka, hakuna hata mhudumu; sasa sijui mlitegemea nani wafanye kazi. Kuna mambo ya *bush clearing,* hao watafiti wana ma-*degree* watakwenda kufyeka kule? Watakwenda kukamua *dairy?* Haiwezekani! Na bahati nzuri kituo kimeajiri vibarua. Wako zaidi ya 76, sasa ni mwaka wa tatu hawajalipwa hata senti tano; na hawa ni binadamu na wana familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba sana hawa vibarua mliowaajiri pale ndio wanaochunga, ndio wanaokamua, ndio wanaofanya kazi zote za nje, walipwe basi haki zao. Mimi nimechoka foleni, kila siku nyumbani kwangu, Mheshimiwa Mbunge tusaidie tulipwe pesa zetu. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, walipwe hela yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Kabla sijagongewa kegele, naunga mkono asilimia 100 Wizara hii lakini Mheshimiwa Waziri ujibu hoja zangu. Usipojibu hizi hoja hasa za kuhamisha Makao Makuu ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo, nakamata shilingi leo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zitto Kabwe, baadae Mheshimiwa Maftaha na Mheshimiwa Charles Tizeba wajiandae.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo. Kwanza napenda niunge mkono Hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni kama ilivyosoma na Dkt. Sware leo, naamini kabisa kwamba Serikali itaweza kuchukua maoni ambayo yameelezwa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na kuweza kuyafanyia kazi kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita kwenye eneo moja tu la uvuvi leo; katika maeneo hayo mawili mifugo na uvuvi mimi nitazungumzia uvuvi peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi kwa mujibu wa takwimu za Serikali unachangia asilimia 2.2 katika Pato la Taifa *(Gross Domestic Product).* Kwa hiyo ukichukua Pato la Taifa la nchi yetu la shilingi trilioni 125 maana yake ni kwamba shughuli za uvuvi, yaani mnyororo wote wa thamani wa uvuvi unachangia shilingi trilioni 3 katika Pato la Taifa la shilingi trilioni 125. Ukichukua Watanzania watu wazima leo, ambao wana uzwezo wa kufanya kazi ambao ni takriban milioni 27 kwa *population* ya watu milioni 54, na kwa takwimu za Serikali kwamba asilimia 50 ya Watanzania wanajishughulisha na shughuli za uvuvi maana yake ni kwamba ukigawa Pato la trilioni 3 kwa mwaka linalotengenezwa na Sekta ya Uvuvi ina maana kila mvuvi nchi hii Pato lake kwa mwaka ni shilingi 230,000 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilinganisha na Pato la mtu *per capita income* ya Mtanzania ya takriban shilingi 2,000,000 unaweza ukaona ni namna gani ambavyo wavuvi katika nchi hii wana hali mbaya sana, wana umaskini wa hali ya juu sana. Tunahitaji mkakati maalum wa kuhakikisha dekta hii kwanza inakuwa inachangia kwa kiwango kikubwa kwa maana ya asilimia 5 kama ambavyo Mpango wa Maendeleo wa Taifa ulivyotaka, lakini tunaona Serikali kiwango cha bajeti ambacho kinawekwa kwenye sekta hii wala huwezi kuamini

kwamba kuna nia ya dhati ya kuweza kuifanya Sekta ya Uvuvi iweze kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la uchaguzi asilimia 30 ya wakazi wake wanategemea uvuvi katika Ziwa Tanganyika, na sasa hivi tumeanza anza pia kufuga samaki. Lakini sasa ukiangalia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapin duzi ukurasa wa 22 Ibara ya 27 kuna ahadi 16 zinazohusiana na Sekta ya Uvuvi. Ahadi 16, ukurasa wa 22 Ibara ya 27 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ambayo ndiyo tunapaswa kuwapima Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Katika ahadi 16 Serikali mpaka sasa tunakwenda kwenye bajeti ya nne haijatekeleza ahadi hata moja ambayo waliitoa kwa wananchi wakati wanaomba kura. Nitawapa mifano ya ahadi tatu tu ambazo mpaka sasa hazijatekelezwa. Chama Cha Mapinduzi waliahidi wakiunda Serikali watanunua meli tano za uvuvi zenye uwezo wa kuvua samaki bahari kuu na kuzalisha ajira 15,000, hakuna hata meli moja imenunuliwa mpaka sasa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama Cha Mapinduzi kiliahidi kujenga bandari ya uvuvi ambayo itaweza kuzalisha ajira 30,000 hakuna hata dalili za kuanza kwa hiyo bandari ya uvuvi. Sasa tunashindwa kuelewa tutawapima namna gani mwaka 2020 sisi wavuvi? Tutawapima kwa nyavu za wannachi ambazo mnazichoma kila siku? Tutawapima kwa mitumbwi ambayo mnawavunjia wananchi kila siku? Tutawapima kwa umaskini ambao mmetengeneza kwa wavuvi katika nchi hii? Naomba Chama Cha Mapinduzi na Wizara ya Mifugo Uvuvi...

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa kidogo.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naom ba Waziri ana nafasi ya kujibu dakiak zake, aniache nitiririke, a-*relax, relax brother!*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto subiri kidogo. Mheshimiwa Waziri, Taarifa.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa Taarifa hii. Naomba nimpe taarifa; kwa kuwa amezungumza jambo kubwa sana linalohusu Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, ingekuwa kama anachangia katika njia ya kawaida pasingekuwa na taabu, lakini anaposema kuwa mpaka kufika sasa mwaka wa nne Serikali ya Chama Cha Mapinduzi katika ahadi tulizozitoa upande wa Sekta ya Uvuvi hakuna tulichokifanya, nataka nimwambie asome vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri ataona yale ambayo tumeyafanya katika kipindi kifupi baada ya Mheshimiwa Waziri Mpina na mimi Naibu wake kuingia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, katika hayo ya uvuvi nataka nimkumbushe atazame liko jambo linalohusu TAFICO. Na nataka nikuambie kaka yangu Zitto ya kwamba huwezi kwenda katiak uvuvi wa bahari kuu bila ya kuanzisha Taasisi ya kusimamia, shirika la kusimamia. Tumeanzisha TAFICO, tumefufua TAFICO kwa lengo la kuhakikisha kuwa tunakwenda kusimamia uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nataka nimuelimishe kidogo katika eneo hili...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umefahamika...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ulishafahamika, Mheshimiwa Zitto, taarifa hiyo.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa siipokei. Mimi nimetaja kurasa ya Ilani ya Chama ambacho yeye ndiyo anapaswa kuitekeleza. Ukurasa wa 22 Ibara ya 27 kuna ahadi 16, hakuna ahadi ya *TAFICO*. Kwahiyo huwezi kujitungia swali na ukajitengenezea jibu, ukajipa tiki, hakuna! Angalieni Ilani yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa uvuvi katika Ziwa Tanganyika tuna malalamiko mengi. Baadhi ya malalamiko yamejibiwa na Serikali lakini pia tutapenda kuona kama wale ambao waliumizwa na maamuzi ambayo sasa Serikali imeyageuza na namna gani ambavyo watakavyofanyiwa *compensations* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza tuna tatizo la tozo, *export,* ushuru wa *export.* Nchi yetu inachimba na inavuna dhahabu. Wawekezaji wa dhahabu wanauza dhahabu nje, hakuna tozo ya *export* ya dhahabu. Kwanini tunaweka tozo ya *export* ya samaki? Tozo ya *export* ya dagaa Ilikuwa dola 1.5 kwa kilo sasa imekuwa dola moja, kiwango kikubwa, tena wanatoza kwa dola. Wavuvi wa Kalya, wavuvi wa Kagunga, wavuvi wa kila mahali wanatozwa kwa dola, ni kwanini? Kwa hiyo naomba tozo hii ya *export* iondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili pamoja na nyavu kuchomwa na pamoja na Serikali kutoa maelezo mengine kuhusiana na suala la nyavu, kama nilivyosema tungependa tufahamu, sasa wale ambao wamechomewa nyavu zao na vyombo vyao ambao Serikali sasahivi imebadilisha sera yake, Serikali itawalipa namna gani? Kwa sababu ni watu ambao wameshaingizwa kwenye umaskini na ningependa kwakweli tuweze kuhakikisha ya kwamba jambo hili linashughulikiwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulisemea ni suala la leseni nyingi kwenye chombo kimoja. Sisi wavuvi boti ya kuvua ndiyo kama trekta kwa mkulima. Trekta kwa mkulima halina leseni sijui ya *SUMATRA,* n.k lakini mvuvi chombo chake cha kufanyia kazi anakata *SUMATRA,* lesseni ya boti, anakata leseni ya mwenye chombo, anakata leseni ya wavuvi, sisi ambao tunatumia vipe kule katika Ziwa Tanganyika unahitaji wavuvi sita kwenye kipe kimoja wote wanahitaji leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeeleza hapa kwamba inaangalia namna ambavyo italirekebisha jambo hili na pia hata leseni ambazo zinaweza kutumika kwenye

zaidi ya halmashauri moja; na nimeona kwamba tayari *GN* namba 383 imeshatoka; lakini jambo ambalo naliomba Serikali ilifanyie kazi ni suala zima la kwamba hakuna haja ya chombo cha uvuvi kuwa na leseni kwa sababu leo hii hata *road license* tumetoa; *road license* tunailipa kwenye mafuta. Mvuvi anapokwenda kuvua ananunua mafuta! Kwa hiyo ina maana na yeye ameshalipia leseni yake moja kwa moja kama ambavyo mwenye trekta alivyo. Kwa hiyo kuna haja kubwa jambo hili liweze kuondolewa kwa sababu ni gharama kubwa kwa wavuvi na haliwezi kuwasaidia wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, pamoja na marekebisho kadhaa ambayo yamefanywa na mapendekezo ambayo tumeyatoa ya tozo n.k. naomba Serikali inipe maelezo kidogo. Ukiangalia takwimu kutoka kwenye kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa utaona kwamba mwaka 2014 tuliuza nje bidhaa za mazao ya uvuvi ya thamani ya dola za Kimarekani million 832. Lakini tangu Serikali ya Awamu ya Tano ya Chama Cha Mapinduzi iingie madarakani mauzo nje ya mazao ya uvuvi yameporomoka mpaka dola milioni 182 kutoka dola milioni 832 mwaka 2014, mwaka mmoja kabla Serikali hii haijaingia madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokiona kila siku na sifa kubwa ambayo Wizara ya Mifugo na Uvuvi inapata ni kuonekana wakiwa na njiti za viberiti wakiwa na mafuta wanachoma nyavu za wavuvi ilhali *exports* zetu kwenye mazao ya uvuvi zinazidi kuporomoka. Tunaomba Wizara hii itakapokuja kujibu hoja za Wabunge hapa waweze kutoa maelezo ya kina ni nini ambacho kinasababisha mauzo nje ya mazao ya samaki yanaporomoka tangu Serikali hii ya Awamu ya Tano iingie madarakani, ni kwasababu ya uchomaji wavuvi wamepungua, ni kwa sababu ya tozo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Kigoma pale kupata mgebuka imekuwa ni tatizo kwa sababu ya amri ambazo Serikali imekuwa inazitoa, mara msitumie vipi, mara msivulie sijui neti, mara msifanye nini. Kwa hiyo, wavuvi wanakuwa hawaelewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia, kuna tatizo kati ya msimamizi wa Wizara, dada anaitwa Judith, mimi simfahamu, nimezungumza na wavuvi, hana mahusiano mazuri na wavuvi wa eneo lote la ukanda wa Ziwa Tanganyika. Naomba Wizara ifanye *consideration* kutazama, kwa sababu kuna *measures* ambazo wamezichukua, basi angalau na msimamizi aweze kubadilika, kwa sababu malalamiko ya wavuvi ni makubwa na tunahitaji wavuvi nao wajione ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa muda ambao umenipatia na hongera sana kwa kazi uliyoifanya leo asubuhi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Maftaha, baadaye Mheshimiwa Charles Tizeba na Mheshimiwa Kiruswa ajiandae.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu wataala* na leo niweze kuongea machache haya kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza naomba nipate ufafanuzi kwa Waziri, Mheshimiwa Zitto kamalizia hapo kusema kwamba, kumekuwa na utaratibu wa Serikali kuchoma nyavu za wavuvi wadogowadogo na hasa maeneo ya ukanda huu wa pwani kutoka Mtwara, pale Mikindani, maeneo ya Kiyanga, lakini pia mpaka kule Kilwa, nyavu zimechomwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kufahamu hapa ni kwamba, wale waliochomewa nyavu zao, wao wanakuwa wamenunua zile nyavu madukani, naomba kujua kutoka kwenye Wizara hii, kwamba Serikali imechukua hatua gani mpaka hivi sasa, ama wanunuzi wangapi walioleta zile nyavu Tanzania wamekamatwa na wameshtakiwa na Wizara hii, badala ya kuwachomea wale wavuvi wadogowadogo ambao wanatafuta fedha kwa shida sana kupata zile fedha

za kununua nyavu na mwisho wa siku wameenda kuwachomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kujua, Mheshimiwa Waziri alipofika Kilwa, amefika Kilwa akawaita wavuvi wa Kilwa wote kwa maneno mazuri sana, akawaambia kwamba tunahitaji hivi sasa tuzungumze na nyinyi kama ndugu, kama rafiki, tunaomba nyavu zenu mzikusanye wenyewe kwa amani. Wale wavuvi wakazikusanya nyavu zao, Mheshimiwa Waziri akasema, nakwenda Dodoma, nakwenda Wizarani halafu nitarudi tena hizi nyavu tumezitunza, lakini anaondoka pale Kilwa, anafika baada ya kilomita tatu, nne, tano, anawaagiza watendaji, chomeni moto hizo nyavu, wakati aliwaahidi kwamba wazitunze! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kujua, kwa nini Mheshimiwa Waziri aliwahadaa wale wananchi akasema zile nyavu za milimita nane zitatunzwa halafu mwisho wa siku akatoka hatua mbili, tatu, akaagiza kwamba zile nyavu zichomwe moto pale Kilwa na wanachi wakawa na majonzi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba kujua, kwamba kulikuwa na hii inaitwa *Operation Jodari* na *Operation Sangala* ambayo Wizara imekuwa inafanya kwenye maziwa makuu kule lakini pia kwenye Bahari ya Hindi kutoa Mtwara mpaka kule Kilwa na maeneo mengine yote mpaka kule Tanga na Zanzibar. Naomba kujua kwa sababu mwaka jana kuna kijana aliuawa pale Mtwara Mjini Kiyanga, mtu ambaye anakwenda kutafuta samaki kwa mikono, kwa kutumia mideki, akapigwa risasi ya kisogoni! Nikazungumza ndani ya Bunge hili, anaitwa Abdillah Abdulrahman, mkazi wa Kiyanga Mtwara Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaeleza kwamba Serikali ichukue hatua juu ya huyu mtu aliyeuawa kwa kisingizio cha *Operation* Jodari ambacho kinafanyika kwenye Bahari ya Hindi. Mpaka leo sijapata majibu, naomba Mheshimiwa Mpina atupe majibu, kwamba yule kijana, ile roho iliyopotea

mpaka leo Serikali imechukua hatua gani, kwa sababu hatujaona tume iliyoundwa, hatujaona chochote, hata kutoa pole Mheshimiwa Waziri, hajaja Mtwara kutoa pole, hata kama mimi nimezungumza humu, zaidi ya mara tatu, mara nne, mara tano ndani ya Bunge hili. Hata nikimsemesha, hata Waziri ukimsalimia, haitikii! Yaani leo ukikutana naye hapo nje, unamsalimia kwa ajili ya kujenga mahusiano, hata kuitikia imekuwa ni shida. Sasa kwa sababu Serikali hii ni sikivu sana, Mheshimiwa Rais anasalimia watu, tunasalimiana naye, Waziri Mkuu anasalimia watu, Mawaziri wengine wanasalimia, lakini Mheshimiwa Waziri Mpina, hata tukimsalimia, mimi mwenyewe zaidi ya mara tatu nimemsalimia anakaa kimya. Sasa, Waziri kama Waziri jambo la kwanza ni kujenga mahusiano na wale ambao unawaongoza, sasa Mheshimiwa Mpina, tunaomba atupe maelezo ya kina kwamba yule kijana aliyeuawa, zimechukuliwa hatua gani mpaka leo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba kujua, kwamba pale Mtwara kuna Chuo cha Uvuvi, chuo ambacho kimekuwa kinazungumzwa kila siku na nilimweleza Mheshimiwa Naibu Waziri hapo juzi, kwamba kile chuo lini kinaanza kazi, Chuo cha Mikindani cha Uvuvi. Pale tunaona kuna madawati yamewekwa, kuna meza zimewekwa lakini hakuna walimu, mpaka leo hawajaletwa walimu, hakuna kifaa chochote, hakuna hata Boti ambayo wale wanafunzi wakidahiliwa wataweza kuzitumia kwa ajili ya kwenda kufanyia mazoezi ya kuvua pale Mikindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naishi Mikindani hapohapo kwenye chuo, niliambiwa kwamba kimeanza, kile chuo mpaka leo nazungumza na watu wa Mtwara hakijaanza. Sasa tunasema, tunataka tuvue uvuvi wenye tija, uvuvi ambao utapelekea Watanzania kujikomboa na umaskini na sisi wananchi wetu wa Pwani wengi ni wavuvi. Wananchi wangu wa Mtwara Mjini maeneo ya Kiyanga, maeneo ya Mikindani, wote ni wavuvi, wanategemea uvuvi katika Bahari ya Hindi ili waweze kujikwamua. Tunaomba kile chuo kifanye kazi isiwe kila mwaka, tunazungumza, tunaahidi lakini utekelezaji unakuwa haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naiomba sana Wizara hii, kwamba, ili tuweze kuvua uvuvi wenye tija, kama ilivyozungumza kwenye Ilani, kwenye nini, lakini pia Serikali inaahidi kila mwaka, lazima tuwe na vifaa vya kisasa vya kuvulia samaki, lazima tuwe na Boti za kisasa za kuvulia samaki. Wakati tuko Chuo Kikuu, mwaka 2008 pale, tuliweza kula samaki wengi sana, ambao Mheshimiwa Rais kipindi kile akiwa Waziri wa Wizara hii alikamata meli, wakaletwa wale samaki Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pale, tukala bure wiki nzima, kwa sababu tu wamevuliwa kitaalam, wale samaki walikuwa ni wengi. Tunaamini kwamba Serikali ikileta maboti, wananchi wetu wataweza kuvua kitaalam kuanzia Mtwara mpaka kule Kilwa, mpaka Dar es Salaam, Tanga na Zanzibar ili tuweze kuondokana na umasikini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maftaha. Tunaendelea na Mheshimiwa Charles Tizeba baadaye Mheshimiwa Kiruswa na Mheshimiwa Hasna Mwilima wajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia naomba nifanye *declaration* ya mambo matatu. La kwanza nimezaliwa nimekuwa na sasa nazeeka katika uvuvi, ufugaji na ukulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, nimebahatika sana kwa fadhira za Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kuwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, lakini *declaration* ya tatu Jimbo ninalotoka mimi, asilimia 90 ya wakazi wa jimbo hilo ni wavuvi na asilimia 10 ni wafugaji. Kwa hiyo, haya ninayoyasema na ninayopanga kuyasema yanatokana na hiyo *background* ambayo nimeitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na sekta ya mifugo, hotuba ya Waziri nzuri, imejaribu kugusa changamoto ambazo wafugaji wa nchi hii wanapitia, lakini nishauri tu

jambo moja, kama mtu ambaye pia nimewahi kukaa kwenye dawati alilopo. Suala la masoko ya masoko ya mazao ya mifugo, haliishii katika kujenga viwanda, kwa sababu hata vile vichache tulivyonavyo, uuzaji wa mazao hayo unakuwa wa tabu kwa sababu ya jambo moja, kwamba, eneo kubwa la ufugaji wa nchi hii halijawa huru kutokana na maradhi mbalimbali ya mifugo, hasa, homa ya mapafu na ile *east cost fever.* Haya maradhi mawili yanazuia uuzaji nje wa nyama ya Tanzania na namna pekee ya kuondokana na hili jambo, hiki kikwazo ni kwa kufanya chanjo kuwa ya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya wafugaji kuchanja kwa hiari ndiyo inatufanya tuendelee kuwa kwenye hicho kibano, kwamba bado nchi yenu siyo *disease free* kwa hiyo, hatuwezi kupokea nyama yenu. Leo Jumuiya nzima ya Ulaya haipokei nyama kutoka Tanzania, Marekani haipokei nyama kutoka Tanzania na huko ndiko kwenye soko lenye bei kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, katika mazao ya mifugo ni hili la ngozi, nimesoma takwimu zilizopo katika kitabu cha hotuba ya Waziri, tunachinja ng'ombe wengi, lakini ngozi haitusaidii chochote, hasa wafugaji. Kwa nini haitusaidii, ile *export levy* iliyowekwa ya asilimia 80, wachakataji hawaitaki, kwa hiyo, hawalipi, lakini *on the other side* wakulima hawauzi ngozi! Sasa *is a zero sum issue,* mimi sijui kama Waziri wa Fedha ananisikiliza, hili jambo tunaishia na *zero sum issue* kwamba, wachakataji hawaji kununua hiyo ngozi na wakulima wafugaji hawana pa kuuza hiyo ngozi, kwa hiyo, ngozi yote inabaki ya kutupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunataka ku-*protect* au ku-*discourage export* ya ngozi, tufanye hivyo tutakapokuwa tumekwishajipanga, tuna viwanda vyetu vya kuchakata. Kwa hiyo, tuvilinde kwa kuweka masharti magumu ya kuondoa ngozi ghafi nje ya nchi. Vinginevyo, tunapoteza tu pande zote, viwanda havijengwi, ngozi haziuzwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ninaloomba kuzungumzia leo, ni uvuvi wa Bahari Kuu. Huu uvuvi nao umekuwa kizunguzungu, nikiri kwamba nilifanya marekebisho makubwa ya kanuni, yameanza kutekelezwa baadhi na mengine hayajaanza kutekelezwa. Leo nilikuwa nazumgumza na Naibu Waziri wa Fedha, mpaka asubuhi ya leo, nchi hii, mwaka mzima, hatujaingiza hata senti tano inayotokana na uvuvi wa Bahari Kuu, sasa maana yake nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetunga sheria ili zitufanye tupoteze mapato au tumetunga sheria na kanuni ili zituingizie mapato? Naomba sana jambo hili lifanyiwe tafakari, ushuru ule wa mrabaha wa 0.4 dola kwa kilo moja, wadau wetu waliukataa. Tukakaa miezi minane bila ku-*issue* leseni hata moja, mpaka tulipo-*rethink*, tukasema hapana, hebu tuigawe hii *issue*, miezi sita wasilipe na miezi sita walipe, wakaja wavuvi 51 wakakata leseni. Sasa hili jambo lisipoangaliwa tunaendelea hivihivi kupoteza mapato wakati samaki wanapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba samaki siyo kama dhahabu, kwamba iko kwenye shimo fulani Bulyang'hulu, haitoki pale milele na milele kama hujaigusa. Hawa samaki wanatembea, leo wako *Mozambique*, leo wako Tanzania, kesho wako Kenya, kesho kutwa wako *Djibouti*. Kwa hiyo, ukisema kwamba tunatunza maliasili hii sijui maliasili, hii siyo maliasili iliyo *stagnant* pale mahali, wanapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *as we are speaking,* hapo *Djibouti* na Kenya kuna meli zaidi ya 300, wanaendelea kusubiria samaki waki-*cross* Tanzania, wanavua. Sisi tunasema tunataka asilimia ngapi sijui, dola 0.4 kwa kilo moja ili tupate mrabaha. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, alitazame hili, Zanzibar wanalia, Zanzibar wanalia, huko natoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo hili la *operations* zinazoendelea katika maeneo mbalimbali. Mheshimiwa Zitto amelizungumzia kidogo, lakini mimi naomba nilizungumzie

kwa mantiki ile kwamba asilimia 90 ya wakazi ya jimbo langu ni wavuvi. Naunga mkono, asilimia mia moja kufanyika kwa hizo *operations* kwa wavuvi haramu, hilo naunga mkono kabisa, lakini siungi mkono kabisa, *operations* hizi kufanyika bila kzingatia sheria za nchi zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu kinachofanyika sasa hivi, mtu anakutwa amevunja Sheria ya Uvuvi, anapigwa faini za Sheria ya Mazingira na anayepiga faini hizo za Sheria ya Mazingira wala siyo Afisa Mazingira aliyesajiriwa. Nilizungumza na Mheshimiwa Makamba, nikamuuliza, hivi maafisa wako hawa, watumikaje katika kumkamata mtu na nyavu halafu akapigwa adhabu ya Sheria ya Mazingira, akasema hili haliruhusiwi na nikaenda kwenye sheria, ni kweli, hata Afisa Mazingira, siyo kila Afisa Mazingira anaruhusiwa kutoza faini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea ukienda leo, amekutwa na nyavu *double* mbili, *double* tatu, anapigwa faini ya shilingi milioni mbili. Ukiuliza, Sheria ya Mazingira, inahusika vipi na kiwango cha nyavu, hii Sheria ya Uvuvi ambayo faini yake haizidi shilingi laki mbili au kifungo cha miezi sita, lakini unakuta mtu amepigwa faini ya shilingi milioni mbili, milioni tatu. Sasa baya zaidi, Mheshimiwa Waziri, Maafisa wake hao, huo umekuwa ndiyo mwanya mkubwa wa rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si vizuri sana kumtaja mtu asiyekuwa ndani ya hili Bunge, si vizuri sana, kanuni zetu zinatuomba tuwe na tahadhali kuwataja watu wasiokuwa ndani ya Bunge, lakini yuko bwana mmoja, kiongozi wa shuguli hii ya *operation* kule Sengerema, ondokana naye huyo. Alikuwepo Ukerewe wa aina hiyo wakamhamishia kwa Mheshimiwa Zitto kule, sasa Mheshimiwa Zitto leo tayari anapiga kelele. Sasa huyu aliyeko Sengerema Mheshimiwa Mpina, amtoe tu, maafisa wako wengi sana wanaoweza kufanya kazi kwa uungwana bila kupaka Serikali picha mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anamkuta mtu kakatiwa leseni na Halamshauri, mwandikaji wa leseni hiyo ni mtumishi wa Halmashauri, kakosea herufi moja kwenye jina, anamchukulia mitumbwi yake, anachukua *engine* anakwenda *compound* kule, anadai milioni moja faini kwa sababu ya jina la mtu limekosewa herufi moja! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay*, nikawaambia basi anapowatoza hizo faini awaandikie na stakabadhi. Stakabadhi haandiki, kwa sababu anajua akiandika stakabadhi ya faini ya milioni moja kwa jina kukosewa atakuwa amevunja sheria, anachukua fedha hizi anaweka mfukoni. Sasa mimi sijui huyu ni mwizi au ni mla rushwa, vyovyote vile, lakini ni mtu anayevunja sheria za nchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tizeba.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona umenikatili. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kengele imelia muda nilikuachia kama dakika mbili. Tunaendelea na Mheshimiwa Kiruswa na Mheshimiwa Hasna Mwilima ajiandae.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye hoja hii ya Wizara ya Mifugo. Nitangulize pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, ndugu yangu Mheshimiwa Luhaga Mpina, Naibu wake Mheshimiwa Abdallah Ulega, Makatibu Wakuu, ndugu yangu Profesa Elisante Ole-Gabriel na Dkt. Rashid Adam kwa kazi kubwa wanayofanya kama Wizara katika kuleta mapinduzi ya sekta ya mifugo ambayo kwa miaka mingi imesahauliwa na kuwekwa pembeni kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa mtoto mdogo wakati nilipokuwa nasikia jinsi Wizara ya Mifugo inavyobebwa na Serikali ya awamu ya kwanza. Wakati ule na nimepitia nyaraka zilizopo, kulikuwa na Sheria inayoitwa *The Ranch Development and Management Act,* ya mwaka 1964.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyakati hizo nyanda za malisho zilipewa hadhi yake, ziliundwa *Commissions*, zikagawanya Kanda, zikaanzishwa na kuhamasishwa Jumuiya za Kifugaji na *Ranch* za Ufugaji, ndiyo wakati ule pia hata katika ukanda mkubwa wa *Masai Steppe* iliyokuwa Wilaya ya Maasai, ambayo leo ina Wilaya karibu sita ndani yake ikiwemo Longido, Monduli, Simanjiro, Ngorongoro, kukawa kuna Masai *Ranch*. Ile taasisi ilikuwa imewezesha, ina mitambo ya kuchimba mabwawa, ina magari, inatoa tiba ya chanjo, *dips* za kuongesha na kwa kweli hata wafugaji wa wakati ule walipoambiwa walipe kodi ya kichwa cha ng'ombe hawakulalamika maana yake wanajua Serikali inawatunzia mifugo na walilipa kwa furaha, kulikuwa na upungufu wa kitu kimoja tu, masoko, lakini Serikali haikujali wanauza wapi ili mradi wanahudumiwa ili uchumi wao uweze kuimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipoangalia nyaraka zilizofuatia, kuna hii Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006, halafu ikaja na Sheria ya Nyanda za Malisho ya Mwaka 2010. Hizi zote zinasisitiza kabisa na kuweka mkazo kwamba, ili mifugo iwanufaishe wafugaji na kuliletea Taifa mapato makubwa, ni lazima mifugo wapewe maeneo ya malisho, maji, tiba, masoko, sambamba na kuimarisha miundombinu ya barabara na viwanda vya kuchakata nyama na mazao ya mifugo. Hivi vitu vyote vimekuwa ombwe kubwa katika kukuza na kuimarisha sekta ya mifugo, lakini katika hotuba hii, iliyoandaliwa kwa makini na mambo ambayo Waziri amebainisha kwamba anakwenda kufanya, imenijaza matumaini na naamini kwamba akiyasimamia tutaona mapinduzi katika sekta hii ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Waziri basi azingatie katika suala la malisho, hata yale maeneo ambayo hayana migogoro kama Longido. Sisi tuna maeneo lukuki ya malisho lakini yana uhaba mkubwa wa maji; na ninakushukuru kwa sababu kwenye ziara yako ya juzi ulipopita ulitujaza matumaini ukatambua mabwawa yaliyovunjika, mabwawa yaliyojaa udongo na ukasema kwamba utatusaidia kukarabati, yatawekwa kipaumbele katika bajeti hii,

sambamba na kutujengea yale mabwawa nane yaliyobomoka ukijua na kutilia maanani kwamba sisi wananchi tumetengeza kwa nguvu zetu kupitia wadau na halmashauri yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikutajie tu baadhi ya nyanda za malisho ili ujue ni kwa jinsi gani Longido ina maeneo ambayo yakiboreshwa na yakawekezwa tuna maeneo ya kutunza mifugo yatakayokuwa na tija kubwa; na sisi tumeimarisha mifugo kweli kweli kwa ajili ya hivi viwanda ambavyo pia vitajengwa na Longido pia ikiwa ni mnufaikaji wa kiwanda kimoja kitakachochinja ng'ombe 500 kwa siku na mbuzi 2,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna nyanda za malisho, sisi tunaita Ngaron, nikutajie tu baadhi. Kuna Loorboro, Oldenja, Engasurai, Naambala, Leleki, Ildonyo-dapashi, Loomunyi, Ngurmausi, Lookinyoyo, Loosikitok, Olesulenge, Kitang'a-engutak, Idonyo-oonyokioo, Ang'ata-eopir, Endonyo-nanyokie, Loolwaa, Ndashat, Orkiloriti, Orpelela, Lekuruki, Kelembusi, Endonyo-emali, Endarakwa, Kitenden, Ndiakakati, Endapitipit, Kesertet, Emesera na Molonjoni. Hizo zote ni nyanda ziko wazi ni maeneo mahususi yanayopata majani kwa haraka, mvua hata wiki moja ikinyesha lakini mara nyingi wakati ule bado hali ya tabianchi haijabadilika ni moto tu na mchwa ndiyo anakula yale majani kwa sababu hakuna maji katika nyanda hizo. Mheshimiwa Waziri tupatie kipaumbele kuweka mabwawa, kuweka visima virefu, mifugo watashamili, mbuzi, ng'ombe, kondoo na hivi viwanda havitatindikiwa malighafi vikapokuwa vimekamiliaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho ni kero. Kwa kweli kwa miaka yote hii Tanzania haijawa na soko la uhakika la mifugo na kwa miaka yote hii hatujaona nguvu ya Serikali katika kutusaidia kutunza hii mifugo. Kwa hiyo hii operesheni iliyoanzishwa inayoitwa Zagamba ambayo imezagaa kule kwetu Longido imewaumiza wafugaji na wachuuzi wa mifugo kutoka sehemu mbalimbali ya Tanzania waliokuwa wanatumia mpaka huu wa Kenya kupeleka

mifugo Kenya kwenye soko lenye tija. Kwa sababu licha ya kwamba walikuwa wanasimamia Sheria lakini pia kwa kanuni ulizoweka. Kwamba akipatikana mtu anayekwenda kuvusha mifugo au akituhumiwa tu anapigwa faini 500,000, hata kama alikuwa anapeleka mbuzi wawili maskini ya Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine bado mifugo haijalipiwa kwenye masoko; nadhani zile tozo zinazojulikana; unakuta yule mtu anawekewa na faini. Kwa mfano kuna watu walikamatwa walikuwa ni watatu wenye ng'ombe kila mtu 500,000, mbuzi 30,000 kwa sababu sasa faini ng'ombe 50,000 halafu bado akifika kule mpakani wanatozwa kodi zingine za kupeleka ng'ombe nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamefilisika kwa sababu ya operesheni, rushwa pia imetumika na kuna pia msimamizi wa kikosi huko amekuwa na unyama wa hali ya juu. Mimi siwezi kumtaja kwa jina lakini ile operesheni Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuja tulikaa tukasema kama wafugaji hatukushirikishwa katika kuweka hizi taratibu. Kama tungelishirikishwa tungeulizwa mnaenda kupata faida kiasi gani mkipeleka mifugo Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakasema kama tungelitozwa hata hizo kodi, kwa mfano kodi ya kupeleka ng'ombe Kenya ni 30,000 ya kupeleka mbuzi ni 7,500, ukiweka na kodi za halmashauri inafika 9,000 na sasa hivi ukiwaambia wafugaji wanawenda kupata faida kiasi gani hawapati. Wakaililia kabisa Serikali wakasema ng'ombe awe 15, 000, mbuzi awe 4,500, wao wenyewe wapewe kazi ya kusimia operesheni ya wanaotaka kutosha mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanatoroshwa kwa sababu hawapati faida tena wakilipa hizo tozo; na mbaya zaidi ni hizo faini ambazo zina wafilisi wengi. Mheshimiwa Waziri nakuomba, kwa sababu hizo ziko ndani ya kanuni, ukiacha Sheria ambayo naomba pia Bunge hili tubadilishe, tuweke kodi zinazoendana zipunguzwe mpaka pale Serikari itakapokuwa imetuwekea masoko ya uhakika na viwanda

ndipo sasa wafugaji wetu waweze kuwekewa faini kubwa wakitaka ng'ombe Kenya kwa sababu hawa sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri abadilishe hizo kanuni zake. Haiwezekani mtu anayekamatwa akipeleka mbuzi watatu alipe 500,000 halafu mtakuwa mmemfilisi hata hao mbuzi wenyewe hawafiki 300,000 wakiwauza laki moja moja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri usipofanya hilo mimi niko tayari kushika shilingi kwa sababu kwa kweli tuna kero kubwa ya watu ambao wamefilisika kwa sababu ya kanuni ulizotunga ambazo zimekuwa kandamizi na za kuumiza wafugaji wetu wanaotafuta riziki kwa sababu hapa nchini kwetu bado hatuna masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kiruswa. Tunaendelea na Mheshimiwa Hasna Mwilima baadaye Mheshimiwa Julius Kalanga na Mheshimiwa Tunza Malapo wajiandae

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana, Wizara inayoshughulika na masuala ya uvuvi pamoja na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jimbo langu mimi asilimia kama 70 hivi au 65 wanajihusisha na masuala ya uvuvi; lakini hapo hapo tena asilimia hiyo hiyo au zaidi wanajihusisha na masuala ya mifugo. Kwa hiyo nitachangia mambo yote mawili; lakini kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja

na Naibu Waziri na timu yake yote ya Wizara kwa namna ambavyo wameweza kuwasilisha taarifa ambayo inatupa matumaini. Nina imani wavuvi na wafugaji wanaweza wakaona mwanga mpya unaotaka kuja katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la uvuvi. Kulifanyika operesheni kwenye Ziwa Tanganyika, wavuvi wetu wakatupigia simu Wabunge na mimi nikamuona Waziri pamoja na Naibu Waziri. Nitoe shukrani zangu za dhati kwamba jana walitupa nafasi ya kuwasikiliza wavuvi zaidi 35 kutoka Ziwa Tanganyika, na tatizo kubwa ilikuwa ni uvuvi kwa kutumia *ring net.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwamba jana tulimaliza mazungumzo salama, lakini bado wale wavuvi wanahitaji kurudishiwa nyavu zao saba ambazo zilishapimwa kwenye ile operesheni ya kwanza na zikaonekana zinafaa. Nashukuru kwamba Mkurugenzi amewaita kesho asubuhi saa mbili ili aweze kukutana nao. Sasa naomba nyavu zao zirudishwe, mashine zao zirejeshwe kwa sababu ndicho wanachokitegemea kupata kipato kwa dhana hizo zilizoshikiliwa nje ya utaratibu na nje ya Sheria ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimzungumzie, Mheshimiwa mwenzangu amesema siyo vizuri kumtaja mtu mimi naomba nimtaje. Namtaja kwa sababu Mheshimiwa Tizeba aliyekuwa anamlenga ni yuleyule mama anayeitwa Judith ambaye leo mmetuletea kwenye Mkoa wetu wa Kigoma. Wabunge wote hapa nyuma, Mbunge wa Ukerewe, Mbunge wa sengerema, Mbunge wa wapi sijui wote wanazungumza kuhusiana na huyu Mama Judith. Huyu mama anaripoti kila mwezi TAKUKURU kutokana na madudu aliyoyafanya Mwanza. Leo mtu anayeripoti TAKUKURU kwa madudu aliyoyafanya Mwanza mnatuletea Kigoma kuja kuua uvuvi na wanachi wanategemea hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mimi nakufahamu, wewe ni msikivu na ndiyo maana ulitupa nafasi ya kutusikia pale Wizarani jana; huyu mama tafuta pa

kumpeleka siyo Kigoma, Kigoma hatumtaki. Kama alitoka Mwanza akaletwa Kigoma na Kigoma hatumtaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu gani, anakamata hizo *ring net*.....

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche.

**TAARIFA**

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa dada yangu Hasna taarifa hivi ule utaalam wa Kigoma siku hizi hawatumii mpaka...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasna umemsikia? Taarifa yako haijasikika Mheshimiwa Hasna endelea.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Heche huwa anapenda kila nikisimama kunipa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu hizo dakika kidogo naomba zilindwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mama ametumwa kutekeleza kazi kwa mujibu wa sheria lakini amefika kule anaharibu utaratibu mzima wa uvuvi kwenye ziwa lote la Tanganyika, kwa maana ya Kigoma, Katavi na eneo kidogo la Rukwa. Jana amewaita baadhi ya wavuvi wa Kigoma Mjini wakiongozwa na mtu anaitwa Francis Kabure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Francis ni Mrundi, mimi nimepiga simu Kigoma nikauliza huyu mtu ni Mtanzania, wananiambia ameshaomba uraia zaidi ya mara tatu bado hajapewa uraia. Mheshimiwa Waziri swali langu hivi Sheria ya uvuvi inasemaje kuhusiana na mtu ambaye si raia na anapewa cheo cha kupambatizwa kwamba yeye ndiye

Mwenyekiti wa Wavuvi Mkoa wa Kigoma kachaguliwa na Judith kwa maslahi yapi? na amemleta mpaka Dodoma na ushahidi tunao na jana amekaa kikao na Mkurugenzi wa Uvuvi. Japo Mkurugenzi ni haki yake kuwasilikiza hilo mimi siwezi kuhoji, lakini je, ana maslahi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri huyu mama hatumtaki tunaomba utuondolee pale Kigoma, tafuta pa kumpeleka. Kwanza hana sifa ya kuendelea kuwa msimamizi iwe Nyasa, iwe Victoria iwe Tanganyika kwa sababu tayari anashutuma za rushwa ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili niendelee kuishukuru pia Wizara. Jana tulikuwa tunazungumzia masuala ya tozo; suala hili la uvuvi linatozo nyingi sana. Naomba Mheshimiwa Waziri kwenye mabadiliko ya kanuni ujaribu kuangalia kidogo hizi tozo mvuvi analipa, mtumbwi unalipwa, akisafirisha dagaa analipa. Jaribu kuziweka iwe ni *win situation*, Serikali mpate na sisi pia tupate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mifugo kwa haraka haraka kabla kengele nyingine haijapigwa. Kuna suala hile.....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasna kengele ya pili hiyo nakuachia kidogo umalizie, hii ni ya pili.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba suala moja tu la Mwanduhu Bantu. Nimeona hapa Mheshimiwa anaonesha Uvinza kuna ekari kama 49 kwa ajili ya kugaiwa wafugaji. Mheshimiwa Waziri ulikuja ukatoa maelekezo eneo la Mwanduhu Bantu umeriridhia tuendelee nalo kama halmashauri tugawe vitalu, wafugaji wagawiwe na wakulima wagawiwe. Naomba utakapokuja kuwasilisha kesho uweze kutupa tamko rasmi, ni lini sasa umeturuhusu ili tuweze kupata mapato haya na wewe pia Wizara yako itapata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naendelea kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu wote pamoja na Mkurugenzi wa Idara hii ya Uvuvi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hasna, tunaendelea na Mheshimiwa Julius Kalanga baadaye Mheshimiwa Tunza Malapo ajiandae.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, na Wizara hii nina maslahi nayo, kwa hiyo naomba dakika zangu ziwekwe vizuri kumi ili niweze kusema vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na watumishi wote wa Wizara kwa juhudi wanazofanya katika kusaidia Wizara hii ambayo ina changamoto nyingi. Nikiri kwamba tangu tumeanza Bunge hili na mpaka sasa kuna *improvement* kubwa na juhudi kubwa ambazo tunaona Wizara inafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekutana na changamoto nyingi, na tangu dunia iumbwe na nchi hii ianze, tangu mimi nimeanza kuwa mtu mzima mpaka leo sijawahi kusikia mahali ambapo Waziri wa Mifugo amesimama upande wa wafugaji bila kujali kwamba Serikali inatakiwa kuwajibika kwa wakati mmoja, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi ambazo unazifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninaomba Mheshimiwa Waziri asipende sana maduhuli kuliko utu wa Watanzania wanaofuga. Wizara hii ukiondoa tozo na faini haikusanyi chochote kwa samaki wala kwa ng'ombe, na nadhani inaweza ikawa ni Wizara inayoongoza kwa tozo na faini kwa wananchi wake. Mimi sijawahi kuona mahali ambapo Wizara, na nadhani nadhani inaweza ikawa ni Wizara ya kwanza imevuka lengho la makusanyo; lakini ukiangalia makusanyo yenu asimilia karibu 50 ni faini na tozo. Hata hivyo ng'ombe hawa hawakuja kwa ajili tozo peke yake na faini, ni rasilimali ambayo lazima tujiulize kama kuna

uvunjaji mkubwa wa sheria kwa nini wafugaji wanavunja sheria, ili changamoto zilizopo mziondoe ili muweze kupata kilicho halali yenu mnachokusanya si halali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema ninaomba niseme mambo mawili kuhusiana na jimboni kwangu. Asilimia 70 ya watu wa Monduli ni wafugaji. Nimeangalia majosho unayokarabati mzee hakuna hata josho moja Monduli. Ninapata mashaka au kwa sababu bado hamjafika, lakini na sisi ni sehemu ya wafugaji wa nchi hii. Naomba wakati unahitimisha utuambie unafanyaje eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, mmetuweka kwenye kundi la halmashauri ambao wanapaswa kunyima wasikusanye tozo ya wafugaji kama hawajaboresha majosho; mtuondoe huko, sisi tumevuka mbali, tumejenga majosho zaidi ya matano na tumekarabati zaidi ya majosho sita. Kwa hiyo aliyokupa taarifa nadhani amekupa *wrong information,* mtuondolee kwenye kundi la kutuzuia kutokukusanya tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba naomba nimpe *challenge* Mheshimiwa Waziri. Kama anasema halmashauri wasikusanye tozo zinazotokana na mifugo kwa sababu hawajakarabati majosho, wao Wizara wanaokusanya zaidi ya bilioni 64 kutoka kwetu wanaturejeshea nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni muhimu tukakubaliana, kwamba kama halmashauri wanapaswa kutoa na ninyi toeni; tuwekeane asilimia; ninyi Wizara mtupe asilimia 30, halmashauri watupe asilimia 20 sisi tupate asilimia 50 tuboreshe miundombinu ya wafugaji. Haiwezekani, ukavuna pasipo kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niwape *challenge*, ukisoma ilani ya uchaguzi ya *CCM* inasema yafuatayo:-

Inasema katika ule ukurasa wa 15 hoja ya kwanza inasema kwamba Serikali itajenga visima zaidi ya 300, lakini inasema itajenga mabwawa kutoka 1,300 kwenda

mabwawa 2,000, pia inasema itatenga maeneo ya malisho na kuyawekea Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka atuambie mpaka sasa kwa mujibu wa ilani mmechimba visima vingapi na mabwawa mangapi mapya ambayo yameboreshwa kwa ajili ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niseme *challenge* ambazo Wizara mkiziondoa itasaidia ninyi kupata fedha kwa haki yenu. Jana nilikuwa napitia kwenye Sekta ya Maziwa. Sekta ya Maziwa ili mtu awe na kiwanda mpaka amalize utaratibu anapaswa awe ameilipa Serikali zaidi ya milioni 30. Usajili tu wa kampuni 400,000, ukaguzi wa eneo la kujenga 120,000, kibali cha ujenzi 300,000, ukaguzi wa kiwanda 350,000, usajili wa leseni ya biashara milioni 3,000,000, namba ya mlipa kodi ya kwanza 500,000, usajili na ukaguzi wa mitambo 245, 000, tathimini ya mazingira milioni 1500, 000, ukaguzi wa kiwanda 350,000, ukaguzi wa usajili wa magari 250,000, ukaguzi wa usalama 400,000 na mengine na mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mnafahamu kabisa mchakato wa ng'ombe hizi gharama anabeba mfugaji; kwamba ukiweka gharama katika uendeshaji wa kiwanda cha maziwa maana yake bei ya maziwa kule kwa mfugaji inashuka. Sasa hamuwezi kupunguza mifugo kama hatuna utaratibu unaomuhamasisha mfugaji kufuga kwa tija, ukiwa na bei nzuri ya maziwa maana yake utakuwa na ng'ombe bora wa maziwa mengi ili uweze kuuza. Kwa hiyo angalieni hizi tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kuhusu mgogoro wetu na ninyi Namanga. Mheshimiwa Waziri unajua kabisa hakuna sheria ya utaifishaji wa ng'ombe; lakini naomba uniambie mchakato wa kutambua kwamba mfugo huu umekosa mwenyewe ukoje, kwa mujibu wa sheria? na mkatangaze na mkabandike. Watu wenu wanatuibia, watu wenu wanatunyang'nya ng'ombe kwa nguvu. Mtu anakamata mbuzi saa mbili asubuhi saa nne anauliza

anasema ng'ombe, mbuzi wamekosa mwenyewe. Ni Mmasai gani anatelekeza mifugo? nani kwenye dunia hii? Sisi tuko tayari kuwafa kwanza mifugo ipone. Yet wewe unakamata mbuzi wangu saa nne saa tano unauza unaniambia umekosa mwenyewe! Hapana bwana! Hapana! Hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tunataka kwa mchakato wenu huu tuelekezeni sharia, watu wenu wanatuonea. kwa Namanga watu wanaovunja sheria wachukuliwe hatua lakini msituonee, fuateni sharia; na *CAG* nanyi mfuatilie, ni mifugo mingapi ambayo imeuzwa kwa kukosa wenyewe Namanga? Halafu mimi niambiwe kwamba Mmasai ameacha mbuzi, ameacha ng'ombe kwa kuogopa faini ya 500,000? si kweli, lakini inaonekana mnatunyang'anya mnatumia mgongo huo kwa sababu sheria hairuhusu kutaifisha, lakini mmetaifisha mifugo ya wafugaji kwa sabaubu tu mnasema imekosa mwenyewe kwa sababu sheria hairuhusu kutaifisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri umetusaidia mengi lakini naomba utusaidie Namanga hali yetu ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja mkono.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kalanga, tunaendelea na Mheshimiwa Tunza Malapo, baadaye Mheshimiwa Charles Mwijage ajiandae.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naskushukuru. Awali ya yote napenda kuipongeza Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ina mambo mengi mazuri, Serikali itulie isome na ifanyie kazi ushauri ambao wameutoa. Pia ukiangalia kwenye kitabu cha Kamati nacho pia kina mambo mazuri, kina ushauri nzuri, pia Serikali itulie isome ifanyie kazi kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea Mtwara, Mtwara kuna Bahali ya Hindi. Ukifika Mtwara Mjini sasa hivi samaki wengi ambao tunakula wanatoka Msumbiji. Wanatoka Msumbiji si kwa sababu sisi watu wa Mtwara hatuna bahari ama hatuwezi kuvua ni kwa sababu vyombo vya uvuvi vilivyopo ni duni. Wavuvi wengi wanatumia mitumbwi kwa makasia hivyo wanashindwa kuvua samaki kwenye kina kirefu. Pia ukienda upande wa Msumbiji nyavu zilezile ambazo Tanzania kwa kiasi kikubwa zinachomwa kule zinatumika na samaki hao wanarudishwa wanakuja kwetu kuuzwa na sisi tunanunua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna bahari kubwa ambayo tulitarajia kitoweo cha samaki kiwe ni chakula kikuu, lakini sasa hivi Mtwara kula samaki ni anasa, kwa sababu samaki utaambiwa wanauza shilingi 2000 au shilingi 3000 ni samaki mdogo lakini bahari tunaiangalia. Sasa ushauri wangu kwa Serikali nawaomba waone haja ya makusudi kabisa ya kuwekeza, tukipigwa kwenye korosho basi tukimbilie kwenye uvuvi. Korosho hali tete kwenye uvuvi hali tete mambo yanakuwa tafrani haipendezi, tunashindwa hata pamoja pa kujishikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifungua katika ukurasa wa 41 wa hiki kitabu cha Kamati unaona wameeleza kuna uvuvi wa samaki aina ya Jodari, wanasema asilimia 67 ya samaki waliouzwa huko nje duniani mwaka 2018 wamevuliwa kutoka ukanda wa bahari kuu ya Tanzania na watu wengine sio sisi Watanzania. Pia ukisoma pale kwenye ukurasa wa 41 Kamati imetoa ushauri ndio maana nikasema, Serikali ijitahidi kusoma hiki kitabu ili wapate ushauri, wamesema kuwa na ujenzi wa viwanda vya kuchakata samaki aina ya jodari kwenye ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia masuala ya viwanda naona kwa asilimia kubwa amelekezwa kwenye maeneo ambayo kuna Ziwa, maeneo ya Ukanda wa Ziwa Victoria, lakini ukija huku kwenye ukanda wa bahari sijajua kama kuna kiwanda chochote, kule kwetu Mtwara najua hakuna kiwanda cha uchakataji wa samaki, lakini tuna bahari

ule ukanda wote ule kutoka Mtwara, Kilwa huko mpaka unakuja Dar es Salaam, sijakiona kiwanda cha kuchakata mazao yanayotokana na samaki wa maji chumvi. Ndio mpaka sasa hivi ukipita humu madukani kwenye mabucha ya samaki, samaki wa maji baridi ni wengi kuliko samaki wa maji chumvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakatoa ushauri mwingine, (b) ununuzi wa meli za kufanya uvuvi katika bahari kuu ya eneo la Tanzania, hakuna meli kubwa za uvuvi, hawa samaki kama jodari ndugu yangu huwezi kuwavua kwa kutumia mitumbwi ile ya kwetu ya asili huwezi. Kwa hiyo, ni lazima wawekeze haya mambo mengine ya kukimbilia vitambulisho, mtu mama anauza mboga unamng'ang'aniza atoe kodi uchumi tunauacha kwenye bahari kuu. Pesa tunaziacha huku, ndio maana kila siku tunataka tuwafinye watu wenye biashara ndogo ndogo lakini huku zinapokuja kupatikana pesa nyingi hatuwekezi ili kusudi tuongeze pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa tuwe *serious,* kuna mambo mengine yangekuwa yanafanyika *for free,* watu wanafanya biashara za mboga mtu ana mchicha wake, lakini wewe mtu wa uvuvi unachotegemea mtu afanye kosa ukamtoze faini, ndio uje hapa maduhuli yameongezeka, maduhuli yameongezeka, lakini ukiangalia mengi ni faini, hatuwekezi vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa huo wa 41, Kamati ikashauri ujenzi wa maeneo ya kuhifadhia samaki na mazao yake, hakuna ya kutosha. Kwa hiyo niwashauri wasome vizuri, hatuna bandari za uhakika za uvuvi, watu wanauza tu holela holela, mtu akienda na hicho kimtumbwi chake, akivua visamaki viwili, vitatu, anakuja anauza, matozo kibao matokeo yake maendeleo ya wavuvi wetu yanakuwa kila siku ni duni yaani mtu ili apate tu kitu cha kula kwa siku ambapo hii ingekuwa ni sekta iliyoendelezwa nafikiri ingesaidia Watanzania na pia ingeongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kidogo kuhusu ufugaji wa kuku wa nyama na mayai. Ukiangalia kwa kiasi kikubwa hii mifugo inawasaidia wajasiriamali wadogo ambao wengi wao ni wanawake ambao mimi nawawakilisha hao wanawake, tumekuwa na tatizo kubwa sana la upatikanaji wa vifaranga, lakini pia hata hao vifaranga wakipatikana kuna changamoto kubwa sana ya masoko, hakuna masoko ya uhakika. Mtu anafuga kuku mpaka wanafikia *stage* ya kuuza hapati soko kuku wanakaa wiki mbili wiki tatu zaidi matokeo yake anaamua kuuza kwa bei ya hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kama Wizara waangalie kwa undani nimekuwa na *interest* kidogo na sehemu hii, waangalie kwa undani na kufuatilia tatizo hasa ni nini, watoe ushauri kwa wafugaji hawa wadogo ili waweze kujiongezea kipato, kwa sababu kama mtu anafuga kuku thamani yake shilingi 5,000 halafu anakuja kuuza kwa shilingi 4,000 anapata hasara, wategemezi wanazidi kuongezeka, Taifa halipati kipato, lakini hizi sekta zikiangaliwa kwa undani kama kuna changamoto wawaaambie watu, kama kuna kuku wanaongia kutoka nje wafanye utaratibu mzuri, kama kuna mayai yanayoingia kutoka nje ili kusudi ili soko litengamae, watu waweze kuuza na kufuga kwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tunza Malapo. Tunaendelea na Mheshimiwa Charles Mwijage baadae Mheshimiwa Mbaraka Dau ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia Wizara hii muhimu. Nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mpina na Mheshimiwa Naibu Waziri mjomba Kerebe wanamsubiri, apitie kwenye *diary* yake kabla hajaenda Kerebe. Jambo la kwanza niwaeleze asilimia 70 ya Halmashauri yangu ni maji, Ziwa Victoria asilimia 70 ya

Wilaya yangu ya Muleba ni maji, kwa hiyo mimi ni mvuvi. Sehemu kubwa ya eneo ambalo Wizara hii inajinasibu nalo katika ufugaji wa ng'ombe *(NARCO)* ni Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia bajeti hii nataka kuzungumzia mafanikio ya kampeni ya uvuvi haramu, ni pale tulipofanikiwa kuweza kupata samaki wale wanaokidhi hata kwenda kwenye ule utamu wa samaki mwenyewe hayo ndio mafanikio. Hakuna aliyejua njia hiyo ndio maana njia zilizotumika mimi siwezi kuziunga mkono, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge wanaosema yale makandokando yaliyofanyika yarekebishwe. Nami nampa Mheshimiwa Waziri makandokando ambayo ningeomba ayarekebishe, atoe *amnesty,* kuna watu walinyang'anywa injini zao, atamke kwamba wale walionyang'anywa injini zao naziachia, wale waliovunjiwa mitumbwi yao hiyo tuiache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena nami nina dhambi hiyo, tuliwahamasisha wana viwanda wa Tanzania wakauze nyavu, tukazuia wana viwanda wa nje, kumbe kuna wana viwanda wa Tanzania wakapeleka nyavu zisizokuwa na viwango, Mheshimiwa Waziri ashirikiane na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda waende walete zile nyavu, wenye viwanda waliouza nyavu *kanyaboya* waweze kuwakamata kusudi mbele ya wananchi tuweze kuonekana ni watu wazuri kwa wananchi. Sio kwamba namchomekea mjomba aende Kerebe kwamba hatarudi, hapana, lakini hawa wavuvi wanaweza kutushangilia kwa mikono lakini moyoni wanaumia. Sasa namna ya kuweza kusawazisha mambo haya ni kukaa pamoja na wao. Mheshimiwa Waziri arudishe injini za watu mambo yaishe, twende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nyavu, Jimbo langu linapakana na Uganda kwa maji na linapakana na Kenya kwa maji, milimita sita linavua dagaa kwa watu wa kutoka Uganda na Kenya, wewe unaniambia mpaka nilete milimita nane. Tukae chini tusawazishe mambo haya, tunachekwa. Mganda anatoka Uganda anavua Goziba, anavua Zilagura anachukua samaki, samaki hana mpaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la leseni; sisi tunafuata sheria za Wizara ya Mifugo, hatuwezi kuruhusu mtu aharibu mazingira, tunatunza eneo letu la maji *square* kilomita saba, siwezi kukubaliana na Serikali kwamba mtu akakate leseni Bunda aje kuvua kwangu, hapana, aende Muleba akate leseni Muleba, ukikata leseni Bunda, kavue huko huko, kila mtu atunze mazingira yake. Hatuwezi kuhakikisha halmashauri hizi tunazinyang'anya mapato, mapato ya Wilaya yangu yanatokana na leseni, kama unaipenda Muleba nenda kwa Shilembi akukatie leseni uvue, kama hutaki nenda huko kwao ambako wanaharibu mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie *cage,* ufugaji wa vizimba Uganda wameanza kufuga kwa vizimba, Tanzania mnaweka masharti, haiwezekani, ndio hayo mambo Profesa Kishimba anakwambia nenda na wenzako. Hata hivyo, ni kuna watu wa Maalia, watu wa Bumbire wakati wa mvua tulikuwa tunapiga samaki kwa fimbo mkaleta *over fishing* kwa teknolojia ya kisasa, wale ambao wamewaondoa kwenye mavuno yao ya asilia, chonde waende wakawape pesa, hizo pesa nyingi wanazovuna warudishe kwa jamii wasaidie vijana waweze kufuga kwa vizimba. Hawezi kwenda mbele akasema amekusanya asilimia 147 hawatamwelewa, hizo kama 147 asilimia 100 wapelekee Mheshimiwa Mzee Mpango atashukuru, 47 arudishe kwa wananchi watampenda sana. Zile njia ambazo wanavuna sizo, hizo waachane nazo, akimnyang'anya nyavu haramu ampe nyavu halali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Sekta ya Maziwa; Tanzania wanachakata maziwa lita 150,000, wengine wanasema hazifiki, Uganda wanachakata lita milioni mbili. Napenda niwashauri walielewe hili, hii ndio sekta na Mheshimiwa Waziri nazungumza ili kumsaidia, yeye ndiye ng'ombe wa maziwa wa uchumi wa nchi hii. Hizi ndizo sekta za kutupelekea uchumi wa kati ulio jumuishi, ukiwalisha wafugaji, ukawalisha wavuvi, uchumi unachangamka, uchumi jumuishi uko kwenye sekta hizi. Kwa hiyo ni suala la Serikali kupeleka pesa nyingi, watu wa Uganda

wanawasaidia watu kuwatengenezea malisho, wanawapa mabirika ya kukusanyia maziwa, wanajengea viwanda. Kiwanda Uganda ni *market* wanatengeneza lita milioni 2,000,000 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, samahani, Mheshimiwa Mwenyekiti, naona unaniangalia nakuchulia mambo mema. Naunga mkono hoja na nitawasilisha kwa maandishi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwijage. Tunaendelea na Mheshimiwa Mbaraka Dau, baadaye Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Ninaze kwa kumpongeza sana mtoa hoja leo asubuhi Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yako yote ndugu yangu Mheshimiwa Ulega, Katibu Mkuu na timu yote pale Wizarani. Nitaanza na ukurasa wa 77 wa kitabu cha leo. Mheshimiwa Waziri pale anasema zimetengwa shilingi milioni 153 kwa ajili ya mgao wa maduhuli katika vijiji ambavyo vipo katika hifadhi ya bahari katika Kisiwa cha Mafia. Matatizo yangu yanaanzia pale, nina mambo mawili pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, hizi milioni 153 zimeandikwa pale kwamba zinakwenda kwenye vijiji 17 na Mheshimiwa Waziri alikuja Mafia tukasomewa taarifa kule Jibondo, Hifadhi ya Bahari ipo katika vijiji 12 tu na vitongoji vitano, hiki kitabu leo kinasema hifadhi ya bahari iko katika vijiji 17, imenishtua sana, hizi takwimu Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku- *wind up* naomba sana atupe maelezo, pengine inawezekana ikawa ni *typing error,* lakini kama sio *typing error,* basi kuna tatizo kubwa sana, kwa sababu moja ya kilio cha watu wa Mafia ni kwamba hifadhi ya bahari imekuwa ikiongeza mipaka kila uchao. Vilianza vijiji vitatu, vikaja saba sasa vipo 12, leo kitabu kinatuambia vijiji 17. Sasa naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie, hivi vilivyoongezeka ni *typing error* au tayari himaya ya hifadhi ya bahari sasa imeongezeka tena kwa vijiji vingine. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuna mgao hapa, kuna taarifa njema ambayo nashukuru sana Mheshimiwa Waziri amesema kuna shilingi milioni 43 zitaendelea kwa ajili ya kutolewa mikopo kwa wanavijiji ambao wamo ndani ya hifadhi ya bahari, ni jambo jema nashukuru sana kwa niaba yao. Hata hivyo, nataka nitoe tahadhari namna ya mikopo hii itakavyotolewa, uwepo utaratibu mzuri sana. Huko nyuma mikopo ilitolewa nje ya utaratibu, matokeo yake fedha nyingi sana hazikwenda kwa walengwa. Kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri, watu wa hifadhi ya bahari, bahati nzuri naamini wapo hapa, wajue mambo yatakapokwenda uwepo utaratibu mzuri ili kusiwe na matatizo yaliyotokea kabla ya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika kitabu chake leo asubuhi hapa ukurasa wa 62, wameeleza vizuri sana na nampongeza sana, kwamba wanafanya mapitio ya Sheria ya Uvuvi, Namba 22, ni jambo jema sana na katika moja ya mambo ambayo alipokuja Mafia Mheshimiwa Waziri tulimlalamikia kwamba kuna mgongano baina ya Sheria ya Uvuvi Namba 22 na Sheria ya Hifadhi ya Bahari. Sasa kwa kilio hiki sasa kuna mambo matatu ningeomba sana Mheshimiwa Waziri ayatilie maanani katika mchakato wake wa kufanya marekebisho ya Sheria ya Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, suala la ukubwa wa nyavu wametuambia samaki watavuliwa kwa nyavu za nchi tatu. Mheshimiwa Waziri alipokuja Jibondo pale alipotamka neno kwamba samaki watavuliwa kwa nyavu ya nchi tatu wananchi walianza kugunaguna kwa sababu kule kwetu kwenye bahari kuna samaki wengine kwa asili ya maumbile yao hawakui zaidi ya ukubwa wa nchi moja na nusu, samaki aina ya ngalala, tili, mbono, samaki wadogo ambao kimaumbile hata ukiwaacha miaka 50 hawawezi kukua.

Sasa wametuletea sheria na sisi tumetoa maoni katika hii sheria mpya wanapoweka nchi tatu kuna baadhi ya samaki kama hawa niliowataja ngalala, misusa, tili, mbono

hawatovuliwa maisha kwa sababu tundu la nchi tatu atapita tu huyo samaki, kwa hiyo naomba sana Mheshimiwa Waziri waliangalie na hao wataalam, namshukuru sana alipokuja Jibondo akatuachia wataalam waje kutoa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yako watalaam wale wavuvi waliwaambia tunashukuru sana mmekuja kutupa elimu, lakini mara ijayo mtakapokuja mje na wataalam wenyewe hasa wa kwenda kuvua baharini, tutachukua nyavu ya nchi tatu, tutakwenda baharini pamoja halafu na sheria kwamba nyavu hairuhusiwi kufungwa mawe chini isiburuze chini ili hao wataalam waende wakaoneshe namna gani ya kumvua samaki, nyavu chini isiguse na nyavu hiyo ni ya nchi tatu, kama utampata samaki hata mmoja. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri kama utaalam upo wa kuvua samaki wa nchi tatu kwa kutumia nyavu bila nyavu kugusa chini, basi tunaomba sana atuletee wataalam hao kwa ajili ya shughuli hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nyavu za milimita...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dau malizia.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nyavu za milimita nane za kuvulia dagaa, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, ametaja kwenye kitabu chake watabadilisha kutoka kwenye milimita 10 kuja kwenye milimita nane, ni jambo jema na tunashukuru sana. Tunaomba sana taarifa hizi ziende kule chini kwa sababu bado kule wataalam watekelezaji wa sheria wanaendelea kuwasumbua wavuvi. Mheshimiwa Waziri dakika moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Uvuvi; hili ni jambo ambalo limezungumzwa sana humu. Namna pekee ya kuleta ukombozi katika uvuvi na kuongeza mapato ya Serikali tuwe na bandari yetu ya uvuvi na nashukuru kwenye kitabu hiki nimeiona bandari ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni lile alilolisema Mheshimiwa Tizeba, Mheshimiwa Waziri akaiangalie ile kanuni ya 0.4 kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu imewakimbiza wakubwa wote wale hawaji sasa hivi, kwa hiyo naomba sana kama watai- *relax* ile ili meli zile zije zivue kwa sababu ile *DSFIA* inakufa na inakufa kwa sababu hakuna mapato yoyote anayekuja kukata leseni kwenda kuvua katika bahari kuu kwa sababu gharama ile ya *loyalty* ya 0.4 wanaiona ni kubwa, iliwekwa kwa nia njema lakini bahati mbaya sana wenzetu hawa hawajakubali kutuletea meli. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dau, muda umepita kwa kweli.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza naanza kwa kuunga mkono hoja ya Wizara hii na kuipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha sasa Tanzania yetu inapata mafanikio katika Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi. Napongeza mikakati na mipango yote iliyopangwa na Wizara na naomba Serikali na sisi wadau tuhakikishe tunaungana na Serikali na Wizara hii kuhakikisha mipango yetu hii inafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi na shukrani hizo na pia naipongeza Wizara kwa kuanzisha kupitia upya Sheria ya Uvuvi na hasa pale walipoamua kwa makusudi kabisa kuwashirikisha wadau wote wa sekta hii ya uvuvi nchini kote Tanzania. Pamoja na hilo pia, naipongeza Wizara kwa kutafsiri Sera ya Uvuvi. Kama tunavyofahamu wavuvi wetu wengi ni masikini hawajasoma Kingereza kwa hivyo naipongeza Wizara hii kwa kuamua kuitafsiri sasahivi ile Sera ya Uvuvi, ili kila mvuvi aweze kutambua sera hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Wizara kwa kufufua Shirika la *TAFICO.* Najua mambo mengi yameshafanyika huko *TAFICO,* lakini pia naomba sasa Serikali iangalie hili jambo ambalo ni mwingiliano wa kisheria na kanuni na majukumu ya utendaji wa kazi kati ya Wizara hii ya Uvuvi na Wizara nyingine za Serikali. Jambo hili likifanyiwa kazi kuna changamoto nyingi zitaweza kutatuka. Pia naomba Serikali iangalie tozo mbalimbali kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara nyingine, kuna tozo zinaingiliana na hivyo kuleta mkanganyiko katika utekelezaji wa majukumu ya kazi ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba nigusie kidogo uvuvi wa bahari kuu. Napongeza sana mchakato wa Wizara na mchakato wa Serikali ulioanza wa ujenzi wa bandari ya uvuvi. Naomba mchakato huo sasa pia uanze na uendelee kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusu uvuvi wa bahari kuu. Sisi kisiwa chetu cha Zanzibar hatuna rasilimali nyingine isipokuwa bahari, tumezungukwa na bahari, mapato yetu yanategemea sana bahari. Naomba sana Serikali iangalie sasa zile tozo ambazo zinatozwa kwa wanaoomba kuvua kwenye bahari kuu, yaani zile leseni za uvuvi ziangaliwe upya zile kodi na tozo ili angalau na sisi hizi leseni zikitolewa nchi yetu nayo itapata mapato kupitia hii sekta ya uvuvi wa bahari kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie kwenye sekta ya ukuzaji wa viumbe kwenye maji. Naipongeza sana Wizara na imepeta fedha hivi karibuni kwa ajili kuimarisha sekta hii ya ukuzaji wa viumbe kwenye maji na hasa ufugaji wa samaki. Pamoja na hilo liende sambamba na Maafisa Ugani ili wawe na teknolojia mpya katika ufugaji samaki na mazao mengine ya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia huu ufugaji hautaki elimu kubwa sana; kwa hivyo naomba kile chuo cha uvuvi kinachofundisha mambo ya ufugaji samaki kiangalie ile mitaala au vile vigezo vya kuingia kwenye chuo kile cha

kujifunza ufugaji wa samaki, kwa sababu tunaona hata majumbani watoto wadogo wa miaka saba wanawafuga wale *gold fish* na wanauza; kwa maana hiyo haitaki elimu kubwa. Hivyo vijana waliomaliza darasa la saba wakiwezeshwa, wakipewa mitaji na wakipewa elimu hii ya ufugaji samaki tunaweza kutatua tatizo la ajira kwa vijana wetu wa darasa la saba na vijana wa *form four* kwa sababu elimu inayohitajika si kubwa sana. Tuandae programu za muda mfupi za kuwafundisha hawa vijana ambao wamemaliza shule mapema ili wajiajiri kwenye sekta hii ya uvuvi na ufugaji wa samaki pamoja na kuwasaidia njia bora za kupata mikopo kwa gharama nafuu au kwa masharti nafuu waweze kukidhi kupata hivyo vifaa vya ufugaji wa samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na huduma mbalimbali za kuwasaidia wavuvi wetu naomba sana Serikali ione Wizara kwamba huduma za kijamii kama vile vyoo, vituo vya afya, vituo vya Polisi kwenye maeneo yale ya madago wanakovua wavuvi vipewe kipaumbele kwa sababu kule nako wanaishi binadamu na kunatokea milipuko ya maradhi, lakini pia kunatokea na hujuma mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo naomba Serikali na Wizara iendelee kuwaboreshea wavuvi wetu zana bora za uvuvi ili kupata uvuvi wenye tija na wenye faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelekea kwenye Wakala wa Maabara na ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija malizia, kengele ya pili imelia.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuipongeza Wizara hii kwa kuanzisha viwanda vya ngozi, viwanda vya usindikaji maziwa

na viwanda vingine vipya vya usindikaji wa nyama. Tuko pamoja tunawapa nguvu viongozi wetu hawa, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Maafisa wote, *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWEYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Mheshimiwa Saada Mkuya, badaye Mheshimiwa Salum Rehani ajiandae.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Kwanza naunga mkono hoja, lakini nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Rais a Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha kuweka mikakati madhubuti kwa ajili ya kuendeleza sekta ambazo ziko katika Wizara hii. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na viongozi wote katika Wizara hii kwa kufanya kazi zao kwa weledi na ufanisi mkubwa, hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda mimi nitajikita katika eneo moja tu, nalo ni uvuvi wa bahari kuu. *Specifically* nitajikita katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu *(Deep Sea Fishing Authority).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hii ni taasisi ambayo kwa kweli ikiweza kufanya kazi vizuri inaweza ikachangia kwa kiasi kikubwa mapato ambayo Serikali zote mbili zinapata. Vilevile mazingira mazuri yatasababisha wavuvi, wananchi ambao wanajishughulisha na shughuli za uvuvi katika bahari kuu nao kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wengi walizungumza kuhusiana na suala la *some percentage* ya hao wanaojishughulisha na uvuvi, lakini ukiangalia Zanzibar, kwa maana ya Unguja na Pemba asilimia 100 kwa sababu ni visiwa ambavyo, kama *definition* ya visiwa, vimezungukwa na bahari, sasa uone kwamba, taasisi hii kwa kiasi gani ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini taasisi hii imekuwa ikikusanya mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali zikiwemo leseni na mambo mengine; lakini katika mwaka 2017 hii *royalty* au mrabaha wa senti 40 za dola zimesababisha kwa kiasi kikubwa taasisi hii kupungua kwa mapato yake ya kujiendesha kama mamlaka, lakini hata mchango wao kwenda katika Serikali Kuu umetoweka, hususan kwa mwaka 2019 hakuna leseni ambayo imekatwa kutokana na tozo hii. Na cha ajabu, maana si kama tumeweka tozo hii kwamba ndiyo tunaimarisha mapato ya ndani, mapato yameondoka na hawa wawekezaji katika sekta hii wanakwenda nchi nyingine ambazo hazina tozo hii. Kwa maana hiyo mapato ambayo sisi tulikuwa tunatarajia kuyapata tunayapeleka katika nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nadhani umepata *concern* za Wabunge lakini vilevile na za wadau mbalimbali kuhusiana na tozo hii. Hii tozo si kwamba uifute moja kwa moja lakini unaweza ukatoa *space* ili tuweze kufanya *review* kuona kwamba je, tunaweza tukaangalia maeneo mengine tupate mapato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwa kinachoonekana sasahivi inaonekana ni kwamba labda utendaji mzuri wa Wizara yetu hii ni kutokana na mapato, lakini utendaji mzuri, yaani mafanikio ya Wizara yetu ni kuona *productivity* katika maeneo mbalimbali imeimarika na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Deep Sea Fishing Authority* mapato yake kwanza inatakiwa asilimia 50 ijiendeshe yenyewe, kama tunavyojua ni mamlaka, lakini asilimia 30 inaingia katika Mfuko wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na asilimia 20 inaingia katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anafahamu, asilimia 20 kwa namna yoyote, kwa mapato ya aina yoyote ni *significant contribution* kwa ajili ya Bajeti ya

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ikiwa Mheshimiwa Waziri bado una-*resist* ku-*review* hii kanuni, maana siyo sharia, ni kanuni, kwa ajili ya kuondoa tozo hii maana yake unaumiza Serikali hizi. Unaumiza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, unaumiza na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sisi Mheshimiwa Tizeba nakwambia Zanzibar tunalia, tunalia kwelikweli, tunalia kwelikweli na tumeshazungumza muda mrefu. Mheshimiwa Waziri hii tozo iondoshe kwa muda ili uwape nafasi mamlaka wafanye *review* waweze kuangalia maeneo mengine. Sisi tunakosa wenzetu wanapata, na si kwamba tunakosa kwa wananchi tu bali unakosesha mapato kwa Serikali zote mbili; Mheshimiwa Waziri liangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aje na majibu ambayo yataleta matumaini. *Otherwise* tutashika shilingi tuone kwamba kwa ujumla wetu sisi kama Wabunge tunalichangia hili maana yake pesa zinaondoka, mapato yanakosekana na hata hao wavuvi, wawekezaji ambao tunatarajia wawepo wanaondoka wanakwenda sehemu nyingine ambapo wenzetu hawana tozo ya aina hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *otherwise* naunga mkono hoja na ninaomba sana Mheshimiwa Waziri utakapokuja utueleze kwa kina ni kwa sababu gani tozo hii inaendelea kuwepo na *impact* yake kuendelea kuwepo kwake. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Saada Mkuya. Tunaendelea na Mheshimiwa Salum Rehani, baadaye Mheshimiwa Gimbi Masaba ajiandae.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi kupata fursa hii kuchangia hoja ya Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilitaka niunge pale ambapo mchngiaji amemaliza. Tanzania takribani tumekosa

kwa wastani, tungeweza kupata, kwa mwaka huu, zaidi ya meli 54 ambazo zingeweza kutuingizia si chini ya bilioni zaidi ya 20 mpaka 30 za pesa ambazo zingeweza kuingia kwa tozo ile ya *0.4.* Kwa kweli lazima tuseme ukweli kile ni kikwazo na hakuna mtu ambaye atakaekuja kwa ile *0.4.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili wenzetu Comoro tu hapo safari hii wamesajili meli 31 kwa kutumia *gape* hilihili, kwamba sisi tumeshindwa kuweza kutoa hiyo fursa ya kuondoa hiyo tozo, imetu-*cost.* Wao wanasema hawajawahi kupata mapato mengi yatokanayo na uvuvi kama mwaka huu kwa vile sisi tumeshindwa kutoa hiyo tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ndani ya maeneo yetu ya bahari tuna zaidi ya maili 360 zinavua katika ukanda wa Tanzania katika meli za mraba zile zaidi ya mia mbili na ishirini na tatu elfu zinavuliwa, watu wanavua; na hayo ni mataifa ya nje; na ndiyo maana ikapatikana ile takwimu ya asilimia 67 ya mapato wanayochukua nje yanatokana katika ukanda wetu wa uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, tunapoteza kiasi kikubwa na hii sekta tuseme ukweli bado haijafanya vizuri. Mimi nakataa kuniambia takwimu ya kwamba, samaki walioko katika Ziwa Victoria ni wengi zaidi kuliko walioko katika ukanda wa bahari, hiyo *data* mimi siikubali. Naomba tupate *reference* iliyo ya uhakika zaidi; kwa sababu meli za mraba zaidi ya 1,400 ukaseme kwamba eneo la Ziwa Viktoria ndio samaki wengi? Si kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *stock fishing* imefanyika juzi baada ya miaka zaidi ya 20 na meli ile ya ki-Norway, taarifa rasmi hazijaja. Kwa hiyo Waziri utupe taarifa zilizokuwa sahihi zaidi kuhusiana na eneo hili. Bahari yetu bado ni *potential,* ina samaki wakutosha, lakini bado hatujafanya uwekezaji ulio sahihi tukaweza kuvuna samaki ambao wako katika maeneo yetu matokeo yake tunawafaidisha watu wengine ambao hawako Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jingine nililotaka kulizungumza ni kwenye sekta ya mifugo. Sekta ya mifugo pamoja na maelezo mengi na mazuri ambayo umeyatoa ya kukusanya maduhuli, lakini bado sekta ya mifugo inakabiliwa na changamoto nyingi; kwanza kwenye ngozi yenyewe. Kitendo kile cha kupiga chapa kimesababisha ngozi yetu ikose thamani na imejazana kwenye magodauni, hainunuliki popote sasahivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ng'ombe wengi wamepigwa chapa, uchinjaji uliofanyika holela, hakuna viwanda vya kuchakata samaki matokeo yake ng'ombe wetu wanakosa thamani ya ubora katika viwanda mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi sasahivi umejitokeza mtindo kwamba wenzetu wa Nigeria wanakuja kuchukua zile ngozi kwa ajili ya chakula na si kutumia kwa ajili ya kuchakata kwenye viwanda mbalimbali. Kwa hiyo nafikiri tunahitaji tujitathmini na sheria zetu na kanuni zetu ili kuona kwamba suala hili ili liweze kuboresha mazingira tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na watu wale wa kiwanda kile cha Magereza cha Luanda, bado wanasema ngozi zetu haziendani na thamani ya viatu ambavyo wanavitengeneza. Wakati mwingine wanalazimika kuchukua ngozi nje ya Tanzania kwa ajili ya uendeshaji wa viwanda vyetu. Tunahitaji tuone tunafaidika na rasilimali tulizonazo ndani ya nchi na si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye suala zima la maziwa na hasa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Bado Serikali au sekta hii ya mifugo haijawekeza kwenye *dairy farm.* Tunahitaji kuwa na ng'ombe wa maziwa na si kuchunga ng'ombe. Watanzania wanachunga ng'ombe sana, lakini hawafugi ng'ombe inavyotakiwa, matokeo yake sasa tunashindwa kuweza kuingia katika soko la maziwa na sisi kuwa ni *dampo* la kuletewa maziwa kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zimbabwe imekuwa Tanzania ndio soko lake kubwa, Malawi sasahivi ndio soko lake vilevile, Uganda wanatuletea, Kenya wanatuletea, lakini sisi tunajisifu kwamba ni wa pili sijui wa tatu kwa kuwa na ng'ombe wengi hapa Tanzania, haileti maana kwa kweli. Tunataka tuone *restructuring* ya maana katika sekta ya mifugo na si hivi tunavyokuwa tunaelezwa kila siku, hatujafanya vizuri katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tunalolisema ni kwamba tunahitaji kuona kwamba viwanda vile vya maziwa vya hapa vinatengeneza bidhaa ambazo zinakubalika katika masoko. Tatizo letu bidhaa za viwanda vyetu haziingii kwenye soko la utalii. Sisi kule Zanzibar wale wanaoleta maziwa zaidi ya tani 40 kila mwezi zinashushwa pale na zinasambazwa katika ukanda wa hoteli za kitalii. Maziwa yale yangekuwa ya Watanzania pato lile lingerudi likaingia Tanzania, lakini maziwa yale unayaona ni ya Wakenya, Waganda, Wazimbabwe na Afrika Kusini, *this is not fair.* Tunataka tuone mabadiliko chanya sasa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rehani, muda umeisha.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Haya, tunaendelea na Mheshimiwa Gimbi Masaba.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani Bungeni. Hotuba yetu ina vitu vizuri, tumeshauri vizuri, naiomba Serikali ichukue ushauri huo utawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite moja kwa moja kwenye Operesheni Nzagamba. Naenda moja kwa moja kwenye Operesheni Nzagamba kwa sababu ninafahamu ni nini ambacho ninakwenda kukizungumza na nini matokeo ya Operesheni Nzagamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposimama hapa, hususan mimi nikisimama ni kwamba si mgeni kwenye suala la ufugaji, hata uvuvi. Operesheni hii naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge, kwamba tunapozungumza hii operesheni inawezekana wapo wachache ambao wanaielewa kwa udogo sana, lakini niwaambie kwamba jambo hili la Operesheni Nzagamba limesababisha matatizo makubwa sana. Limesababisha vifo, watu kufilisiwa ng'ombe wao; limesababisha matatizo mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lililopita hapa tulipitisha Sheria ya Mahakama za Kutembea, tukazibariki. Sasa hiyo sheria tuliyoipitisha mimi nasema imekwenda kutumika kwa wafugaji. Imetumikaje; hawa waliokuwa wanatekeleza Operesheni Nzagamba walikuwa wanakwenda wakiwa na timu nzima; wakiwa na mnunuzi wa ng'ombe, wakiwa na dalali, wakiwa na Mwanasheria, wakiwa na mgambo. Sasa kama ng'ombe wanapigwa Itilima atakayenunua wale ng'ombe si wa Itilima, unakuta ametoka Katavi, unakuta ametoka mikoa mingine. Sasa najiuliza kwamba, hawa waliokuwa wanaenda kununua hawa ng'ombe walikuwa wanajuaje kwamba kuna mnada wa ng'ombe Itilima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni changamoto ambayo ni kubwa. Kilichokuwa kinafanyika, wanakwenda na mgambo wakiwakuta wale wachungajhi wale, wanakimbia wanawaacha, wanawakimbia wale ng'mbe wao. Mgambo wanawazingira wale ng'ombe, wakishawazingira wale ng'ombe dalali anaanza kazi yake. Anaanza kufanya hivi, analeta ng'ombe mmoja-mmoja anasema ng'ombe huyu laki nne, anakosekana mnunuzi, laki tatu, anakosekana, laki mbili, anakosekana, laki moja, anakosekana. Anaweka pembeni analeta tena ng'ombe

mwingine, laki nne, anakosekana, wakifika ng'ombe wanne anawaambia laki tatu kwa pamoja, mununuzi anapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Mheshimiwa Waziri alipoteuliwa, Wasukuma wote tulifurahi katika uteuzi wa Rais, tulishangilia kwa sababu anafahamu jiografia ya wafugaji, lakini umekwenda kututelekeza. Leo wafugaji wanalia anajifanya kwamba hajui umuhimu wa wafugaji, jambo ambalo linasikitisha sana. Naomba wanisamehe kaka zangu wote wanaotoka Mkoa wa Simiyu, Mheshimiwa Mpina ametutelekeza, haendani na kile tulichokuwa tunakitegemea sisi. Haiwezekani leo Mheshimiwa Waziri asisahau... (Makofi)***[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gimbi, Mheshimiwa Jenista kuhusu utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kiutaratibu na watu wanaweza wakaliona ni jambo ambalo halina maana, lakini naomba niseme Kanuni ya 64(1)(b) inampasa kila Mbunge anayechangia humu ndani kuchangia hoja kwa kuzingatia hoja ambayo imewasilishwa ndani ya Bunge. Hoja inayochangiwa inahusu Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Waziri mwenye dhamana ya Mifugo na Uvuvi alipoteuliwa hakuteuliwa kwa muktadha wa kutazama kabila la Wasukuma, aliteuliwa ili kuwa na *fairness,* kusimamia sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza Sekta nzima ya Uvuvi na Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, si sahihi sana kusema kwamba alipoteuliwa Waziri huyu, Wasukuma walifurahi lakini sasa Wasukuma wanasikitika amewatelekeza,

siyo *fair*. Ni lazima tuseme siyo *fair*, tuchangie kwa kuzingatia utaratibu ambao... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Jenista. Mheshimiwa Gimbi maneno hayo ni ya maudhi kwa hiyo naomba uyaondoe.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siamini kama nimezungumza kitu ambacho ni cha ajabu sana, siamini. Nasema hivyo kwa kutumia lugha ya Wasukuma nikiamini kabisa kwamba Wasukuma ndiyo wafugaji wakubwa wakifuatiwa na Wamasai, nimezungumza hivyo. *(Makofi)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Taarifa.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Nimezungumza kwa uhalisia huo.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Taarifa.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naona muda umeisha, hamna taarifa wala nini, Mheshimiwa Gimbi endelea.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gimbi naomba uendelee kutoa mchango wako kwa lugha iliyokuwa inastahiki Bungeni.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Nimezungumza haya kwa uchungu, sikutaka kwenda kwenye kitabu cha Waziri hata kidogo. Mara nyingi kwenye michango yangu nimekuwa nikisimama nazungumzia kuongezewa kwa bajeti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini kuna nini tena. Mheshimiwa Gimbi kidogo, Mheshimiwa *Chief Whip* wa upande wa Upinzani.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepaswa nitoe taarifa hii kwamba hata wafanyabiashara wanafurahi kama Waziri mfanyabiashara ameteuliwa kwa sababu anaifahamu sekta. Kwa hiyo, Gimbi hakuwa na maana ya ukabila ila alikuwa ana maana kwamba kwa sababu Mheshimiwa Mpina ni mfugaji, basi wafugaji watafurahi kwa sababu anaifahamu sekta. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gimbi naomba uendelee.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza uhalisia wa mazingira yenyewe, Mheshimiwa Waziri anajua, pamoja na kwamba wananchi walitaifisha hizo ng'ombe, kuna wananchi walikwenda mahakamani na walishinda kesi.

Sasa anataka kuniambia kwamba wananchi walioshinda kesi Mkoa wa Simiyu, hajui kama wanatakiwa kurudishiwa ng'ombe wao? Mpaka leo hawajawahi kurudishiwa ng'ombe, halafu leo wanataka tuzungumze maneno ya upole, kwa vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la uvuvi, sawa Mheshimiwa Mpina amekulia dagaa lakini leo dagaa kwa wavuvi imegeuka almasi. Mkoa wa Simiyu tuna minada, leo ukienda kwenye mnada unatafuta dagaa huwaoni, lakini muuzaji wa dagaa yupo, maana yake ni kwamba dagaaameficha *guest*, kwa hiyo ukimuuliza dagaa wapo wapi, zipo *guest* unataka? Huko ndiyo anatupeleka Mheshimiwa Mpina, dagaa wanauziwa *guest* halafu wanataka tuzungumze lugha ya kipole hapa, haiwezekani. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ambacho hakifahamu Mheshimiwa Mpina kwa wafugaji na wavuvi, hapana haiwezekani...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gimbi malizia sentensi yako.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kidogo sekunde tu. Huu uanzishaji wa hifadhi za wanyamapori za jamii zimeleta changamoto kubwa sana. Mwaka jana nilizungumzia kuhusu suala la Hifadhi ya *Maswa Reserve* kuhusu kuongeza mipaka, wananchi wanakosa malisho na kila kitu, lakini wametanguliza watu wanakwenda kulaghai viongozi halafu wanachukua maeneo wananchi wanashindwa kupata machungio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yanaudhi sana, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuomba Mwongozo wa mujibu wa Kanuni 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli bado naendelea kuomba sana hili jambo la kuchangia hoja ndani ya Bunge kama lilivyowekwa mbele ya Bunge lako leo na Mbunge kwa kujielekeza katika mitazamo ya kikabila, bado naendelea kusisitiza...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kusisitiza halifai.

**MWENYEKITI:** Sawa Mheshimiwa Jenista umefahamika. Waheshimiwa Wabunge naomba tutulizane, muda wetu umekwisha naomba tusikilizane.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa haiwezekani kila mtu akawa anaongea kama tupo sokoni, kuna mwingine amesimama anaongea, mwingine anataka kusimama, hiyo sheria ya wapi? Mheshimiwa Jenista naomba umalize kwa haraka.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili kwa mujibu wa kanuni haliendeshwi kwa muktadha wa kikabila, udini na ukanda. Naomba sana nilisemee jambo hili kwa sababu tukiliacha, kesho atainuka mtu mwingine atajenga hoja kwa udini na ukabila. Kwa hiyo, naomba jambo hili kwenye *Hansard* na kumbukumbu ya leo liondolewe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa Mheshimiwa Jenista, Waheshimiwa Wabunge ni maneno ambayo siyo ya uongo ni sahihi; hatuendeshi Bunge kwa misingi ya kabila wala dini, tunajenga hoja bila kuudhiana. Mheshimiwa Mwakajoka kaa chini...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakajoka kaa chini. Nasema tunaendelea na michango yetu, Wabunge

waliobaki ni watatu kila mmoja dakika tano, Mheshimiwa Jitu, Mheshimiwa Jacqueline na Mheshimiwa Mattar.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa ya kuchangia siku ya leo. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nimshukuru Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa nia njema na jitihada kubwa anayofanya kuhakikisha kwamba jambo hili, Sekta ya Mifugo na Uvuvi iweze kuchangia katika pato la Taifa lakini pia kulinda maslahi ya wafugaji na wavuvi kwa ujumla. Pia niwashukuru na niwapongeze Waziri, Naibu Waziri na Katibu Wakuu wote kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri katika maeneo machache:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; naomba tuendelee kujikita na kuboresha huduma mbalimbali kwa mfano ya *veterinary,* fedha iliyotengwa ni ndogo lakini tuangalie namna ya kuwapatia mikopo na nini ili huduma ya *veterinary* iendelee kufika katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeendelea kuomba Wizara hii ndiyo ina jukumu la kulinda ardhi zote za wafugaji, leo ardhi za wafugaji zinaendelea kuporwa na kubadilishwa matumizi na yanabadilishwa matumizi kutoka kwenye *general land* na kuingia kuwa maeneo ya hifadhi, lakini pia vijiji vinabadilisha matumizi ya ardhi ya wafugaji ambayo tayari yalishatengwa kabisa na yalipewa na hati, wanakaa kwenye mkutano kwa sababu wafugaji ni wachache, wanabadilisha hayo maeneo yanakuwa ni maeneo ya kilimo. Sasa ndiyo maana inaleta mgongano mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo ningeomba nichangie ni *blueprint*. Ni vizuri Serikali ikasimamia kweye Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi *blueprint* hasa tukiangalia kwenye suala la viwanda vya maziwa. Viwanda vya maziwa vinapata tatizo kubwa na vinashinda kushindana na maziwa kutoka nje kutokana na ada, tozo, kodi na ushuru mbalimbali.

Jambo hili tusipoliangalia vizuri, viwanda hivi na hii ndoto yetu kubwa tutakuwa hatufikii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuwe na maziwa ya kutosha tushindane na wenzetu majirani, ningeomba kwenye kituo kile cha Nike tuwekeze fedha za kutosha, tuwapatie fedha ili waende kuhimilisha ng'ombe katika maeneo mbalimbali, tupate ng'ombe wazuri, bora na pia ule mpango wa kuzalisha mitamba 5,000 kwa mwaka, ningeomba Serikali iangalie kwa juhudi yoyote ile nje ya mfumo wa bajeti namna ya kuzalisha mitamba ya kutosha. Tukitaka kuwa na maziwa ya kutosha na ng'ombe wazuri, lazima tuwe na mifugo ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mbali na hiyo lazima Serikali wakae kwa pamoja kuangalia ule mnyororo wa thamani wa namna ya kuhifadhi bidhaa za uvuvi lakini pia mifugo, *cold storage* na *chillers* nayo waangalie namna ya kuboresha, kuwekeza humo na kuondoa kodi mbalimbali. Tatizo kubwa la wafugaji ni upatikanaji wa maji, majani ya uhakika (malisho), lakini hivyo hivyo njia pekee ya kufanya hivyo ni Serikali kuondoa kodi kwenye mitambo ya kuchimba maji, kutengeneza mabwawa na majosho. Hili siyo lazima Serikali ifanye, Sekta Binafsi wafugaji wakiwawekea mazingira wezeshi na niwapongeze kwamba wana leongo la kuunda ushirika wa wafugaji ili na wao wakakope kwenye Benki ya Kilimo, waweze kukopa kwenye Mfuko wa Pembejeo, wao wenyewe kutokana na mifugo tuliyokuwa nayo tutaweza kuwekeza. Tatizo kubwa linakuja Sekta isiyokuwa rasmi inaendelea kukua kutokana na hiyo *blueprint,* ada, kodi, tozo na ushuru mbalimbali. Hatutafanikiwa kama wasipokaa na kuangalia namna ya kuboresha jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze kwenye suala la *aqua culture,* wanafanya vizuri. Ningeomba elimu hiyo iendelee kutolewa na watusaidie katika maeneo mbalimbali ili tukuze pato la Watanzania kwa wingi, lakini pia wapate chakula na bidhaa za kufanyia kazi kwenye viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naunga mkono hoja, mengi nitaandika kwa maandishi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jitu. Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana; kwanza naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapambano dhidi ya uvuvi haramu; nichukue nafasi hii kuipongeza sana Wizara, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, Naibu Waziri na *delegation* yake yote, hongereni sana kwa kazi nzuri ya mapambano dhidi ya uvuvi haramu. Mapambano haya yameleta tija sana katika nchi yetu lakini pia niwapongeze sana kwa kuvuka lengo la ukusanyaji wa mapato, asilimia 150 haijapata kutokea, hongereni sana. Wizara ina vijana makini wanafanya kazi kwa weledi na ndiyo maana Wizara inaoneka sasa ina uchechemuzi, mambo yanaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika tano ni chache sana lakini naomba kwa ruhusa yako utaniongeze kidogo ili niweze kumalizia. Niwashauri sasa Mheshimiwa Waziri na *delegation* yake, wazingatie sana ushauri ambao Waheshimiwa Wabunge wanautoa humu ndani dhidi ya mapambano ya uvuvi haramu. Ushauri huu utawasaidia sana kuboresha na kuongeza tija katika Sekta hii ya Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Ziwa Nyasa; kupitia suala la uvuvi haramu kwa maana ya ushauri ambao nataka kuutoa. Uvuvi haramu pia umeathiri sana katika Ziwa Nyasa, ndugu zetu wavuvi katika Ziwa Nyasa wamepata shida kwenye suala la nyavu, nao pia wamechomewa nyavu. Kwa hiyo, niombe wale wavuvi wamechomewa nyavu kupitia zao la samaki, lakini pia zao mahsusi sana la samaki anaitwa kituhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituhi ni samaki mdogo sana, mtamu na mwenye virutubisho vingi sana, lakini huyu kituhi kwa umbile lake ni mdogo, ndivyo alivyo. Ni sawasawa na binadamu na sisi nao tuna maumbile tofauti tofauti, huwezi kwamba huyu ni mfupi, basi ni mdogo basi siyo binadamu kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niseme samaki anayeitwa kituhi ni mfupi anafikia inchi karibu mbili au tatu. Kwa hiyo, sasa imekuwa ni shida, wavuvi wemechomewa nyavu na kwamba samaki huyu hawezi kuvuliwa. Sasa nataka niseme hivi Mheshimiwa Waziri kwamba naomba atambue wazi kwamba yule samaki hivyo alivyo ndivyo alivyo, kwa hiyo, naomba arudi Ziwa Nyasa akafanye mambo ambayo yatakuwa yanaleta uzalishaji wenye tija katika Ziwa Nyasa. Pia kutokumvua huyu samaki maana yake Mheshimiwa Waziri na *delegation* yake wanataka sisi Wangoni tuwe wadumavu. Samaki huyu anatusaidia sana kutustawisha kama mnavyotuona katika Bunge hili tumestawi na tumenawiri barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la josho katika Kata ya Linga, naomba Mheshimiwa Waziri atume watu wake kule katika Kata ya Linga kuna wafugaji wengi lakini hakuna josho, tunataka...

**MWENYEKITI:** Nimekuongezea dakika mbili.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba pia tupate mabwawa ya ufugaji wa samaki. Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, kule Ruvuma kuna mama zao na vijana wenzao, wanahitaji kuwekeza kwenye mabwawa ya samaki. Tunawaomba sana waje wafanye uwekezaji kule wawasaidie ili waweze kufanya uwekezaji kwenye mabwawa ya samaki. Pia, walete ng'ombe na sisi tunahitaji kufuga, walete ng'ombe sisi tutawasimamia na umeme sasa hivi wa gridi upo, hivyo tunahitaji kuweka viwanda ili tufanye uchakataji kwenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa ziara yake aliyoifanya Mkoani Tanga kwenye Kiwanda cha *Tanga Fresh.* Alipofika kule alikuta kuna changamoto kubwa sana ambayo ilikuwa ni kikwazo kikubwa sana cha kukuza uzalishaji katika kiwanda kile hasa kwenye uzalishaji wa maziwa ambayo ni *UHT,* haya maziwa ni mazuri lakini pia yana uwezo wa kutunzika kwa muda mrefu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais alichokifanya alikwenda kuondoa changamoto ya suala la ardhi kwenye kiwanda hicho, akatoa maelekezo ardhi ile wakaipata na wakaenda kukopa wakapata bilioni 10. Sasa hivi wamefanya uwekezaji mzuri na leo kila Mbunge hapa alishika kamfuko amepata maziwa, Magufuli oyee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye Kiwanda cha *Asas,* nao pia niwapongeze sana kwa uzalishaji mzuri sana wa maziwa ya *UHT.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Wizara kwa kusimamia kuhakikisha kwamba kunakuwa na viwanda vya uchakataji wa nyama; Kiwanda cha Kibaha na Longido, hongera sana wako vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niseme hivi, nawapongeza tena kwa kuhakikisha kwamba wanaweka mkataba kati yao na nchi ya Misri, Misri wanakuja kuchakata hapa nyama lakini pia Misri wanakuja kuwekeza kwenye ngozi, tutapata ngozi zetu lakini pia tutaweza kutengeneza mikoba, mikanda na mambo mengine... *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wenzetu Ethiopia wameweza...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** ...kama wenzetu Ethiopia wameweza, sisi tunashindwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya nakushukuru sana, naomba...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ametushtua anasema UTI, kuhusu utaratibu.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nani kama Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. Waheshimiwa Mawaziri oyeee. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, dakika zilizobaki Mheshimiwa Mattar.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwakajoka kaa chini.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa muda umeisha, naomba amalizie dakika zake Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa muda huu niweze kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wawili wamezungumza kwa makini kabisa na leo niliseme ili

Mheshimiwa Waziri aweze kulifahamu. Tukiondoa mrabaha wa 0.4 hivi leo, kesho tu asubuhi kuna meli zaidi ya 50 zinataka kuja kuchukua leseni ndani ya Tanzania. Tukiweza kuondoa mrabaha huu ambao ndiyo kikwazo katika uvuvi wa nchi yetu, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aweze kuondoa mrabaha huu ili wavuvi na wawekezaji waweze kuja ndani kuvua katika Bahari Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kuondoa mrabaha huu na siwezi kufahamu tatizo ni nini linalomkwamisha Mheshimiwa Waziri, kuondoa mrabaha huu ambao ni usumbufu mkubwa. Huu mrabaha naamini hata Mheshimiwa Waziri akija anaweza akaja na majibu mazuri kuhusu kuondoa huu mrabaha ambao ni kero kubwa katika kuwekeza katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu bila ya uvuvi hatuwezi kusogea mbele, tukiwekeza kwenye uvuvi tunaweza tukapata mafanikio makubwa kuliko ambayo anayakusudia. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, nilizungumza nyuma ununuzi wa meli kubwa za uvuvi umeshindikana hapa haupo kabisa, mimi mwenyewe nashangaa. Sasa leo wawekezaji wanataka kuja, anawawekea kodi kubwa ambayo itawasumbua hawawezi kuvua katika bahari kuu. Sasa hawa samaki nia yake Mheshimiwa Waziri kuwafanya nini kwa sababu samaki huwa anatembea, samaki siyo mawe, akiwazuia yeye hapa basi huko wenzake wanawavua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, naamini akija hapa, anaweza kuondoa kwa mara moja huu mrabaha ili wawekezaji wetu waweze kuja kuvua ndani ya bahari yetu hii. Tuna shida ya wawekezaji, wawekezaji wapo, tunawazuia kwa vijisheria vidogo vidogo; hili suala Mheshimiwa Waziri siyo kweli na naamini anaweza akafanya hii kazi kwa mara moja ili hizi meli ziweze kufanya kazi. Tunasubiri tuwekeze meli zetu, meli hazipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, ukiangalia hii kodi hata na sisi upande

wa Zanzibar tunafaidika asilimia kubwa tunategemea katika bajeti yetu ya Serikali, sasa leo akisema hizi fedha haziendi, leseni hakuna, sasa kule Zanzibar Mheshimiwa Waziri tufanye nini na sisi katika mategemeo yetu hili suala la uvuvi pia tunategemea kwa sababu Kisiwa cha Zanzibar kimezungukwa na habari kila mahali sasa maendeleo yetu yote yanategemea uvuvi wa bahari kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo akiendelea kuzuia uvuvi huu, hatutafika mahali pazuri. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri akija kesho kutoa majibu, jibu la msamaha wa huu mrabaha, basi namwomba sana aweze kuondoa na siyo kwa muda, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Saada kazungumza aondoe kwa muda; huu unatakiwa kuondolewa kabisa, usiwepo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mattar kwa mchango mfupi lakini wenye msingi mzuri sana.

Waheshimiwa Wabunge kama mtakumbuka asubuhi niliombwa mwongozo na Mheshimiwa Ester Mmasi na nilitoa maelekezo kuwa nitapitia Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* ili nione maneno hayo kama ni kweli yalisemwa kwa namna hiyo ambayo Mheshimiwa Joseph Selasini alizungumza.

Waheshimiwa, nimepitia taarifa hizo na naomba ninukuu maneno ambayo alitamka Mheshimiwa kwa kumalizia sentensi yake, Mheshimiwa Selasini alisema nanukuu: *"Vijana wetu waachwe kupigwa na Mheshimiwa Ester Mmasi ambaye anawakilisha vijana hapa awe na adabu."*

Waheshimiwa Wabunge, katika taarifa rasmi za Bunge, nimeshindwa kumwelewa Mheshimiwa Joseph Selasini ni kwa nini alihusianisha jina la Mheshimiwa Ester Mmasi katika maombi yake ya Mwongozo kwa kuwa siyo vitu vilivyohusiana.

Aidha, maneno ambayo Mheshimiwa Joseph Selasini alitumia si maneno yanayotakiwa kutumiwa na Mbunge, maneno ya awe na adabu yalikuwa ni lugha ya kuudhi ya kumdhalilisha Mheshimiwa Ester Mmasi kinyume na masharti ya Kanuni ya 64(1)(f) na (g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Lugha hii ni kati ya mambo yalisiyoruhusiwa kusemwa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, kauli ya kumtaja Mbunge mwenzako kuwa awe na adabu, tafsiri yake ni kwamba hana adabu. Kwa mujibu wa tafsiri ya Kamusi Kuu ya Kiswahili Sanifu ya Baraza la Kiswahili la Taifa, adabu maana yake ni mwenendo mwema wa mtu kwake na watu wengine, kuwa na heshima katika kufanya mambo hasa yanayokubalika katika jamii, heshima, nidhamu, staha. Kwa upande mwingine kutokuwa na adabu ni kwenda kinyume na mambo ambayo nimeyataja.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ester Mmasi ni Mbunge mwenye adabu na ndiyo aliaminiwa na chama chake na kuchaguliwa na kuwakilisha vijana hapa Bungeni. Hivyo, ni kweli kuwa kauli iliyotolewa hapa Bungeni leo asubuhi na Mheshimiwa Joseph ni kauli ya kumuudhi na kumdhalilisha Mheshimiwa Ester Mmasi.

Kwa hali hiyo, kila mmoja wetu humu Bungeni anapaswa kutumia lugha za kibunge na zenye staha na heshima dhidi ya Mbunge mwenzake, kasoro namna hii haziwezi kuvumiliwa katika Bunge letu na tunapaswa kuzipiga vita. *(Makofi)*

Kwa maelezo hayo na kwa mujibu wa Kanuni ya 5 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naagiza kwamba maneno hayo yasiyoruhusiwa yaliyotolewa na Mheshimiwa Joseph Roman Selasini dhidi ya Mheshimiwa Esther Mmasi wakati alipokuwa anaomba Mwongozo wa kiti yafutwe na yaondolewe kwenye *hansard*. Huo ndiyo mwongozo wangu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo dogo tu hapa, kuna wageni walikuja asubuhi wamesahauliwa, wameingia jioni wa Mheshimiwa Oliver Semguruka ambao ni Ustaadhi Said Juma pamoja na wenzake Ndugu Ali Barongo, Ndugu Mashaka Ramadhan na Ndugu Mohamed Amiri, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge nawapongeza kwa kumaliza shughuli za leo na Mwenyezi Mungu awabariki sana na Ramadhani hii.

Baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.03 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 22 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*